# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Kumi – Tarehe 23 Aprili, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MHE. ABEID R. IGHONDO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali, Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai, Mbunge wa Ngorongoro, sasa aulize swali lake.

Na. 119

### Fedha za Ujenzi wa Daraja la Mto Juhe – Samunge

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatenga fedha za ujenzi wa Daraja la Mto Juhe, Kata ya Samunge?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zainab Katimba majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeliweka Daraja la Mto Juhe kwenye mpango wa madaraja yatakayofanyiwa usanifu kuanzia

Mwaka wa Fedha 2025/2026, ambapo shilingi 114,890,000 zinatarajiwa kutumika katika kufanya usanifu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuihudumia miundombinu ya barabara na madaraja Ngorongoro kwa kujenga, kukarabati na kufanya matengenezo ya miundombinu hiyo kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza swali la kwanza; kwa sasa hivi mvua zinaendelea kunyesha na wananchi wanashindwa kupeleka mazao kwenye masoko yao na wanafunzi wanashindwa kwenda shuleni. Kwa nini Serikali isichukulie ujenzi wa daraja hili au usanifu wake kwa haraka kwa sababu wananchi wanashindwa kufanya shughuli zao?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kuna daraja la aina hiyo hiyo la Mto Piyaya, Serikali ina mpango gani kwa ajili ya kufanya usanifu pamoja na kujenga? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zainab Katimba majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge amekuwa akifanya ufuatiliaji wa hali ya juu kuhusiana na miundombinu ya daraja hili la Mto Juhe katika Kata ya Semunge. Pia amekuwa akifanya ufuatiliaji wa kuhakikisha kwamba, miundombinu ya barabara katika jimbo lake inaimarika. Amekuwa akifuatilia ahadi ya Makamu wa Rais ya kilomita 12 zote hizi amekuwa akihakikisha kwamba anataka kuona kwamba wananchi wake wanaweza kupatiwa suluhu na miundombinu hii inaweza kuimarishwa katika jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama nilivyojibu kwenye majibu ya msingi katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 tutaanza na usanifu wa Daraja hili la Mto

Juhe ili hatimaye tuweze kutenga bajeti na kuijenga daraja hili ili liweze kuwanufaisha wananchi wako.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika katika Daraja hili Mto Piyaya na lenyewe tutalifanyia usanifu ili tuweze kufahamu gharama ya ujenzi wa daraja hilo, tuweze kulijenga kwa ajili ya manufaa mapana ya wananchi wako na tutaendelea kuhakikisha kwamba tunachukua hatua za dharura kwenye mazingira ambayo mawasiliano yamekatika ili wananchi wasikwame katika shughuli zao za uchumi na wasikwame katika kupata huduma za msingi za kijamii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asenga, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, tunaishukuru *TARURA* kwa kutupatia machuma ya kivuko cha Kidatu Kati na Kidatu A inayohusisha na barabara ya Chikago ambayo Mkandarasi ameondoka kwa muda mrefu. Je, ni lini Serikali itamsimamia mkandarasi yule kurudi ili kukamilisha ile barabara ya Chikago na Kivuko…

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa miundombinu ya barabara hizi za wilaya zinazosimamiwa na *TARURA* na Serikali imekuwa ikitenga bajeti kila mwaka kuhakikisha kwamba, inawekeza zaidi katika kuimarisha miundombinu hii.

Mheshimiwa Spika, katika utengaji wa fedha hizo, imehakikisha inasimamia utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa miundombinu hii ya barabara za *TARURA* kwa umakini mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kuendelea kumhakikishia Mheshimiwa Asenga Abubakari kwamba, Serikali itaendelea kufuatilia na kuhakikisha, ujenzi wa miundombinu ya

barabara hii aliyoitaja na eneo hili la daraja alilolitaja unakamilika ndani ya muda wa kimkakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Chaurembo swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, ni lini ujenzi wa Daraja la Mto Majisaku utaanza ambao mkataba wake ulishasainiwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nimtaarifu Mheshimiwa Abdallah Chaurembo kwamba, daraja hilo alilolitaja ujenzi wake utaanza mara moja kwa maana ya mchakato wote wa kumpata mkandarasi umekamilika na sasa punde wataona kabisa kazi hii ya ujenzi wa daraja hili muhimu kabisa kwa wananchi wake unaanza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anton Albert Mwantona Mbunge wa Rungwe sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda.

Na. 120

**Usajili wa Wanafunzi Shule ya Msingi Ushirika – Rungwe**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA K.n.y. MHE. ANTON A. MWANTONA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza kusajili wanafunzi katika shule ya Msingi ya Ushirika Kata ya Mpuguso iliyojengwa kwa nguvu za w ananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Shule ya Msingi ya Ushirika ilisajiliwa rasmi tarehe 9 Januari, 2024 na kupewa namba ya usajili EM.20614, kwa barua yenye kumbukumbu Na. EA.295/315/20A/32 ya tarehe 9 Januari, 2024.

Mheshimiwa Spika, shule hiyo ilianza kupokea wanafunzi tarehe 5 Februari, 2024. Kwa sasa shule ina jumla ya wanafunzi 138, wakiwemo wavulana 74 wasichana 64 ambao wako darasa la awali hadi darasa la tatu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inawapongeza wananchi wa Kata ya Mpuguso kwa michango na jitihada zao zilizowezesha upatikanaji wa elimu karibu na maeneo yao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda swali la nyongeza.

**SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sina swali la nyongeza zaidi ya kupongeza Serikali kwa ajili ya kuhakikisha wanafunzi wameanza kufundishwa. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Nishati Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 121

**Mkoa wa Mtwara Kuunganishwa kwenye Gridi ya Taifa**

**MHE. AGNES E. HOKORORO** aliuliza:-

Je, lini Mkoa wa Mtwara utaunganishwa kwenye Gridi ya Taifa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Judith Kapinga majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mtwara utaunganishwa kwenye Gridi ya Taifa mwezi Septemba, 2026 mara baada ya kukamilika kwa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Songea hadi Mahumbika kupitia Tunduru na Masasi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza, umeme umekuwa ukikatika sana katika Mkoa wa Mtwara na Wilaya zake zote, wakati mwingine inakuwa kama vile kuna mtoto anachezea. Je, ni nini kauli ya Serikali kuhusiana na kukatika huku kwa umeme kunakosababisha wajasiriamali wanaotumia umeme kushindwa kuendelea na shughuli za kiuchumi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa huko nyuma tulipewa mkakati wa muda mfupi ikiwepo kufunga *anti-closure,* lakini imeonekana hazijasaidia. Je, nini hatua ya dharura itakayosababisha changamoto hiyo kwisha kabla ya kuunganishwa kwenye Gridi ya Taifa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa maswali ya Mheshimiwa Mbunge na naomba niyajibu kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa maelekezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu tulifanya hatua za muda mfupi kwa ajili ya kuboresha umeme katika Mkoa wa Mtwara, vilevile katika Mkoa wa Lindi. Katika hatua zile za muda mfupi tuliweza kusimika mashine kubwa zaidi ya kuzalisha umeme wa megawati 20, vilevile tulifanya ujenzi wa njia ya kusambaza umeme msongo wa kilovoti 33 kutoka Nanganga hadi Masasi kwa ajili ya kuimarisha umeme katika Wilaya za Newala pamoja na Masasi.

Mheshimiwa Spika, hatua hizo zilisaidia kwa kiasi chake, kwa sasa hivi tunao mkakati wa kuendelea kufanya marekebisho

makubwa katika laini zetu za umeme na kuendelea kubadilisha nguzo katika maeneo ambayo yanakuwa yana majimaji kuweka nguzo za zege pamoja na kupunguza urefu wa laini ili maeneo ya wilaya nyingine pia yaendelee kupata umeme ambao umeimarika zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumechukua hatua za muda kwa kipindi cha tarehe 23 mpaka 25 katika Mkoa wa Lindi pia tutafanya vilevile katika Mkoa wa Mtwara kwa ajili ya kuendelea kuimarisha hali ya umeme. Niwahakikishie wananchi wa Mkoa wa Mtwara tutaendelea kufanya marekebisho na matengenezo ili hali ya umeme iendelee kuimarika. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi. Sababu inayofanya umeme uache kutulia Wilaya ya Liwale ni kukosekana kwa *substation,* umeme kutoka Maumbika mpaka Liwale umbali ni mrefu sana hatuna *substation* pale kati jambo ambalo linaathiri sana utulivu wa umeme. Je, lini Serikali inafikiria kutujengea *substation* katika njia hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, Serikali tunatekeleza mradi wa kuimarisha nguvu ya umeme mradi unaojulikana kama gridi imara na utekelezeka kwa hatua mbalimbali. Kwa sasa tumeshafikia zaidi ya 40% kwa hatua ya kwanza, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge *substation* na yenyewe ipo katika mpango kadri tunavyoendelea kutekeleza kwa hatua na wenyewe vilevile watafikiwa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahya Mhata swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, ili kuunganishwa na Gridi ya Taifa wananchi wa Jimbo langu la Nanyumbu wameachia maeneo yao ili kupisha mradi huo, sasa ni mwaka wa pili hawajalipwa fidia. Ni lini watalipwa fidia? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli mradi wa kuunganisha gridi kwenye Mkoa wa Mtwara kutokea Songea - Tunduru – Masasi – Maumbika kuna wananchi wameachia maeneo yao kutoka eneo la Tunduru – Namtumbo – Masasi - Maumbika hadi kwenye jimbo la Mheshimiwa Mbunge. Tumewaelekeza *TANESCO* kwa maelekezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu wachukue fedha za ndani waanze kulipa fidia na zoezi hilo litaanza hivi karibuni. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, Miongoni mwa hatua ambazo zilipendekezwa hapo awali ili kutatua changamoto za kukatika kwa umeme katika maeneo ya Nanyamba, Tandahimba na Newala ni kuibadilisha laini ile na kujenga nguzo za zege. Je, Wizara ina mpango gani wa kukamilisha mradi huo? Ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tunao mkakati wa mradi huo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutafanya. Kwa sasa hivi tumeweka nguvu kubwa katika kuendeleza mradi huu wa kufikisha gridi katika Mikoa ya Mtwara na Lindi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na itatekelezeka. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sebastian Kapufi, swali la nyongeza.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Spika, mara ya mwisho mwezi Desemba mwaka 2024, tuliambiwa Gridi ya Taifa ingefika Mkoani Katavi, sasa ni miezi minne imepita. Je, ni lini Gridi ya Taifa itafika Katavi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, Mradi wa kupeleka umeme wa gridi katika Mkoa wa Katavi umeshafikia zaidi ya 95%. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ndani ya kipindi kifupi tutakamilisha mradi huu na Mkoa wa Katavi na wenyewe utakuwa umeunganishwa katika Gridi ya Taifa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Fedha Mheshimiwa Constantine John Kanyasu Mbunge wa Geita Mjini, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Ighondo Ramadhani.

Na. 122

**Makampuni Kutojiorodhesha *Dar es Salaam Stock Exchange***

**MHE. ABEID R. IGHONDO K.n.y. MHE. CONSTANTINE J. KANYASU** aliuliza:-

Je, nini hasara na faida kwa kampuni kutotekeleza Sheria ya kujiorodhesha kwenye *Dar es Salaam Stock Exchange*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria ni makampuni ya simu pekee ndio hulazimika kuuza hisa kwa umma na kuorodheshwa katika soko la hisa isipokuwa yale makampuni ambayo Serikali ina umiliki wa hisa kwa 25% au zaidi na makampuni ambayo yanatoa huduma ya minara ya simu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kampuni kujiorodhesha kwenye soko la hisa kuna faida lukuki ikiwa ni pamoja na: kuongeza mtaji, kuongeza ufanisi na tija, kuiwezesha Serikali kupata mapato stahiki, kutambua thamani halisi ya hisa zake ambapo wanahisa watapata thamani ya hisa zao wanapotaka

kuuza kwa kufuata mwenendo wa soko yaani *demand and supply*, kuwapa wananchi fursa ya kununua hisa na hivyo kuwezeshwa kushiriki katika uchumi wa nchi. Aidha, soko la hisa pia hutoa fursa kwa wawekezaji wanaotaka kuuza uwekezaji wao kipindi wanapohitaji fedha.

Mheshimiwa Spika, wanahisa wa kampuni ambayo haijaorodheshwa katika soko la hisa hukutana na changamoto za kutofahamu thamani halisi ya uwekezaji walioufanya kutokana na kukosekana kwa ukwasi wa hisa zao. Kampuni hizi hutawaliwa na kukosekana kwa uwazi na hivyo Serikali na wanahisa kushindwa kupata taarifa stahiki za mwenendo wa biashara na fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ighondo Ramadhani, swali la nyongeza.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu haya mazuri ya Serikali ninayo maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kampuni za madini mathalani *Geita Gold Mine (GGM), Barrick* pamoja *Shanta mine,* zinaaminika kuwepo katika masoko ya hisa ya nje. Kama tulipitisha sheria hapa kwamba Serikali inapaswa kuwa na 16% ya *share as free carried interest*. Ni lini Serikali itasema ni lazima kampuni hizi kuwepo katika *Dar es Salaam Stock Exchange Market*?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Soko la Hisa linatoa taswira ya Kampuni zinazofanya vizuri kwa namna ya watu wanavyonunua na kuuza. Je, Serikali sasa haioni haja ya kubadili sheria ili iwe ni lazima kwa kampuni zote kubwa kujiunga? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Abeid kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba uridhie nijibu maswali yote mawili kwa pamoja kwa sababu yote yanahusu mabadiliko ya sheria. Tumepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, tunaenda kuufanyia kazi na wadau wa sheria tunawajua likiwa ni pamoja na Bunge lako Tukufu. Kwa hiyo, tukiona kwamba jambo hili litakuwa na tija kwenye kubadilisha sheria hiyo basi Serikali haitosita kulifanyia kazi na kuleta hapa katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 123

**_SIDO_ Kuwakopesha Vifungashio Wajasiriamali**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA** aliuliza:-

Je, *SIDO* ina mpango gani kukopesha Wajasiriamali vifungashio kama ambavyo benki zinavyokopesha fedha ili kuongeza ubora wa bidhaa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exaud Kigahe majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** ajliibu:-

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Serikali kupitia *SIDO* huwarahisishia Wajasiriamali kupata vifungashio kwa kununua kwa jumla *(bulk procurement)* na Wajasiriamali kuweza kupata vifungashio hivyo katika ofisi za *SIDO* mikoani kwa kuuziwa rejareja na kwa bei nafuu. Utaratibu huo umewawezesha Wajasiriamali kupata vifungashio kwa wakati na kwa kutumia mikopo ya *NEDF* inayotolewa na *SIDO*.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa upatikanaji wa vifungashio kwa wajasiriamali, Serikali imeendelea kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vya vifungashio hapa nchini ili kurahisisha upatikanaji wake na kwa bei nafuu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ntara, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi vijana wengi sana hasa waliomaliza vyuo wamejishikiza katika ajira ya ujasiriamali na wanahitaji vifungashio. Swali la kwanza; je, *SIDO* imefanya tathmini ya changamoto zinazowakabili wajasiriamali wadogo na hasa hao vijana waliotoka vyuo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, *SIDO* haioni haja ya kuwa na utaratibu wa kushirikiana na taasisi za kifedha ili wanufaika wa mafunzo hasa vijana waweze kupata mitaji ya kuanzisha au kupanua shughuli zao za kiuchumi? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana na kumshukuru Mheshimiwa Ntara kwa weledi na ushauri wake na huyu ni daktari msomi maana yake amesema kwamba vijana wajasiriamali wengi wana changamoto ya mtaji.

Mheshimiwa Spika, *SIDO* moja ya kazi zake ni kufanya au kuendeleza teknolojia mbalimbali za viwanda, lakini pia wanatoa mafunzo na uendelezaji wa biashara. Zaidi, wanafanya kutafuta masoko na uwekezaji na zaidi ni hii ambayo Mheshimiwa Mbunge amesema kuhusiana na mikopo ya kifedha kwa vijana na wajasiriamali wengine.

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue ushauri wake kwamba *SIDO* sasa tuna nafasi ya ziada ya kufanya tathmini ya kina ili kuhakikisha tunaona changamoto zilizopo kwa vijana na hasa kwenye sehemu hii mahususi ya vifungashio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la pili, tayari Serikali kupitia *SIDO* inashirikiana na baadhi ya taasisi za kifedha kupitia mifumo hasa hivi viwanda ambao unasaidia, lakini mahususi unakwenda kwenye viwanda vikubwa au vya kati ambavyo wajasiriamali wengi hawana uwezo huo wa kukopa zaidi ya shilingi milioni tano na kuendelea. Kwa hiyo nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwamba tunachukua ushauri wake, lakini zaidi tutaendelea kuboresha kwa kuhamasisha ujenzi wa viwanda zaidi hapa nchini vya vifungashio, ambalo ndiyo tatizo kubwa katika nchi yetu kwa bidhaa ambazo ni nzuri zinazozalishwa. Kwa sababu bidhaa inaweza kuwa nzuri lakini ukifungasha kwenye kifungashio ambacho hakivutii au hakina ubora maana yake hata thamani ya bidhaa hiyo inakuwa ni ndogo. Ninakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maji, Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, Mbunge wa Igunga sasa aulize swali lake.

Haya sasa ngoja nielewe jambo moja. Mheshimiwa Almas Maige umesimama kwenye hili swali 124, lakini 128 nimepewa pia taarifa na Mheshimiwa Rehema Migilla kwamba yeye ndiye amepewa kuuliza. Sasa 128 ni wewe una majibu au Mheshimiwa Rehema?

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, 128 pia majibu ninayo mimi.

**SPIKA:** Mheshimiwa hebu rudia.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, 128 majibu ya Mheshimiwa Mwakasaka ninayo mimi.

**SPIKA:** Unayo wewe?

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Basi keti, utauliza 128. Mheshimiwa Sanga, kuna wenzio waliowahi kusimama, Mheshimiwa Ritta Kabati.

Na. 124

**Mradi wa Maji Ziwa Victoria kwenda Kata za Igunga**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI K.n.y. MHE. NICHOLAUS G. NGASSA** aliuliza:-

Je, lini Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria kwenda Kata za Mwamashiga, Mbutu, Isakamaliwa, Kining'inila Mwamakona, Igurubi na Kinungu utakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa *Engineer* Kundo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na upanuzi wa Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria kutoka Kijiji cha Igogo kwenda Igurubi Wilayani Igunga Mkoa wa Tabora. Kazi zinazotekelezwa kupitia mradi huo ni pamoja na ujenzi wa tanki moja (1) lenye ujazo wa lita 1,000,000, uchimbaji wa mitaro na ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 150 sanjari na ujenzi wa vituo 57 vya kuchotea maji.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa 60% na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2025 na kunufaisha wananchi 71,726 waishio kwenye vijiji 18 vilivyopo katika Kata saba (7) za Mwamashiga, Mbutu, Isakamaliwa, Kining'ila, Mwamakona, Igurubi pamoja na Kinungu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, katika mradi huo utajengwa na matenki kwa ajili ya kuhifadhia maji kwa sababu imekuwa ni

changamoto kubwa sana kwani vijiji vingi vinakuwa vinajengewa miradi, lakini watu wanapata shida kwenda kuyafuata?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; Mradi wa Maji wa Kijiji cha Mkalanga, Wilaya ya Kilolo lini utakamilika kwa sababu wananchi wamepata shida sana na wameusubiri kwa muda mrefu sana? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la kwanza la nyongeza. Kama nilivyojibu katika jibu la msingi, Serikali imekamilisha ujenzi wa tenki la lita 1,000,000. Pia, tunaendelea kulaza mabomba umbali wa kilometa 150. Tumeangalia pia vijiji vya Mwamharanga pamoja na Bukama vyenyewe viunganishiwe maji wakati mradi ukiwa unaendelea kutekelezwa kwani wenyewe una *existing infrastructure* ambazo wanaweza kuendelea kupata huduma ya maji bila kuwa na tatizo lolote.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; upande wa Mkalanga, mradi huu unagharimu takribani shilingi milioni 391 ambapo mradi huu umefikia 95% na tunatarajia ufikapo mwezi Mei, mradi huu utakamilika. Nimuahidi Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati tutaenda nae mpaka Kilolo kuuzindua mradi huu ili wananchi wa eneo hilo waweze kupata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mliosimama nimewaona, maswali kwa kifupi. Mheshimiwa Zacharia Issaay swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wakandarasi wengi nchini wameshindwa kuomba Miradi ya Maji mara baada tunapotangaza mfano wake uko katika Jimbo la Mbulu Mjini, tumetangaza visima viwili lakini hakuna mkandarasi aliyeomba kwa mara mbili na pengine nchi nzima; je, utaratibu ukoje sasa kwa pale ambapo Wizara imetangaza ama Serikali mara mbili, lakini hakuna aliyejitokeza? Ninakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kama nimelisikia vizuri swali lake. Tumekuwa na changamoto nchi nzima katika baadhi ya maeneo ambapo uchimbaji wa visima inategemea pia na aina ya vifaa mkandarasi anavyokuwanavyo. Kuna maeneo mengine kwa mfano Mkoa wa Singida tulipata changamoto katika Mradi wa Miji 28. Katika mradi huo wakandarasi wengi walikuja walijaribu kuchimba, lakini mashine zao zilishindwa kumudu hali halisi ya eneo husika na baadaye tukatangaza tena ili kupata ambae ataweza kuwa na vifaa kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, kesi kama hiyo imeendelea kutokea katika maeneo mbalimbali, lakini Serikali imeendelea kuhakikisha kwamba inafanya utafiti wa kina kuona namna gani wakandarasi watashauriwa wanapoomba kazi hizi waangalie namna ambayo itaendana na eneo husika ili waweze kutimiza mahitaji ya kandarasi hiyo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itatekeleza miradi ya maji iliyoahidiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka 2021 katika Vitongoji vya Nasaya na Masaninga? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ahadi za viongozi wa kitaifa akiwemo Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais pamoja na Waziri Mkuu na Naibu Waziri Mkuu, sisi Wizara ya Maji tunachukua kwa uzito kabisa. Pale ambapo fedha zinapatikana, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge suala lake tutalifanyia kazi kwa uzito stahiki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Minza Mjika, swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ziwa Victoria kwenda Mkoa wa Simiyu unasuasua sana. Ninataka kujua, ni lini mradi huu utakwisha ili wakazi wa Mkoa wa Simiyu wanufaike na maji? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Minza Mjika kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ziwa Victoria ni ndoto ya Wanasimiyu na ni ndoto ya Wabunge wote wa Mkoa wa Simiyu ambao wameendelea kuupambania sana. Mheshimiwa Rais aliridhia kutoa shilingi bilioni 440 kwa jili ya ujenzi wa mradi huu ambapo awamu ya kwanza tayari umeshaanza kutoka Nyashimo – Bariadi kwenda Itilima.

Mheshimiwa Spika, tumeshatangaza pia kandarasi ya pili kwa ajili ya mradi huu wa *extension* yake kupita Maswa mpaka Meatu. Nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, Mradi huu kwa Sekta ya Maji na Wizara ya Maji, sisi tunauchukulia kwa uzito kwa sababu una maslahi mapana kwa sababu unaenda kuhudumia wakazi takribani laki saba wanaokaa katika Mkoa wa Simiyu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, Serikali imechimba Mradi wa Maji wa Qaloda pale Dongobesh na Mradi wa Maji wa Getesh pale Tumati, imebaki tu kuleta fedha za mabomba ili kumaliziwa mradi ule. Je, lini mnaleta fedha za mabomba ili mradi ukamilike?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Maji, Jumaa Hamidu Aweso alitoa maelekezo kwa Mameneja wetu wa Mikoa kuhakikisha kwamba tunapomaliza kuchimba visima cha kwanza ni kuhakikisha tunatengeneza *point source* wananchi waanze kupata huduma ya maji safi salama, lakini tukiwa tunatafuta fedha za kupanua mtandao ili wananchi walioko mbali na eneo la *point source* waweze kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, maelekezo ya Mheshimiwa Waziri tayari Katibu Mkuu ameshaanza kufanya mchakato wa kupeleka fedha ili bomba hizo ziweze kutandazwa na wananchi wa Mheshimiwa Flatei waweze kufurahia uwepo wa maji katika maeneo hayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Je, ni lini Mradi wa Maji kutoka Milima ya Nongwe katika Halmashauri ya Wilaya ya Gairo utakamilika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, mradi huo ninafahamu kwamba uko katika hatua nzuri kabisa ya utekelezaji wake, lakini pia tunafahamu kwamba uko ndani ya mkataba kulingana na utekelezaji ambao tumeingia na mkandarasi. Kwa hiyo, ninaamini kabisa kwamba utakamilika ndani ya mkataba ambao tumesaini na mkandarasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, ahadi za viongozi zimekuwa zikipewa kipaumbele katika utekelezaji wa miradi na Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa ahadi toka mwaka 2017 ya kuchimba kisima kirefu katika Kata ya Kalulu, leo hii takribani miaka nane ahadi ile haijatekelezwa. Ninataka kufahamu; je, ni lini hasa kile kisima kitakwenda kuchimbwa na kutekeleza ahadi ya Waziri Mkuu? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana lakini pia ninashukuru sana swali la Mheshimiwa Hassan na kwa kazi nzuri sana anayoifanya kwa wananchi wake. Ninatambua kwamba ahadi hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya mwaka 2017 kwa upekee kabisa na kwa heshima na unyenyekevu ninaomba niipokee ili twende tukaifanyie kazi. Pia, nimwombe Mheshimiwa Mbunge tushirikiane ili tuone tunatatua kwa namna gani ili waweze kupata huduma ya maji safi na salama yanayotokana na kisima hicho. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo sasa aulize swali lake. (Makofi)

Na. 125

**Kusafisha na Kuweka Uzio Uwanja wa Ndege Urambo**

**MHE. MARGARET S. SITTA** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kusafisha na kuweka uzio Uwanja wa Ndege Urambo kwa kuwa ni muhimu kwa Biashara ya Tumbaku na ni Uwanja wa dharura?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa David Kihenzile majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana na pendekezo la ujenzi wa uzio ili kuimarisha usalama katika Kiwanja cha Ndege Urambo na tayari suala hili limejumuishwa katika Rasimu ya Mpangomkakati wa *TAA* wa miaka mitano ijayo ili kutoa wigo wa matumizi ya rasimalifedha inayotengwa katika bajeti ya miradi ya maendeleo kwa ajili ya kukamilisha miradi mbalimbali ya ukarabati na upanuzi wa viwanja vya Ndege ikiwemo Ujenzi wa

Jengo Jipya la Abiria katika Kiwanja cha ndege cha Tabora ambalo ujenzi wake umefikia 94.1%.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na uhakikishaji wa Kiwanja cha Ndege cha Urambo kipo salama, *TAA* inaendelea na utekelezaji wa maagizo ya kitaifa kuhusiana na ulinzi na usalama, ikiwemo na ushirikishwaji wa wananchi ili kulinda mipaka kupitia uhamasishaji wa ulinzi shirikishi. Hali kadhalika, kiwanja hiki kina hati miliki ili kuepuka uvamizi wa ardhi unaoweza kufanyika kutokana na idadi ndogo ya shughuli za kiuendeshaji zinazofanyika kiwanjani hapo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize maswali. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu swali nililouliza bado narudi kwa Serikali kuiuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kutokana na kwamba Uwanja wa Ndege wa Urambo upo katikati ya Mji na umuhimu wake kwa ajili ya dharura ya ndege kutua pale na kadhalika, kweli Serikali yetu ilivyo makini inaweza kushindwa kuweka uzio ili kuutunza uwanja wenyewe lakini pia kwa ajili ya usalama wa wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, kwa jinsi ilivyo makini Wizara ya Uchukuzi, kweli imeshindwa kuweka watu wa kufanya usafi ili na sisi mji wetu upendeze? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kupitia Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Mbarawa nimpongeze sana Mheshimiwa Mama yetu Sitta kwa ufuatiliaji mkubwa anaoufanya wa shughuli za maendeleo katika eneo lake na pia, kwa kutambua kwamba Serikali hii ni makini. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Mama yetu Sitta kwamba Serikali kama nilivyosema ni makini na inao mpango huo, lakini atupe muda tu kama nilivyokuwa nimeeleza kwenye jibu la msingi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na jambo la pili la usafi. Ninamwelekeza Mkurugenzi wa Viwanja vya Ndege kupitia timu yake waende kwenye eneo hilo na waendeleze programu ya kufanya usafi ili uwanja huo uweze kuwa msafi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Mtenga, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Spika, Mtwara ni Mji ambao unakua na tukilinganisha tupo mpakani mwa Msumbiji na Comoro. Ni lini Serikali itatujengea meli kwa jili ya kuendelea na suala letu la kibiashara Mtwara - Comoro na Mtwara – Mozambique. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, sijamsikia vizuri, anazungumzia meli siyo?

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Spika, ninazungumzia meli.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, *okay*. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mtenga anavyofuatilia maendeleo katika Jimbo lake. Serikali inajenga meli mbalimbali katika Maziwa Makuu na hivi mwezi uliopita imekamilisha mpango wa kumkabidhi msanifu. Tumeshaanza usanifu wa kina na upembuzi yakinifu kwenye Bahari ya Hindi ili tuanze kujenga meli ambayo itakuwa inafanya shughuli zake kwenye Mwambao wa Bahari Hindi ikiwemo Mtwara, Lindi, Tanga, Zanzibar na maeneo mengine yote ambayo yanapakana na Bahari hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Priscus Tarimo, swali la nyongeza.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana. Ni lini Serikali itakamilisha ukarabati wa Uwanja wa Ndege wa Moshi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nimshukuru Mheshimiwa Tarimo kwa ufatiliaji na yeye ni shahidi tulikuwa wote kutembelea uwanja huo hivi majuzi kwenye eneo hilo. Tunaendelea na taratibu mbalimbali za ndani ili kuweza kumlipa Mkandarasi aweze kuendelea na hatimaye akamilishe ujenzi wa uwanja huo wa Moshi ambao ni muhimu sana kwa maslahi ya nchi yetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, Uwanja wa Ndege wa Iringa umewekewa uzio na una usalama wa kutosha, lakini ndani ya ule uwanja kuna Shule ya Msingi inayotumika. Je, watatusaidiaje ili kuondoa watoto mle ndani kwa sababu ndege kubwa zimeanza kushuka pale?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge wa Iringa Mjini kwa ufuatiliaji wake makini wa Uwanja wetu wa Iringa. Ninataka nimhakikishie kwamba taratibu mbalimbali zinaendelea kufanyika ili kuhakikisha jambo hilo linafanyika kwa kuzingatia sheria na taratibu za nchi yetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mifugo na uvuvi, Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso.

Na. 126

**Mabwawa ya Samaki Kalemawe - Same Kukabidhiwa kwa Wananchi**

**MHE. CECILIA D. PARESSO K.n.y. MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA** aliuliza:-

Je, kwa nini Mabwawa ya Samaki yaliyopo Kata ya Kalemawe – Same yasikabidhiwe kwa wananchi wa Kata hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mradi wa Mabwawa ya Samaki yaliyopo Kata ya Kalemawe yapo chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Same. Aidha, Wizara itashirikiana na Halmashauri ya Same ili kuona namna bora ya usimamizi wa matumizi ya mabwawa hayo, ili ikiwezekana yakabidhiwe kwa wananchi wa Kata ya Kalemawe ili yaweze kuwanufaisha kiuchumi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ninaomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa, Serikali imekiri kwamba mabwawa hayo yapo chini ya halmashauri na tunaelewa uwezo wa halmashauri zetu kimapato wakati mwingine ni madogo na hayakidhi mahitaji. Je, Serikali haioni umuhimu sasa kupitia Miradi ya *BBT* kuziwezesha Kata husika ili ziweze kuendeleza mabwawa haya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ukiacha kwamba samaki ni biashara lakini ni chakula muhimu kwa afya na wananchi wengi pia wanaona kwamba, kufuga samaki kupitia mabwawa madogo madogo ni gharama kubwa, lakini pia wanashindwa kutumia fursa zilizopo katika maeneo yao. Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba, inatoa elimu na mitaji kwa wale wananchi ambao wana utayari ili na wao waweze kufuga samaki hao kuliko kutegemea tu samaki walioko katika mabwawa na maziwa makubwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Moja, ni kwamba Wizara tumeshakubali kwamba tutashirikiana na halmashauri ili tuone

namna bora ambapo yale mabwawa yatakabidhiwa kwa wananchi. Unapotaka kukabidhi mabwawa yale kwa wananchi maana yake ni lazima Wizara tuwawezeshe wananchi wale ili waweze kuwa na uwezo wa kuyaendesha yale mabwawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuna Mradi wa *BBT Life* kwa maana ya *livestock and fisheries* ambao unatekelezwa katika maeneo mbalimbali nchini. Kwa hiyo, jambo lako tumelipokea na tutaliweka katika huo mpango. Ahsante.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mkakati ni kwamba hilo lipo la kuendelea kuelimisha wananchi ili waweze kuchimba mabwawa na kuwapatia mitaji, ndiyo maana imehimizwa sasa hivi watu wengi waweze kufanya ufugaji wa samaki kupitia haya mabwawa. Kwa hiyo, hilo jambo lipo na linafanyiwa kazi. Kwa hiyo, kikubwa sisi tutaaongeza msukumo tu kuwafikia wananchi. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nashon Bidyanguze, swali la nyongeza.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kuiuliza Serikali ni lini itapeleka vifaranga kwa ajili ya wale ambao wamekwishapewa vizimba katika Ziwa Tanganyika? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli anachokisema Mheshimiwa Mbunge Bidyanguze. Moja kati ya mkakati wa Serikali ni kuhakikisha wananchi wengi hususan katika maeneo ambayo wana maziwa kwa maana ya *Lake* Victoria, Tanganyika na Nyasa wanaingia katika ufugaji wa samaki kupitia vizimba.

Mheshimiwa Spika, moja ya wajibu wetu ni kuendelea kuzalisha vifaranga vingi kuwawezesha wavuvi ili waweze kufuga

kisasa, hivyo jambo hili lipo na nikitoka hapa nitazungumza na Katibu Mkuu nione wamefikia wapi katika uzalishaji wa vifaranga ambavyo vitawawezesha kuwafikia wavuvi wote. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Angeline Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ufugaji wa samaki kwa njia ya mabwawa pamoja na vizimba unaonekana una tija kubwa. Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba vijana wanojitokeza kuomba mikopo kwa ajili ya ufugaji wa vizimba wanapata mikopo hiyo? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ni kweli anachokisema Mheshimiwa Mbunge moja ya mkakati wa Serikali ni kuingia katika ufugaji wa samaki kupitia vizimba. Sasa hivi msisitizo umekuwa mkubwa sana. Moja ya mkakati mkubwa katika kuwawezesha hawa watu ni kwamba, kupitia Rais alitoa maelekezo kwa benki zote nchini katika lile dirisha la kilimo ambalo linalisha kilimo, mifugo na uvuvi kupunguza riba kwa kiwango kikubwa. Vilevile, tuna fedha ambazo zipo katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa ajili ya kuwawezesha wafugaji. Kwa hiyo, vijana wajitokeze watimize hayo masharti na wapatiwe mikopo kwa ajili ya huo ufugaji wa samaki kupitia vizimba. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri sasa ninaona Wizara inayofuata ni ya kwako kwa hiyo maana yake ubaki hapo, lakini tunakushukuru kwa kwa majibu kwa niaba ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Sasa, Wizara ya Kilimo Mheshimiwa Aloyce John Kamamba Mbunge wa Buyungu swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix.

Na. 127

**Mkakati wa Kuimarisha Kilimo cha Alizeti – Kakonko**

**MHE. KAVEJURU E. FELIX K.n.y. MHE. ALOYCE J. KAMAMBA** aliuliza:-

Je, nini mkakati wa Serikali wa kuimarisha kilimo cha alizeti katika Wilaya ya Kakonko?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kakonko ni miongoni mwa maeneo yanayofaa kwa kilimo cha zao la alizeti. Katika kuimarisha kilimo cha alizeti Wilayani Kakonko, mkakati wa Serikali ni kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora, kuwapa vitendea kazi Maafisa Ugani ili waweze kuwafikia wakulima na kutoa ushauri wa kilimo bora cha alizeti.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mikakati hiyo, katika msimu wa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Halmashauri ya Kakonko imeanzisha mashamba manne ya mbegu katika Kata za Kiziguzigu na Rulenge. Pia, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imetoa pikipiki 13 na kifaa cha kupima afya ya udongo *(soil scanner)* kwa Maafisa Ugani. Kifaa hicho kitawezesha kushauri wakulima matumizi sahihi ya mbolea.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutekeleza mikakati hiyo na uzalishaji kuongezeka, Serikali itaendelea kuhamasisha wawekezaji kuanzisha viwanda vya kuzalisha mafuta ya kula. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kavejuru, swali la nyongeza.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Serikali imekiri kuwa Kakonko ni eneo zuri

kwa kilimo cha alizeti na nchi yetu bado ina uhitaji mkubwa wa mafuta ya kula. Je, Serikali ipo tayari kugawa bure mbegu bora za alizeti kwa wakulima katika Wilaya ya Kakonko? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; pamoja na umuhimu wa zao la alizeti bado wakulima hawana ufahamu wa kutosha. Je, Serikali imejipangaje kutoa elimu ya kilimo cha alizeti kwa wakulima hapa nchini? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli matarajio ya wananchi wengi ambayo Mheshimiwa Mbunge ameeleza ni pamoja na kutoa mbegu bure, lakini mkakati wa Serikali tulionao sasa hivi tumeweka ruzuku katika mbegu ili kupunguza gharama kwa wananchi kwa maana ya wakulima. Kwa hiyo, hatua ya sasa tumeongeza ruzuku, ninafikiri kadiri uwezo utakavyoongezeka wazo lake Serikali tutalifikiria kwa baadaye.

Mheshimiwa Spika, pia, kuhusu kuongeza elimu zao la alizeti katika Wilaya ya Kakonko jambo hilo tumelipokea. Tutawatuma Maafisa Ugani wetu waweze kuwafikia wananchi kwa kutoa elimu, ili wananchi hao waweze kuingia katika kilimo cha alizeti. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nimewaona. Maswali kwa kifupi. Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi. Je, ni upi mkakati wa Serikali kugawa mbegu za alizeti, ufuta pamoja na mpunga kwenye Kata ya Ivuna ambao walipata maafa na mazao yao yakaharibiwa ili kuwapooza? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa hapo mwishoni ili kuwapooza?

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, ili kuwatoa machungu ya kuharibikiwa na mazao yao?

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nimwondoe shaka tu Mbunge wa Jimbo la Momba Mheshimiwa Condester kwamba, moja ya mkakati wetu Serikali maeneo yakiwa na maafa yanapotokea, kama mafuriko na wananchi kuondokewa na mazao yao, mkakati ambao tumekuwa tukiufanya ni pamoja na kutoa mbegu. Kwa hiyo, tuandikieni hayo mahitaji nasi tutaleta mbegu bure kwa ajili ya kusaidia hao wananchi ambao wamepatwa na maafa hayo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mkakati gani wa kutekeleza falsafa ya *BBT* kwenye Majimbo ambayo hayana maeneo makubwa ya kilimo kama Vunjo? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba mkakati ambao tupo nao sasa hivi ni kuhakikisha kwamba, mradi wa *BBT* unakwenda katika majimbo yote nchini. Kwa hiyo, jambo hili lipo na tumesha-*identify* karibu maeneo mengine yote na tulishaziomba halmashauri kutuletea maeneo kulingana na ukubwa wake. Kwa hiyo, lipo katika utekelezaji na tunapotekeleza haina maana kwamba tutatekeleza katika maeneo makubwa kama ambavyo tunayo hapa Chinangali, Ndogoye na maeneo mengine. Kwa hiyo, hata katika maneeo ambayo ni madogo bado tutatekeleza mradi huo ikiwemo katika Jimbo la Vunjo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Mkoa wa Iringa ni miongoni mwa mikoa ambayo pia inalima alizeti, lakini kunakuwa na changamoto ya wakulima kupata mbegu bora na viuatilifu. Je, ni nini mkakati wa

Serikali kuhakikisha wanapata mbegu bora na viuatilifu hasa Jimbo la Kalenga? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, mkakati tulionao sasa hivi moja, tunaongeza uzalishaji kwa kuingia makubaliano na wakulima, kwa maana ile tunaita *contract farming* ili waweze kuzalisha mbegu ya alizeti. Vilevile, tumeruhusu uagizaji wa mbegu bora za alizeti kutoka nje kuingia ndani ya nchi, lakini mbegu hizo zote zitaingia katika mpango wa ruzuku ambao tunaufanya katika mbegu za alizeti na mahindi. Kwa hiyo, niseme tu kwamba sisi tutaongeza hiyo kasi ili tuweze kuwafikia wananchi wa Mkoa wa Iringa na Jimbo la Kalenga. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aysharose Mattembe, swali la nyongeza.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi. Kwa kuwa, Singida ni kinara wa kilimo cha alizeti nchini. Je, Serikali ina mpango gani wa kusambaza pembejeo bora na kuwapatia mafunzo wakulima wake ili kuongeza tija katika kilimo hicho? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli katika zao la alizeti Mkoa wa Singida ni miongoni mwa mikoa ambayo Wizara ya Kilimo tunaitegemea, ndiyo mkoa ambao hata kazi kubwa ambayo tumekuwa tukiifanya ikiwemo kupeleka aina mbalimbali za mbegu za alizeti katika Mkoa huo kama vile *OPV* na zile mbegu za *Hybrid,* kwa hiyo, hayo yamekuwa yakifanyika.

Mheshimiwa Spika, ninamwondoa shaka Wizara tutaendelea kuleta mbegu bora katika Mkoa wa Singida na vilevile tutaendelea kutoa elimu kupitia Maafisa Ugani wetu ili kuhakikisha kwamba, alizeti inaendelea kuzalishwa kwa wingi ili tuweze kuondoa hii adha ya uhaba wa mafuta hapa nchini. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, mwaka juzi, mwaka jana na mwaka huu wananchi wa Mkoa wa Rukwa wamepata mbegu za alizeti zisizofaa. Ni mkakati gani wa Serikali ambao wameufanya wa kufanya tafiti za kina kugundua mbegu hizo zisizofaa na zisirudi tena kwa wakati mwingine kuwatia hasara wananchi? Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba, mbegu kabla hatujaipeleka kwa wananchi huwa tunaichunguza kupitia taasisi yetu ya utafiti ya *TARI* na vilevile *TOSCI* kwa ajili ya kuithibitisha ubora wake na *ASA* wanalo jukumu la kusambaza mbegu hizo ambazo zimeshathibitishwa. Kwa hiyo, kama kuna makosa inawezekana yalitokea kutokana na mbegu ambazo wananchi walichukua katika maeneo mengine na ikaonekana sisi ndani tumesambaza.

Mheshimiwa Spika, jambo hilo tutalipitia na kuliangalia. Vilevile, tutachukua hatua thabiti kwa ajili ya kuhakikisha mbegu zisizofaa haziwafikii wakulima. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Almas Maige.

Na. 128

**Malipo ya Madeni ya Wazabuni wa Jeshi la Polisi na Magereza**

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE K.n.y. MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA** aliuliza:-

Je, upi mpango wa Serikali wa kulipa madeni ya wazabuni hasa ya Polisi na Magereza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua madeni wanayodai wazabuni mbalimbali wanaotoa huduma, ambapo kwa Jeshi la Polisi kiasi cha fedha shilingi 651,730,893,477.29 kinadaiwa na katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imelipa kiasi cha fedha shilingi 3,188,596,251.62. Aidha, deni la wazabuni katika Jeshi la Magereza ni jumla ya shilingi 33,527,055,286.00/= na kiasi cha fedha shilingi 15,072,994,270.00 kimefanyiwa uhakiki na Hazina na kinachosubiriwa ni malipo kutoka Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kulipa madeni hayo kwa kadri ya upatikanaji wa fedha toka kwenye bajeti ya Serikali inayotengwa kila mwaka wa fedha. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Almas Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wazabuni ambao mali zao zinauzwa na benki na wanafilisika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kuna juhudi gani mahsusi za kulipa madeni haya makubwa ambayo wazabuni wanaidai Serikali? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Almas Maige, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika swali la kwanza namna ya kuwasaidia wazabuni. Ni kweli tunatambua kwamba wazabuni wanafanya kazi kubwa ya kutoa huduma katika taasisi mbalimbali za Serikali mbalimbali ikiwepo Majeshi yetu ya Polisi na Magereza. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itaongeza kasi ya uhakiki wa madeni haya ili kuweza kulipa kwa wakati na kuepukana na adha ya kuuziwa bidhaa zao na benki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, juhudi za Serikali kama nilivyosema ni kuongeza kasi ya uhakiki wa madeni ili kuwalipa kwa wakati na kuondokana na adha hii kama nilivyosema kwenye jibu la msingi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Rehema Migilla, swali la nyongeza.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, Kata ya Uyowa na Kata ya Kona Nne hazina vituo vya polisi, hivyo shughuli za kipolisi zinafanyika kwenye nyumba za kupanga. Hali hiyo imesababisha wapangishaji kulidai Jeshi la Polisi fedha nyingi sana. Je, upi mpango wa Serikali kuhakikisha inatujengea vituo vya polisi ili kuepukana na kulipa madeni makubwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rehema Migilla, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kujenga vituo vya polisi kwenye Kata zote hapa nchini pamoja na shehia kwa upande wa Zanzibar, vituo hivyo vitajengwa awamu kwa awamu. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge Kata zake alizozitaja pia zitaingizwa kwenye mpango na kutengewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya polisi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Askari wa Jeshi la Magereza wengine ni wastaafu na wengine bado wapo kazini wanadai madeni ambayo ni malimbikizo ya muda mrefu tangu 2010 ya safari za kikazi, uhamisho na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, ninataka kujua ni lini Serikali itahakikisha inawalipa Askari hawa madeni yao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Askari wetu wanaostaafu na wanaopata safari za kikazi wamekuwa wakilipwa madai yao na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hata hawa ambao anawasema baadaye tuwasiliane, kama kuna Askari ambao wanadai madeni tutawasiliana kwa ajili ya kuwatengea fedha kuwalipa stahiki zao. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri ni lini fedha za kukamilisha Kituo cha Polisi Nyegezi zitapelekwa, lakini nimegundua swali la msingi halihusiani na ujenzi wa vituo vya polisi. Ninakushukuru. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Stanslaus Mabula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli nilifika Kituo cha Polisi cha Nyegezi kule Mwanza na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tayari tumeshakichukua tumekiweka kwenye mpango tutakitengea fedha kwa ajili ya kumalizia kazi kubwa iliyofanywa

na wananchi wa Jimbo lake. Ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa iliyofanyika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, mbali ya kwamba Jeshi la Magereza na Polisi wanadaiwa na wazabuni, lakini pia Jeshi la Polisi Askari wake wamekuwa wakidai madeni mbalimbali ya uhamisho na wengine ambao wamestaafu bado hawajalipwa malipo ya mizigo na madeni mengine wakiwepo na Askari wa Bunda. Sasa, ni lini mtawalipa, maana tunao wajibu kwa kuwatetea hata kama wanatukamata na kutupiga virungu. Ninakushukuru. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli wapo baadhi ya Askari ambao wanadai fedha zao za uhamisho pamoja na mizigo kama ambavyo amesema. Serikali imekuwa ikitenga fedha kila mwaka na tumekuwa tukiendelea kuwalipa askari wetu kila mwaka kila mwaka. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hata hawa wanaodai pia bado tutawatengea fedha na watalipwa wakiwemo Askari wa Jimbo la Bunda, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Ng’wasi Damas Kamani, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 129

**Kuwasaidia Wahitimu Waliosoma Vyuo vya Jumuiya ya Afrika Mashariki**

**MHE. NG'WASI D. KAMANI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia Wahitimu waliosoma katika Vyuo vya Jumuiya ya Afrika Mashariki kupata usajili ili kuajiriwa nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, usajili wa wahitimu kutoka vyuo vya nje ya nchi ikiwa ni pamoja na Vyuo vya Jumuiya ya Afrika Mashariki hufanywa na Mamlaka za Usajili au Bodi za Kitaaluma *(Professional Bodies)*, kwa kuzingatia taratibu zilizopo. Kabla ya usajili mhitimu hutakiwa kupeleka vyeti vya taaluma Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania *(TCU)* na wale wa stashahada na cheti hupeleka vyeti Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na mafunzo ya ufundi stadi *(NACTVET)*, ili kufanya uthibitisho, ulinganifu wa sifa na kiwango cha elimu. Hivyo ninapenda kuwasihi wahitimu wote kutoka vyuo vya nje ya nchi kufuata utaratibu uliopo, ili kupata usajili. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, swali la nyongeza.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; pamoja na utaratibu uliopo, lakini bado tuna vijana wengi ambao wamesoma katika vyuo vya nje katika nchi hizi za Afrika Mashariki ambao pamoja na kufuata utaratibu huu, lakini wakifika katika Bodi za Kitaaluma ambazo ni muhimu wao wasajiliwe ili kuanza kazi katika nchi hii wanakataliwa usajili. Sasa, ni nini kauli ya Serikali juu ya changamoto wanazopata vijana hawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kumekuwa na mifano hai ya hawa vijana ambao, baadhi au wengi wao, nimewapeleka hata kwa Mheshimiwa Waziri, anafahamu changamoto zao, ambao wametumia gharama kubwa na muda mrefu kujielimisha katika vyuo vya nchi mbalimbali ndani ya Afrika Mashariki, lakini na wao wamekataliwa usajili. Sasa hivi wako mtaani wamekata tamaa na wanaishi kama watu ambao hawakusoma kabisa kwa sababu, wamekataliwa kutambuliwa elimu walizopata. Sasa, ni nini kauli ya Serikali juu ya kuwasaidia vijana hawa na changamoto wanazopitia sasa hivi? Ninashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, Kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge, amekuwa akifuatilia jambo hili kwa karibu sana.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia taasisi yetu ya Elimu ya Juu *(TCU)* hivi sasa imetengeneza utaratibu wa kutoa Hati ya Ruhusa au *Certificate of No Objection*. Huu ni mkakati maalum wa Serikali wa kuhakikisha kwamba, mwanafunzi kabla hajaondoka kwenda nje kwa ajili ya kusoma anapata cheti hiki au *certificate* hii, ambayo itamwezesha kutambua au Serikali itawezesha kutambua uhalali wa chuo anachokwenda kusoma na uhalali wa kozi anayokwenda kusoma, ili anaporudi sasa Serikali iweze kutambua na kusajili kwa haraka sana taaluma aliyokwenda kusomea.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni hili ambalo amezungumza Mheshimiwa Mbunge. Ni kweli, wapo vijana wetu ambao wamekwenda nje na wamerudi na imekuwa changamoto kidogo. Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge tutofautishe hizi mamlaka za ithibati pamoja na zile mamlaka za kitaaluma. Kwa sasahivi tumetengeneza utaratibu, tunakaa na Bodi zetu zile za Kitaaluma, ili kuhakikisha kwamba, tunakwenda ku-*harmonize* mazingira yote yatakayojitokeza huko mbele na hawa vijana wetu tutakaa nao ili kuhakikisha kwamba, tunakwenda kuliweka jambo hili sawasawa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitoe rai, wito na ushauri kwa wanafunzi; watu wote ambao wanataka kwenda nje ya nchi, basi waweze kufuata utaratibu wa kupata kwanza hii *Certificate* ya *No Objection*, ili wanapokwenda kusoma tujue wanakwenda kusoma kwenye chuo gani na wanakwenda kusoma taaluma gani. Lengo ni kuwalinda wao, lakini vilevile kuwalinda Watanzania dhidi ya taaluma ambazo watakuja kuwatumikia Watanzania wote ili zisiweze kuleta athari ndani ya nchi. Ninakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Nitaleta tangazo nililo nalo hapa, nalo linahusu wageni walioko Bungeni asubuhi hii.

Tutaanza kwanza na wageni wangu na hawa ni vijana wa Kundi la *Gen Z* wa Chama cha Mapinduzi kutoka Uyole Mkoani Mbeya, wakiongozwa na Ndugu Ektori Omary, ambaye ni Mwenyekiti. Pia yupo Ndugu Happy Matola, ambaye ni Katibu, karibuni sana. *(Makofi)*

Hawa wameongozana na Ndugu Clemence Mwandemba, ambaye ni mlezi wao na Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi, Mbeya Mjini, karibuni sana. Sasa msimame wote kwa pamoja. Karibuni sana, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine waliokaa Jukwaa la Spika; tutaanza na wageni wa Mheshimiwa George Boniface Simbachawene ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Yupo Ndugu Mululi Mahendeka ambaye ni Katibu Mkuu Ikulu; Ndugu Juma Mkomi, Katibu Mkuu Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Ndugu Xavier Daudi ambaye ni Naibu Katibu Mkuu Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Mheshimiwa Jaji Sivangilwa

Mwangesi, ambaye ni Kamishna wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Ndugu Crispin Chalamila, ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Shadrack Mziray, Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF);* Mhandisi Benedict Ndomba, Mtendaji Mkuu Mamlaka ya Serikali Mtandao *(e-GA); Capt.* Budodi Budodi, Afisa Mtendaji Mkuu Wakala wa Ndege za Serikali Tanzania *(TGFA);* Ndugu Mick Kiliba ambaye ni Mtendaji Mkuu Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; Ndugu Firimin Msiangi, Mtendaji Mkuu Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa; na Ndugu John Mbisso, Kaimu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma, karibuni sana. *(Makofi)*

Vilevile tunao Ndugu Ernest Mabonesho, Kaimu Mkuu wa Chuo cha Utumishi wa Umma; Ndugu Solomon Sephania, Kaimu Mtendaji Mkuu *Watumishi Housing Investment;* Dkt. Florence Turuka, Mjumbe wa Sekretarieti ya Baraza la Kumshauri Rais Masuala ya Chakula na Kilimo; na Ndugu Cyrus Kapinga, Mkurugenzi wa Uendelezaji Sera, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, katika watu waliokaa Jukwaa la Spika, yupo pia Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Mheshimiwa Petro Magoti ambaye amewaongoza wageni 80 wa Mheshimiwa Dkt. Sulemani Said Jafo ambaye ni Waziri wa Viwanda na Biashara. Hawa ni Wajumbe wa Baraza la Wilaya, Jumuiya ya Wazazi kutoka Kisarawe Mkoa wa Pwani, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 15 wa Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamisi ambaye ni Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, hawa ni Mashujaa wa Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii Tanzania *(SMAUJATA),* karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma ambaye ni Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, huyu ni mjasiriamali kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu mpigakura wake kutoka Goba, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane ambao ni wadau wa maendeleo kutoka Wilaya ya Kilwa Mkoani Lindi, karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate ambaye ni rafiki yake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Aloyce Andrew Kwezi, ambao ni wachimbaji wadogo wa madini kutoka Kahama, Mkoani Shinyanga, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani, ambaye ni mtoto wake na mdogo wake kutoka Singida, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, ambo ni wapigakura wake kutoka Vwawa Mkoani Songwe, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 24 wa Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya, ambao ni watumishi na wanufaika wa *Compassion Muhalala* kutoka Manyoni Mkoani Singida, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge, kwa ajili ya mafunzo: Kwanza ni Ndugu Dickson Daudi Mkubwa kutoka Kata ya Kizota, Jijini Dodoma, karibu sana. *(Makofi)*

Walimu watano na wanafunzi 42 wa darasa la saba kutoka Shule ya Msingi Hannah Bennie iliyoko Kibugumo, Wilaya ya Kigamboni, Mkoa wa Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wanachama 48 wa Taasisi ya *Pink Hijab* kutoka Mkoani Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 60 wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya *(MUST),* karibuni sana Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni waliopo hapa Bungeni na wengine tutaendelea kuwataja kadri watakapopata nafasi ya kuingia hapa ndani.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Orodha ya Shughuli zetu za leo ilikuwa ifuate Hoja ya Serikali, lakini mtakumbuka jana wakati wa kuhitimisha hoja hapa ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, niliahidi kwamba tutapata nafasi ya kusikiliza majibu ya Mheshimiwa Waziri kuhusu tuhuma alizokuwa amezitoa Mheshimiwa Gambo. Kwa hivyo, nitampa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, atoe huo ufafanuzi, kisha tutaendelea na ratiba yetu.

Mheshimiwa Omary Mchengerwa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, katika mjadala wa hoja za bajeti, Mheshimiwa Mrisho Gambo, Mbunge wa Jimbo la Arusha Mjini, aliwasilisha tuhuma kuhusu miradi minne mikubwa inayotekelezwa na Halmashauri ya Jiji la Arusha, kama ifuatavyo:-

(1) Ujenzi wa jengo la utawala la halmashauri;

(2) Ujenzi wa Soko la Machinga;

(3) Utengaji wa bajeti ya shilingi biloni 1.6 kwa ajili ya kubomoa maduka eneo la stendi ndogo, kutokuwa na tija kwa halmashauri; na

(4) Ujenzi wa Barabara ya *TACTIC* kutoka Stendi Mpya kwenda Mbauda.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue nafasi hii kutoa ufafanuzi katika hoja zote nne kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri ya Jiji la Arusha. Kwa heshima ya Bunge hili na kwa maslahi mapana ya Taifa, ninaomba kuweka bayana ukweli wa

hoja hii kama ifuatavyo: Kuhusu ujenzi wa jengo la utawala la Jiji la Arusha, alitoa tuhuma nzito dhidi ya utekelezaji wa ujenzi wa jengo hilo, akidai kuwepo kwa ongezeko lisilo halali la takribani shilingi bilioni nane. Pamoja na madai ya mchanganyiko wa vipimo vya *BOQ* uliosababisha malipo ya fedha isiyostahili, Mradi wa Jengo la Utawala ulianza mwaka 2019 wakati huo Mheshimiwa Mrisho Gambo akiwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, kama msimamizi mkuu.

Mheshimiwa Spika, ujenzi ulifanyika kwa njia ya *Force Account* na baadaye ukahama kutoka *Force Account* na kuingia kwa mkandarasi. Akapatikana Mkandarasi Mshauri, ambaye alisaidia kupatikana kwa Mkandarasi wa Ujenzi, Mheshimiwa Mrisho Gambo akiwa Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii yote ilitokana na malumbano yaliyokuwepo kati ya Mheshimiwa Mbunge, Baraza la Madiwani na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wakati huo, Mheshimiwa John Mongela. Malumbano hayo yalisababisha mradi kusimama kwa muda mrefu mpaka mwaka 2023 baada ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuingilia kati na baadhi ya watumishi kushtakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Fedha. Mbunge alikuwa ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha wakati huo, hakushiriki kikao husika kwa ruhusa, lakini posho alichukua, hii ilikuwa ni mwaka 2023, ikampa mkandarasi Ndugu *Trive Construction*, lakini hakuweza kuendelea na kazi tena. Yakatokea malumbano baina ya mkandarasi na kazi ikaanza tena upya mwezi Aprili, 2024 na kuomba kulipwa malipo ya awali, ndiyo jengo likaanza kujengwa na sasa lipo ghorofa ya sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa mkandarasi amekwishalipwa hati mbili, pamoja na malipo ya awali. Jumla ya hati zote mbili ni shilingi 1,200,000,000 pamoja na malipo ya awali, jumla inakuwa ni shilingi 2,200,000,000 na jengo lipo ghorofa ya sita. Kilicholipwa mpaka sasa ni kidogo kulingana na uhalisia wa jengo mpaka hivi sasa, hivyo mkandarasi analipwa malipo yake kwa kazi alizofanya, zikihakikiwa pia na Mhandisi wa Jiji kwa kazi zilizofanyika tu.

Mheshimiwa Spika, kwa ujenzi unaofanywa na mkandarasi na Mkandarasi Mshauri, Mkandarasi Mshauri huandaa hati ya malipo kulingana na kazi iliyofanyika. Hivyo basi, hakuna fedha ya Serikali iliyoibiwa mpaka sasa. Ninasisitiza, hakuna fedha ya Serikali iliyoibiwa mpaka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia dhamira ya dhati ya kulinda fedha za Umma, tuhuma zilizotolewa na Mheshimiwa Gambo zimechunguzwa. Pia, niliagiza kufanyika kwa uchunguzi wa kina, uchunguzi huo ulibaini hitilafu za kiufundi zilizojitokeza katika uingizaji wa taarifa kwenye Mfumo wa Ununuzi wa Umma *(NeST)*, ambapo vizio vya vipimo vilichanganywa. Katika uchunguzi uliofanyika, kilichoonekana ni vizio vya vipimo *(units of measurement)* kuchanganywa katika vipengele viwili wakati wa kuingiza kwenye Mfumo wa Ununuzi wa Umma *(NeST),* kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kipengele cha zege la sakafu ya chini kwa unene wa milimita 200 ilikadiriwa kuwa meta za mraba 1,128, kama ilivyooneshwa kwenye *BOQ* ya Mhandisi Mshauri. Hata hivyo, wakati wa kupandisha kipengele hicho kwenye Mfumo wa Manunuzi *(NeST)*, kipengele hicho kilipandishwa kama mita za ujazo 1,128.

Mheshimiwa Spika, mbili; kipengele cha zege la sakafu ya juu kiliainishwa kuwa ni meta za mraba 7,034, kama ilivyooneshwa katika *BOQ* ya Mhandisi Mshauri. Katika kupandisha kwenye Mfumo wa Ununuzi wa Umma, kipengele hicho kiliingizwa kama mita za mraba 7,034.

Mheshimiwa Spika, Menejimenti ya Jiji la Arusha ilibaini kasoro hizo na kumjulisha Mshauri Mwelekezi kuhusu makosa katika vizio vya upimaji uliojitokeza katika barua yenye Kumb. Na. BC.3/253/0IE/149 ya tarehe 10 Februari, 2025 na barua Kumb. Na. BC.3/253/0IE/150 ya Tarehe 18 Februari, 2025. Mtaalam Mshauri alijibu barua hizo kwa barua yenye Kumb. Na. KA/ACC/ADM/2024/20 ya Tarehe 28 Februari, 2025, kwa kukiri kupokea mapungufu hayo na alichukua hatua za kumwandikia

mkandarasi kumweleza mapungufu yaliyojitokeza kwa barua yenye Kumb. Na. *KA/ACC/ADM/2024/24* ya Tarehe 7 Machi, 2025.

Mheshimiwa Spika, mkandarasi alimjibu Mtaalam Mshauri kwa barua yenye Kumb. Na. *TRB.JV.TBW/ADM/ACC/HQ* ya tarehe 08 Machi, 2025, akikubali mabadiliko hayo ya vipimo tangu Mwezi Machi, kama yalivyoonekana katika mkataba. Taratibu za kuandaa mabadiliko *(Addendum)* zinaendelea kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura Na. 410. Hivyo, gharama halisi za mkataba zitazingatia vipimo sahihi, ambapo mradi utatekelezwa kwa gharama ya shilingi 3,461,712,000. Aidha, fedha za ziada ambazo ni shilingi 416,983,000.27, ikiwa ni sehemu ya malipo ya awali, zitazingatia utekelezaji wa kazi na makubaliano ya mabadiliko ya mkataba.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, hoja hii iliibuliwa na Halmashauri ya Jiji kuhusu vipimo husika na kukubaliana na pande zote mbili, tangu mwezi Machi, si hoja mpya. Ilikwishafanyiwa kazi na ndiyo desturi za mikataba. Hoja hii inasimamiwa na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa na TAKUKURU wanaifanyia kazi kujiridhisha, tangu mwezi Machi 2025 na muda wowote *Addendum* itasainiwa na mkandarasi yupo eneo la mradi mpaka jengo litakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, haya si matamko tu, ni matendo yaliyokwishafanyika. Kuibua hoja ambazo zimekwishafanyiwa kazi kwa makusudi na mamlaka husika au zipo kwenye mchakato ni sawa na kusisitiza kuwa, Serikali ni kipofu na bubu. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Sita, Serikali ya Awamu ya Sita inasimamia misingi ya uwajibikaji, misingi ya uadilifu na kujifunza kutokana na kila changamoto.

Mheshimiwa Spika, hatufichi makosa tunayoyakabili. Tunayakabili kwa ujasiri kwa sababu, kama alivyosema Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, "Hatupaswi kuwa na Serikali ya kuogopwa, bali Serikali ya kuheshimika kwa uadilifu wake". Kwa njia hii tunawaonesha Watanzania kuwa, Serikali yao ni ya watu, kwa watu na kwa ajili ya watu. Tunapambana na

dosari kwa uwazi, tunalinda rasilimali kwa uaminifu na kusimamia kila senti kwa jicho la uzalendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali hii imedhamiria kuwa si tu msimamizi wa maendeleo bali ni nguzo ya maadili ya Taifa. Tuna amini kuwa kuaminiwa ni mtaji mkubwa kuliko hata fedha; na kwa kila hatua tunayochukua kurekebisha dosari tunazidi kuijenga Serikali ambayo Watanzania wanaweza kuiamini, Serikali inayosema kweli inachukua hatua na hatua hizi zilizokwishachukuliwa, niruhusu nisistize tena hakuna mahalI popote katika taarifa niliyoletewa inayoonesha kuwa shilingi bilioni nane italiwa. Kwa kuwa mkataba ni mchakato, ni mwendelezo wa kazi thamani halisi itaendelea kubaki kuwa kwa mujibu wa marekebisho ya mkataba na hakuna senti ya Watanzania itakayoliwa baada ya kukamilika kwa mkataba.

Mheshimiwa Spika, ningependa kulikumbusha Bunge lako Tukufu kuwa masuala yote ya maendeleo huanzia kwenye Kamati ya Maendeleo ya Kata, Kamati za Kisekta za Halmashauri na mwisho Baraza la Madiwani, ambapo sisi wabunge ni wajumbe kote huko. Kama miongoni mwetu kuna kitu hujaridhika turejee kwenye halmashauri zetu kwenye vikao vya kisheria kwenda kupata ufafanuzi zaidi wa jambo mahsusi ambalo hatujalielewa sisi kama Wabunge.

Mheshimiwa Spika, katika hoja hii pia Mheshimiwa Mbunge, alisisitiza kuwa kuna wafanyakazi hawakuchukuliwa hatua kabisa. Tuhuma hizo zilibainika baada ya ukaguzi maalum ulioagizwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na utekelezaji wake kufanywa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* aliyebaini mapungufu ya kiutaratibu. Baada ya mapendekezo yote ya kisheria watumishi sita walishtakiwa; lakini zaidi kulikuwa pia na kesi tatu za jinai za uhujumu uchumi zilizosajiliwa na Mahakama dhidi ya baadhi ya watumishi. Watumishi watatu kati yao waliwekwa rumande kwa takribani miaka miwili kabla ya kufutiwa kesi kwa maamuzi ya Mahakama ya Rufani Kanda ya Arusha tarehe 16 Februari, 2024 kupitia rufaa Na.116 ya mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, kesi nyingine ziliondolewa na Mahakama kwa mujibu wa kifungu cha 91(1) cha Sheria ya Mwenendo wa Jinai, Sura ya 20. Hii inaonesha kuwa Serikali ilifuata hatua zote za kisheria na kiuadilifu katika kushughulikia tuhuma, ikiwa ni pamoja na kusimamia haki, uwajibikaji na misingi ya utawala bora ambapo Kamati ya Uchunguzi iliundwa kushughulikia tuhuma hizo ilibainisha kuwa makosa waliyonayo ni ya kufukuzwa kazi.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu kusisitiza kwamba Mheshimiwa Gambo, mwenyewe aliomba adhabu hiyo ya kufukuzwa kazi isichukuliwe na badala yake ipunguzwe. Mheshimiwa Mbunge alikuwa ni sehemu ya mchakato huu, alishiriki kikamilifu katika kikao cha Kamati ya Fedha na cha Baraza la Madiwani kilichotoa adhabu kwa watumishi waliyobainika na makosa ya kinidhamu. Mheshimiwa Mbunge aliridhia na kushawishi kikao wapewe adhabu ya chini kabisa kwa watumishi wengine waliyobaki kukatwa mishahara yao kwa 15% kwa miaka mitatu na bado wanakatwa mpaka sasa. Adhabu hii haijaisha, kama njia ya kuhitimisha mjadala wa kinidhamu hakuwasilisha pingamizi rasmi katika uamuzi huo. Kwa hivyo ni jambo la kushangaza kuona yeye sasa akiwasilisha hoja hiyo Bungeni kana kwamba ni jambo jipya au lenye sura ya kifisadi linaloendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa Soko la Machinga kiasi cha shilingi milioni 500 kutotumika hadi sasa. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri la Jiji la Arusha ilipokea kiasi cha shilingi milioni 500 kwa ajili ya Ujenzi wa Soko la Wafanyabiashara Ndogondogo (Wamachinga) eneo la Engutoto. Baada ya mapokezi ya fedha taratibu za utekelezaji wa miradi zilianza ikiwa ni pamoja na kutaarifu vikao rasmi kuhusu mapokezi ya fedha hizo na madhumuni ya Serikali ya kujenga soko hilo katika eneo la Engutoto.

Mheshimiwa Spika, baada ya taarifa hiyo kuwasilishawa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya, Mbunge Mrisho Gambo, Meya wa Jiji pamoja na Mkurugenzi wa jiji walifanya ziara kutembelea eneo la Engutoto na kubaini kuwa eneo hilo sio eneo sahihi kwa ajili ya ujenzi wa soko tajwa. Viongozi hawa wa Wilaya pamoja na Mbunge, walielekeza soko

hilo lijengwe Samunge maarufu kama eneo la kwa Mchina. Katika hali hiyo ilibidi kiitishwe kikao cha dharura cha Kamati ya Fedha, tarehe 11/06/2022 ambacho kiliridhia soko lijengwe eneo lililopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, baadaye ilibainika kuwa eneo lililopendekezwa ni eneo la viwanja vya watu binafsi ambavyo ni viwanja namba 16,17,19,20,21 na 22 *Block U* Kata ya Kati, hivyo aliwezi kutumika kwa ajili ya ujenzi wa soko. Tarehe 1/7/2022 kikao cha Kamati ya Fedha cha dharura kiliitishwa na iliazimiwa soko hilo lijengwe eneo la Engutoto kwa kuwa hapakuwa na eneo lingine linaloweza kujengwa soko hilo. Katika kuendelea kutafuta eneo kwa ajili ya kujenga soko hilo kilifanyika kikao cha tarehe 7/3/2024 na walipendekeza maeneo matatu kama ifuatavyo; eneo la pembeni ya dampo, eneo la Intel na eneo la *Bondeni City*.

Mheshimiwa Spika, kikao kingine kilifanyika tarehe 30/1/2025 kati ya wataalamu wa halmashauri na uongozi wa wafanyabiashara wadogo wilaya (SHIUMA) na kukubaliana kuwa soko lijengwe Bondeni City kwa kuwa Mradi wa *TACTIC* wa Ujenzi wa Stendi Kuu ya Mabasi umeanza, kwa kuanza na barabara. Baada ya makubaliano hayo wataalam wanaendelea na hatua ya kufanya marejeo ya michoro pamoja na makisio ya gharama kulingana na hali ya wakati huu. Tunatarajia kuwa zabuni ya ujenzi itatangazwa tarehe 28/4/2025. Soko hili litajengwa katika kiwanja namba 178 *Block B* Oljoro Bondeni City, chenye hati namba 9127.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia ninapenda kusisitiza kuwa ucheleweshwaji wa mradi huu haukuwa matokeo ya uzembe bali wa busara katika kuhakikisha kuwa jambo sahihi linafanyika kwa njia sahihi. Hili ni somo la uongozi kwamba wakati mwingine kukubali kutafakari upya si dalili za udhaifu bali ni uthibitisho wa dhamira ya kweli ya kutoa suluhisho endelevu.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa tumefikia makubaliano ya kutumia kiwanja namba 178 *Block B* katika eneo la Bondeni city, eneo lililo halali, wazi na linalokidhi matakwa ya kimazingira na

kimkakati. Zabuni ya ujenzi inatarajiwa kutangazwa tarehe 28/4/2025 na Serikali itaendelea kusimamia kila hatua kwa weledi na kwa uwazi. Ni muhimu tukumbuke maneno ya Mwanafalsafa John Stuart Mill, aliyesema, maendeleo ya jamii yanapimwa kwa namna taasisi zake zinavyowajibika kwa waliodhurumiwa au kusahaulika. Kwa muktadha huu ujenzi wa soko hili ni zaidi ya majengo, ni sehemu ya heshima kwa maisha na juhudi za wamachinga wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Serikali, ninaomba kuwahakikishia Watanzania hasa Wamachinga wa Jiji la Arusha kuwa soko hili linakuja tena kwa heshima, kwa hadhi na kwa matarajio waliyonayo. Kama ambavyo wahenga walisema, penye nia pana njia. Nasi tumejifunza kujirekebisha na sasa tunatekeleza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la utengaji wa bajeti ya shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya kubomoa maduka eneo la stendi ndogo kutokuwa na tija kwa halmashauri. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Halmashauri ya Jiji la Arusha imetenga kiasi cha shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya ujenzi wa maduka ya kisasa katika eneo la stendi ndogo. Fedha hizi hazikulengwa kwa ajili ya ubomoaji pekee. Ninasisitiza; fedha hizi hazikutengwa kwa ajili ya ubomoaji pekee kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesisitiza kwenye Bunge lako hili, bali kwa utekelezaji wa mradi wa maendeleo unaolenga kubadilisha taswira ya eneo hilo kuwa eneo la kisasa kabisa, la kibiashara na la kuvutia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uamuzi huu umetokana na maazimio ya vikao halali vya Baraza la Madiwani vilivyofanyika kuanzia tarehe 24 hadi 25 Februari, 2025, ambapo Mheshimiwa Mbunge, Ndugu Mrisho Gambo alishiriki kikamilifu katika mjadala na mchakato wa maamuzi hayo. Ushiriki wake unathibitisha kuwa haya si maamuzi ya upande mmoja bali ni matokeo ya maridhiano ya pamoja yenye lengo la kuleta maendeleo ya kweli.

Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa eneo hili unalenda si tu kuongeza mapato ya halmashauri bali pia kuboresha mazingira ya biashara kwa wafanyakazi na wafanyabiashara na kuongeza

mvuto wa Jiji la Arusha. Mradi huu mpya utajumuisha maduka takribani 800 yanayolengwa kujengwa kwa mfumo wa gorofa mbili na maegesho ya kisasa, tofauti na hali halisi ya sasa ya maduka 364 yaliyochakaa. Ujenzi huu utaleta mapinduzi ya kiuchumi kwa kuongeza mapato kutoka wastani wa shilingi milioni 850 kwa mwaka hadi shilingi takribani bilioni 1.9 kwa mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunajifunza kutoka kwenye fikra za mwanafalsafa maarufu Aristotle aliyesema, *"the whole is greater than the sum of its parts"*. Maana yake ni kuwa nguvu ya pamoja ya maamuzi ya viongozi wetu ikiwa ni pamoja na ushirika wa Mheshimiwa Gambo, imezaa mpango mkubwa wa kimkakati ambao utaimarisha mapato ya jiji, kuinua kipato cha wananchi na kuboresha maisha ya wote. Aidha Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwahi kusema, "Maendeleo hayaji kwa miujiza bali kwa mipango madhubuti na kazi ya pamoja". Hivyo huu ni ushahidi kuwa Arusha haijapumzika imechagua kutenda, kupanga na kutekeleza kwa nia njema ya kizazi cha leo na kizazi kijacho.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huu, matumizi ya shilingi bilioni 1.6 hayawezi kuchukuliwa kama gharama tu bali ni uwekezaji wa kimkakati katika mustakabali wa Jiji la Arusha, uwekezaji unaolenga kujenga mazingira bora ya kibiashara, kuchochea ukuwaji wa kiuchumi wa Jiji la Arusha hadi Taifa kwa ujumla, na kuweka historia ya maendeleo tunayojivunia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ya ujenzi wa barabara ya *TACTIC* kutoka Stendi Mpya kwenda Mbauda. Katika hoja hii Mheshimiwa Mrisho Gambo, aliwasilisha hoja zinazohusiana na uboreshaji wa miundombinu ya barabara pamoja na Mradi wa *TACTIC*. Mheshimiwa Mbunge aliishauri Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia Mradi wa *TACTIC* wakae pamoja na *TANROADS* ili kuhuisha rasilimali za ujenzi wa barabara kutoka Stendi Mpya kwenda Mbauda. Kwa kuwa sasa wote wametenga bajeti ya ujenzi huo hivyo fedha zingine ziende kujenga miundombinu mingine ya barabara.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara kutoka Stendi Mpya kwenda Mbauda ambayo Barabara hiyo inaitwa Oljoro ni moja wapo ya barabara zinazojengwa na Mradi wa *TACTIC package one*, ambapo kwa sasa barabara hiyo itajengwa kilometa 1.475 ili kuunganisha stendi mpya ya mabasi inayotarajiwa kujengwa pamoja na *round about* ya kwa Morombo. Makubaliano yaliyofanyika ni kuwa barabara hii ijengwe na Mradi wa *TACTIC* kwa kufuata kiwango cha barabara kuu zinazosimamiwa na *TANROADS*, hivyo barabara hii imetengewa fedha katika Mradi wa *TACTIC* pekee.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na tahadhima, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Waheshimiwa Wabunge ufafanuzi wa hoja alizokuwa amezitoa Mheshimiwa Gambo umetolewa na Mheshimiwa Waziri; lakini sasa kuna jambo moja hapa linatofautiana kitakwimu Mheshimiwa Waziri. Ninakusubiri ufike mahali ambapo unaweza kuketi ili usikilize. Nenda tu kwenye kiti chako Mheshimiwa, usijekuwa umeacha pale karatasi ambazo zinaweza zikasaidia. Ahsante sana.

Kwenye mchango wa Mheshimiwa Gambo *Hansard* inasomeka kwamba, alisema, kwenye ile shilingi bilioni 1.6 ya kubomoa maduka ama stendi, anasema kwa ajili ya kwenda kubomoa eneo la stendi ndogo, eneo ambalo linaingiza mapato halmashauri shilingi milioni 800 kwa mwezi. Katika taarifa uliyotusomea ukurasa wa 17 Mheshimiwa Waziri, wa hii niliyonayo sijui kama na wewe ni ukurasa wa 17; unasema ujenzi huu utaleta mapinduzi ya kiuchumi kwa kuongeza mapato kutoka wastani wa shilingi milioni 850 kwa mwaka hadi takribani shilingi bilioni 1.9 kwa mwaka. Hii shilingi milioni 850 ni kwa mwezi ambayo itakuwa inashabihiana na ya Mheshimiwa Gambo ya 800 au hii ya kwako ni kwa mwaka, lakini yeye alisema kwa mwezi; ninataka tu kujua hapo. Ni 800 kwa mwezi au 800 kwa mwaka? Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kauli yangu ndiyo kauli halisi. Kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge yeye ameonesha kwamba

kuna shilingi milioni 850 kwa mwezi pengine anaweza kuwa na ushahidi wa hili.

**SPIKA:** Sawa, mimi ninataka tu hili eneo ili taarifa zetu zikae sawasawa. Mheshimiwa Gambo, ni milioni 800 kwa mwaka, kwamba ulimi uliteleza ulivyosema kwa mwezi au ni milioni 800 kwa mwezi?

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, siku ile nilitamka kwa mwezi.

**SPIKA:** Ulitamka kwa mwezi, lakini sasa kwa taarifa aliyoitoa Mheshimiwa Waziri, na wewe unakubali kwamba ni kwa mwaka au bado unasimamia ni kwa mwezi sio kwa mwaka.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, pale kuna vibanda zaidi ya 300 karibia 400 na kila kibanda kinalipa zaidi ya laki mbili kwa mwezi.

**SPIKA:** Haya hebu tufanye hiyo hesabu, jamani tufanye *faster*. Vibanda vingapi Mheshimiwa Gambo?

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, vinavyokadiriwa kufikia...

**SPIKA:** Fanya tu kadirio tutajua, mia tau?

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, kati ya 360 mpaka 400.

**SPIKA:** Haya fanya 360 mara laki mbili ni ngapi?

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, vibanda 400 ni shilingi milioni 80.

**SPIKA:** Eeeh, Mheshimiwa wa Momba, mtaalam wa hesabu.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nimeweka *maximum* yake amesema vibanda 400...

**SPIKA:** Eeh, imekuwa ngapi?

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, ukiweka 400 mara laki mbili ni shilingi milioni 80.

**SPIKA:** Shilingi milioni 80 na sio shilingi milioni 800?

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, aah, haifiki, inafika shilingi milioni 80.

**SPIKA:** Inakuwa shilingi milioni 80.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, ukiweka vipanda 360 mara laki mbili ni shilingi milioni 72.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Gambo.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, maana yake sasa ni kwa mwaka, ukiangalia kwa makadirio ya laki mbili mpaka laki mbili na nusu.

**SPIKA:** Sawa, kwa hivyo wewe ulisema shilingi milioni 800 kwa mwezi, sasa tunachukua taaria ya Mheshimiwa Waziri, kwamba ni kwa mwaka, ni sawasawa? Mheshimiwa Waziri naona umesimama. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa mwezi ni shilingi milioni 74, kwa mujibu wa taarifa ya mapato ya Mkurugenzi wa Jiji la Arusha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Gambo, alipata nafasi ya kuchangia kwenye makadirio ya mapato na matumizi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, akatoka takwimu nyingi nyingi hapa, sehemu ya hizo takwimu ndizo hizi ambazo Mheshimiwa Waziri amezieleza hapa kwa kirefu. Pia jana nimeletewa *Hansard* wakati tupo kwenye Kamati ya Matumizi yakatajwa hapo mabilioni tena.

Sasa kwa taarifa hii ya Mheshimiwa Waziri ilivyoeleza mtagundua kwa nini ilikuwa ni muhimu kutoa huu muda ili taarifa zetu Rasmi za Bunge zikae sawasawa, kwa sababu zinapotolewa tuhuma nzito kama hizo lazima, haziwezi tu kwenda kama hivi, kama Mbunge amesema tu hapana lazima tutilie maanani kwa sababu ni fedha za wananchi.

Sasa Mheshimiwa Gambo, kwenye ule mchango wako ulieleza mambo kwa machungu sana lakini sasa hii ndio taarifa ya Mheshimiwa Waziri. Sasa, picha ambayo inajengeka kwa aina ya michango ikitolewa kwa sura hii ni kama vile Mbunge anasema lakini kuna watu mahali hawasikii, hawasikilizi. Sasa hii kidogo inakuwa haileti picha nzuri, hasa ikiwa na wewe ni sehemu ya vikao. Kuwa sehemu ya vikao ni suala moja, kushiriki ni suala la pili, la tatu ni jukumu lako kushiriki vikao Mheshimiwa Gambo; kwa nini; kwa sababu kwenye hii *Hansard* niliyoisoma hapa kuna mahali Mheshimiwa Gambo, unasema, siendi kwenye taarifa zote, maana na mimi nitakuwa narejea tena, nasoma tu hapa ili Waheshimiwa Wabunge wapate picha lakini pia wananchi waelewe.

*"Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa na ushauri kwamba, mapato ambayo yanapatikana kwenye majiji yetu hasa haya makubwa Arusha, Mbeya, Dar es Salaam na Mwanza, hebu kaeni na watu wa halmashauri wasipange bajeti ki-traditionally, wapange bajeti kulingana na changamoto za watu. Leo kule kuna shida ya vivuko, leo kuna shida ya barabara, mnakwenda, maana yake hawa ni watu wengine, mnakwenda kutenga fedha shilingi bilioni 1.6 Jiji la Arusha eti kwa ajili ya kwenda kubomoa eneo la stendi ndogo, eneo ambalo linaingizia, mapato halmashauri shilingi milioni 800 kwa mwezi, leo mnakwenda kubomoa eti mjenge".*

Sasa haya maneno yanaashiria yaani wewe upo pembeni, ni watu wengine ndio wanafanya hii kazi. Sasa Mheshimiwa Gambo, maneno kama haya ni Dhahiri; mimi huwa ninapitia huko kwenye mitandao, hata mimi yale maamuzi niliyoyatoa nimesoma huko, inaonekana kama kuna jambo hivi linafichwa

fichwa linafanywa nini. Sasa tuhuma za namna hii hazipendezi ikiwa zinaelekezwa mahali ambapo hakuna uthibitisho.

Milioni 800 zimetajwa kwa mwezi, kumbe ni kwa mwaka, mabilioni haya yanayotajwa kumbe taarifa zipo ni mfumo wa *NeST* ulikosea vipimo ukaweka vipimo sawasawa. Kwa hiyo lazima tuliweke sawa ili tusilete taharuki kwa wananchi. Ikiwa litakuwepo jambo lingine la ziada sasa, maana jana ulizitaja hapa shilingi bilioni saba, kama hizo nazo bado una hoja nazo mimi nipo tayari kabisa, kwa sababu Bunge hili haliwezi kuvumilia ubadhirifu mahali popote, na ndiyo maana nilitoa nafasi wewe ukamaliza mchango na pia nikatoa nafasi kwa Mheshimiwa Waziri. Hata hivyo, wakati huo huo Bunge hili haliwezi kuvumilia taarifa ambazo zinakuwa hazina ukweli. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ni lazima kila jambo liwe linakaa sawa kwa sababu hiki ni chombo cha wananchi na wananchi wanatutarajia sisi tufanye kazi kwa sura ambayo tunaleta tija na ndiyo maana tunafanya yale maombi asubuhi. Kwa hiyo hata lile ulilokuwa umelisema jana maana hukupata nafasi pa kulisemea kama hayo mabilioni kuna mahali unaona yamepotelea pia naweza kukupa nafasi, lakini ni vyema ukakaa pale na Mheshimiwa Waziri, mwambie hapa napo nahisi zimepotea hebu nipe taarifa, atakupa taarifa.

Nina hakika utaridhika kama ambavyo leo taarifa hii imekuja kwetu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge sasa Taarifa zetu Rasmi za Bunge zinakaa sawasawa. *(Makofi)*

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Gambo, ninaona umesimama.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, ninaomba mwongozo wako kwa sababu Mheshimiwa Waziri ametoa majibu na mimi nilitoa maelezo nikiomba uchunguzi ufanyike kutokana na tuhuma ambazo zilikuwepo. Sasa nilikuwa ninadhani kuna

mambo yamesemwa, lakini hayakusema sawasawa. La kwanza, kuhusiana na jengo la utawala, nilijenga hoja mbili…

**SPIKA:** Sawa. Sasa ili twende sawasawa Mheshimiwa Gambo umetumia neno hayakusema sawasawa. Kwa hivyo, ili twende sawasawa na Kanuni zetu katika hii taarifa aliyotoa Mheshimiwa Waziri hicho unachotaka kunieleza sasa hivi ni kwamba Waziri amesema taarifa isiyo ya kweli, ndicho unachotaka kusema?

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu amepewa nafasi ametoa taarifa ningepewa nafasi nikatoa utetezi wangu kwa sababu hili jambo lina maslahi mapana kwa Jiji lile.

**SPIKA:** Hapana. Keti Mheshimiwa Gambo. Waheshimiwa Wabunge, isije ikaonekana kwamba kuna upande mmoja umesikilizwa mwingine hujasikilizwa hapana na ndiyo maana nilitoa upande wa Serikali usikilizwe kwa sababu, wewe ulishasikilizwa na *Hansard* niko nayo hapa mbele. Kwa hivyo, wewe ulisikilizwa na Bunge na Wabunge wenzako. Sasa ilikuwa nafasi ya Serikali kusikilizwa na Bunge na Wabunge wenzako, ndicho kilichofanyika hapa. *(Makofi)*

Sasa umesimama, ndiyo maana nimekuuliza jambo moja siyo kwa nia ya kukusikiliza wewe tena maana vinginevyo itabidi nimpe na Waziri nafasi tena. Sasa katika zile taratibu zetu za kusikiliza hili Bunge haliwezi kufanya hivyo ndio maana tunafanya kazi kwenye Kamati. Waziri alichokisema kwenye taarifa yake umetumia neno ambalo halisemi kama ni uongo ama si sahihi lakini umeweka hapo siyo sawasawa. Nimeuliza ili sasa nichukue hatua kikanuni taarifa aliyotoa Mheshimiwa Waziri kuna mahali amelidanganya Bunge? Ili tuanzie hapo.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** *Mheshimiwa Spika, kwanza, amesema hili jengo limeanza nikiwa Mkuu wa Mkoa, hapo amesema uongo. Lilianza nikiwa Mbunge.* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**SPIKA:** Kwa mwaka 2019 ulikuwa umeshaondoka? Ama halikuanza mwaka 2019?

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, lilianza 2021.

**SPIKA:** Sawa. Kuna nyingine au ni hiyo tu? Maana ninataka niende hapa, mnaniona nimeshika Kanuni tayari. Kuna lingine Mheshimiwa Gambo, kwenye taarifa ya Waziri?

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, lingine ni msingi wa hoja yangu, hoja yangu nili…

**SPIKA:** Ambayo yeye amedanganya, msingi wa hoja yako yeye kadanganya? Hajauelewa yaani huo msingi?

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, ninadhani kuna mahali ninahitaji kufanya *clarification* ili nipate majibu vizuri zaidi. Kama itakupendeza, kwenye…

**SPIKA:** Keti Mheshimiwa Gambo.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Ungeniruhusu hata sekunde 30 kwa sababu ni kitu kidogo tu.

**SPIKA:** Keti Mheshimiwa Gambo, kwa sababu nikikupa wewe nafasi lazima na yeye nimpe na ndiyo maana humu ndani Bunge huwa tunafanya kazi kwa Kamati, hatufanyi huu utaratibu wa *back and forth*. Kwa hiyo, keti.

Waheshimiwa Wabunge, jambo hili kwa sababu kama nilivyosema Mheshimiwa Mbunge alipata nafasi ya kusikilizwa mchango wake na alisikilizwa mpaka mwisho, nikatoa nafasi kwa Serikali ili ilete taarifa Bungeni. Serikali imeleta taarifa kupitia Waziri na imesomwa hapa. Mheshimiwa Gambo inaonekana kwenye ile taarifa iliyosomwa na Serikali yeye anasema Waziri amedanganya kwenye taarifa yake. Kwa hivyo, jambo hili kwa sababu sina uwezo sasa hapa wa kuanza kufuatilia kila mmoja, ninalipeleka kwenye Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Maadili kule wataenda kusikilizwa. *(Makofi)*

Sawa. Kwa hivyo, Kamati yetu ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itaanza kazi mara moja. Leo ni tarehe ngapi jamani? Leo ni tarehe 23 kazi hii ifanyike wiki ijayo watapewa nafasi ya kuleta hiyo taarifa hapa Bungeni na mnazijua Kanuni zetu vizuri kwa sababu ndio tupo mwishoni sasa hivi. Kwa hiyo, hamna mtu atakuwa hazijui hizi Kanuni. Kwa hivyo, Kamati yetu itawasikiliza halafu itakuja ituambie nani mwongo hapa ndani na kisha hatua zitachukuliwa baada ya hapo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo.

**SPIKA:** Baada ya kusema hayo. Mheshimiwa Gambo ninaona umesimama, hii itakuwa ni mara ya mwisho kusimama.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, sawa. Mimi ninaona kama sijatendewa haki kwa sababu sibishani na …

**SPIKA:** Unalijua jina la Kamati ile nilikokutuma? Ngoja unalijua jina la Kamati nilikokutuma linaitwaje?

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, ninalijua na sibishani…

**SPIKA:** Inaitwaje ile Kamati?

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, ya Maadili. Sibishani na wewe.

**SPIKA:** Siyo Maadili pekee. Inaitwaje ile Kamati?

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, Maadili, Haki, Kinga na Madaraka…

**SPIKA:** Sasa ukisema sijakutendea haki kule ninakokupeleka ni ili ukafanywe nini Mheshimiwa Gambo? *(Makofi)*

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, sawa. Ninashukuru.

**SPIKA:** Kule ninakokupeleka ni ili ukafanye nini? Si ili usikilizwe hayo yote unayotaka nikusikilize mimi hapa ndani tukiwa watu wote tunakusikiliza. Bunge linafanya kazi kupitia Kamati na wewe umepelekwa kwenye Kamati na hujapelekwa peke yako umepelekwa wewe na uliyemtuhumu kwamba amesema uongo. Sasa hujatendewa haki na mimi ama hujatendewa haki na nani maana hamna hoja?

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** *Mheshimiwa Spika, no, sasa kipengele nilichosema amesema uongo ni kwamba kusema mimi nilikuwepo wakati nikiwa Mkuu wa Mkoa wakati nilikuwa Mbunge. Kwa hiyo, nilikuwa ninatoa tu clarification kwamba katika hicho kipengele cha kusema kwamba, nilifanya nikiwa Mkuu wa Mkoa ndiyo nilikuwa ninataka record zikae sawa kwamba nilishiriki nikiwa Mbunge…***[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**SPIKA:** Unahisi Kamati italeta taarifa gani hapa ndani? Maana ninaona umeshajua italeta taarifa fulani ambayo itasisitiza kwamba wewe ulikuwa Mkuu wa Mkoa wakati hukuwa Mkuu wa Mkoa?

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** *Mheshimiwa Spika, Hapana. Sijasema italeta taarifa gani. Ninasema kwa sababu unasema nimesema amesema uongo. Ndiyo ninasema kile kipengele ambacho***…[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**SPIKA:** Kwa hiyo, unataka tena…*(Kicheko)*

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** *Mheshimiwa Spika, kile kipengele ambacho ninasema amesema uongo… (Makofi)* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**SPIKA:** Mheshimiwa Gambo sasa hapo tena unaleta tuhuma zinazonihusu kwamba nimeingiza maneno mdomoni mwako. Maana mimi nitaitisha *Hansard* sasa hivi?

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, Hapana. Ninasisitiza kwamba nilichokisema uliniuliza …

**SPIKA:** Hamna kusisitiza. Hebu keti chini, kaa chini Mheshimiwa Gambo. Keti. Utaenda ukajieleze kule kwenye Kamati sawasawa? Eeh, maana sasa nisijekuwa nimetoa hapa maamuzi huyataki wakati wewe mwenyewe ulikuwa unajibu huku kana kwamba kuna mahali unataka kufafanua. Ufafanuzi utatoa kwenye Kamati, Kamati italeta hapa ndani Waheshimiwa Wabunge. Tumeelewana? Ndiyo utaratibu, Bunge letu linafanya kazi kwenye Kamati. *(Makofi)*

Haya. Baada ya kusema hayo tunaendelea.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea na ratiba yetu, nimwite Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, aje awasilishe hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Bunge lako lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka 2024/2025 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais: Ikulu (Fungu 20 na Fungu 30); Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Fungu 33); Menejimenti ya Utumishi wa

Umma na Utawala Bora (Fungu 32); Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (Fungu 67); Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 94); na Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa (Fungu 4) kwa Mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii ninayosoma hapa ni muhtasari tu, lakini Kumbukumbu Rasmi za Bunge zitachukua hii taarifa ambayo ni kubwa. Kama ilivyo ada ninaomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na neema kwa kutuwezesha kuwa na afya njema na kuendelea kuijalia nchi yetu amani, utulivu na mshikamano ambazo ni tunu zinazotuwezesha kushiriki katika Mkutano huu wa Kumi na Tisa ambao ni Mkutano wa mwisho wa Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini kusimamia Utumishi wa Umma kwa kuzingatia misingi ya Utawala Bora, Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali na hatimaye kuwa na Utumishi wa Umma wenye ufanisi na uwajibikaji kwa ustawi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, aidha, ninawashukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kazi kubwa wanayofanya ya kumsaidia Rais na Amiri Jeshi Mkuu na Mwenyekiti wa Chama chetu Cha Mapinduzi kutekeleza majukumu yake ya kusukuma maendeleo ya Taifa letu na kuiweka nchi yetu katika hali ya usalama na amani. Vilevile, ninawashukuru viongozi wangu wote kwa maelekezo, ushauri na miongozo wanayonipatia ambayo imenisaidia kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutumia fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, akiwa anaelekea kuhitimisha awamu ya kwanza ya kipindi cha uongozi wake.

Uongozi wake thabiti unadhihirishwa na maendeleo kwenye nyanja mbalimbali hususan kwenye maboresho makubwa yaliyofanyika katika Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ikiwemo mifumo ya kiutawala na usimamizi wa rasilimali watu ya kidijiti. Maboresho hayo yameleta mageuzi ya kiutendaji na utoaji wa huduma katika utumishi wa umma ikiwa ni dalili tosha kuwa nchi ipo katika njia sahihi ya kufikia malengo tuliyojiwekea katika mipango yetu ya Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda nichukue fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, kwa hotuba yake aliyoiwasilisha hapa Bungeni ambayo imetoa dira na mwongozo wa utekelezaji wa shughuli za Serikali katika mwaka ujao wa fedha. Aidha, ninampongeza kwa kuendelea kusimamia na kuratibu utendaji kazi na uwajibikaji Serikalini ambapo ufuatiliaji wake umetoa mwangwi wa uwajibikaji katika Utumishi wa Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba Bunge lako Tukufu liungane nami katika kumpongeza Komredi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu 2025 na ninaomba tumwombee kwa Mwenyezi Mungu azidi kumjalia uzima na afya njema ili aweze kufikia kipindi cha kulitumikia Taifa katika nafasi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukupongeza kwa dhati wewe binafsi; Naibu Spika, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu; Wenyeviti wa Bunge; Wenyeviti wote wa Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge; pamoja na watendaji wote wa Ofisi yako kwa namna mmeliendesha Bunge letu Tukufu kwa weledi na umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025, Bunge lako Tukufu limempoteza mwakilishi mwenzetu ambaye ni Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni, Mkoani Dar es

Salaam na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani Ukanda wa Afrika. Aidha, pia tumepoteza mwenzetu Profesa Philemon Sarungi aliyekuwa Mbunge mstaafu na Waziri mstaafu ambaye amehudumu katika Wizara mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, tumempoteza vilevile Jaji mstaafu Frederick Mwita Werema, aliyekuwa Mwanasheria Mkuu mstaafu. Aidha, tumempoteza Ndugu Lawrence Mafuru ambaye alikuwa Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango na Ndugu Gissima Nyamo-Hanga, aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa *TANESCO*. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu wote peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, aidha, niungane na Wakatoliki wenzangu duniani na niungane na Baba Kadinali Protase Rugambwa Kiongozi wa Kanisa Katoliki Tanzania na Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania na Wakatoliki wote duniani. Katika kuombeleza kifo cha Baba Mtakatifu Francis, Kiongozi Mkuu wa Kanisa Katoliki duniani ambacho kilitokea tarehe 21 mwezi huu Aprili, 2025.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba; Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Florent Kyombo, Mbunge wa Nkenge; na Wajumbe wa Kamati wote kwa ujumla kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Mapendekezo ya Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Maoni, ushauri na ushirikiano wa Kamati umetuwezesha kuboresha utendaji kazi wa Ofisi yetu na maandalizi ya hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua nafasi hii kwa namna ya pekee kumshukuru Mheshimiwa George Huruma Mkuchika, Waziri wa Nchi, Kazi Maalum kwa namna anavyosaidia utekelezaji wa kazi maalum za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakika yeye ni hazina na mchango wake umekuwa nguzo muhimu ya maamuzi mengi ya uendeshaji wa shughuli za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua nafasi hii pia kumshukuru Naibu Waziri wangu, Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge, kwa jinsi alivyonisaidia katika kuratibu, lakini pia kusimamia mambo mbalimbali ambayo tumefanikiwa katika Ofisi yetu ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ni kijana hodari, kijana makini, kijana mpole, kijana mwenye weledi na mwenye uwezo mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru Dkt. Moses Kusiluka, Katibu Mkuu Kiongozi; Bwana Mululi Mahendeka, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Ikulu; Ndugu Juma Mkomi, Katibu Mkuu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Naibu Katibu Mkuu, Bwana Xavier Daudi; Makamishna, Watendaji Wakuu wa Taasisi; Wakurugenzi; na Watumishi wote wa Ofisi ya Rais Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kutekeleza majukumu yanayoiwezesha Ofisi kufikia malengo yake, ikiwa ni pamoja na kukamilisha Hotuba hii kwa wakati. Aidha, ninapenda kuwashukuru waajiri na watumishi wa umma wote kwa kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi, uzalendo pamoja na imani yao kwa uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita. Utendaji wao umeiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake ya kuwahudumia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wa pekee kabisa ninawashukuru sasa wananchi wenzangu wa Jimbo la Kibakwe kwa kuendelea kunipa ushirikiano na imani wakati wote kwangu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, ninaomba sasa kuwasilisha Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ina mafungu saba kama ambavyo nimeyaeleza; nianze na Ofisi ya Rais – Ikulu. Ofisi ya Rais – Ikulu, Fungu 20 - iliidhinishiwa shilingi 33,544,557,000.00 kwa ajili ya

matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Machi, 2025 shilingi 25,292,595,000 sawa na 75.4% zilipokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Fungu 30, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri; liliidhinisha shilingi 969,585,000,000 Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 805.6 sawa na 83.12% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 163.6 sawa na 16.8% ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2025 kiasi cha shilingi bilioni 721.512 sawa na 74.44% ya bajeti iliyotengwa kilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 611.186 zilikuwa ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 110.328 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Taasisi zote ambazo ni Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, *TASAF*, Mamlaka ya Serikali Mtandao, Taasisi ya Uongozi, Wakala wa Ndege za Serikali na Baraza la Kumshauri Rais kuhusu Masuala ya Chakula na kilimo imetekeleza shughuli mbalimbali kama ilivyoonekana kuanzia ukurasa wa 10 hadi ukurasa wa 40 wa hotuba yetu kubwa na kwa uchache nitaje tu machache.

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa ilikuwa ni ushauri kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao umetolewa katika masuala ya siasa, uchumi, sheria, mambo ya kijamii, diplomasia, mawasiliano na habari, uhusiano wa kikanda na kimataifa na masuala mengine muhimu kwa lengo la kumsaidia Mheshimiwa Rais kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Spika, majukumu mengine yaliyofanyika yanapatikana katika hotuba yetu ndefu.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Bunge lako Tukufu liliidhinisha shilingi 13. 142 kwa Fungu 33 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 11.6 sawa na 88.5% kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 1.5 sawa na 11.41% kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2025 kiasi cha shilingi

bilioni 9.2 sawa na 70.36% ya bajeti iliyotengwa kilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 8.5 zilikuwa ni Matumizi ya Kawaida na shilingi milioni 718.5 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi kufikia Machi, 2025 Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imetekeleza shughuli mbalimbali kama zinavyoonekana kuanzia ukurasa wa 41 hadi 44. Nizitaje tu kwa uchache, pamoja na mambo mengine shughuli zilizofanyika ni kutoa tamko la rasilimali na madeni kupitia njia ya Mtandao *(Online Declaration System),* pia zoezi la uhakiki wa taarifa kupitia mfumo na tamko la rasilimali na madeni kwa njia ya mtandao.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2024/2025, Bunge lako Tukufu liliidhinisha shilingi bilioni 58.3 kwa Fungu 32, ikijumuisha Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, Watumishi *Housing Investment (WHI)* na Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 48.2 sawa na 82.75% kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 10.06 na asilimia 17.25 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2025 kiasi cha shilingi bilioni 42.7 sawa na 73.24% ya bajeti iliyotengwa kilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 37.7 zilikuwa ni Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 4.9 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na taasisi zake yaani Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, Watumishi *Housing,* imetekeleza shughuli mbalimbali ambazo zinapatikana katika ukurasa wa 46 na 63 ya hotuba yetu. Nitaje kwa uchache tu maeneo mawili.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni maadhimisho ya Mkutano wa Umoja wa Jukwaa la Umoja wa Mataifa la Tuzo za Utumishi wa Umma *(2024 UN Public Service Forum)* yalihudhuriwa ambapo, Mfumo wa e-Mrejesho uliotambuliwa na Umoja wa Mataifa na kushinda Tuzo ya Ubunifu katika Huduma za Umma kwa mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, pili ni jumla ya vibali 12,936 vya ajira mpya vilivyotolewa, ikijumuisha nafasi 11,960 kati ya nafasi 45,000 zilizoidhinishwa kwa Taasisi ambazo hulipwa mishahara kupitia Mfumo wa e-Watumishi na nafasi 976 kwa Taasisi zinazolipa mishahara ya watumishi kupitia mapato yao ya ndani. Aidha, vibali 1,739 vya ajira mbadala vilitolewa kwa waajiri mbalimbali. Maandalizi ya kutekeleza ajira mpya 33,040 zilizosalia yanaendelea na yanatarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, jukumu jingine lilikuwa ni ujenzi wa kampasi ya Singida awamu ya pili katika eneo la Mungu Maji kwa fedha za ndani umefikia 98%.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha shilingi bilioni 13.179 kwa ajili ya Fungu 67 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 10.8 sawa na 82.18% kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida; na shilingi bilioni 2.348 sawa na 17.82% kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2025, kiasi cha shilingi bilioni 8.8 sawa na 66.99% kilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 7.218 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni1.6 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi kufikia Machi, 2025, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imetekeleza shughuli mbalimbali kama zinavyoonekana katika ukurasa wa 64 hadi 68.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Bunge lako tukufu liliidhinisha kiasi cha shilingi bilioni 9. 24 kwa ajili ya Fungu 94 - Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 8.7 sawa na 94.59% ni matumizi ya kawaida na shilingi milioni 500 sawa na 5.41% ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2025 shilingi 7.135 sawa na 77% zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni

6.6 ni matumizi ya kawaida na shilingi milioni 500.176 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Tume imetekeleza shughuli mbalimbali kama zinavyoonekana kuanzia ukurasa wa 69 hadi wa 71.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha shilingi bilioni 4.3 kwa ajili ya Fungu 4 - Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 4.06 sawa na 93% ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida; na shilingi milioni 295. 7 sawa na 6.78% kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2025, shilingi bilioni 3.482 sawa na 79.86% zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 3.362 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi milioni 120,000,000 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka ya Taifa imetekeleza shughuli kama inavyoonekana katika ukurasa wa 72 hadi 74.

Mheshimiwa Spika, Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, imeandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, maelekezo ya Ilani ya uchaguzi wa Chama Cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 - 2025, Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano unaishia 2025/2026, lakini pia hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyoitoa tarehe 25 Aprili, 2021 na maelekezo ya mamlaka na maoni na ushauri wa Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi ya Rais Ikulu Fungu 20 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 34.8 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, Ofisi ya Rais, Sekretariet ya Baraza la Mawaziri Fungu 30 linaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi trilioni 1.197.3 kati ya fedha hizo shilingi trilioni 1.39.8 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 88.9 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa fedha za ndani shilingi milioni 68.5 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, kupitia maombi haya Ofisi ya Rais, Ikulu na taasisi zake ambazo ni Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, *TASAF*, Mamlaka ya Serikali za Mtandao, Taasisi ya Uongozi, Wakala wa Ndege za Serikali na Baraza la Kumshauri Rais kuhusu Masuala ya Chakula na Kilimo imepanga kutekeleza shughuli mbalimbali kama zinavyoonekana kwenye ukurasa wa 75 hadi 88, baadhi ya shughuli ni pamoja na kutoa ushauri wa Mheshimiwa Rais katika masuala kama ni sehemu ya uchumi, siasa, jamii, sheria, diplomasia na mambo yote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kuhawilisha ruzuku kwa kaya maskini 906,669 zinazokidhi vigezo vya Mpango. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma: Fungu 33 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni16.9 Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni13.95 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 3,000,000,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kupitia maombi haya, ofisi hii imepanga kutekeleza shughuli mbalimbali kama zinavyoonekana kwenye ukurasa wa 89 hadi 90. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Fungu 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 75.8 kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 55.08 sawa na 73.6% ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 19.755 sawa na 26.4% kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kupitia maombi hayo, ofisi hii imepanga kutekeleza shughuli mbalimbali kama zinavyoonekana kwenye ukurasa wa 91 hadi wa 100, baadhi ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kushughulikia vibali 41,500 vya ajira ili kujaza nafasi zilizoidhinishwa katika ikama.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Fungu 67 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 14.6 Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 13.195 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 1.4 ni fedha za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kupitia maombi haya ofisi imepanga kutekeleza shughuli mbalimbali kama inavyoonekana kwenye ukurasa wa 101 hadi 102 na baadhi ya shughuli ni kuendeleza ujazaji wa nafasi za ajira kulingana na vibali vya ajira, lakini kuendelea na maboresho ya mfumo wa upimaji wa uelewa na ufahamu wa wasailiwa kwa njia ya mtandao *(online aptitude test system)* ili kupunguza gharama za waombaji.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma Fungu 94, inaomba kuidhinishiwa kiasi shilingi bilioni 9.6 ili kutekeleza fedha zilizotajwa hapo juu. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 9.177ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi milioni 500.176 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kupitia maombi haya, ofisi hii imepanga kutekeleza shughuli mbalimbali kama inavyoonekana kwenye ukurasa wa 103 hadi 104. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Ofisi ya Rais - Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa Fungu 4, inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 6.150, kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 4. 9 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 1.177 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kupitia maombi hayo, ofisi hii imepanga kutekeleza shughuli mbalimbali kama zinavyoonekana kwenye ukurasa wa 105 hadi 106.

Mheshimiwa Spika, nihitimishe hotuba yangu kwanza kabisa kwa kutoa salamu aliyoiasisi Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan na kusema "Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kazi iendelee" *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa hati idhini, Ofisi ya Rais ikiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeendeleza utekelezaji wa dhamana ya kufanya maamuzi kuhusu nchi na kwa umuhimu wake Menejimenti ya Utumishi wa Umma na utawala bora imepewa kipaumbele kwa kuzingatia mkakati wa *4R*, yaani *reconciliation*, *resilience, reforms* na *rebuilding* ambavyo kwa

pamoja inakuwa ni nguzo kuu katika uendeshaji na uendelezaji wa nchi.

Mheshimiwa Spika, maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kuwa na Utumishi wa Umma wenye Ufanisi na Uwajibikaji katika kustawisha Taifa kwa kusimamia uendeshaji wa shughuli za Serikali na usimamizi wa rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma kwa kutumia Sera, Sheria Miundo na mifumo iliyoboreshwa. Ndiyo maana mipango iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu imejikita katika kuweka misingi ya utekelezaji wa mwelekeo huo.

Mheshimiwa Spika, Utumishi wa Umma na utawala bora una mchango mkubwa katika maendeleo ya Taifa na ni dhahiri kuwa mchango endelevu wa watumishi wa umma utaliendeleza Taifa na kuleta ustawi kwa Watanzania wote. Aidha, maendeleo haya yanatarajiwa kuongezeka kwa kuimarisha uchumi shindani na viwanda kwa manufaa ya watu, kama ilivyoasisiwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, imelenga kuandaa mazingira ambayo yatasaidia nchi katika kipindi cha kuelekea kwenye Uchaguzi Mkuu na kuingiza Serikali mpya madarakani. Hayo yote yatafanyika kwa kutii Katiba na kuzingatia ipasavyo Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo katika kujenga imani zaidi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza tena Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutuwezesha kuimarisha utumishi wa umma kuendana na wakati, ambapo maelekezo yake na uwezeshaji kifedha umesaidia hatua zaidi kupigwa kwenye kujenga uwezo na mifumo ya kimenejimenti na utoaji huduma ikiwemo matumizi sahihi na salama ya fursa zinazopatikana katika utoaji huduma kwa TEHAMA ndani ya Serikali. Hali hiyo imesaidia kuondokana na vitendo visivyo na tija katika uzingatiaji wa maadili ya utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Hati Idhini, nawajibika kuwasilisha mapitio ya utekelezaji mipango na bajeti ya Ofisi ya Rais Ikulu; Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma; na Ofisi ya Rais, Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.

Mheshimiwa Spika, hivyo, nalihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Mipango na Bajeti kwa Mafungu niliyoyataja yamezingatia vipaumbele vya Serikali ya Awamu ya Sita kwenye eneo la kuimarisha utendaji kazi katika Utumishi wa Umma na kuifanya nchi yetu iondokane na matumizi mabaya ya rasilimali fedha, ukiukwaji wa maadili ya uongozi na kupunguza urasimu usio na lazima katika utoaji huduma kwa kufanya mapitio ya michakato ya utoaji huduma na hivyo kuongeza tija katika kutekeleza masuala yenye maslahi mapana kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, sasa naomba kuwasilisha rasmi mapendekezo ya maombi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kwa muhtasari kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Fungu 20 - Ofisi ya Rais, Ikulu matumizi ya kawaida ni bilioni 34,804,735,000. Fungu 30 - Ofisi, ya Baraza la Mawaziri, matumizi ya kawaida ni shilingi 1,039,839,675,000. Matumizi ya miradi ya maendeleo ni shilingi 157,773,084,000. Fungu 33 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Matumizi ya kawaida ni shilingi 13,958,139,000, matumizi ya miradi ya maendeleo ni shilingi 3,000,000,000.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Fungu 32, matumizi ya kawaida ni shilingi 55,086,788,000 na matumizi ya miradi ya maendeleo ni shilingi 19,755,541,000. Fungu 67, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; matumizi ya kawaida ni shilingi

13,195,060,000 na matumizi ya miradi ya maendeleo ni shilingi 1,408,828,000.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Fungu 94 - Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma. Matumizi ya kawaida ni shilingi 9,177,599,000 na matumizi ya miradi ya maendeleo ni shilingi 500,176,000.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Fungu Namba 4 - Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa. Matumizi ya kawaida ni shilingi 4,973,241,000 na matumizi ya miradi ya maendeleo ni shilingi 1,177,458,000.

Mheshimiwa Spika, muhtasari wa Mafungu yote unafanya jumla kuu kuwa, matumizi ya kawaida, shilingi 1,171,035,237,000 na matumizi ya miradi ya maendeleo, shilingi 183,315,087,000.

Mheshimiwa Spika, jumla kuu ya fedha inayoombwa katika Mafungu yote ya Ofisi ya Rais Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama nilivyopitia katika jedwali hapo juu ni shilingi 1,354,350,324,000. Kati ya fedha hizo shilingi 1,171,035,337,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 183...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, hebu isome upya hiyo, kati ya fedha hiyo trilioni moja...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, *yes*. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,171,035,237,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 183,315,087,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika na Wabunge wenzangu, mwisho ninaomba kuwasilisha maombi haya ili muweze kuyajadili na kuyaidhinisha ili tuweze kwenda kufanya kazi ya kumalizia miaka yetu mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

## HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE) KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Bunge lako lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka 2024/25 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais: Ikulu (Fungu 20 na 30); Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Fungu 33); Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (Fungu 32); Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (Fungu 67); Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 94); na Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa (Fungu 04) kwa Mwaka 2025/26.

**Mheshimiwa Spika,** Kama ilivyo ada naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na neema kwa kutuwezesha kuwa na afya njema na kuendelea kuijalia nchi yetu amani, utulivu na mshikamano ambazo ni tunu zinazotuwezesha kushiriki katika mkutano huu wa 19 ambao ni mkutano wa mwisho wa Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini kusimamia Utumishi wa Umma kwa kuzingatia misingi ya Utawala Bora, Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali na hatimaye kuwa na Utumishi wa Umma wenye ufanisi na uwajibikaji kwa ustawi wa Taifa.

Aidha, niwashukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kazi kubwa wanayofanya ya kumsaidia Rais, Amiri Jeshi Mkuu na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kutekeleza majukumu yake ya kusukuma maendeleo ya Taifa letu na kuiweka nchi katika hali ya Usalama na Amani. Vilevile, ninawashukuru viongozi wangu wote kwa maelekezo, ushauri na miongozo wanayonipatia ambayo imenisaidia kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kutumia fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa anaelekea kuhitimisha awamu ya kwanza ya kipindi cha uongozi wake. Uongozi wake thabiti unadhihirishwa na maendeleo kwenye nyanja mbalimbali hususan kwenye maboresho makubwa yaliyofanyika katika Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ikiwemo mifumo ya kiutawala na usimamizi wa rasilimaliwatu ya kidijitali. Maboresho hayo yameleta mageuzi ya kiutendaji na utoaji wa huduma katika utumishi wa umma ikiwa ni dalili tosha kuwa nchi ipo katika njia sahihi ya kufikia malengo tuliyojiwekea katika mipango yetu ya kitaifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kipekee nampongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uchapakazi wake mahiri na uzalendo katika kuliletea Taifa letu maendeleo. Aidha, tunamtakia kila la kheri katika majukumu yake mapya baada ya kuamua kupumzika. Tunamuahidi kuendelea kuyaenzi yale yote mazuri aliyoyatekeleza kupitia uongozi wake thabiti. Hakika, mchango wake katika kuendeleza maendeleo na ustawi wa Taifa letu hautosahaulika.

Halikadhalika, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa jitihada zake za dhati za kuboresha utendaji na

kusimamia maendeleo ya Zanzibar katika nyanja za kijamii, kiuchumi, kisiasa na kidiplomasia.

**Mheshimiwa Spika,** Ninapenda nichukue fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) kwa hotuba yake aliyoiwasilisha hapa bungeni ambayo imetoa dira na mwongozo wa utekelezaji wa shughuli za Serikali katika mwaka ujao wa fedha. Aidha, nampongeza kwa kuendelea kusimamia na kuratibu utendaji kazi na uwajibikaji Serikalini ambapo ufuatiliaji wake umetoa mwangwi wa uwajibikaji katika Utumishi wa Umma. Vilevile, nampongeza Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.) kwa kuendelea kumsaidia Waziri Mkuu na kutusimamia sisi mawaziri katika kutekeleza majukumu yetu.

**Mheshimiwa Spika,** naomba Bunge lako tukufu liungane nami katika kumpongeza Komredi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu 2025 naomba tumuombee kwa Mwenyezi Mungu azidi kumjalia uzima na afya njema ili aweze kufikia kipindi cha kulitumikia Taifa katika nafasi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** Nakupongeza kwa dhati wewe binafsi, Naibu Spika Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb.), Wenyeviti wa Bunge, Wenyeviti wote wa Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge pamoja na watendaji wote wa Ofisi yako kwa namna mnavyolisimamia na kuliendesha Bunge letu tukufu kwa weledi na umahiri mkubwa. Juhudi na maarifa yenu yameendelea kuupa heshima Muhimili huu muhimu mbele ya umma wa watanzania na kuwezesha kuisimamia na kuishauri Serikali ipasavyo.

Aidha, ninawapongeza waheshimiwa wabunge wote kwa ujumla kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa miaka hii mitano (5) ya kuwawakilisha wananchi katika Bunge hili.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/25 Bunge lako tukufu limempoteza mwakilishi mwenzetu mmoja ambaye ni Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni, mkoani Dar es Salaam na Mkurugenzi mteule wa Shirika la Afya Duniani Ukanda wa Afrika. Pia kwa masikitiko makubwa, tulimpoteza aliyewahi kuwa Mbunge wa Jimbo la Rorya na Waziri wa Ulinzi, Mhe. Prof. Philemon Mikol Sarungi; na vile vile, aliyewahi kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Frederick Mwita Werema. Naungana na wabunge wenzangu kutoa pole kwa Bunge lako tukufu, familia ya marehemu, ndugu, jamaa, marafiki na wote walioguswa na misiba hii. Aidha naomba kuungana na Watanzania wote kutoa pole kwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa msiba wa Marehemu Mhandisi Gissima Nyamo-hanga, Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO aliyefariki katika ajali ya gari kule Bunda Mkoani Mara, pamoja na dereva wake. Ninapotoa pole naomba kutoa rai kwa viongozi na watumishi wa umma na watanzania wote tujiepushe visababishi vya ajali ambazo zinapoteza rasilimaliwatu muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa. Vilevile, natoa pole kwa waheshimiwa wabunge na wananchi wote waliofiwa na ndugu na wapendwa wao kutokana na maradhi, ajali, majanga na matukio mbalimbali yaliyotokea katika nchi yetu. Tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina!

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Joseph K. Mhagama, Mbunge wa Madaba na Makamu Mwenyekiti Mhe. Florent L. Kyombo, Mbunge wa Nkenge na Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/25 na Mapendekezo ya Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/26. Maoni, ushauri na ushirikiano wa Kamati umetuwezesha kuboresha utendaji kazi wa Ofisi yetu na maandalizi ya hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua nafasi ya namna ya pekee kumshukuru Mheshimiwa George Huruma Mkuchika, Waziri

wa Nchi, Kazi Maalumu kwa namna anavyosaidia utekelezaji wa kazi maalumu za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakika yeye ni hazina na mchango wake umekuwa nguzo muhimu ya maamuzi mengi ya uendeshaji wa shughuli za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa Deus Clement Sangu (Mb.) kwa jinsi anavyonisaidia kwa karibu katika kutekeleza majukumu ya Ofisi yetu kwa uhodari na umakini mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** nawashukuru Dkt. Moses M. Kusiluka, Katibu Mkuu Kiongozi; Bw. Mululi M. Mahendeka, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Ikulu; Bw. Juma S. Mkomi, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Bw. Xavier M. Daudi, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Makamishna, Watendaji Wakuu wa Taasisi; Wakurugenzi na Watumishi wote wa Ofisi ya Rais Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kazi nzuri wanazofanya katika kutekeleza majukumu yanayoiwezesha Ofisi kufikia malengo yake, ikiwa ni pamoja na kukamilisha Hotuba hii kwa wakati. Aidha, napenda kuwashukuru waajiri na watumishi wa umma wote kwa kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi, uzalendo pamoja na imani yao kwa uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita. Utendaji wao umeiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake ya kuwahudumia wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee napenda kuzishukuru Nchi Wahisani na Washirika wa Maendeleo ambao wamechangia jitihada zetu za kuleta maendeleo kwa wananchi. Hivyo, nachukua fursa hii kuwashukuru na kuwataja wachache ambao ni: Jamhuri ya Watu wa China, Japan, Uingereza, India, Jamhuri ya Korea, Canada, Marekani, Sweden, Australia, Umoja wa Ulaya, Denmark, Norway, Uholanzi, Finland, Uswisi, Italia, Malaysia, Misri, Singapore, Cuba, Thailand na Ireland. Vile vile, nayashukuru Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa ambayo ni: Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), OFID-OPEC Fund for International Development, FCDO, KOICA, GIZ, USAID, SIDA, UNDP, Jumuiya ya Madola, DANIDA, JICA, UNICEF,

ILO, WFP, UN Women, Global Fund, Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF) na Taasisi ya Bill and Melinda Gates Foundation.

**Mheshimiwa Spika,** kwa umuhimu wa pekee kabisa ninawashukuru sana wananchi wenzangu wa jimbo la Kibakwe kwa kuendelea kunipa ushirikiano na imani wakati wote ninapoendelea kuwawakilisha kwa kipindi hiki cha miaka mitano (5). Aidha, napenda kuishukuru familia yangu ikiongozwa na mke wangu kipenzi mama Mariana William Naano na watoto wangu kwa kunipa ushirikiano, kuniombea na kuwa wavumilivu katika kipindi chote ninapokuwa katika kutekeleza majukumu ya kitaifa.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa kuwasilisha Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/26.

## MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2024/25

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ina mafungu saba (07) ya kibajeti ambayo ni: Ofisi ya Rais, Ikulu (Fungu 20 na 30); Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Fungu 33); Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (Fungu 32); Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (Fungu 67); Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 94); na Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa (Fungu 04). Utekelezaji wa majukumu kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo:

## OFISI YA RAIS - IKULU NA TAASISI ZAKE

### A. Ofisi ya Rais – Ikulu

**Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka wa fedha 2024/25, Fungu 20 - Ofisi ya Rais, Ikulu iliidhinishiwa **shilingi 33,544,557,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2025 **shilingi 25,292,595,978.47** sawa na **asilimia 75.40** zilipokelewa na kutumika.

**Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka wa fedha 2024/25, Bunge lako Tukufu liliidhinisha **shilingi 969,285,723,000.00** kwa Fungu 30, linalojumuisha Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri; TAKUKURU; TASAF; Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA); Taasisi ya UONGOZI; Wakala ya Ndege za Serikali; na Baraza la Kumshauri Rais kuhusu Masuala ya Chakula na Kilimo. Kati ya fedha hizo, **shilingi 805,676,639,000.00** sawa na **asilimia 83.12** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 163,609,084,000.00** sawa na **asilimia 16.88** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2025 kiasi cha **shilingi 721,515,243,932.00** sawa na **asilimia 74.44** ya bajeti iliyotengwa kilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo **shilingi 611,186,952,300.06** zilikuwa ni Matumizi ya Kawaida na **shilingi 110,328,291,631.94** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika;** katika kipindi hicho, Ofisi ya Rais, Ikulu ilitekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Ushauri kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania umetolewa katika masuala ya Siasa, Uchumi, Jamii, Sheria, Diplomasia, Mawasiliano na Habari, Uhusiano wa Kikanda na Kimataifa, na masuala mengine muhimu kwa lengo la kumsaidia Rais kufanya maamuzi;

(ii) Utekelezaji wa ratiba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kila siku umewezeshwa;

(iii) Huduma zimetolewa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nafamilia yake;

(iv) Mikutano 10 ya Baraza la Mawaziri imefanyika ambapo nyaraka 31 zilijadiliwa na kutolewa uamuzi. Vikao vitano (5) vya Baraza la Mawaziri vilifanyika ambapo miswada 15 ilijadiliwa na kikao cha Kamati ya Maendeleo ya Jamii na Mazingira kilifanyika na nyaraka moja (1) ilijadiliwa.


Mhe. Dkt. S. S. Hassan
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania





*1 - 3: Kikao cha Baraza la Mawaziri cha tarehe 16 Januari 2025, kikiongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Ikulu Chamwino, Mkoani Dodoma.*

Aidha, mikutano minne (4) ya Kamati ya Katiba na Bunge ya Baraza la Mawaziri ilifanyika ambapo miswada 15 ilijadiliwa na kutolewa maoni na ushauri;

(v) Mikutano 16 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) ilifanyika nanyaraka 45 zilichambuliwa na ushauri kutolewa. Aidha, mikutano ya kazi tisa (9) ya Makatibu Wakuu ilifanyika ambapo mada 27 ziliwasilishwa na kujadiliwa;

(vi) Mikutano 23 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ilifanyika ambapo nyaraka 46 zilichambuliwa na kutolewa maoni na ushauri. Aidha, mikutano ya kazi sita (6) ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ilifanyika ambapo taarifa nane (8) zilijadiliwa na kutolewa maoni na ushauri;

(vii) Kumbukumbu za Mikutano ya Baraza la Mawaziri, Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ziliandaliwa na kusambazwa kwa wahusika kwa rejea na hatua za utekelezaji. Aidha, ufuatiliaji na tathmini ya maamuzi ya Baraza la Mawaziri ulifanyika na taarifa kuandaliwa;

(viii) Mafunzo kuhusu maandalizi ya Nyaraka za Baraza la Mawaziri yalitolewakwa baadhi ya watumishi wa Tume ya Taifa ya Mipango, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki;

(ix) Mafunzo ya matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Baraza la Mawaziri (eCabinet) kwa Mawaziri, Makatibu Wakuu na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, waratibu wa shughuli za Baraza la Mawaziri wa wizara (CLOs) na Maafisa TEHAMA wa Wizara yalifanyika;

(x) Mkutano wa Faragha (Retreat) wa mwaka 2024/25 wa Makatibu Wakuu, Makatibu Tawala wa Mikoa na Naibu Makatibu Wakuu ulifanyika;

(xi) Miradi ya kimkakati ya Julius Nyerere Hydro-Electric Power; STAMICO mining plants maeneo ya Kiwira; STAMIGOLD Biharamulo; Buckref Gold Mine; na Lwamgasa Gold Mine ilifanyiwa ufuatiliaji na tathmini na ushauri wa namna bora ya kuiendesha na kuiendeleza ulitolewa;

(xii) Mafunzo ya kujenga uwezo kuhusu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Nne (NACSAP IV) kwa viongozi 989 kutoka katika Taasisi za Umma yalitolewa. Kati yao, 359 ni Wakurugenzi wa Utawala na Rasilimaliwatu, 30 ni Wajumbe wa Kamati Maalum za Menejimenti na 600 ni Wakuu wa Taasisi na Wenyeviti wa Bodi;

(xiii) Vikao viwili (2) vya Waratibu wa Programu za Maboresho vimefanyika ili kuimarisha usimamizi, uongozi na umiliki wa mchakato wa maboresho katika sekta ya umma nchini;

(xiv) Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu Kitaifa yaliratibiwa na kufanyika tarehe 10 Desemba, 2024 yakijumuisha Taasisi za Umma na AZAKI;

(xv) Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa umefanyika katika mikoa ya Iringa, Njombe, Ruvuma, Mtwara na Lindi pamoja na halmashauri za wilaya za Kilolo, Ludewa, Mbinga, Kilwa na Halmashauri ya Mji Nanyamba;

(xvi) Rufaa 225 za watumishi zilipokelewa na kati ya rufaa hizo rufaa 62, zimechambuliwa na kutolewa uamuzi. Aidha, malalamiko 600 yamepokelewa, kuchambuliwa na kutolewa uamuzi/maelekezo;

(xvii) Ujenzi wa jengo la Ofisi (Samia Building) Chamwino umefikia asilimia 19.5, uzio wa kuzunguka jengo la Ofisi ya Chamwino umefikia asilimia 95 na uzio kuzunguka eneo la Mapokezi Chamwino umefikia asilimia 95; na

(xviii) Ujenzi wa jengo la makazi katika Ikulu Ndogo Arusha umefikia asilimia 83 na ukarabati wa jengo la Ofisi na ujenzi wa majengo saidizi katika Ikulu ya Dar es Salaam umefikia asilimia 30.

**B. Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)**

**Mheshimiwa Spika;** Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ina majukumu ya msingi ya: Kuzuia na kupambana na rushwa kwenye sekta ya umma, mashirika na sekta binafsi; kuishauri Serikali kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu rushwa; na kuchunguza tuhuma za makosa ya rushwa kwa kuzingatia Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329.

**Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Machi, 2025, TAKUKURU imetekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Miradi ya maendeleo 1,407 yenye thamani ya shilingi trilioni 2.007 imefuatiliwa na kubaini kuwa miradi 129

yenye thamani ya shilingi bilioni 44.76 ilikuwa na kasoro mbalimbali na kusababisha kuanzishiwa uchunguzi ili hatua stahiki zichukuliwe. Aidha, elimu kuhusu namna bora ya kusimamia miradi imetolewa kwa watekelezaji wa miradi 280 na miradi mingine 668 imefanyiwa udhibiti ili ikamilishwe kama ilivyopangwa kwa mujibu wa mikataba;

(ii) Uchambuzi wa mifumo 460 umefanyika kwa lengo la kubaini mianya ya rushwa katika maeneo ya afya, elimu, maji, ujenzi, huduma za jamii, fedha, mawasiliano, utawala, usafirishaji, biashara, umeme, kilimo na misitu. Kutokana na chambuzi hizi mapendekezo ya kuziba mianya ya rushwa yalitolewa;

(iii) Vikao kazi 294 vya wadau vimefanyika na kazi 112 zimefanyika ili kufuatilia utekelezaji wa mikakati ya kuziba mianya ya rushwa iliyobainishwa katika matokeo ya kazi za utafiti, uchambuzi wa mifumo na ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali za umma katika miradi ya maendeleo;





*1&2: Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa akikabidhi magari kwa Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU Bwana Crispin Chalamila kwa ajili ya ufuatiliaji kwenye maeneo mbalimbali katika kutekeleza majukumu ya kupambana na rushwa.*

(iv) Kupitia Mpango wa TAKUKURU RAFIKI, mikutano 1,088 imefanyika na jumla ya kero 5,697 ziliibuliwa ambapo kati ya kero hizo, 3,127 zimepatiwa ufumbuzi katika sekta za Afya, Elimu, Maji, Nishati, Mawasiliano, Mahakama, Maendeleo ya jamii, Mazingira, Ujenzi, Utawala, Ardhi, Kilimo, Polisi, Usafirishaji, biashara, madini, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, TCRA, TASAF, Misitu na Mifugo, Ulinzi, Utalii, Viwanda na Barabara;

(v) Maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa Barani Afrika yaliyoratibiwa kwa kushirikiana na Mamlaka ya Kuzuia na Rushwa na Uhujumu Uchumi – Zanzibar (ZAECA) yalifanyika Zanzibar tarehe 11 Julai, 2024. Maadhimisho hayo yalijumuisha kurusha vipindi kupitia redio na runinga na mashindano ya michezo mbalimbali yaliyoeneza elimu kuhusu mapambano dhidi ya rushwa;

(vi) TAKUKURU imeendelea kushirikiana na Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) kuingiza maudhui ya kuzuia na kupambana na rushwa katika somo la ‘Historia ya Tanzania na Maadili’ kwa darasa la IV, kidato cha II na cha VI. Aidha, maudhui husika yameingizwa katika somo tajwa kwa darasa la III, kidato cha I na cha V

ambapo uingizaji wa maudhui unafanyika sambamba na uboreshaji wa mitaala ya elimu unaoendelea nchini;

(vii) Klabu 185 za wapinga rushwa zilifunguliwa na 5,474 ziliimarishwa katika shule za msingi, sekondari na vyuo. Vilevile, TAKUKURU imeingia makubaliano ya ushirikiano na Chama cha Skauti Tanzania na Tanzania Girl Guides Association (TGGA) kwa lengo la kuwaelimisha vijana wa skauti kuhusu kuzuia na kupambana na rushwa;

(viii) Elimu ya utambuzi wa haki na wajibu wa namna ya kutoa taarifa za vitendo vya rushwa imetolewa kwa wadau mbalimbali wa kupambana na rushwa wakiwemo viongozi na watumishi wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, watumishi wa sekta binafsi, wanachama wa vyama vya ushirika, wanafunzi wa shule za msingi, sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu, viongozi na waumini wa dini, viongozi na wanachama wa vyama vya siasa na wananchi kwa ujumla. Elimu hiyo imetolewa kupitia semina 3,817 na mikutano ya hadhara na mijadala ya wazi 3,436;

(ix) TAKUKURU imeshirikiana na vyombo vya habari na imetumia mitandao ya kijamii kuhabarisha na kuelimisha umma kuhusu mapambano dhidi ya rushwa, ambapo vipindi 558 vya redio na televisheni vimerushwa, makala za video 66 zimeandaliwa na kurushwa kupitia televisheni mtandao ya TAKUKURU TV. Aidha, matangazo 23 yameandaliwa na kusambazwa kupitia vituo vya redio, televisheni na mitandao ya kijamii;

(x) Uelimishaji wakati wa Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2024 umefanyika katika halmashauri zote za Tanzania Bara ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kusimamia miradi ya maendeleo na kushiriki uchaguzi wa Serikali za mitaa pasipo kujihusisha na vitendo vya rushwa;

(xi) Katika kipindi cha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024, TAKUKURU ilipata fursa ya kutumia huduma ya "bulk SMS" kusambaza ujumbe wa kuhamasisha wananchi kuzuia vitendo vya rushwa katika uchaguzi. Aidha, TAKUKURU iliendesha semina kwa viongozi wa dini, wahariri wa vyombo vya habari, wadau wa taasisi zisizo za kiserikali na asasi za kiraia na wajumbe wa Baraza la Vyama vya Siasa ili kuimarisha ushiriki wao katika kudhibiti vitendo vya rushwa katika uchaguzi;

(xii) Makala maalum zimeandaliwa kuhusu mafanikio ya utekelezaji wa Programu ya TAKUKURU - Rafiki katika Mikoa 13 ambayo ni Mwanza, Mara, Shinyanga, Geita, Arusha, Singida, Simiyu, Tanga, Dodoma, Kagera, Kigoma, Manyara na Kilimanjaro. Aidha, Makala hizo zilirushwa kupitia TAKUKURU TV kwa lengo la kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu Programu hii na kuhamasisha ushiriki wa wadau katika kuzuia vitendo vya rushwa. Pia, Programu ya TAKUKURU - Rafiki ilifanyika katika wilaya mbili za Temeke na Kinondoni;

(xiii) TAKUKURU imeshiriki maonesho mbalimbali ya kitaifa yanayojumuisha Wiki ya Sheria, Sabasaba, Nanenane, Madini, Wiki ya Vijana na Mbio za Mwenge wa Uhuru;

(xiv) Kesi 867 ziliendeshwa mahakamani zikiwemo kesi mpya 461. Kati ya kesi mpya zilizofunguliwa mahakamani 10 ni kesi kubwa ambazo zilifunguliwa katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi. Kesi 451 ziliamuliwa mahakamani ambapo Jamhuri ilishinda kesi 352 kwa watuhumiwa kuhukumiwa kifungo au/na kulipa faini ikiwa ni asilimia 76.4. Aidha, hadi kufikia Machi, 2025 kesi 416 zilikuwa zinaendelea mahakamani. Vilevile, kiasi cha shilingi bilioni 9.01 na USD 620,000 zimeokolewa kutokana na operesheni mbalimbali za uchunguzi uliofanyika kote nchini ambapo shilingi bilioni 6.01 ni fedha taslimu

zilizorejeshwa serikalini na shilingi bilioni 3.00 na USD 620,000 zilidhibitiwa na kurejeshwa katika miradi mbalimbali ya Serikali na kwa walalamikaji wa Sekta binafsi; na

(xv) Ujenzi wa majengo ya Ofisi za TAKUKURU katika Mkoa wa Iringa na Wilaya za Nzega, Kishapu, Monduli na Rombo umekamilika. Aidha, Ujenzi katika maeneo mengine 17 unaendelea na hatua ya utekelezaji ipo kama ilivyooneshwa kwenye kiambatisho Na 2.




*Mwonekano wa Jengo la TAKUKURU Wilayani Rombo.*

### C. Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

**Mheshimiwa Spika;** Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) pamoja na majukumu mengine una majukumu ya msingi ya kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato, kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii, na kujenga ari ya uwajibikaji.

**Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Machi, 2025; Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) Awamu ya Tatu umetekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Uhakiki ulifanyika na kubaini kuwa Kaya 394,505 zimeimarika kiuchumi na zinaweza kuendesha maisha

kwa kujitegemea bila uhitaji wa ruzuku ya Mpango na zilihitimishwa mwezi Julai, 2024. Aidha, kufikia Machi, 2025 Kaya 906,669 zenye hali duni ya kiuchumi zimeendelea kuwepo kwenye Mpango;

(ii) Ruzuku ya shilingi bilioni 162 ilihawilishwa kwa kaya za walengwa 906,669 zenye jumla ya wanakaya 3,769,582 ili waweze kujikimu na mahitaji ya msingi. Wanakaya hao ni kutoka katika maeneo 186 ya utekelezaji wa Mpango kwa Tanzania Bara, na Unguja na Pemba kwa Zanzibar;

(iii) Jumla ya miradi 4,920 ya ajira za muda iliibuliwa na jamii na kutekelezwa katika maeneo ya utekelezaji 63 ambapo kaya za Walengwa 227,198 zilishiriki kutekeleza na jumla ya shilingi bilioni 23.7 zimetumika kununulia vifaa na shughuli za awali za maandalizi ya utekelezaji miradi hiyo;

(iv) Miradi 181 ya kuendeleza miundombinu iliibuliwa na utekelezaji wake upo katika hatua mbalimbali katika sekta ya elimu, afya, maji, mazingira, barabara za vijijini na ujasiriamali. Jumla ya shilingi bilioni 17.1 zimetumika katika utekelezaji wa miradi hiyo;


1
SMZ
TASAF
DAHALIA YA WANAFUNZI
SKULI YA KIZIMKAZI DIMBANI


2





*1.Mwonekano wa Dahalia ya kisasa ya wanafunzi wa Skuli ya Kizimkazi Dimbani, Unguja*

*2. Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Utawala, Katiba na Sheria wakiwa kwenye daraja jipya lililojengwa kwa ufadhili wa TASAF huku wakiangalia daraja lililokuwa likitumika zamani na wananchi wa kijiji cha Samanga*

*3. Jengo jipya la shule ya sekondari Magila, Muheza mkoani Tanga lililojengwa kwa ufadhili wa TASAF.*

*4. Jengo la zamani ya shule ya sekondari Magila, Muheza mkoani Tanga.*

(v) Jumla ya vikundi 8,019 vyenye wanachama 68,717 katika Mamlaka 44 za Maeneo ya Utekelezaji Tanzania Bara vimeundwa. Aidha, Walengwa 16,257 kutoka kwenye maeneo ya utekelezaji 27 wamepewa ruzuku ya uzalishaji yenye thamani ya shilingi bilioni 5.5 ili waweze kuanzisha shughuli za kiuchumi;

(vi) Walengwa 443,025 sawa na asilimia 48.86 ya walengwa wote walilipwa kwa njia ya kielektroniki kwa malipo ya kipindi cha Novemba – Disemba, 2024 yaliyofanyika mwezi Januari 2025 ambapo asilimia 56.9 walilipwa kupitia Benki na asilimia 43.1 walilipwa kwa njia ya mitandao ya simu. Zaidi ya shilingi bilioni 15.6 zililipwa kwa walengwa hao katika kipindi hicho cha malipo. Katika kuongeza uwazi na uwajibikaji mfumo umewezeshwa kutuma muhtasari wa taarifa za malipo

kwa njia ya simu kwa viongozi wa Vijiji/Mitaa/Shehia kabla ya siku ya malipo;

(vii) Mapitio ya pamoja baina ya Timu ya Serikali na Wadau wa Maendeleokuhusu utekelezaji wa Mpango yamefanyika katika kipindi cha Julai, 2024 na Januari 2025. Aidha, Wadau wa Maendeleo na walengwa walionesha kuridhishwa na namna Serikali inavyotekeleza kwa ufanisi shughuli za Mpango; na

(viii) Usanifu na maandalizi ya awamu inayofuata ya utekelezaji wa Mpango yamefanyika kwa ushirikiano wa Serikali na Wadau wa Maendeleo.

**D. Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)**

**Mheshimiwa Spika;** Mamlaka ya Serikali Mtandao ina jukumu la la kuratibu, kusimamia na kukuza matumizi ya Serikali mtandao katika utumishi wa umma.

**Mheshimiwa Spika;** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Mamlaka ya Serikali Mtandao imetekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Tathmini ya usalama wa mifumo ya TEHAMA inayopatikana mtandaoni imefanyika kwa Taasisi za Umma 395 ili kuhakikisha kuwa Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA Serikalini inafanya kazi kwa ufanisi na kutoa huduma bora na salama kwa wananchi wakati wote;

(ii) Mpango wa kujenga mifumo mipya ya Kisekta kwa Taasisi zenye taratibu za utendaji kazi zinazofanana umefanyika kwa lengo la kupunguza wingi wa Mifumo ya TEHAMA Serikalini ambapo e-GA kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha inaendelea na ujenzi wa Mfumo Jumuishi wa Utoaji wa Ankara (Universal Billing System). Mfumo huu utaongeza ufanisi na uthibiti wa makusanyo ya Serikali pamoja na kupunguza idadi ya mifumo ya kutolea ankara;

(iii) Mifumo 215 kutoka kwenye Taasisi za Umma 182 imewezeshwa kubadilishana taarifa kupitia Mfumo wa GovESB ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi katika Taasisi za Umma, na utoaji wa huduma bora kwa wananchi;

(iv) Tathmini ya kina ya uzingatiwaji wa viwango na miongozo ya usalama wa Serikali mtandao katika mifumo na Miundombinu ya TEHAMA (Compliance and Security Assessment) imefanyika kwa Taasisi za Umma 62;

(v) Tathmini ya usalama wa mifumo ya TEHAMA 112 imefanyika ili kujiridhisha kuhusu hali ya usalama wa mifumo hiyo kabla ya kuhifadhiwa katika vituo vya kuhifadhi taarifa vya Serikali na kuruhusiwa kuanza au kuendelea kutoa huduma kwa wananchi. Aidha, doria ya kimtandao ya saa 24 kwa kila siku (24/7) kwa mifumo na miundombinu ya TEHAMA ya Serikali (Monitoring of Government ICT Systems and Infrastructure) zimefanyika kwenye mifumo yote iliyohifadhiwa kwenye vituo vya Serikali vya kuhifadhi taarifa;

(vi) Mafunzo ya usalama wa mtandao ili kuzijengea uwezo wa kujilinda na mashambulizi ya kimtandao yametolewa kwa taasisi za umma 208;

(vii) Mifumo Jumuishi/shirikishi ya TEHAMA ya kutolea huduma imeboreshwa ili kuendana na mahitaji mapya, maendeleo ya teknolojia na kuhakikisha mifumo hiyo inafanya kazi muda wote. Baadhi ya mifumo iliyofanyiwa maboresho ni pamoja na: Mfumo wa e-Mrejesho; Mfumo Shirikishi wa Kusimamia Shughuli na Rasilimali za Taasisi – ERMS; Mfumo wa Kuwezesha Mifumo ya TEHAMA Kuwasiliana na Kubadilishana Taarifa – GovESB; na Mfumo wa Barua Pepe Serikalini– GMS;

(viii) Utafiti na ubunifu wa matumizi ya teknolojia mpya za TEHAMA zinazoibuka umefanyika ili kuibua huduma mpya kwa umma na kuwezesha kuwa na matumizi

sahihi ya teknolojia mpya. Maeneo husika ni Internert of Things (IoT), Artificial Intelligence (AI), Machine Learning (ML), Blockchain, Cybersecurity na Augumented Reality/Virtual Reality (AR/VR). Aidha, katika kukuza uwezo wa vijana wa kitanzania, Serekali kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao imeendelea kuwajengea uwezo kwenye teknolojia mpya kwa kuwawezesha kuandaa kwa vitendo, kubuni na kutengeneza masuluhisho ya matatizo mbalimbali;

(ix) Mradi wa upanuzi wa Mtandao wa Mawasiliano Serikalini (Government Network - GovNet) kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijitali (DTP) umetekelezwa ili kufikisha mawasiliano katika ngazi ya Halmashauri. Kupitia mradi huo, wakandarasi wanaendelea kusanikisha vifaa katika vituo vya kuungia taasisi za umma kwa ngazi ya Mikoa na Wilaya za Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na Mbeya;

(x) Mapitio ya ufanisi wa Mifumo ya TEHAMA katika Taasisi za Umma 55 yamefanyika ili kuhakikisha imetengenezwa na inatumika kulingana na matakwa ya Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao. Miongoni mwa Mifumo hiyo, ni GOTHOMIS na TAUSI ya OR-TAMISEMI, SGR Ticketing System ya Shirika la Reli Tanzania (TRC), Student Records Management System ya Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Mining Cadastre Information Management System (FLEXICADASTRE) na Mining Data Information Management System (MDIMS) ya Tume ya Madini, Project Management System (PMS) wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), na e-Paper, Billing na Circulation ya Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN);

(xi) Maboresho yamefanyika kwa miundombinu shirikishi ya TEHAMA inayotumiwa na taasisi za umma kwa pamoja ili kuongeza uwezo wa miundombinu, usalama wa taarifa na data zinazohifadhiwa au kupita katika mindombinu hiyo;

(xii) Watumishi wa umma 275 kutoka taasisi za umma 68 wamepatiwa mafunzo ya usimamizi na uendeshaji wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA. Aidha, taasisi za umma 83 zilipatiwa mafunzo kuhusu usimamizi wa usalama wa TEHAMA, na wakaguzi wa ndani kutoka kwenye taasisi za umma 368 walipatiwa mafunzo ya kuwawezesha kukagua maeneo mbalimbali ya TEHAMA katika taasisi zao; na

(xiii) Taasisi za umma 533 zimepewa ushauri wa kitaalam kwenye maeneo ya TEHAMA na taasisi za umma 98 zimepewa ushauri wa kitaalam kuhusu ujenzi wa mifumo ya TEHAMA ili kuhakikisha kunakuwepo uzingatiwaji wa viwango na miongozo kwenye matumizi ya TEHAMA serikalini.







1. *Makamu wa Rais, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, akifungua kikao kazi cha 5 cha Serikali Mtandao Jijini Arusha*
2. *Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene akizungumza katika kikao kazi cha 5 cha Serikali Mtandao Jijini Arusha.*
3. *Sehemu ya Washiriki wa kikao kazi cha 5 cha Serikali Mtandao kilichofanyika jijini Arusha.*

## E. Taasisi ya UONGOZI

**Mheshimiwa Spika;** Taasisi ya UONGOZI ina jukumu la kukuza na kuendeleza uongozi bora kwa maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii barani Afrika. Walengwa ni Viongozi Waandamizi waliopo na wanaojitokeza wakiwemo wanasiasa, watumishi wa Serikali na Mahakama.

**Mheshimiwa Spika;** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Taasisi ya UONGOZI imetekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Mafunzo ya Stashahada ya Uzamili ya Uongozi yametolewa kwa Maafisa Waandamizi 39 kutoka Wizara, Taasisi na Mashirika ya Umma, Taasisi za Kiraia na Taasisi Binafsi, ambapo Moduli saba (7) zilitolewa kama ilivyopangwa. Moduli hizo zilihusu Ujuzi wa Fedha kwa Wasimamizi, Kuongoza kwa Matokeo, Mbinu za Ubunifu kwa Maendeleo ya Shirika, Maendeleo Endelevu, Uongozi wa Kimaadili Mawasiliano ya Kimkakati naUsimamizi wa Rasilimaliwatu Kimkakati;

(ii) Mafunzo ya Uongozi kwa ngazi ya cheti yametolewa kwa njia ya mtandao kwa viongozi 69 kutoka Wizara, Taasisi na Mashirika ya Umma, Taasisi za kiraia na Taasisi Binafsi. Jumla ya moduli nne (4) zilitolewa kwa washiriki juu ya Misingi ya Ufahamu wa Kihisia, Misingi ya Kuongoza Mabadiliko, Matumizi ya Takwimu na uchambuzi katika Uongozi pamoja na Usimamizi wa Rasilimali Fedha;

(iii) Programu maalumu ya kujenga uwezo kwa viongozi wanawake 100 kutoka Taasisi za Umma, Taasisi Binafsi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ilitekelezwa. Aidha, baadhi ya washiriki walitoka nje ya nchi zikiwemo; Ethiopia, Zambia, Cameroon, Malawi, Msumbiji, Kenya, Afrika Kusini, Botswana na Uganda. Programu inalenga kuchangia jitihada za kitaifa katika kushughulikia suala la uwakilishi mdogo wa wanawake katika nafasi za juu za maamuzi serikalini, kwenye siasa, biashara na taasisi za kiraia;







1. *Katibu Mkuu Kiongozi, Bal. Dkt. Moses M. Kusiluka, akifungua mafunzo ya uongozi kwa Wenyeviti wa Bodi za Ushauri na Wakuu wa Vyuo Vikuu Tanzania, Septemba 2024.*

2. *Mwenyekiti wa Taasisi ya Pemandu na Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sunway - Malaysia, Prof. Dato Sri Idris Jala, akiwasilisha mada kuu (kwa njia ya mtandao) katika mafunzo ya uongozi kwa Wenyeviti wa Bodi za Ushauri na Wakuu wa Vyuo Vikuu Tanzania, Septemba 2024.*

(iv) Kozi 28 za muda mfupi zimetolewa kwa viongozi 996, miongoni mwaviongozi hao, 95 ni wakuu wa taasisi na mashirika ya umma. Viongozi hao walipatiwa mbinu na mikakati madhubuti ya kuongoza mashirika katika kuleta mageuzi makubwa ya kiuchumi na kiutendaji;

(v) Wakurugenzi 459 wa Bodi za Taasisi na Mashirika ya Umma 42 walipatiwamafunzo ya kuongeza ufanisi katika utendaji kazi katika nyanja za uongozi wa kimkakati, usimamizi wa rasilimali za umma. usimamizi warasilimaliwatu, na usimamizi wa viashiria hatarishi;

(vi) Utafiti kuhusu mchango wa viongozi wanawake kwenye maendeleo ya Taifa umekamilishwa. Utafirti katika maeneo matano (5) unaendelezwa katika maeneo yafuatayo: Uendelezaji wa Viongozi Nchini; Mfumo wa Utawala katika Kukuza Ustahimilivu Dhidi ya Mabadiliko ya Tabianchi Zanzibar; Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Maji kwa Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi Zanzibar; Ukuaji wa Miji ya Kijani Nchini Tanzania; na Matumizi ya Nishati Safi za Kupikia;

(vii) Kitabu kinachoelezea wasifu wa Hayati Edward Moringe Sokoine aliyekuwa Waziri Mkuu katika awamu ya kwanza ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kilichapishwa na kuzinduliwa rasmi na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, uandishi wa Tawasifu ya Hayati Rashid Mfaume Kawawa uko katika hatua ya ukusanyaji taarifa;

(viii) Jumla ya makongamano manne (4) yaliyokuwa na ushiriki wa viongozi 1,656 yaliandaliwa kwa kushirikiana na taasisi za ndani na nje ya nchi. Makongamano haya yalifanyika kwa lengo la kubadilishana taarifa, maarifa na uzoefu na kuwaongezea uelewa wa masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu;

(ix) Kipindi kimoja cha mahojiano na Bi. Itumeleng Dlamini, Mshauri wa Utawala Bora katika Mpango wa Mapitio ya Maridhiano ya Afrika (APRM) wa Umoja wa Afrika, kuhusu mada ya "Kukuza Uongozi Wenye Kuleta Mabadiliko Barani Afrika," kiliandaliwa na kufanyika;

(x) Ushauri wa kitaalam umetolewa kwa Taasisi nne (4) za Serikali ambazo ni Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, na Ofisi ya Waziri Mkuu, kuhusu kuandaa mwongozo wa ujumuishaji wa jinsia katika sekta za umma, kutathmini utendaji wa Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim, na kuimarisha masuala ya ufuatiliaji na tathmini ndani ya Serikali; na

(xi) Taarifa tatu (3) za tafiti tumizi zimeandaliwa na kuchapishwa na zilihusu Masuala ya Madini ya Kimkakati Nchini, Mchango wa Uwekezaji Kutoka Nje Kwenye Sekta ya Viwanda Nchini, na Fursa ya Biashara ya Kaboni Tanzania.









1. *Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akizindua kitabu cha Hayati Sokoine. Kulia kwake ni Bal. Joseph Sokoine, Mtoto wa Hayati Sokoine ambaye ni Balozi wa Tanzania nchini Canada.*

2. *Baadhi ya viongozi wakifuatilia tukio la uzinduzi wa kitabu cha Sokoine. Kutoka kushoto kwenda kulia: Mhe. Albert Chalamila, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam; Mhe. George Simbachawene (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Bal. Joseph Sokoine, Mtoto wa Hayati Sokoine ambaye ni Balozi wa Tanzania nchini Canada; Mhe. Jakaya Kikwete, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mhe. Joseph Warioba, Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*

3. *Kutoka kushoto kwenda kulia: Bal. Joseph Sokoine, Mtoto wa Hayati Sokoine ambaye ni Balozi wa Tanzania nchini Canada; Mama Nekiteto Sokoine, Mke wa Pili wa Hayati Sokoine; Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mama Napono Sokoine, Mke wa Kwanza wa Hayati Sokoine; na Namelok Sokoine, Mtoto wa Hayati Sokoine.*

## F. Wakala wa Ndege za Serikali

**Mheshimiwa Spika;** Wakala ya Ndege za Serikali ina majukumu ya: Kutoa huduma ya usafiri wa anga kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Viongozi wengine Wakuu wa Kitaifa; kuratibu kwa niaba ya Serikali ununuzi wa

ndege; kukodisha ndege kwa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL); na kusimamia mikataba ya ukodishwaji wa ndege.

**Mheshimiwa Spika;** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Wakala ya Ndege za Serikali imetekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Huduma ya usafiri wa anga kwa viongozi wakuu wa Kitaifa imeendeleakutolewa;

(ii) Ununuzi wa ndege mpya moja ya kibiashara umeratibiwa kwa niaba ya Serikali na mikataba ya ukodishwaji wa ndege za Serikali kwa Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL) imesimamiwa;

(iii) Gharama za bima za ndege pamoja na bima za Wanaanga 41 zimelipwa;

(iv) Wanaanga 41 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi ili kuhuisha leseni zao; na

(v) Ukarabati na upanuzi wa Karakana ya Ndege za Serikali iliyopo katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere - Terminal I umefikia asilimia 75.

**G. Baraza la Kumshauri Rais Kuhusu Masuala ya Chakula na Kilimo**

**Mheshimiwa Spika;** Baraza la Kumshauri Rais kuhusu Masuala ya Chakula na Kilimo (*Presidential Food and Agriculture Delivery Council*) linajukumu la kumshauri Rais kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu chakula na kilimo.

**Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Baraza la Kumshauri Rais kuhusu Masuala ya Chakula na Kilimo limetekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Taarifa za msingi (baseline information or commodity profiles) za mazao ya kipaumbele katika Food and

Agriculture Delivery Compact ambazo zinaweka msingi wa ufuatiliaji wa maendeleo katika mazao ya ngano, alizeti, parachichi, nyama (red meat) na maziwa zimeandaliwa;

(ii) Ufuatiliaji wa upatikanaji wa fedha kutoka AGRA kwa ajili ya kujenga uwezo wa Baraza na Agriculture Transformation Office (ATO) umefanyika na kiasi cha dola za Marekani 1,000,000 kimepatikana;

(iii) Mikutano na mashauriano yamefanyika na wadau kuhusu namna bora ya kuendeleza na kufanya mageuzi katika kilimo kupitia fursa ya Baraza kushiriki katika Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo yaliyofanyika Jijini Dodoma na Maonesho ya Kilimo ya Kanda ya Mashariki yaliyofanyika Morogoro kuanzia tarehe 1 - 8 Agosti, 2024;

(iv) Baraza limefanya majadiliano na Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) kuhusu namna ya kuwezesha majukumu ya Baraza pamoja na upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa malengo yaliyoainishwa katika Food and Agriculture Delivery Compact;

(v) Baraza lilishiriki Mkutano wa Jukwaa la Kimataifa la Masuala ya Mifumo ya Chakula (Agri-Food System Summit) uliofanyika Kigali, Rwanda kuanzia tarehe 5-8 Septemba, 2024. Baraza lilitumia fursa hiyo kupata uzoefu wa nchi nyingine duniani zinavyoweza kuimarisha upatikanaji wa chakula na kufanya mageuzi katika kilimo;

(vi) Baraza lilifanya Mkutano Maalum Septemba 2024. Mkutano huo ulitoa taarifa za Mkutano wa Agri Food Systems Summit uliofanyika Kigali, Rwanda na juhudi zilizopo za kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali ikiwemo The Gates Foundation na Umoja wa Ulaya kwa

ajili ya kuimarisha mifumo ya chakula na kilimo nchini Tanzania;

(vii) Baraza lilishiriki katika mkutano wa Programu iitwayo *"Youth Enterpreneurship for the Future of Food and Agriculture – YEFFA"* ulioandaliwa na AGRA. Mkutano huo ulishirikisha nchi mbalimbali Barani Afrika na kuongeza wigo wa kujifunza namna ambavyo nchi nyingine za Afrika zinavyoshirikisha vijana katika kilimo na fursa za upatikanaji wa fedha kupitia Mastercard Foundation. Mkutano huo ni mwendelezo wa Mkutano wa uzinduzi wa Programu ya YEFFA ambao utachangia kuongeza ajira zenye staha zinazokadiriwa kufikia 261,000 kwa vijana na hasa vijana wa kike;



*Waziri Mkuu Mstaafu na Mwenyekiti wa Baraza la Kumshauri Rais Kuhusu Masuala ya Chakula na Kilimo, Mhe. Mizengo Pinda, akitoa hotuba katika Maonesho ya Kilimo ya Kanda ya Mashariki yaliyofanyika Morogoro, Agosti, 2024.*

(viii) Baraza lilishiriki Mkutano wa Kilele wa Nchi 25 za Afrika zinazozalisha kahawa uliofanyika Jijini Dar es Salaam tarehe 21 - 22 Februari, 2025. Katika Mkutano huo, Baraza lilipata nafasi ya kujifunza kuhusu ubunifu wa namna ambayo mazingira yanaandaliwa katika kushirikisha vijana kwenye uzalishaji wa kahawa katika Halmashauri ya Muleba, Mkoa wa Kagera; na

(ix) Baraza lilishiriki Mkutano wa Wadau wa Parachichi uliofanyika Januari, 2025 katika Mkoa wa Njombe uliolenga kujadiliana fursa, mikakati na changamoto zilizopo katika tasnia hiyo inayokuwa kwa kasi na kuchangia mapato ya wakulima na kuongeza mauzo nje ya nchi.

**OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA**

**Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka wa fedha 2024/25, Bunge lako tukufu liliidhinisha **shilingi 13,142,650,000.00** kwa Fungu 33 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Kati ya fedha hizo, **shilingi 11,642,650,000.00** sawa na **asilimia 88.59** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 1,500,000,000.00** sawa na **asilimia 11.41** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2025 kiasi cha **shilingi 9,247,385,780.58** sawa na **asilimia 70.36** ya bajeti iliyotengwa kilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo **shilingi 8,528,815,348.98** zilikuwa ni Matumizi ya Kawaida na **shilingi 718,570,431.60** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi kufikia Machi, 2025 Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imetekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Tamko la Rasilimali na Madeni kupitia Njia ya Mtandao (Online Declaration System) ya Viongozi wa Umma 15,903 yalipokelewa. Kati ya matamko hayo, 15,480 sawa na asilimia 98 yalirejeshwa ndani ya muda uliopangwa kisheria na matamko 423 sawa na asilimia 2 hayakurejeshwa na hatua kwa mujibu wa sheria zinachukuliwa;

(ii) Zoezi la uhakiki wa taarifa za Mfumo baada ya matokeo ya awali limefanyika na linaendelea ili kupata takwimu halisi za wale ambao hawakurejesha taarifa zao mwaka 2024/25 kutokana na changamoto za

mfumo zilizojitokeza zikiwemo: Baadhi ya Viongozi kujisajili zaidi ya mara mbili; kuchagua vyeo na nyadhifa tofauti na walizonazo; kutumia namba ya simuzaidi ya moja; kuwatumia watu ambao sio Viongozi (Rafiki, Ndugu) kuwasaidia kujaza Tamko na kusahau kutumia namba zao za simu; na kuchanganya katika kuchagua aina ya Tamko badala ya lile la mwaka na Viongozi wengine kuchagua Tamko la cheo kipya au lile la mwisho wa uongozi;

(iii) Malalamiko 85 ya ukiukwaji wa maadili dhidi ya Viongozi wa Umma yalipokelewa na kuchambuliwa. Kati ya malalamiko hayo, malalamiko 60 yalihusu sheria ya maadili ya viongozi wa umma na malalamiko 25 hayakuhusu sheria ya maadili ya viongozi wa umma hivyo yalipelekwa kwa taasisi husika. Aidha, kwa malalamiko yanayohusu sheria ya maadili ya viongozi wa umma asilimia 80 yake, uchunguzi umekamilika na asilimia 20 uchunguzi unaendelea;

(iv) Uhakiki wa matamko ya Rasilimali na Madeni ya viongozi wa umma pamoja na utambuzi wa Mgongano wa Maslahi kwa viongozi wa Umma ulifanyika kwa viongozi 224 katika Mikoa ya Arusha, Dodoma, Geita, Mwanza, Dar es salaam, Kigoma, Shinyanga, Tanga, Mtwara, Mbeya na Songwe. Matokeo ya uhakiki yanaonesha kuwa asilimia 15 wamebainika kuwa na kasoro katika matamko yao. Hatua mbalimbali zimechukuliwa kwa viongozi wenye kasoro ikijumuisha kurekebisha kasoro husika, kufanyiwa uchunguzi wa awali na ambao tuhuma zitathibitika watafikishwa kwenye Baraza la Maadili kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi wa kina;

(v) Elimu ya maadili kwa wadau 19,719 ilitolewa ambapo kati ya hao viongoziwalikuwa 2,642, watumishi 6,511 na wananchi 10,566. Aidha, mafunzo kwa viongozi wa umma yalijikita katika eneo la uwajibikaji wa pamoja. Vilevile, elimu ya maadili ilitolewa kupitia vyombo vya

habari hususan redio na runinga ambapo jumla ya vipindi 165 vya redio na saba (7) vya runinga vilirushwa hewani;

(vi) Makubaliano ya kuwafundisha viongozi na watumishi wa umma kupitia programu za mafunzo zinazotolewa na Chuo cha Uhasibu Arusha yalifanyika kwa lengo la kuimarisha uadilifu na kuwajengea uwezo viongozi kuwa na mwamko wa kufahamu zaidi masuala ya maadili pamoja na kuwajengea mazingira wezeshi wanafunzi ambao ndio viongozi wa baadae;

(vii) Klabu 389 za Maadili katika shule za msingi 241, sekondari 141 na vyuosaba (7) zilianzishwa zikiwa na wanachama 12,000. Aidha, klabu za maadili 236 zilitembelewa kwa lengo la kuziimarisha na kuwajengea uwezo wanachama katika misingi ya uadilifu na kusisitiza katika uzingatiaji wa maadili kwa maendeleo ya taaluma;

(viii) Usimamizi wa utekelezaji wa Kiapo cha Hati ya Ahadi ya Uadilifu kwa viongozi wa Umma umefanyika ikiwa ni pamoja na viongozi wanapopata nyadhifa mpya kusaini hati husika. Viongozi 289 walisaini Hati ya Ahadi ya Uadilifu ambapo kati yao, wanaume ni asilimia 68 na wanawake ni asilimia 32;

(ix) Vikao viwili (2) vya Baraza la Maadili kwa ajili ya kusikiliza malalamiko 10 ya ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa uchunguzi wa kina viliandaliwa na kufanyika hadi kufikia mwezi Machi, 2025; na

(x) Ujenzi wa Jengo la Ofisi za Maadili Makao Makuu Dodoma na ile ya Kandaya Kati umefikia asilimia 99 na Sekretarieti imehamia katika Jengo hilo. Aidha, ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Kanda ya Ziwa Mwanza umefikia asilimia 28.

**OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA NA TAASISI ZAKE**

**Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka wa fedha wa 2024/25, Bunge lako tukufu liliidhinisha **shilingi 58,314,993,000.00** kwa Fungu 32, inayojumuisha Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, Watumishi Housing Investiment (WHI) na Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania. Kati ya fedha hizo, **shilingi 48,254,069,000.00** sawa na **asilimia 82.75** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 10,060,924,000.00** sawa na **asilimia 17.25** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2025 kiasi cha **shilingi 42,707,937,831.31** sawa na **asilimia 73.24** ya bajeti iliyotengwa kilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo **shilingi 37,731,823,831.31** zilikuwa ni Matumizi ya Kawaida na **shilingi 4,976,114,000.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**A. Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

**Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Machi, 2025 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilitekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Maadhimisho ya Mkutano wa Umoja wa Jukwaa la Umoja wa Mataifa la Tuzo za Utumishi wa Umma (*2024 UN Public Service Forum*) yalihudhuriwa ambapo Mfumo wa e-Mrejesho uliotambuliwa na Umoja wa Mataifa na kushinda Tuzo ya Ubunifu katika Huduma za Umma kwa mwaka 2024 (*2024 UN Public Service Innovation Awards*);

(ii) Jumla ya vibali 12,936 vya ajira mpya vimetolewa, ikijumuisha nafasi 11,960 kati ya nafasi 45,000 zilizoidhinishwa kwa Taasisi ambazo hulipwa mishahara kupitia Mfumo wa e-Watumishi na nafasi 976 kwa Taasisi zinazolipa mishahara ya watumishi kupitia mapato yao ya ndani. Aidha, vibali 1,739 vya ajira mbadala vimetolewa kwa waajiri mbalimbali. Maandalizi ya kutekeleza ajira mpya 33,040 zilizosalia

yanaendelea na yanatarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka 2024/25;

(iii) Jumla ya vibali vya utawala wa utumishi wa umma 5,130 vimetolewa. Katiya vibali hivyo: 476 vya uteuzi; 418 vya kukaimu; 455 vya ajira za mikataba; 2,509 vya uhamisho; 477 vya likizo bila malipo; na vibali 795 vya mserereko;

(iv) Mwongozo wa Bajeti ya Mishahara kwa kuzingatia vipaumbele vya Taifa na maandalizi ya Ikama na Bajeti ya Mishahara ya mwaka 2025/26 umeandaliwa na kupelekwa kwa waajiri 433 wanaotumia Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (*e-Watumishi*);

(v) Taarifa 272,097 za kiutumishi na mishahara katika Orodha ya Malipo ya Mishahara (Payroll) zilifanyiwa uchambuzi na kuidhinishwa kupitia Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (e-Watumishi). Uidhinishaji huu unajumuisha taarifa za Ajira Mpya/Mbadala 34,195; Mabadiliko ya Hali ya Kiutumishi 1,206; Usafishaji wa Taarifa (*Data Cleaning*) 20,107; Mabadiliko ya Mishahara 1,912; Mshahara Binafsi 1,142; Uidhinishaji wa Posho 50,649; Kurejeshwa katika Utumishi wa Umma 979; Ubadilishwaji Kada 10,872; na Upandishwaji vyeo 144,883 (Taarifa hizi ni za nafasi zilizokasimiwa katika Ikama na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/24 ambazo utekelezaji wake umefanyika Mwaka wa Fedha 2024/25);

(vi) Madai ya malimbikizo ya mishahara kwa watumishi wa umma 18,755 yenyejumla ya shilingi 22,198,682,580.61 kutoka Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika na Taasisi za Umma yamehakikiwa na kulipwa kwa watumishi stahiki;

(vii) Madai ya malimbikizo ya mishahara kwa watumishi wa umma 1,254 waliokoma utumishi wao kwa

sababu mbalimbali yenye jumla ya shilingi 4,224,800,264.47 kutoka Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa, na taasisi za umma yamehakikiwa, kuidhinishwa, na kulipwa;

(viii) Mafunzo ya matumizi ya Mfumo wa e-Watumishi yamefanyika kwa watumishi wa umma 438 wakiwemo maafisa utumishi 342, wakuu wa idara za utumishi na utawala 18, wakaguzi wa ndani 35 na wahasibu 43 wa taasisi za umma;

(ix) Taasisi za fedha 27 zimeunganishwa kwenye Mfumo wa e-Mikopo, hatua hii imewezesha watumishi wa umma kukopa, kuongeza kiasi cha mkopo (*Loan Top-up*) au kuuza mkopo baina ya taasisi za fedha (*Loan take over*) kwa njia ya kielektroniki;

(x) Dirisha la Watumishi Portal limeboreshwa na kuwezesha watumishi kubadilitaarifa zao za msingi ikiwa ni pamoja na taarifa za wategemezi, kituo cha kazi, elimu na masomo ya kufundishia kwa watumishi wa kada ya ualimu;

(xi) Moduli ya e-Uhamisho imeboreshwa kwa kuwezesha kutoa barua za Vibalivya uhamisho kwa njia ya kidigitali;

(xii) Rasimu ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma, Toleo la Nne laMwaka 2025 imeandaliwa baada ya kufanyiwa mapitio kwa Toleo la Tatu la Kanuni hizo za mwaka 2009. Mapitio yalilenga kujumuisha masuala mbalimbali ya kiutumishi yaliyobadilika, na kurekebisha Kanuni ambazo hazisadifu mazingira ya Utumishi wa Umma wa sasa;

(xiii) Uchambuzi wa Nyaraka 360 za Utumishi za kuanzia mwaka 1957 hadi 2022 umefanyika kwa lengo la kubaini nyaraka zinakidhi mazingira na hali halisi ya

Utumishi wa Umma kwa sasa. Kati ya Nyaraka hizo, 107 zimebainika kufutwa, 220 zimependekezwa kufutwa, 23 zinatakiwa kuendelea kutumika, na 10 zitahuishwa;

(xiv) Ufuatiliaji wa uzingatiwaji wa Sera, Sheria na Kanuni za Utumishi umefanyika katika Mikoa 26 ya Tanzania Bara;

(xv) Wizara na Idara Zinazojitegemea 20 zimewezeshwa kuhuisha Miundo ya Maendeleo ya Utumishi (scheme of service). Aidha, Miundo katika Taasisi na Mashirika ya Umma 20 imehuishwa na kuidhinishwa. Pia, visahihisho na nyongeza za Miundo ya Maendeleo ya Utumishi katika Taasisi na Mashirika ya Umma 60 zimeidhinishwa;

(xvi) Mipango ya Motisha ya taasisi na mashirika ya umma 26 imehuishwa na kuidhinishwa;

(xvii) Maandalizi ya Ikama na Bajeti ya Mishahara kwa Mwaka wa Fedha 2025/26 kwa Waajiri 448 yameratibiwa na kukamilika;

(xviii) Taasisi 46 kati ya 50, ambazo awali hazikuwa kwenye Mfumo wa e-Watumishi, zimewezeshwa na zimeingiza watumishi wao katika mfumo huo;

(xix) Miundo na Mgawanyo wa Majukumu ya Taasisi za Umma 60 imefanyiwa uchambuzi na kufikishwa katika Vikao vitatu (3) vya Kamati ya Rais ya Utekelezaji (Presidential Implementation Committee - PIC). Aidha, miundo ya Taasisi 30 sawa na asilimia 50 imeidhinishwa na Mamlaka kwa ajili ya utekelezaji;

(xx) Maboresho ya Mfumo wa Tathmini ya Mahitaji ya Watumishi (HR Assessment System) yamefanyika na matokeo yake yametumika katika zoezi la uandaaji

wa Bajeti ya Mishahara kwa mwaka wa Fedha 2025/26;

(xxi) Zoezi la kuhakiki na kuingiza huduma katika Daftari la Huduma za Serikali (GSD) limefanyika kwa Taasisi 56, zikiwemo Wizara sita (6) na taasisi zilizo chini yake 50 ambapo jumla ya huduma 1,005 zimeainishwa kwenye Daftari;

(xxii) Uwakilishi wa nchi katika Mikutano saba (7) ya Kikanda na Kimataifa inayohusu masuala ya usimamizi wa rasilimaliwatu na Utawala ulifanyika. Mikutano hiyo inajumisha Mikutano miwili (2) ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC); miwili (2) ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC); na mitatu (3) ya Kamati ya Umoja wa Afrika. Aidha, Mkutano mmoja (1) wa masuala ya Muungano umefanyika Jijini Dodoma;

(xxiii) Ufuatiliaji katika Taasisi za Umma 22 kuhusu uzingatiaji wa ujumuishwaji wa masuala ya Anuai za jamii katika utumishi wa umma na utoaji huduma kwa VVU/UKIMWI, Magonjwa Yasiyoambukizwa (MYA), Jinsia na Ulemavu umefanyika;

(xxiv) Programu ya upimaji wa afya kupitia Tiba Mkoba imefanyika kwa watu wapatao 640 wanaojumuisha watumishi wa Umma, familia zao na wananchi wanaozunguka mji wa Serikali Mtumba kwa kushirikiana na Hospitali ya Rufaa ya Benjamin Mkapa;

(xxv) Taarifa na takwimu za watumishi 2,019 wanaoishi na VVU/UKIMWI na watumishi 5,238 wenye Magonjwa Yasiyoambukiza (MYA) walioweka wazi taarifa zao kwa waajiri zimehuishwa;

(xxvi) Semina elekezi ya utekelezaji wa Mwongozo wa Ujumuishwaji wa Jinsia katika Utumishi wa Umma

(2023) ilitolewa kwa Wakurugenzi wa Utawala na Rasilimaliwatu pamoja na waratibu wa jinsia ngazi ya Wizara kwa washiriki 84 (Wanaume 34 na wanawake 50);

(xxvii) Mafunzo kuhusu utekelezaji wa afua za kudhibiti VVU, UKIMWI na Magonjwa Yasiyoambukiza yalitolewa kwa Makatibu Tawala Wasaidizi (Utawala) kutoka katika mikoa 26 ya Tanzania Bara;

(xxviii) Ujenzi wa uzio wa Klabu ya Viongozi - Makao Makuu Dodoma eneo la Nzuguni umekamilika;



*Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais - UTUMISHI, Bw. Juma Mkomi, akitembelea mabanda ya maonesho kwenye maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma.*

(xxix) Usanifu wa ujenzi wa nyumba ya Rais wa Awamu ya Sita umekamilishwa;

(xxx) Huduma kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa Wastaafu 19 (Viongozi tisa (9) na wajane 10) zimetolewa kwa mujibu wa sheria;

(xxxi) Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliratibiwa ambapo taasisi za umma zilipata fursa ya kutoa elimu kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali. Aidha, huduma za papo kwa papo zilitolewa kwa watumishi, wananchi na wadau;

(xxxii) Taasisi za Umma 525 kati ya 570 sawa na asilimia 91.9 zimepatiwa huduma za usaidizi katika kutekeleza Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma (*e-Utendaji*);

(xxxiii) Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma (*e-Utendaji)* umefanyika katika taasisi za umma 126 kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa mfumo huo katika taasisi husika;




*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa, akifungua Mkutano wa Mtandao wa Wasimamizi na Mameneja wa Rasilimaliwatu Katika Sekta ya Umma Barani Afrika (APS-HRMnet) jijini Arusha.*

(xxxiv) Vikao 10 na wadau vimefanyika kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma (*e-Utendaji*);

(xxxv) Uratibu wa mafunzo kwa watumishi wa umma 1,001 umefanyika, ambapo watumishi 816 walipata ufadhili wa mafunzo ya muda mfupi na 185 walipata ufadhili wa mafunzo ya muda mrefu. Mafunzo ya muda mrefu yalihusisha Shahada za Uzamili na Uzamivu kutoka kwa Serikali ya Jamhuri ya Korea, Serikali ya Japan, Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, Serikali

ya Jamhuri ya India, na Serikali ya Jamhuri ya Thailand;

(xxxvi) Mkutano wa tisa (9) wa Mtandao wa Mameneja Rasilimaliwatu katika Sekta ya Umma Barani Afrika uliratibiwa na Ofisi kwa kushirikiana na Mtandao wa Mameneja Rasilimaliwatu Barani Afrika (APS-HRMnet). Mkutano huo ulihusisha washiriki takribani 767, wakiwemo viongozi wabobezi katika eneo la usimamizi wa Rasilimaliwatu na Menejimenti kutoka Nchi mbalimbali. Mkutano ulitoa fursa ya kujadiliana na kubadilishana uzoefu ili kuwezesha ufanisi katika mazingira ya kazi na kutafuta ufumbuzi wa changamoto mbalimbali za usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Sekta ya Umma BaraniAfrika;

(xxxvii) Taasisi za Umma 24 zimewezeshwa kuandaa na kutekeleza Mipango yaRasilimaliwatu, Mipango ya Mafunzo na Mipango ya Urithishanaji Madaraka;

(xxxviii) Maombi 724 ya vibali vya kazi vyenye msamaha wa ada kwa Wataalamu wa Kigeni yameshughulikiwa. Wataalamu hao wanaofanya kazi kwenye Taasisi za Umma, miradi na programu mbalimbali za kimkakati zenye manufaa katika Utumishi wa Umma;

(xxxix) Nafasi 50 za ajira kutoka Mashirika ya Kikanda na Kimataifa zimeratibiwa na kutangazwa. Mashirika husika yanajumuisha Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Taasisi ya Usimamizi ya Mashariki na Kusini mwa Afrika (ESAMI), Mkutano wa Kimataifa wa Nchi za Maziwa Makuu (ICGLR), Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO);

(xl) Kanzi Data ya Watanzania wenye sifa na nia ya kuajiriwa katika Mashirika ya Kikanda na Kimataifa imetengenezwa ambapo hadi sasa taarifa za watumishi 500 zimehifadhiwa;

(xli) Malalamiko 1,210 kuhusu masuala ya kiutumishi na rasilimaliwatu yatokanayo na ukiukwaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali inayosimamia Utumishi wa Umma yameshughulikiwa;

(xlii) Kampeni za Uhamasishaji wa Uzingatiaji wa Maadili kwa Taasisi za Umma 20 zilizo katika Sekta ya Afya zimefanyika katika Mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma, ambapo jumla ya watumishi 1,539 walifanyiwa mafunzo ya Kanuni za Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma;

(xliii) Uhamasishaji wa Uzingatiaji wa Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma umefanyika kwa kuendesha Mafunzo ya Maadili ya Utendaji kulingana na mahitaji yaliyojitokeza (*Demand Led*) ambapo jumla ya watumishi 2,673 kutoka katika Taasisi za Umma 19 wamepatiwa mafunzo hayo;

(xliv) Usanifu na ujenzi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Maktaba (*POPSM eLibrary*) umeanzishwa. Aidha, Mfumo huo utawezesha wadau kupata huduma mbalimbali za maktaba ikiwemo mchakato mzima wa upatikanaji wa Gazeti la Serikali. Pia, mfumo utawezesha wadau wa Gazeti la Serikali kuwasilisha taarifa zao kwa njia ya kielektroniki na zitahaririwa na kupelekwa kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kielektroniki;

(xlv) Elimu ya Maadili na Ushughulikiaji wa Mrejesho wa Wananchi imetolewa kupitia vyombo mbalimbali vya Habari nchini ikiwemo Redio na Runinga (AZAM, TBC1, ITV na E-FM); na

(xlvi) Fomu ya Hati ya Ahadi ya Uadilifu kwa Watumishi wa Umma (PL Na. 4) imehuishwa ili kuendana na mabadiliko yaliyofanyika katika miongozo inayosimamia Maadili ya Utumishi wa Umma.

**B. Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC)**

**Mheshimiwa Spika;** Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC) kina majukumu ya kutoa mafunzo, ushauri, kufanya tafiti tumizi na kutoa machapisho mbalimbali katika nyanja za Uongozi, Menejimenti na Utawala. Aidha, Chuo kinasimamia Kampasi sita (6) zilizopo kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Tabora, Mtwara, Singida, Tanga na Mbeya.

**Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania kimetekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Mitihani ya watumishi wa umma 845 iliratibiwa na kufanyika kwa ajili ya maendeleo ya kimuundo kulingana na mahitaji ya kada mbalimbali za utumishi wa umma;

(ii) Watumishi wa umma 3,728 walipatiwa Mafunzo ya Uongozi na Maendeleo, Menejimenti, Utawala na Usimamizi wa Ofisi ili kuimarisha taswira nzuri ya utumishi wa umma;

(iii) Watumishi wa umma 2,576 ambao ni waajiriwa wapya walipatiwa mafunzo ya awali ya kujenga uwezo wa kutenda kazi za Serikali kwa usahihi na kwa mujibu wa sera, sheria, kanuni, taratibu na miongozo na inayoongoza utumishi wa umma;

(iv) Mafunzo ya muda mrefu yalitolewa kwa wanachuo 10,013 katika fani za utunzaji wa kumbukumbu, uhazili, kompyuta, utunzaji wa fedha za umma, menejimenti ya rasilimaliwatu, usimamizi wa manunuzi ya umma, uongozi

na utawala bora kwa lengo la kuwapatia ujuzi na stadi za kazi za Serikali;

(v) Ushauri wa kitaalam katika maeneo nane (8) ulitolewa ili kuwawezesha watumishi wa umma kuboresha mifumo na mbinu za utekelezaji wa majukumu ya taasisi zao kwa mujibu wa hati za kuanzishwa kwake na mahitaji ya wadau;

(vi) Tafiti tumizi mbili (2) zimefanyika na kukamilika katika maeneo mawili ya utumishi wa umma yaliyolenga kuboresha utoaji huduma kwa wananchi;

Mafunzo kwa njia ya Mtandao yametolewa kwa washiriki 148, njia ambayo imesaidia kuepuka muingiliano wa mafunzo na majukumu ya kazi na kupunguza safari nje ya vituo vya kazi;

Watumishi 30 wa chuo wamewezeshwa kuendelea na masomo katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu, Shahada ya Uzamili na Shahada ya Kwanza;

Ujenzi wa majengo ya kampasi ya Singida awamu ya pili katika eneo la Mungumaji kwa fedha za ndani umefikia asilimia 98. Ujenzi huo unajumuisha madarasa ya kufundishia, ofisi, kumbi za mikutano/mafunzo na vyoo; na

Ujenzi wa majengo ya kampasi ya Tanga awamu ya kwanza eneo la Kange unaojumuisha madarasa ya kufundishia, ofisi na vyoo umeanza kwa ruzuku ya maendeleo na upo katika hatua za awali za ujenzi wa boma.



*1- 3: Mwonekano wa majengo ya Chuo cha Utumishi wa Umma, Kampasi ya Singida.*

### C. Watumishi Housing Investment (WHI)

**Mheshimiwa Spika;** Taasisi ya Watumishi Housing Investment (WHI) ina majukumu ya kutekeleza Mpango wa Makazi kwa Watumishi wa Umma na wanachama wa mfuko wa hifadhi ya jamii; na kutoa huduma za ujenzi na ushauri wa majenzi.

**Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Machi, 2025 WHI imetekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Ujenzi wa nyumba 57 za Mradi wa Makazi kwa Watumishi wa UmmaWilayani/Halmashauri umefikia asilimia 35 ya utekelezaji. Kati ya nyumba hizo, 42 zinajengwa katika wilaya/Halmashauri zilizo na mazingira yasiyofikika kwa urahisi na nyumba 15 zinajengwa jijini Dodoma;

(ii) Mradi wa ujenzi wa ghorofa tano (5) wenye nyumba 58 katika eneo la Kisasa Hilltop, Njedegwa Dodoma umeanza na unatarajiwa kukamilika Septemba, 2026;

(iii) Ujenzi wa ghorofa pacha wenye nyumba 101 katika Mradi wa Ghorofa Mikocheni Dar es Salaam umeanza Septemba, 2024 na unatarajiwa kukamilika Machi, 2026;






1. *Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akikata utepe kuashiria Uzinduzi wa Mpango wa Makazi kwa Watumishi wa Umma wakati wa hafla iliyofanyika katika eneo la Njedengwa Mkoani Dodoma.*

2. *Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akizindua Mpango wa Makazi kwa Watumishi wa Umma wakati wa hafla iliyofanyika katika eneo la Njedengwa Mkoani Dodoma.*

(iv) Viwanja 223 vilivyopimwa USA River jijini Arusha vimeuzwa na gharama za ununuzi zinaendelea kulipwa kwa awamu ambapo hadi sasa kiasi cha shilingi bilioni 2.29 kimekusanywa;

(v) Huduma za ujenzi na ushauri zimetolewa kwa taasisi za Serikali ikiwemo usimamizi wa: Kipindi cha matazamio katika ujenzi wa jengo la Ofisi ya Rais - UTUMISHI katika Mji wa Serikali Mtumba Jijini Dodoma; ujenzi wa jengo la Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC) Mjini Tanga; jengo la ofisi la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) Geita; na ukarabati na ujenzi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi mikoa ya Dar es Salaam na Ruvuma; na

(vi) Mfuko wa Faida umesimamiwa na umeendelea kukua na kufikia thamani halisi ya shilingi bilioni 36.6 ikiwa ni asilimia 91 ya lengo la shilingi bilioni 40. Aidha,

wawekezaji wameongezeka na kufikia 7,553 kutoka 4,160 sawa na ongezeko la asilimia 82.

**OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA**

**Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka wa fedha 2024/25, Bunge lako tukufu liliidhinisha kiasi cha **shilingi 13,179,878,000.00** kwa ajili ya Fungu 67 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma. Kati ya fedha hizo, **shilingi 10,831,831,000.00** sawa na **asilimia 82.18** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida; na **shilingi 2,348,047,000.00** sawa na **asilimia 17.82** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Machi, 2025, **shilingi 8,829,151,680.72** sawa na **asilimia 66.99** zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo, **shilingi 7,218,204,680.72** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 1,610,947,000.0**0 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi hicho, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ilitekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Matangazo ya kazi 59 yalitolewa na waombaji kazi 909,991 walituma maombi. Kati ya hao, wanaume walikuwa 483,493 na wanawake walikuwa 426,498.

(ii) Mchakato wa Ajira katika Taasisi mbalimbali za Umma umefanyika kulingana na vibali vilivyopokelewa vyenye jumla ya nafasi 42,249 ambazo zinajumuisha wataalamu wa sekta za Afya, Elimu (Walimu na Mafundi Sanifu wa Maabara za Shule), Walimu wa Amali na Biashara; na kada nyingine. Nafasi zilizojazwa ni 36,453, kati ya hizo wanaume ni 21,252 na wanawake ni 15,201. Nafasi 5,796 ambazo hazijajazwa kwa mujibu wa kibali, utaratibu wake unaendelea. Aidha, usaili huo ulifanyika katika mikoa yote Tanzania Bara na Zanzibar na idadi ya waliopangiwa vituo vya kazi inajumuisha baadhi ya wasailiwa waliokuwa kwenye kanzidata;

(iii) Taarifa za wasailiwa 35,467 wa kada mbalimbali waliofaulu usaili wa mahojiano zimehifadhiwa kwenye kanzidata na zitakuwemo kwa muda wa miezi 12. Aidha, watapangiwa kazi kulingana na mahitaji ya wataalamu wa kada husika kutoka kwa waajiri mbalimbali katika utumishi wa umma ndani ya kipindi hicho;

(iv) Usaili kwa kada mbalimbali zilizokasimiwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 144, na Vyuo Vikuu vya Umma 10 zimesimamiwa ambapo wasailiwa 2,758 waliofaulu usaili wamepata ajira;

(v) Maswali 26,652 ya kada mbalimbali yamekusanywa, kuhakikiwa kutoka kwa wataalam na kuhifadhiwa kwenye mfumo "*Question DataBank System*";

(vi) Jumla ya vyeti 43,365 vinavyojumuisha vyeti vya taaluma, vyeti vya kuzaliwa na leseni za udereva vimehakikiwa kwa kushirikiana na NECTA, RITA na TRA. Kati ya vyeti hivyo, 42,954 vimehakikiwa na NECTA, 398 RITA na 13 TRA. Aidha, kati ya vyeti hivyo, 29 vimebainika kuwa vya kughushi na hatua za kuwafungia kwenye mfumo zilichukuliwa;

(vii) Ujenzi wa Mfumo wa Kupima Uelewa na Ufahamu wa Wasailiwa (Online Aptitude Test System) umekamilika na kuwezesha wasailiwa kufanya usaili katika vituo vilivyopo mikoa yote ya Tanzania bara na Zanzibar. Jumla ya kada 60 zenye wasailiwa 28,144 wa Shahada ya Kwanza na Stashahada wameweza kufanya usaili kwa njia ya mtandao (Online Aptitude Test System).



*Wasailiwa wa Kada ya Afya wakifanya usaili wa vitendo.*



*Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Deus Sangu, na jopo la wataalam wa Afya wanaoendesha usaili wa mahojiano ya ana kwa ana kwa waomba kazi katika kada ya Afya jijini Arusha.*



*Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Ummana Utawala Bora, Mhe. Deus Sangu, akiwa katika picha ya pamoja na jopo la wataalam wa Afya wanaosimamia usaili wa waomba kazi za Afya jijini Arusha.*

(viii) Maboresho ya mfumo wa Ajira Portal yamefanyika na kuwezesha barua kusainiwa kidigitali, hatua hii imesababisha kuongezeka kwa kasi ya kuwapangia wasailiwa vituo vya kazi kwa waajiri mbalimbali. Sambamba na hilo, barua za ajira kwa wasailiwa zitatolewa kupitia akaunti zao za Ajira Portal hatua inayolenga kupunguza gharama na muda kwa walipangiwa vituo vya kazi;

(ix) Mfumo wa Ajira Portal umeboreshwa ili kuwezesha ajira kada za Walimu na Afya pamoja na kuchukua barua moja kwa moja kwa waliofaulu usaili. Aidha, mfumo umefanyiwa miunganiko na mifumo ya e-Watumshi, NACTVET, na Mfumo wa Usimamizi wa Mikopo unaosimamiwa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu;

(x) Ujenzi wa mfumo wa kielektroniki wa kupima tabia na haiba za wasailiwa (Psychometric Testing System) umefikia asilimia 60. Mfumo utaiwezesha Serikali kutambua haiba na tabia za waajiriwa wapya ili waweze kujengewa uwezo katika maeneo mahsusi yatakayobainishwa baada ya kupimwa kitaalam. Pia, utawasaidia waajiri kufahamu maeneo ambayo waajiriwa wapya wanaonesha kuwa na umahiri ili

waweze kuwatumia ipasavyo katika shughuli zao kwa lengo la kuleta ufanisi wa Taasisi wanazozisimamia;

(xi) Huduma za dawati la msaada na utatuzi kwa watumiaji 201,897 wa Mfumo wa '*Ajira Portal*' zimetolewa. Kati ya watumiaji hao, 151,919 walihudumiwa kwa njia ya simu, na 49,978 walihudumiwa kwa njia ya barua pepe;

(xii) Umma umehabarishwa kuhusu mchakato wa ajira kupitia vyombo mbalimbali vya habari vikiwemo TBC I, Azam TV, Clouds FM, Channel TEN, Star TV, Wasafi TV, A-FM, C-FM, Ayo TV, tovuti na mitandao rasmi Kijamii ya Sekretarieti ya Ajira (Instagram, Ajira TV, X (twitter) na Facebook); na

(xiii) Elimu imetolewa kuhusu mchakato wa ajira katika utumishi wa Umma katika Vyuo vya Elimu ya Juu vinne (4) ambavyo ni: St. Joseph University, Chuo cha Mipango, Chuo Kikuu Mzumbe, na Chuo Kikuu cha Dodoma.

**OFISI YA RAIS, TUME YA UTUMISHI WA UMMA**

**Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka wa fedha 2024/25, Bunge lako tukufu liliidhinisha kiasi cha **shilingi 9,240,889,000.00** kwa ajili ya Fungu 94 - Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma. Kati ya fedha hizo, **shilingi 8,740,713,000.00** sawa na **asilimia 94.59** ni matumizi ya kawaida na **shilingi 500,176,000.00** sawa na **asilimia 5.41** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Machi, 2025 **shilingi 7,135,981,761.00** sawa na asilimia 77 zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo, **shilingi 6,635,805,761.0**0 ni matumizi ya kawaida na **shilingi 500,176,000.00** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi hicho, Tume ilitekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Rufaa 300 za watumishi wa umma ambao hawakuridhika na uamuzi wa mamlaka zao za nidhamu ziliamuliwa, ikiwa ni sawa na asilimia 85 ya rufaa 353 zilizopokelewa. Aidha, rufaa 23 zinaendelea kuchambuliwa na rufaa 30 vielelezo vyake vinafuatiliwa kwenye mamlaka husika;

(ii) Malalamiko 387 ya watumishi wa umma ambao hawakuridhika na namna masuala yao ya kiutumishi yalivyoshughulikiwa na waajiri wao yaliamuliwa, hii ni sawa na asilimia 87 ya malalamiko 443 yaliyopokelewa. Aidha, malalamiko 11 yanaendelea kuchambuliwa na malalamiko 22 vielelezo vyake vinafuatiliwa kwenye mamlaka husika;

(iii) Warufani 84 na Warufaniwa 10 walioomba kufika na kusikilizwa mbele ya Tume, walipewa nafasi ya kutoa ufafanuzi wa hoja zao kwa mujibu wa Kanuni ya 62 (1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022;

(iv) Taasisi 160 zilifanyiwa ukaguzi wa uzingatiaji wa Sheria katika Utumishi wa Umma ambapo Taasisi za Serikali Kuu zilikuwa 26, Mamlaka za Serikali za Mitaa 55 na Taasisi za Umma 79. Taarifa ya ukaguzi imekamilika na kuwasilishwa kwenye mamlaka husika;

(v) Taasisi 161 zilifanyiwa ukaguzi maalum ambapo Taasisi 160 zilikaguliwa kuangalia uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu katika ujazaji wa nafasi wazi za madaraka na Taasisi moja (1) ilikaguliwa na kufanyiwa tathmini ya utendaji wake wa kazi;

(vi) Elimu kuhusu uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo inayosimamia Utumishi wa Umma ilitolewa kwa washiriki 387 kutoka katika Taasisi 81. Aidha, elimu ilitolewa kupitia vyombo vya habari sita (6), mitandao ya kijamii saba (7), Magazeti manne (4) na tovuti ya Tume;

(vii) Watumishi wa umma 1,038 kutoka taasisi 458 walijengewa uwezo na TUME kupitia mafunzo kuhusu ushughulikiaji wa masuala ya kiutumishi sambamba na namna bora ya uendeshaji wa mashauri ya nidhamu;

(viii) Mwongozo wa Uwasilishaji wa Taarifa Tume na Mwongozo wa Mashauri ya Nidhamu, Rufaa na Malalamiko ilihuishwa;

(ix) Maafisa 66 wa Tume walijengewa uwezo kuhusu ukaguzi wa uzingatiaji wa masuala ya kiutumishi na ushughulikiaji wa rufaa na malalamiko kwa lengo la kuwawezesha kutekeleza majukumu yao ipasavyo; na

(x) Mashauri saba (7) kati ya 24 yaliyopelekwa mahakamani na watumishi wa umma ambao hawakuridhika na uamuzi wa mamlaka ya rufaa yamekamilika, ambapo Tume ilitoa ufafanuzi na kujibu hoja za Warufani kwa kushirikiana na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.



*1.Katika Shamra shamra za Maadhimisho ya Siku ya Tume "Tume day" Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene (Mb), alishiriki zoezi la kupanda miti katika ofisi mpya za Tume zinazojengwa katika Mji wa Serikali - Mtumba, Septemba 2024.*

## OFISI YA RAIS, IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA TAIFA

**Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka wa fedha 2024/25, Bunge lako tukufu liliidhinisha kiasi cha **shilingi 4,360,777,000.00** kwa ajili ya

Fungu 04 - Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa. Kati ya fedha hizo, shilingi **4,065,013,000.00** sawa na **asilimia 93.22** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida; na **shilingi 295,764,000.00** sawa na **asilimia 6.78** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Machi, 2025, **shilingi 3,482,402,531.18** sawa na **asilimia 79.86** zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo, **shilingi 3,362,402,531.18** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 120,000,000.00** nikwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi hicho, Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa ilitekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kumbukumbu 324 za Waasisi wa Taifa letu (Mwl. Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume) na kumbukumbu 480 za Marais wengine wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zimetambuliwa, kukusanywa na kuhifadhiwa;

(ii) Nyaraka na taarifa 20,000 za Viongozi wengine zilizokusanywa kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zimechambuliwa, kuhakikiwa na kupangwa;

(iii) Huduma za upatikanaji wa nyaraka mbalimbali kwa ajili ya kukamilisha tafiti zilitolewa kwa viongozi na watafiti. Viongozi waliohudumiwa katika kipindi hiki ni pamoja na Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete (Rais mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania) na watafiti wanaoandika wasifu wa Hayati Rashid Mfaume Kawawa aliyekuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(iv) Usanikishaji na uhuishaji wa Mfumo wa Utunzaji wa Kumbukumbu za Kiutendaji (Keyword Filing System) ulifanyika katika Taasisi za Umma 33 kati ya 40 zilizopangwa kuwekewa mfumo;

(v) Usanikishaji na uhuishaji wa Mfumo wa Masijala Mtandao (*e-Office*) umekamilishwa katika Taasisi za Umma 23 kati ya 40 zilizopangwa kuwekewa mfumo;

(vi) Taasisi za umma saba (7) ziliwezeshwa kuandaa Mwongozo wa Utunzaji na Uteketezaji Kumbukumbu kwa mujibu wa Sheria;

(vii) Ukaguzi wa hali ya utunzaji wa kumbukumbu katika Taasisi za Umma 29 kati ya 30 umekamilishwa kwa lengo la kujua hali halisi ya utunzaji wa kumbukumbu ili kubaini changamoto wanazokabiliana nazo na kuzipatia ufumbuzi;

(viii) Mafunzo ya utunzaji wa kumbukumbu yalitolewa katika Taasisi za Umma 7 kati ya 10 zilizopangwa;

(ix) Mkutano wa Bodi ya Baraza la Nyaraka la Kimataifa Tawi la Mashariki na Kusini mwa Afrika (*The Eastern and Southern Africa Regional Branch of International Council on Archives - ESARBICA*) uliratibiwa na kufanyika Arusha, kuanzia tarehe 19 hadi 21 Agosti, 2024;

(x) Utiaji saini wa Mkataba wa Mpango wa Utekelezaji wa mashirikiano ya utunzaji na uhifadhi wa kumbukumbu na nyaraka kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Oman uliratibiwa na kufanyika Jijini Dar es Salaam tarehe 5 Desemba, 2024; na

(xi) Majalada 839 ya iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na majalada 1,000 ya iliyokuwa Serikali ya kikoloni ya Mwingereza yamefanyiwa urudufu (*scanning*) kwa ajili ya kuhifadhiwa katika mfumo wa kidigitali.

**MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2025/26 NA MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIWA**

**Mheshimiwa Spika;** Mpango na Bajeti kwa mwaka 2025/26 umeandaliwa kwa kuzingatia: Dira ya Taifa ya Maendeleo ya

2025; Maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26); Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akihutubia Bunge tarehe 22 Aprili 2021; na Maelekezo ya Mamlaka na Maoni na Ushauri wa Bunge lako tukufu. Shughuli zitakazotekelezwa na kila taasisi ni kama ifuatavyo:

**OFISI YA RAIS - IKULU NA TAASISI ZAKE**

**A. Ofisi ya Rais – Ikulu**

**Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka 2025/26 Ofisi ya Rais, Ikulu imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kutoa ushauri kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala ya Siasa, Uchumi, Jamii, Sheria, Diplomasia, Mawasiliano na Habari, Uhusiano wa Kikanda, Kimataifa na ushauri mwingine kwa lengo la kumsaidia Rais kufanya maamuzi;

(ii) Kuwezesha ratiba ya kila siku ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(iii) Kutoa huduma kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na familia yake;

(iv) Kuratibu, kuandaa na kushiriki mikutano 35 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, mikutano 20 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) na mikutano 15 ya Baraza la Mawaziri;

(v) Kuendesha vikao 10 vya mashauriano na wadau kwa ajili ya mapitio ya mfumo na uchambuzi wa sera mbalimbali na masuala ya kimkakati ya umma;

(vi) Kutoa mafunzo kuhusu utayarishaji na uwasilishaji wa Nyaraka za Baraza la Mawaziri na uchambuzi wa sera

kwa maofisa wa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na waratibu wa shughuli za Baraza la Mawaziri;

(vii) Kuchambua na kutoa ushauri kwa Katibu Mkuu Kiongozi katika masuala ya kiuchumi, kijamii, kisheria, kiulinzi na kiusalama, kimataifa na masuala mengine yote yanayowasilishwa;

(viii) Kufanya mafunzo na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Programu za Maboresho katika ngazi za Wizara, Mikoa na Serikali za Mitaa;

(ix) Kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa kwa kushirikisha wadau wa Sekta ya Umma na Binafsi;

(x) Kuendelea kujenga uwezo wa Taasisi za Umma kuhusu uzingatiaji wa utawala bora katika kutoa huduma kwa umma;

(xi) Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa programu za maboresho katika ngazi za utekelezaji;

(xii) Kupokea, kupitia na kuchambua rufaa 400 na malalamiko 500 ya watumishi wa umma na wananchi;

(xiii) Kutoa mafunzo ya kushughulikia rufaa na malalamiko ya Watumishi wa Umma kwa viongozi 364 wa Serikali;

(xiv) Kufanya ziara ya ufuatiliaji wa uzingatiaji wa sheria na maelekezo yanayotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi na Mkuu wa Utumishi wa Umma yanayohusu masuala ya usimamizi wa utawala wa Utumishi kwenye Wizara, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na

(xv) Kuratibu na kusimamia Miradi ya Maendeleo ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na Programu ya Kujenga Uwezo wa Taasisi za Serikali Kupambana na Rushwa (BSAAT).

## B. Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)

**Mheshimiwa Spika;** katika Mwaka 2025/26, TAKUKURU imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kufanya utafiti na uchambuzi wa mifumo ya kiutendaji na utoaji huduma katika ajira, elimu, afya, na mifumo ya ukusanyaji mapato ili kubaini maeneo yenye mianya ya rushwa na kushauri namna ya kuziba mianya hiyo;

(ii) Kufuatilia matumizi ya fedha za umma katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuhakikisha utekelezaji wake unazingatia thamani halisi ya fedha;

(iii) Kufanya warsha/vikao vya kuwashirikisha wadau kuweka mikakati ya kudhibiti mianya ya rushwa na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikakati hiyo;

(iv) Kutekeleza Mkakati wa Habari, Elimu na Mawasiliano (*Information, Education and Communication Strategy – IECS*) wa TAKUKURU ili kujenga uwezo na uelewa kuhusu rushwa, ufisadi na juhudi za Serikali katika kuzuia na kupambana na rushwa kwa makundi mbalimbali katika jamii kwa kutumia njia mbalimbali za uelimishaji na mawasiliano ili kuyashawishi makundi haya kuunga mkono na kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa nchini;

(v) Kufanya kazi za uelimishaji umma ikiwa ni sehemu ya kutekeleza Awamu ya Nne ya Mpango Kazi wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa (NACSAP IV) hususan kipindi cha Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025;

(vi) Kutekeleza Programu ya TAKUKURU Rafiki ili kuwashirikisha wadau wengi zaidi kwenye kuzuia vitendo vya rushwa hivyo kuboresha utoaji wa huduma kwa umma na utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

(vii) Kushirikisha umma katika mapambano dhidi ya rushwa kwa kuandaa ajenda zenye maudhui ya mapambano hayo kupitia njia mbalimbali ikiwemo semina, mikutano ya hadhara, vyombo vya habari na mitandao ya kijamii hususan kuelekea Uchaguzi Mkuu 2025;

(viii) Kukamilisha uchunguzi wa majalada ya tuhuma za rushwa unaoendelea pamoja na tuhuma mpya zitakazojitokeza;

(ix) Kuendesha mashauri ya rushwa mahakamani kwa kibali cha Mkurugenzi wa Mashataka;

(x) Kutengeneza mfumo wa takwimu na uchunguzi kwa kutumia wataalam wa ndani;

(xi) Kusanikisha 'data centre' katika jengo jipya la Makao Makuu na kuunganisha ofisi za TAKUKURU wilaya ya Malinyi na Ukerewe;

(xii) Kuimarisha mfumo wa TEHAMA katika taasisi ili kurahisisha na kuwezesha mtiririko mzuri wa majalada, takwimu na mawasiliano kutoka ngazi za wilaya, mkoa na makao makuu; na

(xiii) Kutoa mafunzo ya kuimarisha weledi kwa watumishi na kuwajengea umahiri wa utendaji kazi ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Taasisi.

**C. Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)**

**Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2025/26, TASAF imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kuhawilisha ruzuku kwa kaya maskini 906,669 zinazokidhi vigezo vya Mpango;

(ii) Kuwezesha utekelezaji wa miradi ya jamii ya kutoa ajira ya muda kwa kaya za walengwa katika mamlaka za

utekelezaji 63. Aidha, jumla ya miradi 4,4920 imepangwa kutekelezwa katika ngazi ya Vijiji/Mitaa/Shehia na inategemewa kutoa ajira za muda kwa Walengwa 227,198;

(iii) Kuwezesha jamii kutekeleza miradi 149 ya kuendeleza miundombinu yahuduma za jamii katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta za afya, elimu, maji, mazingira na ujasiriamali katika Vijiji/Mitaa/shehia;

(iv) Kuimarisha miundombinu ya mifumo ili kulinda usalama wa taarifa za walengwa na kuungamanisha mfumo wa walengwa na mifumo mingine ya Serikali ili kuweza kubadilishana taarifa kwa urahisi. Aidha, mfumo wa sasa utafanyiwa mapitio kwa ajili ya maboresho yanayoendana na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya taarifa za walengwa kwa Taasisi na wadau wangine;

(v) Kutangaza ripoti ya Matokeo ya tathmini na utekelezaji wa shughuli za Mpango kwa wadau mbalimbali. Ripoti itaonesha ni kwa kiwango gani malengo ya Mpango yamefikiwa, itabainisha changamoto na kutoa mapendekezo ya namna ya kuzishughulikia ili kuboresha utendaji kazi na utekelezaji wa awamu ya Mpango inayofuata;

(vi) Kufanya mapitio ya pamoja baina ya timu ya Serikali na Wadau wa Maendeleo kuhusu utekelezaji wa shughuli za Mpango;

(vii) Kukamilisha usanifu na uidhinishwaji wa awamu inayofuata ya Mpango wa Kunusuru Kaya za Walengwa; na

(viii) Kutambua na kuandikisha kaya za walengwa zinazokidhi vigezo kuingizwa kwenye Mpango unaofuata katika Maeneo ya Utekelezaji 186 Tanzania Bara na Zanzibar.

**D. Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)**

**Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2025/26, Mamlaka ya Serikali Mtandao imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kusimamia, kutathmini na kuboresha hali ya usalama wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA ya Serikali, na kushauri maeneo ya kuboresha na kufuatilia utekelezaji wake ili kuhakikisha kuwa mifumo na miundombinu ya TEHAMA serikalini inafanya kazi kurahisisha uendeshaji wa Serikali na kutoa huduma kwa wananchi wakati wote kwa ufanisi na usalama;

(ii) Kusimamia, kuendesha na kuendeleza mifumo na miundombinu shirikishi ya TEHAMA ya Serikali na Taasisi zake, ikiwa ni pamoja na mtandao wa mawasiliano katika Mji wa Serikali Mtumba, na kusimamia na kuboresha Vituo vya Kuhifadhi Mifumo na Taarifa za Serikali pamoja na Vituo vya Kujikinga na Majanga;

(iii) Kuendeleza Utafiti na Ubunifu katika matumizi ya teknolojia mpya za TEHAMA ili kuibua huduma mpya kwa umma kupitia TEHAMA na kuwezesha matumizi sahihi ya teknolojia mpya zinazoibuka;

(iv) Kufanya uchambuzi, kusanifu na kujenga mifumo mipya ya kisekta kwa taasisi zenye taratibu za utendaji kazi zinazoendana kwa lengo la kupunguza wingi wa mifumo ya TEHAMA serikalini;

(v) Kuhuisha na kufanya maboresho katika mifumo ya TEHAMA shirikishi, mifumo ya kisekta na mifumo ya kitaasisi inayotumika kuiwezesha uendeshaji na kutoa huduma kwa ufanisi na usalama zaidi ili kuboresha utoaji huduma katika utumishi wa umma na wananchi kwa ujumla;

(vi) Kuendeleza uunganishaji mifumo ya taasisi za Serikali kwenye Mfumo wa Kuwezesha Mifumo ya Serikali

Kuwasiliana na Kubadilishana Taarifa (*Government Enterprise Service Bus - GovESB*);

(vii) Kupanua miundombinu ya Mtandao wa Mawasiliano Serikalini (*Government Network*) ili kuifikisha katika Wilaya zote nchini na kuziwezesha Taasisi nyingi kuwafikishia huduma wananchi kupitia mtandao;

(viii) Kukagua Mifumo ya Kimkakati, Kisekta na Kitaasisi ili kuhakikisha kuwa imetengenezwa na inatumika kwa kufuata Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo iliyopo na kushauri maeneo ya kuboresha na kufuatilia utekelezaji wake;

(ix) Kuwajengea uwezo watumishi katika kusimamia mifumo na miundombinu ya TEHAMA katika taasisi za umma, pamoja na kutoa mafunzo kwa watumiaji kuhusu matumizi sahihi na salama ya mifumo na miundombinu ya TEHAMA; na

(x) Kutoa ushauri wa kitaalamu na msaada wa kiufundi kwenye maeneo ya TEHAMA kwa taasisi za serikali ili kuhakikisha kuwa viwango na miongozo inafuatwa.

**E. Taasisi ya UONGOZI**

**Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2025/26, Taasisi ya UONGOZI imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kutoa mafunzo ya Stashahada ya Uzamili ya Uongozi kwa lengo la kuwajengea uwezo viongozi 40 katika maeneo ya maamuzi ya kimkakati, usimamizi wa rasilimaliwatu na rasilimali nyingine;

(ii) Kutoa mafunzo ya Cheti cha Uongozi kwa njia ya mtandao kwa lengo la kuwajengea uwezo viongozi 65 katika maeneo ya maamuzi ya kimkakati, usimamizi wa rasilimaliwatu na rasilimali nyingine pamoja na matumizi ya takwimu (*data analytics*);

(iii) Kutekeleza programu maalum ya mafunzo ya Uongozi kwa lengo la kuwajengea uwezo viongozi wanaochipukia 35 katika maeneo ya maamuzi ya kimkakati, mawasiliano ya kimkakati, Uchambuzi wa Sera, na matumizi ya takwimu (*data analytics*);

(iv) Kutekeleza programu maalum ya mafunzo ya uongozi kwa wanawake viongozi waandamizi na viongozi wanaochipukia 100 kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kufanya maamuzi ya kimkakati, usimamizi wa rasilimali za Serikali na rasilimaliwatu. Vilevile, mafunzo haya yana lengo la kukuza vipaji vya uongozi kwa viongozi wanawake wanaochipukia;

(v) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kupitia kozi 40 kwa lengo la kuwajengea uwezo viongozi 1,400 katika maeneo ya uongozi na maendeleo endelevu kwa ajili ya kuimarisha utendaji wao kwa kuzingatia mahitaji na maombi ya walengwa;

(vi) Kutekeleza programu maalum ya mafunzo ya uongozi kwa bodi 35 za Mashirika ya Umma, Taasisi za Umma na Wakala za Serikali kwa lengo la kuimarisha usimamizi na utendaji kwa Wakurugenzi wa Bodi 350. Mafunzo yatahusu uongozi wa kimkakati, usimamizi wa Mashirika ya Umma, usimamizi wa rasilimali za umma na rasilimaliwatu na usimamizi wa viashiria hatarishi;

(vii) Kufanya tafiti tumizi sita (6) kuhusu masuala ya uongozi na maendeleo endelevu ili kutoa ushauri wa kisera kwenye masuala muhimu yanayohusu maendeleo ya nchi ikiwemo maendeleo ya Nne ya Viwanda, Uchumi wa Buluu, na mabadiliko ya Tabianchi;

(viii) Kukamilisha uandishi wa kitabu kinachoelezea Wasifu wa maisha ya Hayati Rashid Mfaume Kawawa, aliyekuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kuanza kuandika kitabu kinachoelezea Wasifu wa maisha ya Hayati Abeid

Amani Karume, aliyekuwa Rais wa kwanza wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kuweka kumbukumbu za viongozi mashuhuri wa Taifa letu katika maandishi;

(ix) Kuandaa mikutano minne (4) ya kitaifa na miwili (2) ya kimataifa katika masuala ya uongozi kwa viongozi 1,280 kwa lengo la kubadilishana taarifa, maarifa na uzoefu na kuwaongezea uelewa wa masuala ya uongozi na maendeleo endelevu;

(x) Kuandaa vipindi sita (6) vya runinga vitakavyoshirikisha viongozi waandamizi na wataalam mbalimbali wa ndani na nje ya nchi, juu ya uongozi na maendeleo endelevu;

(xi) Kutoa ushauri wa kitaalam kwa taasisi tano (5) za Serikali katika maeneo yanayohusu uongozi na maendeleo endelevu; na

(xii) Kutoa machapisho tisa (9) juu ya masuala ya uongozi na maendeleo endelevu ikiwemo Tawasifu ya Hayati Rashidi Mfaume Kawawa.

**F. Wakala wa Ndege za Serikali**

**Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2025/26, Wakala ya Ndege za Serikali imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kutoa huduma ya usafiri wa anga kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa;

(ii) Kuratibu ununuzi pamoja na kusimamia mikataba ya ukodishaji wa ndege kwa Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL);

(iii) Kufanya matengenezo ya ndege zinazotoa huduma kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa;

(iv) Kulipia gharama za bima za ndege na wanaanga kama inavyotakiwa kisheria ili kupata kibali ya kuruka katika anga;

(v) Kugharamia uendeshaji wa Ofisi na kulipia gharama za vipuri na mafuta ya ndege; na

(vi) Kutoa mafunzo ya kisheria kwa wanaanga kwa ajili ya kuhuisha leseni zao.

**G. Baraza la Kumshauri Rais Kuhusu Masuala ya Chakula na Kilimo**

**Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2025/2026 Baraza la Kumshauri Rais kuhusu Masuala ya Chakula na Kilimo imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kuandaa mpango mkakati wa Baraza la Kumshauri Rais kuhusu chakula na kilimo;

(ii) Kushauri kuhusu mikakati ya utafutaji wa rasilimali za uendeshaji wa shughuli za Baraza;

(iii) Kukusanya rasilimali ili kutekeleza kazi za Mpango wa Masuala ya Chakula na Kilimo (Tanzania Food Agriculture Delivery Council-TFADC);

(iv) Kushauri kuhusu mikakati ya kuhamasisha uwekezaji wa mitaji katika sekta ya kilimo kutoka sekta binafsi;

(v) Kuandaa ushauri kuhusu mipango ya ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi katika mnyororo wa thamani wa bidhaa za kipaumbele;

(vi) Kutoa ushauri kuhusu mbinu za kuboresha upatikanaji wa huduma za kifedha vijijini;

(vii) Kuandaa ushauri kuhusu mikakati ya kuongeza ushiriki wa vijana katika kilimo;

(viii) Kuandaa ushauri kuhusu mbinu za kimataifa za utoaji katika mifumo ya chakula na mabadiliko katika kilimo;

(ix) Kuandaa ushauri kuhusu sera na mikakati ya kuongeza ubunifu wa mifumo ya chakula;

(x) Kufanya ufuatiliaji wa shughuli za TFADC na utekelezaji wa masuala ya chakula na kilimo nchini;

(xi) Kufanya mikutano ya wadau kwa mazao ya kipaumbele (Ngano, Alizeti, Parachichi, Nyama na Maziwa);

(x) Kuandaa ushauri kuhusu usimamizi wa ardhi ya kilimo wenye ufanisi;

(xi) Kuandaa ushauri katika kuendeleza masoko jumuishi yenye ufanisi na yenye faida katika mnyororo wa thamani za mazao ya kipaumbele; na

(xii) Kuandaa ushauri kuhusu utendaji wa sekta ya kilimo na kubainisha maeneo ya kimkakati ya kuboresha mageuzi ya sekta ya kilimo nchini.

**Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2025/26, Ofisi ya Rais, Ikulu: Fungu 20 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi **34,804,735,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri: Fungu 30 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **shilingi 1,197,312,759,000.00** kati ya fedha hizo, shilingi **1,039,839,675,000.00** ni matumizi ya kawaida na **shilingi 88,934,306,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa fedha za ndani na shilingi **68,538,778,000.00** fedha za nje.

**OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA**

**Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2025/26, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kupokea Tamko la Viongozi wa Umma kuhusu Rasilimali na Madeni linalopaswa kutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(ii) Kupokea malalamiko na taarifa za ukiukwaji wa Maadili kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kutoka kwa wananchi;

(iii) Kuchunguza tuhuma yoyote ya kuvunjwa kwa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma dhidi ya Viongozi wa Umma;

(iv) Kufanya uhakiki wa matamko ya Rasilimali na Madeni kwa Viongozi wa Umma;

(v) Kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Baraza la Maadili ya Viongozi wa Umma;

(vi) Kuelimisha Viongozi wa Umma na Wananchi kwa ujumla kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Hati ya Ahadi ya Uadilifu;

(vii) Kuandaa Taarifa ya mwaka ya Utekelezaji wa shughuli za Sekretarieti na kuiwasilisha kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(viii) Kuanzisha na kuendeleza Klabu za Maadili katika shule na vyuo nchini; na

(ix) Kuendelea na ujenzi wa Ofisi za Kanda (Mwanza, Mbeya na Morogoro) na Kukamilisha ujenzi wa Makao Makuu na Kanda ya Kati Jijini Dodoma.

**Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2025/26, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma: Fungu 33 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **shilingi 16,958,139,000.00**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 13,958,139,000.00** ni matumizi ya kawaida na **shilingi 3,000,000,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

## OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA NA TAASISI ZAKE

### A. Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

**Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka 2025/26, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kushughulikia vibali 41,500 vya ajira ili kujaza nafasi zilizoidhinishwa katika Ikama;

(ii) Kuhakiki na kuidhinisha madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi kwa taasisi 425;

(iii) Kusafisha taarifa za kiutumishi na mishahara (*Data Cleaning*) kwa watumishi waliopo katika Taasisi 433 zinazotumia Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (*e-Watumishi*);

(iv) Kuhakiki na kuidhinisha mabadiliko ya taarifa zinazohusu kiutumishi na mishahara katika Mfumo wa *e-Watumishi* kwa taasisi 524;

(v) Kufanya uhakiki maalum wa watumishi katika taasisi za umma za Mkoa wa Dodoma;

(vi) Kuwezesha taasisi 35 ambazo kwa sasa hazitumii Mfumo wa *e-Watumishi* kuanza kutumia mfumo tajwa katika kusimamia masuala ya kiutumishi na mishahara;

(vii) Kukamilisha uandaaji wa Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za mwaka 2009, Toleo la Nne la Mwaka 2025 baada ya kufanyiwa mapitio kwa Toleo la Tatu la Kanuni hizo za mwaka 2009;

(viii) Kufanya uchambuzi wa Miundo ya Wizara na Taasisi za Umma 30 baada ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025;

(ix) Kufanya vikao vitatu (3) vya Kamati ya Rais ya Utekelezaji (*Presidential Implementation Committee - PIC*);

(x) Kuboresha Mfumo wa e-Utendaji kuendana na miundo ya taasisi ili kuimarisha utendaji kazi na uwajibikaji serikalini;

(xi) Kujenga mfumo utakaounganisha mifumo ya TEHAMA ya Sekta ya Utumishi na Utawala Bora (*Utumishi Data Sharing Gateway*) utakaorahisisha ubadilishanaji wa taarifa baina ya mifumo iliyopo ndani na nje ya Sekta ya Utumishi na Utawala Bora;

(xii) Kuongeza huduma za kiutumishi katika dirisha la Watumishi Portal Pamoja na watoa huduma za kifedha katika moduli ya e-Mkopo;

(xiii) Kuanza usanifu na ujenzi wa mfumo wa kielektroniki wa fursa za ufadhili wa masomo zinazotolewa na Washirika wa Maendeleo (*Scholarship Portal*). Lengo la mfumo huo ni kuwezesha watumishi kuona nafasi zilizotanganzwa, kufanya usajili na kufuatilia hatua ya maombi na kupata mrejesho;

(xiv) Kuendeleza mafunzo ya usalama wa mifumo kwa watumishi wa umma kwa mifumo ya TEHAMA ya Kiutawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu Serikalini na huduma mbalimbali za kiutumishi zinazopatikana kwenye Dirisha la Watumishi Portal, *e-Msawazo* na *e-Watumishi*;

(xv) Kufanya tathmini/utafiti wa athari za Mipango ya Motisha kwenye kuongeza tija katika Taasisi za Umma;

(xvi) Kuwezesha uandaaji na uhuishaji wa Miundo ya Maendeleo ya Utumishi katika Taasisi na Mashirika ya Umma, Wakala wa Serikali na Idara Zinazojitegemea kwa mujibu wa Miongozo;

(xvii) Kuendeleza ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miundo ya Maendeleo ya Utumishi katika Utumishi wa Umma;

(xviii) Kuwezesha uandaaji na uhuishaji wa Mipango ya Motisha katika Taasisi na Mashirika ya Umma kwa kuzingatia mwongozo;

(xix) Kufuatilia utekelezaji wa Mipango ya Motisha katika Taasisi na Mashirika ya Umma;

(xx) Kufanya uchambuzi wa Kanuni za Utumishi na Kanuni za Fedha za Taasisi 35 za Umma na kuwezesha kupata idhini;

(xxi) Kuendeleza ufuatiliaji wa ujumuishwaji wa masuala ya Anuai za jamii katika Utumishi wa Umma ili kuimarisha ustawi wa Watumishi wa Umma na kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa viwango vinavyotakiwa;

(xxii) Kuendeleza uboreshaji wa Mfumo wa Tathmini ya Hali ya Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma (*e-Msawazo*) na kusafisha taarifa za watumishi;

(xxiii) Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miundo na Mgawanyo wa Majukumu katika Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za kimkakati;

(xxiv) Kuhuisha Sheria ya Wakala za Serikali Sura, 245;

(xxv) Kuziwezesha Taasisi za Umma 516 ambazo ni Wizara na Taasisi zilizo tayari kuandaa huduma na kuziingiza kwenye Mfumo wa Daftari la Kielektroniki la Huduma za Serikali (*Government Service Directory –GSD*) na kujenga uelewa kwa Wananchi kuhusu mfumo huu;

(xxvi) Kuratibu ushiriki wa taasisi za umma kwenye maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma ili kutoa

huduma za papo kwa papo kwa watumishi wa umma na wananchi kwa ujumla;

(xxvii) Kupokea matangazo mbalimbali ya wadau, kuhariri na kuyawasilisha kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali;

(xxviii) Kutoa elimu ya matumizi ya Mfumo wa e-Utendaji kwa watumishi wa umma katika taasisi za umma 570 ili kuboresha utendaji kazi na uwajibikaji;

(xxix) Kufanya ufuatiliaji endelevu wa utekelezaji wa Mfumo wa *e-Utendaji* katika Taasisi za Umma 570;

(xxx) Kutoa mafunzo ya mbinu za Uongozi na Utawala Bora kwa Viongozi wa Serikali watakaoteuliwa baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025;

(xxxi) Kuwezesha Taasisi za Umma 45 kuandaa Mipango ya Rasilimaliwatu, Mipango ya Urithishanaji Madaraka na Mipango ya Mafunzo;

(xxxii) Kukamilisha maandalizi na kupeleka kwa wakuu wa taasisi za umma Mwongozo wa Kuandaa Mpango wa Urithishanaji Madaraka katika utumishi wa umma;

(xxxiii) Kuratibu mafunzo ya watumishi katika Utumishi wa Umma kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo;

(xxxiv) Kuratibu mikutano na vikao vya jumuiya na mtandao wa wataalam wa masuala ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma;

(xxxv) Kuhuisha kanzidata ya watanzania wenye sifa na nia ya kuajiriwa katika mashirika ya kikanda na kimataifa;

(xxxvi) Kufuatilia malalamiko yatokanayo na ukiukwaji wa sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia Utumishi wa Umma;

(xxxvii) Kuwezesha ujazaji nafasi wazi za ajira, uteuzi na kuthibitisha kazini nafasi za uteuzi kwa Watumishi wa Umma Waandamizi katika Taasisi 570 za Umma;

(xxxviii) Kufuatilia uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu za usimamizi wa Utumishi wa Umma na Taasisi katika Taasisi 570 za Umma;

(xxxix) Kushiriki Maadhimisho ya Kitaifa ya Wiki ya Maadili, Haki za Binadamu na Rushwa kwa Mwaka 2025;

(xl) Kutoa ushauri wa Kitaalamu katika Usimamizi wa Uzingatiaji wa Maadili katika Taasisi za Umma 30;

(xli) Kufanya Ufuatiliaji wa Uzingatiaji wa Maadili kwa Taasisi za Umma 50;

(xlii) Kufanya ufuatiliaji wa malalamiko ya wananchi yanayohusu ukiukwaji wa Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma unaofanywa na watumishi wa umma;

(xliii) Kuendeleza ujenzi wa Klabu ya Viongozi - Makao Makuu Dodoma eneo la Nzuguni;

(xliv) Kuanza ujenzi wa nyumba ya kiongozi wa Kitaifa mstaafu; na

(xlv) Kutoa huduma kwa Viongozi wa Kitaifa Wastaafu 19 (Viongozi tisa (9) na wajane 10) kwa mujibu wa sheria.

**B. Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC)**

**Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2025/26, Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC) kimepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kutoa mafunzo ya kujiandaa kufanya mitihani ya Utumishi wa Umma kwa watumishi 1,755;

(ii) Kutoa mafunzo ya Uongozi na Maendeleo, Menejimenti na Usimamizi wa ofisi kwa watumishi wa umma 7,970. Vile vile, mafunzo hayo yatatolewa kwa njia ya mtandao kwa watumishi wa umma 600;

(iii) Kutoa Mafunzo ya Awali kwa watumishi wa umma wapya 5,770 ili kuwajengea uelewa wa utendaji kazi serikalini na misingi ya utumishi wa umma;

(iv) Kuratibu midahalo ya kitaalam ya ndani na nje ya nchi kwa njia ya mtandao katika maeneo 5 kwa watumishi wa umma 800 na wa Sekta Binafsi;

(v) Kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa washiriki 11,686 katika fani za: Utunzaji wa Kumbukumbu; Uhazili; Kompyuta; Utunzaji wa Fedha za Umma; Menejimenti ya Rasilimaliwatu; Usimamizi wa Manunuzi ya Umma; Uongozi; na Utawala Bora;

(vi) Kutoa ushauri wa kitaalam katika maeneo mbalimbali kwa taasisi za umma 20 kwa ajili ya kutambua changamoto halisi za utendaji na kuchangia katika utoaji wa maamuzi yanayozingatia matokeo ya utafiti;

(v) Kufanya utafiti tumizi katika maeneo 12 ya Utumishi wa Umma yanayolenga kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi;

(vi) Kuwezesha mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi nane (8) wa Chuo cha Utumishi wa Umma katika ngazi za Shahada ya Uzamivu na Shahada ya Uzamili;

(vii) Kuendelea na ujenzi wa majengo ya kampasi ya Tanga awamu ya kwanza katika eneo la Kange unaojumuisha madarasa ya kufundishia, ofisi na vyoo kwa ruzuku ya maendeleo; na

(viii) Kuendelea na ukarabati wa hosteli na nyumba za watumishi kwa kampasi ya Tabora kwa fedha za ndani ikiwa ni maandalizi ya kuhamishia huduma ya utoaji wa mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi ya Shahada hasa Shahada ya Utunzaji wa Kumbukumbu na Uhazili.

**C. Watumishi Housing Investment (WHI)**

**Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2025/26, Watumishi Housing Investment imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kuendeleza ujenzi wa ghorofa tano (5) zenye nyumba 58 katika Mradi wa ghorofa Kisasa Hilltop, Njedegwa Dodoma;

(ii) Kuendeleza ujenzi wa nyumba 42 za Mradi wa Makazi kwa Watumishi wa Umma Wilayani;

(iii) Kuendeleza ujenzi wa ghorofa lenye nyumba 15 katika eneo la Mlezi/Makole Dodoma;

(iv) Kuanza ujenzi wa nyumba 75 za Mradi wa Makazi kwa Watumishi wa Umma Wilayani. Kati ya hizo, nyumba 60 zitajengwa katika Halmashauri zilizopo maeneo ya vijijini na nyumba 15 maeneo ya mijini;

(v) Kuendeleza Ujenzi wa ghorofa pacha wenye nyumba 101 katika Mradi wa Ghorofa Mikocheni Dar es Salaam;

(vi) Kukuza Mfuko wa Faida hadi kufikia thamani ya shilingi bilioni 50 ifikapo tarehe 30 Juni,2026;

(vii) Kuendeleza ukusanyaji wa fedha za mauzo ya viwanja 223 vilivyopo USA River jijini Arusha na kufuatilia maombi ya uwekaji wa miundombinu ya maji na umeme; na

(viii) Kujumuisha moduli ya e-Wekeza kwenye dirisha la Watumishi (*Watumishi Portal*) litakalowezesha watumishi wa umma kuwekeza katika Mfuko wa Faida kupitia

mishahara. Aidha, hatua hizo zinalenga kuwajengea watumishi tabia ya kuwekeza kidogo kidogo ili kujenga uwezo wa kifedha wa kununua nyumba na kujiandaa kifedha baada ya kustaafu na hivyo kupunguza utegemezi katika kikokotoo.

**Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2025/26, Fungu 32 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi **74,842,329,000.00** kati ya fedha hizo, **shilingi 55,086,788,000.00** sawa na **asilimia 73.60** ni matumizi ya kawaida na **shilingi 19,755,541,000.00** sawa na **asilimia 26.40** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA**

**Mheshimiwa Spika;** katika mwaka wa fedha 2025/26 Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma inatarajia kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kuendeleza ujazaji wa nafasi za ajira kulingana na vibali vya ajira mpya,ajira mbadala, na ajira za muda kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa masuala ya ajira ikiwemo; Wizara ya Fedha, Waajiri, Taasisi za Elimu ya Juu na Kati, pamoja na waomba kazi wenyewe;

(ii) Kuendeleza maboresho ya Mfumo wa Kupima Uelewa na Ufahamu waWasailiwa kwa Njia ya Mtandao (*Online Aptitude Test System*) ili kupunguza gharama kwa waombaji kazi;

(iii) Kuendeleza matumizi ya kanzidata kuwapangia vituo vya kazi wasailiwa waliofaulu usaili wa mahojiano ambao watakuwa ndani ya ukomo wa miezi 12 kadri nafasi wazi zitakavyopatikana;

(iv) Kuunganisha mifumo ya Sekretarieti ya Ajira na mifumo mingineinayotegemeana ili kurahisisha utoaji wa huduma;

(v) Kutoa elimu kwa umma kuhusu mchakato wa ajira kupitia vyombo vyahabari, makongamano, mitandao ya kijamii, maonesho, matukio ya kitaifa na matamasha mbalimbali;

(vi) Kuendeleza ujenzi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Kupima Tabia na Haiba za Wasailiwa (*Psychometric Testing System*);

(vii) Kufanya mikutano na wadau wa elimu ili kuwashauri kuzalisha wataalamambao watakidhi mahitaji ya mabadiliko ya Sera ya Elimu na mahitaji ya soko la ajira la sasa na baadaye; na

(viii) Kuimarisha ufuatiliaji, tathmini na upatikanaji wa takwimu za ajira.

**Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2025/26, Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Fungu 67 inaombakuidhinishiwa jumla ya **shilingi 14,603,888,000.00**. Kati ya fedha hizo **shilingi 13,195,060,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 1,408,828,000.00** ni fedha za miradi ya maendeleo.

**OFISI YA RAIS, TUME YA UTUMISHI WA UMMA**

**Mheshimiwa Spika;** katika mwaka wa fedha 2025/26, Tume ya Utumishi wa Umma itatekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kufanya mikutano minne (4) ya kisheria itakayojadili na kutolea uamuzirufaa, malalamiko na taarifa za masuala ya kiutumishi;

(ii) Kufanya Ukaguzi wa kawaida katika taasisi za umma 160 na ukaguzimaalum katika taasisi za umma 10 ili kutambua viwango vya uzingatiaji wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma;

(iii) Kuendeleza uhuishaji wa Mwongozo wa Masuala ya Ajira na Mwongozo kuhusu Masuala ya Kinidhamu;

(iv) Kutoa elimu kwa taasisi 570 za umma kuhusu majukumu ya Tume na uzingatiaji wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya usimamizi wa utumishi wa umma;

(v) Kuandaa Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Tume kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/25 na kuiwasilisha kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(vi) Kuendeleza uboreshaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa Kushughulikia Rufaa, Malalamiko, Ukaguzi wa Uzingatiaji wa Sheria na Uwasilishaji wa Taarifa za Kiutumishi;

(vii) Kufuatilia na kuhakiki vielelezo vya rufaa na malalamiko kutoka kwa Warufani na Mamlaka za Nidhamu; na

(viii) Kushirikiana na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kutoa ufafanuzi na kujibu hoja za mashauri ya Warufani yanayofikishwa Mahakamani.

**Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2025/2026, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma Fungu 94, inaomba kuidhinishiwa kiasi **shilingi 9,677,775,000.00**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 9,177,599,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 500,176,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**OFISI YA RAIS, IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA TAIFA**

**Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2025/26 Ofisi ya Rais - Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kutambua, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu, nyaraka na vitu vya Waasisi waTaifa (Mwl. Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume) na Marais wengine wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(ii) Kukusanya taarifa, kumbukumbu, nyaraka na machapisho mbalimbaliyanayohusu historia ya nchi yetu kutoka katika Taasisi za Umma na watu binafsi;

(iii) Kufanya ukarabati wa nyaraka kongwe zilizohifadhiwa katika Ghala Kuu la Nyaraka na zile zinazotarajiwa kukusanywa;

(iv) Kusanikisha na kuhuisha mifumo ya utunzaji wa kumbukumbu katika Taasisiza Umma ili kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma Serikalini;

(v) Kujenga uwezo wa Taasisi za Umma katika usimamizi wa kumbukumbu nanyaraka za Serikali kwa kuandaa mikutano na mafunzo kazi kwa watumishi wa umma kuhusu Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya utumiaji na utunzaji wa taarifa, kumbukumbu na nyaraka za Serikali;

(vi) Kufanya tathmini ya kumbukumbu tuli za Taasisi za Umma zilizohifadhiwa katika vituo vya kumbukumbu vya idara ili kubaini kumbukumbu zenye umuhimu wa kuendelea kuhifadhiwa na zile ambazo umuhimu wake wa matumizi umefikia ukomo kwa lengo la kuziteketeza kwa mujibu wa Sheria;

(vii) Kukagua, kuchambua na kuhamisha kumbukumbu tuli kutoka katika Taasisiza Umma na kuzihifadhi katika vituo vya kumbukumbu vya idara;

(viii) Kuwezesha Taasisi za Umma kutengeneza Mwongozo wa Kuhifadhi na Kuteketeza Kumbukumbu (*Record Retention and Disposal Schedules*) kwa mujibu wa Sheria;

(ix) Kufanya ukaguzi wa hali ya utunzaji wa kumbukumbu katika Taasisi za Umma 20;

(x) Kuendeleza uimarishaji wa Mfumo wa Kielektroniki katika Usimamizi wa Taarifa, Kumbukumbu na Nyaraka

kwa ajili ya kuzihifadhi kidijitali ili kurahisisha upatikanaji wake na kulinda nakala halisi; na

(xi) Kufanya ukarabati wa mashine za kurudufu (*Heavy Duty scanner*) nyaraka.

**Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2025/26, Ofisi ya Rais - Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa Fungu 4, inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi 6,150,699,000.00**. Kati ya fedha hizo, s**hilingi 4,973,241,000.00** ni matumizi ya kawaida na **shilingi 1,177,458,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**MAJUMUISHO**

**Mheshimiwa Spika,** katika kuhitimisha naomba tuanze kwa salamu iliyoasisiwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. KWAMBA:

***JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA! KAZI IENDELEE!!!***

**Mheshimiwa Spika,** maombi ya kuidhinishiwa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora yatawezesha uendelevu wa maamuzi ya kimkakati na maamuzi mengine muhimu kwa mustakabali wa nchi yetu. Sambamba na maamuzi mengine muhimu kwa nchi yetu kwa kuzingatia uendelevu wa utawala bora. Ofisi ya Rais Ikulu imekuwa karibu sana na miradi ya Kimkakati kama ilivyooneshwa katika Utekelezaji. Pia, ukamilishaji wa kuhamia Makao makuu Dodoma kwa kuweka miundombinu ya ofisi imekuwa kipaumbele na Taasisi za Ofisi yetu zinaendelea kukamilisha majengo yake na nyingine zimehamia kabisa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa hati idhini, Ofisi ya Rais ikiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeendeleza utekelezaji wa dhamana ya kufanya maamuzi kuhusu nchi na kwa umuhimu wake Menejimenti ya Utumishi wa Umma na utawala bora imepewa kipaumbele kwa kuzingatia mkakati wa 4R, ambavyo kwa pamoja inakuwa ni nguzo kuu katika uendeshaji na uendelezaji wa nchi. Maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu

Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kuwa na Utumishi wa Umma wenye Ufanisi na Uwajibikaji katika kustawisha Taifa kwa kusimamia uendeshaji wa shughuli za Serikali na usimamizi wa rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma kwa kutumia Sera, Sheria Miundo na mifumo iliyoboreshwa. Ndio maana mipango iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako tukufufu imejikita katia kuweka misingi ya utekelezaji wa mwelekeo huo.

**Mheshimiwa Spika,** Utumishi wa Umma na utawala bora una mchango mkubwa katika maendeleo ya taifa, na ni dhahiri kuwa mchango endelevu wa watumishi wa umma utaliendeleza taifa na kuleta ustawi kwa Watanzania wote. Aidha, maendeleo haya yanatarajiwa kuongezeka kwa kuimarisha uchumi shindani na viwanda kwa manufaa ya watu, kama inavyosisitizwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP III).

**Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imelenga kuandaa mazingira ambayo yatasaidia nchi katika kipindi cha kuelekea kwenye Uchanguzi Mkuu na kuingiza Serikali mpya. Hayo yote yatafanyika kwa kutii Katiba na kuzingatia ipasavyo Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo katika kujenga imani zaidi kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua fursa hii kumpongeza tena Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutuwezesha kuimarisha utumishi wa umma kuendana na wakati, ambapo maelekezo yake na uwezeshaji kifedha umesaidia hatua zaidi kupigwa kwenye kujenga uwezo na mifumo ya kimenejimenti na utoaji huduma ikiwemo matumizi sahihi na salama ya fursa zinazopatikana katika utoaji huduma kwa TEHAMA ndani ya Serikali. Hali hiyo imesaidia kuondokana na vitendo visivyo na tija katika uzingatiaji wa maadili ya utumishi wa umma.

**Mheshimiwa Spika,** maombi ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora yatawezesha vyombo vinavyosaidia kwenye maamuzi ya nchi, usalama na kuimarisha vita dhidi ya rushwa. Hivyo, kupitisha Bajeti

ya Ofisi hii ni kuchangia katika uimarishaji na uwezeshaji wa vyombo hivyo na malengo yake kwa Taifa. Aidha, kupitisha bajeti hii ni hatua muhimu katika kukuza na kuimarisha maadili ya viongozi wote na watumishi wa umma, huku ikichangia katika ufanisi wa matumizi ya rasilimaliwatu na rasilimali fedha za nchi. Bajeti hii pia itawezesha Serikali kutekeleza hatua muhimu kama vile kutoa fursa za ajira mpya, kupandisha vyeo watumishi, kufanya mabadiliko katika muundo wa utumishi, na kulipa malimbikizo ya mishahara. Kipaumbele kikubwa kitaelekezwa katika eneo la usimamizi wa rasilimaliwatu na rasilimali fedha, ili kuhakikisha kuwa matumizi yanakuwa yenye tija na yanayolingana na malengo ya maendeleo ya kitaifa.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi kupitia bajeti ya mwaka 2025/26 itahakikisha kunakuwepo na utawala bora ulio imara katika ngazi zote za uongozi ndio maana hata mafunzo kwa watakaoteuliwa kuingia katika Serikali mpya wanapata mafunzo ili kuwa watumishi wa umma wenye weledi katika kutekeleza shughuli za umma. Msisitizo wa mafunzo utakuwa ni kuimarisha misingi ya utawala bora ushirikishwaji, uwazi na uwajibikaji. Ofisi ya Rais pia utaweka mifumo ya kuhakikisha kuwa wananchi wanapata taarifa sahihi kuhusu maamuzi ya Serikali na kuimarisha mifumo ya kutoa mrejesho kuhusu huduma zinazotolewa kwa umma. Mmeona kuwa hata umoja wa mataifa umetambua ubunifu wa nchi yetu katika kushirikisha wananchi katika uendeshaji wa shughuli za Serikali kupitia mfumo wa *e-Mrejesho* ambao nawaomba waheshimiwa Wabunge mkawahamasishe wananchi kuutumia kutoa pongezi wanapoona Serikali yao imefanya vizuri na kutoa maoni ya mahali wanapoona panahitaji maboresho zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Hati Idhini, nawajibika kuwasilisha mapitio ya utekelezaji mipango na bajeti ya Ofisi ya Rais Ikulu; Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma; na Ofisi ya Rais, Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa. Hivyo, nalihakikishia Bunge lako tukufu kuwa Mipango na Bajeti kwa Mafungu niliyoyataja yamezingatia vipaumbele vya Serikali ya Awamu ya Sita kwenye

eneo la kuimarisha utendaji kazi katika Utumishi wa Umma na kuifanya nchi yetu iondokane na matumizi mabaya ya rasilimali fedha, ukiukwaji wa maadili ya uongozi na kupunguza urasimu usio na lazima katika utoaji huduma kwa kufanya mapitio ya michakato ya utoaji huduma na hivyo kuongeza tija katika kutekeleza masuala yenye masilahi mapana kwa Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2024/25 na Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora sasa naomba kuwasilisha rasmi mapendekezo ya maombi kwa mwaka 2025/26 kwa muhtasari kama ifuatavyo: -

**Mheshimiwa Spika na Wabunge wenzangu,** Jumla kuu ya Bajeti ninayoomba kwa Mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais (Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) kwa mwaka 2025/26 kama ilivyoanishwa katika jedwali hapo juu ni **shilingi 1,354,350,324,000.00**. Kati ya kiasi hicho **shilingi 1,171,035,237,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 183,315,087,000.00** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika na Wabunge wenzangu,** mwisho naomba kuwasilisha maombi haya ili muweze kuyajadili na kuyaidhinisha.

**Ahsanteni kwa kunisikiliza, naomba kutoa hoja.**

**George B. Simbachawene (Mb)**
**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS**
**(MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA)**

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Sasa tunaendelea na utaratibu wetu. Mwenyekiti anakuja kunipokea. *(Makofi)*

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria. Mheshimiwa Florent Kyombo ambaye ni Makamu Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninaomba taarifa yote hii iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge. Sehemu ya kwanza, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, kuhusu Utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuliwezesha Bunge kufuatilia taarifa hii ipasavyo, ninaomba kutambulisha sehemu nne za taarifa hii ambazo ni:-

(i) Sehemu ya Kwanza inahusu maelezo ya jumla, inabainisha msingi na muundo wa taarifa hii;

(ii) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi wa Utekelezaji wa bajeti kwa kuangalia mwenendo wa upatikanaji wa fedha na uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati;

(iii) Sehemu ya Tatu inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati; na

(iv) Sehemu ya Nne ni Hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa Kamati kuchambua Taarifa hii ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge. Kifungu cha 6(2)(a) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, zinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka taarifa ya utekelezaji na makadirio ya ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Ninaomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mawanda ya uchambuzi; katika uchambuzi huo, Kamati ilipitia jumla ya Mafungu saba ambayo ni: -

(i) Fungu 20: Ofisi ya Rais, Ikulu;

(ii) Fungu 30: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri;

(iii) Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma;

(iv) Fungu 33: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(v) Fungu 67: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;

(vi) Fungu 94: Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma; na

(vii) Fungu 04: Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matokeo ya uchambuzi na tathmini. Matokeo ya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa bajeti na makadirio ya mapato na matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja hii ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kwa msingi huo, ili kuwezesha ufuatiliaji mzuri wa wasilisho hili, Taarifa hii imejielekeza kwenye maeneo yafuatayo: -

(i) Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(ii) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(iii) Uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge; na

(iv) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Ninapenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati ilizingatia Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kazi hiyo ilifanyika tarehe 26 na 27 Machi, 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi huo umejikita kwenye kulinganisha uwiano wa fedha zilizoidhinishwa, fedha zilizopokelewa pamoja na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Uchambuzi huo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu Namba 20 na Fungu Namba 30 – Ofisi ya Rais, Ikulu na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Kuhusu Fungu 20; kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Fungu Namba 20 – Ofisi ya Rais (Ikulu) iliidhinishiwa jumla ya shilingi 33,544,557,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Kati ya fedha hizo, shilingi 10,706,049,000 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi 22,838,508,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari 2025, Fungu Namba 20 lilipokea jumla ya shilingi 22,494,979,924.20 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, sawa na 67.06% ya kiasi kilichoidhinishwa. Ambapo shilingi 7,237,861,948.29 sawa na 67.62% ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 15,257,117,975.91, sawa na 66.80% ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Fungu Namba 30. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Fungu Namba 30 – Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri iliidhinishiwa jumla ya shilingi 805,676,639,000, kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 801,397,341,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 4,279,298,000 zilitengwa kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2025 fungu hili lilipokea jumla ya shilingi 561,268,055,905.49 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, sawa na 69.66% ya kiasi kilichoidhinishwa ambapo shilingi 2,853,007,976.60 sawa na 66.67% ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 558,415,047,928.89 sawa na 69.68% ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, fedha zilizopokelewa zimetumika kwa 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bajeti ya maendeleo; Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri – Fungu 30 iliidhinishiwa fedha za matumizi ya maendeleo jumla ya shilingi 163,609,084,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 110,439,177,000 ni za ndani na shilingi 53,169,907,000 ni za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2025 kiasi cha shilingi 100,918,998,288, sawa na 61.68% kimepokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Fungu Namba 32 – Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, fungu hili liliidhinishiwa jumla ya shilingi 58,314,993,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 48,254,069,000 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo shilingi 17,182,556,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 31,071,513,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, shilingi 10,060,924,000 zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo shilingi 9,933,174,000 ni fedha za ndani na shilingi 127,750,000 ni kwa ajili ya fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2025 fungu hili lilipokea jumla ya shilingi 39,092,298,613.98, sawa na 67.04% ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi 34,116,184,613.98 sawa na 70.70% zilipokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo shilingi 24,153,262,300.37, sawa na 77.73% zilipokelewa kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 9,962,922,313.61, sawa na 57.98% zilipokelewa kwa ajili ya mishahara. Aidha, shilingi 4,976,114,000 sawa na 49.46% zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Fungu Namba 33 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 fungu hili liliidhinishiwa jumla ya shilingi 13,142,650,000 kwa ajili ya matumizi ya Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Viongozi wa Umma. Kati ya fedha hizo shilingi 11,642,650,000 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo shilingi 7,869,966,000 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 3,772,684,000 zilitengwa kwa ajili ya mishahara. Aidha, shilingi 1,500,000,000 zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2025, Fungu hili lilipokea jumla ya shilingi 7,624,797,245.65, sawa na 65% ambapo shilingi 5,339,169,305.65 zilipokelewa kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 2,885,627,940 zilipokelewa kwa ajili ya

mishahara. Aidha, shilingi 426,078,837.48 zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Fungu Namba 67 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya shilingi 10,831,831,000 ambazo zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Ambapo kati ya fedha hizo, mishahara ilikuwa ni shilingi 2,263,460,000, sawa na 20.9% na matumizi mengineyo ilikuwa ni shilingi 8,568,371,000, sawa na 79.10%. Aidha, shilingi 2,348,047,000 zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2025, Fungu hili lilipokea jumla ya shilingi 5,054,476,665.27, sawa na 46.66% zilipokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo shilingi 5,054,476,665.27, sawa na 100% ilikuwa ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 3,756,057,675.03 sawa na 43.84% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, shilingi 1,610,947,000 sawa na 68.61% zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Fungu Namba 94 – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi wa Umma ilitengewa jumla ya shilingi 9,240,889,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo; ambapo kati ya fedha hizo, shilingi 8,740,713,000 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo kati ya fedha hizo, shilingi 6,304,687,000 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 2,436,026,000 zilitengwa kwa ajili ya mishahara. Aidha, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya shilingi 500,176,000 fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2025, Fungu hili lilipokea jumla ya shilingi 6,092,509,505, sawa na 69.7% zilipokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo shilingi 1,452,996,744, sawa na 59.6% ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 4,639,512,761, sawa na 73.6% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, shilingi 500,176,000, sawa na 100% zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Fungu Na.4 – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa; kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 fungu hili liliidhinishiwa jumla ya shilingi 4,065,013,000 ambazo zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Ambapo shilingi 2,520,394,000 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 1,544,619,000 zilitengwa kwa ajili ya mishahara. Aidha, shilingi 295,746,000 zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2025, Fungu hili lilipokea jumla ya shilingi 3,005,044,599.85, sawa na 68.91% ya fedha iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi 2,885,044,599.85, sawa na 70.97% zilipokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Ambapo shilingi 940,361,000 zilipokelewa kwa ajili ya mishahara na shilingi 1,944,683,599.85 zilipokelewa kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, shilingi 120,000,000, sawa na 40.58% zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa upatikanaji wa fedha hizo unaonesha kwamba:-

(i) Kwa ujumla, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora iliidhinishiwa shilingi 934,316,396,000 kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Hadi kufikia Februari, 2025 ofisi hii ilipokea jumla ya shilingi 622,159,677,514.44, sawa na 66.6% ya bajeti iliyoidhinishiwa na Bunge.

(ii) Taasisi tano kati ya taasisi saba za Ofisi hii zilifanikiwa kupata kiasi cha fedha ambacho kinaendana na uwiano wa upatikanaji wa fedha kwa 66.6% hadi kufikia Februari, 2025.

(iii) Ofisi hii pia inaweza kukusanya maduhuli kupitia taasisi zinazofanya biashara kama vile Wakala wa Ndege za Serikali anayekodisha ndege zake kwa Kampuni ya Ndege Tanzania *(ATCL)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kwamba, mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ujumla ni wa kuridhisha. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali ihakikishe kwamba fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya taasisi zilizopo chini ya ofisi hii zinapatikana kabla ya kuisha kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchanganuo wa fedha hizo kwa taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni kama inavyoonyeshwa katika Jedwali Na.1 na Jedwali Na.2 yaliyopo kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa mipango na majukumu ya Ofisi ya Rais; Bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ililenga kufanikisha utekelezaji wa mipango na majukumu ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na taasisi zilizopo chini ya Ofisi hiyo. Ili kuliwezesha Bunge kujiridhisha na mwenendo wa matumizi unaoakisi madhumuni ya kuidhinishwa kwa bajeti hiyo, Kamati ilichambua utekelezaji wa mipango na majukumu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa bajeti umezingatia mipango na majukumu yaliyoombewa fedha. Aidha, Ofisi hii ilitumia fedha zilizopatikana kusimamia na kuimarisha misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo, Kamati inampongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa usimamizi madhubuti wa utawala bora nchini. Ni maoni ya Kamati kuwa, usimamizi na uratibu wa shughuli za utumishi wa umma umeimarika sana katika misingi ya haki, uwajibikaji na utawala bora, hali ambayo imeendelea kuipandisha nchi yetu katika medani za utawala bora Afrika na duniani kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo; kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Ofisi hii ilitengewa jumla ya shilingi 178,313,977,000 kwa ajili ya miradi ya

maendeleo. Hadi kufikia Februari, 2025, Ofisi hii ilipokea jumla ya shilingi 108,552,314,125.48 ya fedha za maendeleo sawa na 60.88% ya fedha za maendeleo zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitembelea miradi minne inayosimamiwa na Wizara na kuchambua utekelezaji wa miradi hiyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi Na. 6220, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)*.

(a) Ujenzi wa madarasa Bagamoyo Mwavi. Kwa Mwaka Wa Fedha 2024/2025, Mradi huu ulitengewa jumla ya shilingi 203,511,528.74 kwa ajili ya utekelezaji wa Ujenzi wa madarasa manne, matundu sita ya choo na ujenzi wa ofisi ya walimu. Kamati ilielezwa kuwa mradi huu unatekelezwa kwa wanufaika 150 ambao ni wanafunzi wa shule za msingi na wanafunzi 31 ambao ni wanafunzi wa shule ya awali wanaolazimika kutembea umbali mrefu kutoka Vitongoji vya Kudibaha na Senganga ili kuitafuta elimu. Mradi huo unatekelezwa na *TASAF* katika Kijiji cha Mwavi, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2025 mradi umepokea kiasi cha shilingi 139,479,416.11 sawa na 68.54% ya gharama ya mradi. Kamati ilielezwa kuwa hakuna madai yoyote ya Mkandarasi yaliyowasilishwa. Aidha, utekelezaji wa ujenzi wa mradi huo mpaka wakati Kamati imetembelea umefikia 38%;

(b) Ujenzi wa madarasa na jengo la utawala - Muheza *(TASAF)*. Kamati ilielezwa kuwa shule ilipokea kiasi cha shilingi 347,622,637.84 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba sita vya madarasa, ofisi tatu za Walimu, matundu 12 ya vyoo na jengo la utawala ambao utawawezesha walengwa kupata mazingira mazuri ya kujifunzia na walimu kufundishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo umekamilika kwa 100% ukiwa umeshatumia kiasi chote cha fedha kama ilivyoidhinishwa. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa mradi umekabidhiwa kwa Serikali ya Kijiji chini ya uangalizi wa Shule ya Sekondari Magila. Mchanganuo wa fedha na matumizi ya fedha hizo, unaonekana katika jedwali namba tatu hapa chini ambalo limeambatishwa pamoja na picha za mradi huo kama zinavyoonekana kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kamati kukagua mradi huu na kukutana na wanufaika wa *TASAF*, Kamati ilipokea shukrani za dhati zilizoelekezwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali yake kwa ujumla kwa kuboresha miundombinu ya elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati ilibaini kuwa miundombinu mibovu ya majengo ya shule yalikuwa ni changamoto iliyosababisha wanufaika hao kuwa na mahudhurio hafifu shuleni na ufaulu wa wanafunzi kutokuwa mzuri. Hivyo, mradi huu ni tija kwa Taifa na Kamati inaipongeza Serikali na wananchi wa Tarafa ya Muheza na Ngomeni kwa ujumla kwa utekelezaji mzuri wa mradi huo.

(c) Kutembelea na Kukagua utekelezai wa mradi wa ujenzi wa Kivuko Sembeti - Moshi Vijijini *(TASAF)*. Mradi wa ujenzi wa kivuko umekusudia kutatua changamoto ya usafiri iliyokuwa ikisababishwa na ubovu wa daraja. Hivyo, ujenzi wa daraja hili utawezesha wananchi kuendelea na shughuli za kiuchumi katika maeneo hayo bila kikwazo. Aidha, mradi huu utaunganisha Wananchi wa Kijiji cha Samanga na Sembeti ambavyo vinapatikana katika Kata ya Marangu Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa mradi umetumia jumla ya shilingi 131,658,312 kutoka *TASAF*. Pia, mradi umepokea mchango wa wananchi pamoja na wadau mbalimbali, hii ni kutokana na masharti ya miradi ya *TASAF* kuwa na sharti la jamiii kuchangia 10% ya gharama za mradi kwa kutoa fedha au mahitaji yanayopatikana kwa urahisi katika eneo husika.

Mradi huo umekamilika kwa 93% na umekabidhiwa kwa wananchi, asilimia saba iliyobaki ni ukarabati mfereji wa asili wa kupitisha maji ambao uliathiriwa na maporomoko ya udongo wakati wa utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inawapongeza wananchi wa Sembeti, Samanga na Serikali kwa ujumla kwa utekelezaji mzuri wa mradi huo. Viambatisho vya ujenzi wa daraja hilo, vinaonekana katika picha namba nne hadi sita kuonesha hali ya daraja ilivyokuwa awali na ilivyo kwa sasa. Picha namba nne, inaonyesha mwonekano wa daraja kabla ya mradi na picha namba tano, inaonyesha picha ya daraja baada ya utekelezaji wa mradi kama zinavyoonekana kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi Na. 6203, ujenzi wa jengo la Ofisi ya TAKUKURU, Wilaya ya Rombo. Kamati ilielezwa kuwa mradi ulipokea kiasi cha shilingi 299,969,119.9 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Ofisi za TAKUKURU – Rombo hadi kukamilika kwake. Mradi umetumia kiasi cha shilingi 290,187,386, kiasi kilichobaki ni shilingi 9,781,733.90 sawa na asilimia 3.26 ya makadirio ya gharama ya utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iliambiwa kuwa, kutokana na uwepo wa bakaa ya fedha, iliamuliwa kuongeza kazi ya kusawazisha ardhi *(landscaping)*, kuweka *paving blocks* na kuweka kinga ya pembeni kwa ajili ya watu wenye mahitaji maalum. Aidha, kutokana na kuongezeka kwa kazi za nyongeza, mradi ulipokea nyongeza ya shilingi 20,941,431 ili ziweze kukamilisha mradi. Mradi huo umekamilika kwa 100% ukiwa umeshatumia kiasi chote cha fedha. Mradi huo utaiwezesha ofisi hii katika mapambano dhidi ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uzingatiaji wa ushauri wa Kamati. Wakati wa kupitia na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo kumi na mbili. Ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa kiasi kikubwa ushauri wa Kamati umezingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Kanuni za Kudumu za Bunge zimetambua umuhimu wa uzoefu unaopatikana katika mwaka wa fedha unaoisha ili kuchambua makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Bunge. Kamati imezingatia umuhimu huo na masharti ya Kanuni za Bunge kwa kuchambua makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, uchambuzi wa matumizi ya kawaida. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Ofisi Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na taasisi zilizo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 1,171,035,237,000 ikiwa ni fedha za matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya matumizi ya kawaida katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 imeongezeka kwa 25.54% ukilinganisha na mwaka wa fedha unaoisha, ambapo bajeti ya matumizi ya kawaida ilikuwa shilingi 932,816,396,000. Kamati imebaini ongezeko kubwa la bajeti, hivyo ni maoni ya Kamati kuwa Serikali ipange bajeti kulingana na mahitaji halisi. Aidha, ongezeko hilo linaakisi mahitaji ya kifedha kulingana na sababu mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kuongezeka kwa watumishi, kupanda kwa bei ya bidhaa na huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazoombwa zinatumika vizuri, ili kuhakikisha hili linatekelezwa ipasavyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inawasilisha mbele ya Kamati taarifa mbalimbali za utekelezaji wa bajeti kwa mujibu wa Sheria. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama unavyoonekana kwenye jedwali Namba Nne lililopo kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, uchambuzi wa miradi ya maendeleo. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 183,315,087,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi

114,776,309,000 ni fedha za ndani na shilingi 68,538,778,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 imeongezeka kwa shilingi 5,001,110,000 sawa na asilimia 2.81 ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama unavyoonekana kwenye jedwali namba tano lililopo kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza jitihada za Serikali kuendelea kupanga bajeti ili kutekeleza miradi mingi zaidi kwa kutumia fedha za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu, maoni na ushauri wa Kamati. Maoni, baada ya maelezo hayo, ninaomba kukamilisha uchambuzi kwa kubainisha maoni ya Kamati yanayolenga mtazamo ambao ni msingi wa ushauri wa Kamati. Maoni hayo ni kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ihakikishe upatikanaji wa kiasi chote cha fedha ya bajeti kama iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii ili kutekeleza mipango iliyokusudiwa kwa mwaka wa fedha unaoisha;

(b) Serikali itengeneze Mfumo wa malipo ambao utakuwa ni mwongozo kwa ofisi za umma na Serikali kwa lengo la kuwasaidia vijana wanaojitolea katika nafasi mbalimbali;

(c) Baada ya Mpiga Chapa wa Serikali kuboreshewa mazingira ya utendaji kazi kwa kiwango kinachoendana na wakati, ni maoni ya Kamati kuwa, machapisho yote na nyaraka za Serikali, zichapishwe na wakala huyu wa Serikali ili kulipunguzia Taifa gharama;

(d) Suala la kuajiri watumishi wa kada mbalimbali katika Utumishi wa Umma lisimamiwe na taasisi moja;

(e) Ili kupunguza wimbi la ukosefu wa ajira kwa vijana, Serikali ibadilishe kipaumbele cha kutoa mkopo kutoka kada ya elimu na kuzingatia kada nyingine muhimu ambazo Taifa lina upungufu wa wataalam kwa maendeleo mapana ya Taifa; na

(f) Kwa kuwa vijana wengi wamekosa ajira, Serikali iangalie namna nzuri ya kuwafanyia mafunzo na kuwatafutia nafasi katika soko la ajira nje ya nchi ili kuwakwamua vijana kutoka katika wimbi la kukosa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ushauri wa Kamati; kwa maoni niliyobainisha kutokana na uchambuzi, naomba kutoa ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ihakikishe kuwa fedha inayoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya ofisi hii na taasisi zake inapatikana ipasavyo ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu yaliyopangwa;

(b) Serikali iendelee kuimarisha misingi ya utawala bora pamoja na kuboresha mifumo ya utendaji kazi katika Utumishi wa Umma sambamba na kuboresha mishahara na maslahi ya watumishi;

(c) Serikali iendelee kusimamia na kutoa mafunzo maalum ya mara kwa mara kwa Watumishi wa Umma ili kuwezesha utendaji kazi unaozingatia weledi na ustadi mkubwa;

(d) Ili kuondoa tatizo la kila taasisi kuajiri watumishi wake, Serikali ihakikishe kuwa mifumo ya ajira inasomana, na mamlaka ya kuajiri yanabaki kwa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; na

(e) Serikali iboreshe mfumo wa Kufanya Usaili kwa njia ya Mtandao *(Online Aptitude Test)* ili maswali yaendane na nafasi za kazi zinazohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Nne; hitimisho. Ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa uongozi wao na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Ninapenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Ninaomba majina yao yaingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ushirikiano mkubwa ambao ameendelea kuipa Kamati pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Deus Clement Sangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia niwashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioupatia Kamati wakiongozwa na Makatibu Wakuu wa Ofisi hiyo Ndugu Juma Selemani Mkomi Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Ndugu Majula Mahendeka Katibu Mkuu Ikulu na Wakuu wote wa Taasisi ndani ya Ofisi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninapenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Baraka Ildephonce Leonard kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya nchi. Aidha, kiupekee nawashukuru Sekretarieti ya Kamati kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho katika shukrani zangu kwa ruhusa yako niwashukuru pia wananchi wa Jimbo la Nkenge, Wilaya ya Missenyi kwa kuendelea kuniamini, ninaomba waendelee kunituma na mimi niko tayari kendelea kuwatumikia kwa ajili ya maendeleo ya Jimbo la Nkenge, Wilaya ya Missenyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

## TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMANA UTAWALA BORA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

---

### SEHEMU YA KWANZA

1.0 **UTANGULIZI**

**1.1** Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118(9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, kuhusu Utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge kufuatilia taarifa hii ipasavyo, naomba kutambulisha sehemu nne za Taarifa hii ambazo ni:-

(a) Sehemu ya **Kwanza** inahusu maelezo ya jumla, inabainisha msingi na muundo wa Taarifa hii;

(b) Sehemu ya **Pili** inahusu uchambuzi wa Utekelezaji wa bajeti kwa kuangalia mwenendo wa upatikanaji wa fedha na uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati;

(c) Sehemu ya **Tatu** inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati;

(d) Sehemu ya **Nne** ni Hitimisho.

**1.2** Msingi wa Uchambuz**i**

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa Kamati kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge. Kifungu cha 6(2)(a) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, zinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

**1.3 Mawanda ya Uchambuzi**

**Mheshimiwa Spika,** Katika uchambuzi huo, Kamati ilipitia jumla ya mafungu saba (7) ambayo ni:-

(a) **Fungu 20**: Ofisi ya Rais, Ikulu;

(b) **Fungu 30:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri;

(c) **Fungu 32:** Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma;

(d) **Fungu 33:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(e) **Fungu 67:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;

(f) **Fungu 94:** Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma; na

(g) **Fungu 04:** Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.

**SEHEMU YA PILI**

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI

### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja hii ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kwa msingi huo, ili kuwezesha ufuatiliaji mzuri wa wasilisho hili, Taarifa hii imejielekeza kwenye maeneo yafuatayo:-

(a) Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(b) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(c) Uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge; na

(d) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

## 2.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati ilizingatia Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kazi hiyo ilifanyika tarehe 26 na 27 Machi, 2025. Uchambuzi huo umejikita kwenye kulinganisha uwiano wa fedha zilizoidhinishwa, fedha zilizopokelewa pamoja na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Uchambuzi huo ni kama ifuatavyo: -

### 2.2.1 Fungu Na. 20 na Fungu Na. 30 – OFISI YA RAIS (IKULU) NA SEKRETARIETI YA BARAZA LA MAWAZIRI.

**FUNGU 20**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2024/2025 **Fungu Na. 20** - Ofisi ya Rais (Ikulu) iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 33,544,557,000.00 /=** kwa ajili ya Matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Sh. 10,706,049,000.00/=** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) ya Watumishi na **Sh. 22,838,508,000/=** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Februari 2025, Fungu 20 lilipokea jumla ya **Sh. 22,494,979,924.20/=** kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 67.06 ya kiasi** kilichoidhinishwa ambapo **Sh. 7,237,861,948.29 /=** sawa na asilimia **67.62** ni kwa ajili ya mishahara na **Sh. 15,257,117,975.91/=** sawa na asilimia **66.80** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**FUNGU 30**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Fungu 30 -Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 805,676,639,000.00/=**, kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida kati ya fedha hizo **Sh. 801,397,341,000.00/=** kwa ajili ya matumizi

mengineyo (OC) na **Sh. 4,279,298,000.00/=** zilitengwa kwa ajili ya mishahara (PE).

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2025 Fungu hili lilipokea Jumla ya **Sh. 561,268,055,905.49/=** kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia **69.66** ya kiasi kilichoidhinishwa ambapo **Sh. 2,853,007,976.60** sawa na asilimia **66.67** ni kwa ajili ya mishahara na **Sh. 558,415,047,928.89** sawa na asilimia **69.68** kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, fedha zilizopokelewa zimetuumika kwa asilimia **100.**

**BAJETI YA MAENDELEO**

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri – Fungu 30 iliidhinishiwa fedha za matumizi ya maendeleo **Sh.163,609,084,000.00/=** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Sh.110,439,177,000.00/=** ni za Ndani na **Sh. 53,169,907,000.00**/= ni za Nje.

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Februari, 2025 kiasi cha **Sh. 100,918,998,288.00** sawa na asilimia **61.68** kimepokelewa na kutumika.

**2.2.2 Fungu Na. 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **Sh. 58,314,993,000.00/=**. Kati ya fedha hizo **Sh. 48,254,069,000.00/=** zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo **Sh. 17,182,556,000.00/=** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) na **Sh. 31,071,513,000.00/=** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Aidha **Sh. 10,060,924,000.00/=** zilitengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo **Sh. 9,933,174,000.00/=** ni fedha za ndani na **Sh. 127,750,000.00 /=** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2025 Fungu hili lilipokea jumla ya **Sh. 39,092,298,613.98/=** sawa na **asilimia 67.04** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo **Sh. 34,116,184,613.98/=**

sawa na **asilimia 70.70** zilipokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo **Sh. 24,153,262,300.37/=** sawa na asilimia **77.73** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Sh. 9,962,922,313.61/=** sawa na Asilimia **57.98** zilipokelewa kwa ajili ya Mishahara (PE). Aidha, **Sh. 4,976,114,000.00/=** sawa na **asilimia 49.46** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**2.2.3 Fungu Na. 33 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **Sh.13,142,650,000.00/=** kwa ajili ya matumizi ya Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Viongozi wa Umma, kati ya fedha hizo **Sh. 11,642,650,000.00**/= zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Sh. 7,869,966,000.00/=** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Sh. 3,772,684,000.00/=** zilitengwa kwa ajili ya mishahara (PE). Aidha, **Sh. 1,500,000,000.00/=** zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2025 Fungu hili lilipokea Jumla ya **Sh. 7,624,797,245.65/=** sawa na **asilimia 65** ambapo **Sh. 5,339,169,305.65/=** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Sh. 2,285,627,940.00/=** zilipokelewa kwa ajili ya Mishahara (PE) na **Sh. 426,078,837.48/=** zilipokelewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**2.2.4 Fungu Na. 67 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **Sh. 10,831,831,000.00/=** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo kati ya fedha hizo, Mishahara (PE) ni **Sh. 2,263,460,000.00/=** sawa na asilimia **20.90** na Matumizi Mengineyo (OC) ni **Sh. 8,568,371,000.00/=** sawa na asilimia **79.10**. Aidha, **Sh. 2,348,047,000.00/=** zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2025 Fungu hili lilipokea Jumla ya **Sh. 5,054,476,665.27/=** sawa na **asilimia 46.66**

zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Sh. 5,054,476,665.27 sawa na asilimia 100** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) na **Sh. 3,756,057,675.03** sawa na **asilimia 43.84** ni kwa ajili ya matumizi ya Kawaida (OC). Aidha, **Sh. 1,610,947,000.00** sawa na **asilimia 68.61** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

### 2.2.5 Fungu Na. 94 – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi wa Umma ilitengewa jumla ya **Sh.9,240,889,000.00/=** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo; ambapo kati ya fedha hizo **Sh**. **8,740,713,000.00/=** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo **Sh. 6,304,687,000.00/=** zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na Sh. **8,740,713,000.00/=** zilitengwa kwa ajili ya mishahara (PE).

Aidha, Fungu hili liliidhinishiwa **Sh.500,176,000.00/=** fedha za ndani kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2025 Fungu hili lilipokea Jumla ya **Sh.6,092,509,505** sawa na **asilimia 69.7** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Sh. 1,452,996,744.00/=** sawa na **asilimia 59.6** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) na **Sh. 4,639,512,761.00/=** sawa na **asilimia 73.6** ni kwa ajili ya matumizi ya Kawaida (OC). Aidha, **Sh. 500,176,000.00/=** sawa na **asilimia 100** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

### 2.2.6 Fungu Na. 04 – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **Sh. 4,065,013,000.00/=**. zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo **Sh. 2,520,394,000.00/=** zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na **Sh. 1,544,619,000.00/=** zilitengwa kwa ajili ya Mishahara (PE). Aidha, **Sh. 295,746,000.00/=** zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2025 Fungu hili lilipokea Jumla ya **Sh. 3,005,044,599.85/=** sawa na **asilimia 68.91** ya fedha iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo **Sh. 2,885,044,599.85/=** sawa na **asilimia 70.97** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo **Sh. 940,361,000.00/=** zilipokelewa kwa ajili ya Mishahara (PE) na **Sh. 1,944,683,599.85/=** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Aidha, **Sh. 120,000,000.00/=** sawa na **asilimia 40.58** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa upatikanaji wa fedha hizo unaonesha kwamba:

(a) Kwa ujumla, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora iliidhinishiwa **Sh. 934,316,396,000/=** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, hadi kufikia Februari, 2025 Ofisi hii ilipokea Jumla ya **Sh. 622,159,677,514.44/=** sawa na **asilimia 66.6** ya bajeti iliyoidhinishiwa na Bunge.

(b) Taasisi tano (5) kati ya Taasisi saba za Ofisi hii zilifanikiwa kupata kiasi cha fedha ambacho kinaendana na uwiano wa upatikanaji wa fedha kwa **asilimia 66.6** hadi kufikia Februari, 2025.

(c) Ofisi hii pia inaweza kukusanya Maduhuli kupitia taasisi zinazofanya biashara kama vile Wakala wa Ndege za Serikali anaekodisha ndege zake kwa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL).

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kwamba, mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ujumla ni wa kuridhisha. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali ihakikishe kwamba fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya taasisi zilizo chini ya Ofisi hii zinapatikana kabla ya kuisha kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, Mchanganuo wa fedha hizo kwa taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 1** na **Jedwali Na. 2**

## Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida 2024/2025

| FUNGU | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2024/2025 | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2025 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 20** – Ofisi ya Rais (Ikulu) | 33,544,557,000/= | 22,494,979,924.20/= | 69.06 |
| **Fungu 30** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri | 805,676,639,000/= | 561,268,055,905.49/= | 69.66 |
| **Fungu 32** – Ofisi Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora | 58,314,993,000/= | 39,092,298,613.98/= | 67.04 |
| **Fungu 33** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma | 13,142,650,000/= | 7,624,797,245.65/= | 65 |
| **Fungu 67** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma | 10,831,831,000/= | 5,054,476,665.27/= | 46.66 |
| **Fungu 94** – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma | 8,740,713,000/= | 6,092,509,505/= | 69.7 |
| **Fungu 04** – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa | 4,065,013,000/= | 3,005,044,599.85/= | 68.91 |
| **JUMLA KUU** | **934,316,396,000/=** | **622,159,677,514.44/=** | **66.6** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, 2025.*

## Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo 2024/2025

| FUNGU | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2024/2025 | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2025 | AS ILIMIA YA MAPOKE ZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 30** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri | 163,609,084,000/= | 100,918,998,288/= | 61. 68 |
| **Fungu 32** – | 10,060,924,000/= | 4,976,114,000/= | 49. |

| FUNGU | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2024/2025 | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2025 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| Ofisi Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora | | | 46 |
| **Fungu 33** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma | 1,500,000,000/= | 426,078,837.48/= | 28.41 |
| **Fungu 67** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma | 2,348,047,000/= | 1,610,947,000/= | 68.61 |
| **Fungu 94** – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma | 500,176,000/= | 500,176,000/= | 100 |
| **Fungu 04** – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa | 295,746,000/= | 120,000,000/= | 40.58 |
| **JUMLA KUU** | **178,313,977,000/=** | **108,552,314,125.48/=** | **60.88** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, 2025.*

## 2.3 Utekelezaji wa Mipango na Majukumu ya Ofisi ya Rais

**Mheshimiwa Spika**, bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ililenga kufanikisha utekelezaji wa mipango na majukumu ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na taasisi zilizopo chini ya Ofisi hiyo. Ili kuliwezesha Bunge kujiridhisha na mwenendo wa Matumizi unayoakisi madhumuni ya kuidhinishwa kwa bajeti hiyo, Kamati ilichambua utekelezaji wa mipango na majukumu ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa bajeti umezingatia mipango na majukumu yaliyoombewa fedha. Aidha, Ofisi hii ilitumia fedha zilizopatikana kusimamia na kuimarisha misingi ya Utawala Bora.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hali hiyo, Kamati inampongeza kwa dhati **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu** kwa usimamizi madhubuti wa Utawala Bora nchini. Ni maoni ya Kamati kuwa, usimamizi na uratibu wa shughuli za Utumishi wa Umma umeimarika sana katika misingi ya haki, uwajibikaji na utawala Bora, hali ambayo imeendelea kuipandisha nchi yetu katika medani za utawala Bora Afrika na Duniani kote.

### 2.4 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi hii ilitengewa jumla ya **Sh. 178,313,977,000/=** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Februari 2025 Ofisi hii ilipokea Jumla ya **Sh. 108,552,314,125.48/=** ya fedha za Maendeleo sawa na Asilimia **60.88** ya fedha za maendeleo zilizoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea miradi Minne inayosimamiwa na Wizara na kuchambua utekelezaji wa miradi hiyo kama ifuatavyo: -

#### 2.4.1 Mradi Na. 6220: Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

#### a) Ujenzi wa Madarasa Bagamoyo Mwavi

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Mradi huu ulitengewa jumla ya **Sh**. **203,511,528.74/=** kwa ajili ya utekelezaji wa Ujenzi wa madarasa manne, matundu Sita ya choo, na ujenzi wa ofisi ya walimu. Kamati ilielezwa kuwa Mradi huu unatekelezwa kwa wanufaika 150 ambao ni wanafunzi wa shule za msingi na wanafunzi 31 ambao ni wanafunzi wa shule ya awali wanaolazimika kutembea umbali mrefu kutoka vitongoji vya Kudibaha na Senganga ili kuitafuta Elimu.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huo unatekelezwa na TASAF katika Kijiji cha Mwavi, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, Mkoa wa Pwani.

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Februari, 2025 mradi umepokea kiasi cha **Sh. 139,479,416.11/=** sawa na **asilimia 68.54** ya gharama ya mradi, Kamati ilielezwa kuwa hakuna madai yoyote ya Mkandarasi yaliyowasilishwa. Aidha, Utekelezaji wa Ujenzi wa mradi huo mpaka wakati Kamati imetembelea umefikia **asilimia 38**.

**b) Ujenzi wa Madarasa na Jengo la Utawala-Muheza (TASAF)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa Shule ilipokea kiasi cha **Sh. 347,622,637.84/=** kwa ajili ya ujenzi wa Vyumba 06 vya Madarasa, Ofisi 03 za Walimu, Matundu 12 ya Vyoo na Jengo la Utawala ambao utawawezesha walengwa kupata mazingira mazuri ya kujifunzia na walimu kufundishia

**Mheshimiwa Spika**; Mradi huo umekamilika kwa **asilimia 100** ukiwa umeshatumia kiasi chote cha fedha kama ilivyoidhinishwa. Aidha, kamati ilielezwa kuwa mradi umekabidhiwa kwa serikali ya kijiji chini ya uangalizi wa Shule ya Sekondari Magila.

**Mheshimiwa Spika;** Mchanganuo wa fedha na matumizi ya fedha hizo, unaonekana katika jedwali Namba 3 hapa chini ambalo limeambatishwa pamoja na picha za mradi huo.

**Jedwali Na. 3: Miradi iliyotekelezwa kwa fedha zilizopokelewa**

| a | Aina ya Jengo | Idadi ya Majengo | Gharama | Matumizi |
|---|---|---|---|---|
| | Jengo la Utawala | 1 | 105,625,000.00 | 105,625,000.00 |
| | Jengo la Vyumba 02 vya madarasa, Ofisi ya mwalimu na Matundu 04 ya vyoo-Kijiji cha Kwedunda | 2 | 71,214,877.96 | 71,214,877.96 |
| | Jengo la Vyumba 02 vya madarasa, Ofisi ya mwalimu na Matundu 04 ya vyoo-Kijiji cha Misongeni | 1 | 72,720,778.96 | 72,720,778.96 |
| | Jengo la Vyumba 02 | 1 | 63,612,891.07 | 63,612,891.07 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | vya madarasa, Ofisi ya mwalimu na Matundu 04 ya vyoo- Kijiji cha Mikwamba. | | | |
| | Fedha za Usimamizi na Ufuatiliaji | - | 34,449,090.24 | 34,449,090.24 |
| | **JUMLA** | | **347,622,637.84** | **347,622,637.84** |

**Picha mbalimbali za muonekano wa mradi**

**Picha No. 01: Inaonesha ujenzi wa vyumba vya madarasa 06, ofisi ya mwalimu**



**Picha No. 02: Inaonesha ujenzi wa Jengo la Utawala**



**Picha No. 03: Inaonesha ujenzi wa matundu 12 ya vyoo vya wanafunzi wasichana**



**Mheshimiwa Spika,** Baada ya Kamati kukagua mradi huu na kukutana na wanufaika wa TASAF, kamati ilipokea shukrani za dhati zilizoelekezwa kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali kwa ujumla kwa kuboresha miundombinu ya elimu nchini.

Aidha, Kamati ilibaini kuwa miundombinu mibovu ya majengo ya shule yalikuwa ni changamoto iliyosababisha wanufaika hao kuwa na mahudhurio hafifu shuleni na ufaulu wa wanafunzi kutokuwa mzuri. Hivyo mradi huu ni tija kwa Taifa na Kamati inaipongeza Serikali na Wananchi wa Tarafa ya Muheza na Ngomeni kwa ujumla kwa utekelezaji mzuri wa mradi huo.

c) **Kutembelea** na Kukagua utekelezai wa mradi wa Ujenzi wa Kivuko SEMBETI - Moshi Mjini (TASAF)

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Ujenzi wa kivuko umekusudia kutatua changamoto ya usafiri iliyokuwa ikisababishwa na ubovu wa Daraja, Hivyo ujenzi wa Daraja hili utawezesha wananchi kuendelea na shughuli za kiuchumi katika maeneo hayo bila kikwazo. Aidha Mradi huu utaunganisha wananchi wa Kijiji cha Samanga na Sembeti ambavyo vinapatikana katika Kata ya Marangu Mashariki.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati ilielezwa kuwa mradi umetumia jumla ya **Sh. 131,658,312.00/=** kutoka TASAF, pia Mradi umepokea mchango wa Wananchi pamoja na Wadau mbalimbali, hii ni

kutokana na masharti ya Miradi ya TASAF kuwa na sharti la Jamiii kuchangia asilimia 10 ya gharama za mradi kwa kutoa fedha au mahitaji yanayopatikana kwa urahisi katika eneo husika. Mradi huo umekamilika kwa **asilimia 93** na umekabidhiwa kwa wananchi, na 7% iliyobaki ni ukarabati mfereji wa asili wa kupitisha maji ambao uliathiriwa na maporomoko ya udongo wakati wa utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inawapongeza Wananchi wa Sembeti; Samanga na Serikali kwa ujumla kwa utekelezaji mzuri wa mradi huo.

**(Viambatisho vya ujenzi wa Daraja hilo, vinaonekana katika picha Namba 4 hadi 6 kuonesha** hali ya daraja ilivyokuwa awali na ilivyo kwa sasa.)

**Mheshimiwa Spika**, Picha Namba 4, inaonesha mwonekano wa Daraja kabla ya mradi, na picha Namba 5, unaonesha Picha ya Daraja baada ya Utekelezaji wa Mradi.

**Picha 4; Daraja la Sembeti Samanga Kabla ya utekelezaji.**





**Picha Na. 5 Daraja baada ya Utekelezaji wa mradi**

### 2.4.2 Mradi Namba 6203 Ujenzi wa Jengo la Ofisi za TAKUKURU Wilaya ya Rombo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa Mradi ulipokea kiasi cha **Sh. 299,969,119.90/=** kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Ofisi za TAKUKURU – Rombo, hadi kukamilika kwake, mradi umetumia kiasi cha Sh. **290,187,386.00/=,** kiasi kilichobaki ni Sh. **9,781,733.90** sawa na Asilimia **3.26** ya makadirio ya gharama ya utekelezaji wa mradi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliambiwa kuwa, kutokana na uwepo wa bakaa ya fedha, iliamuliwa nkuongeza kazi ya kusawazisha ardhi (Landscaping), kuweka paving blocks na kuweka kinga ya pembeni (balustrades) katika njia ya watu wenye mahitaji maalumu (ulemavu).

**Aidha,** kutokana na kuongezeka kwa kazi za nyongeza, mradi ulipokea nyongeza ya **Sh. 20,941,438.00/=** ili ziweze kukamilisha mradi.

Mradi huo umekamilika kwa asilimia 100 ukiwa umeshatumia kiasi chote cha fedha. Mradi huo utaiwezesha Ofisi hii katika Mapambano dhidi ya Rushwa.

### 2.5 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Kamati ilitoa Maoni na Ushauri katika maeneo Kumi na Mbili (12). Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa ushauri wa Kamati umezingatiwa.

### 2.6 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni za Kudumu za Bunge zimetambua umuhimu wa uzoefu unaopatikana katika mwaka wa fedha unaoisha ili kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge. Kamati imezingatia umuhimu huo na masharti ya Kanuni za Bunge kwa kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kama ifuatavyo: -

#### 2.6.1 Uchambuzi wa Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Ofisi Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na taasisi zilizo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 1,171,035,237,000/=** Ikiwa ni Fedha za Matumizi ya Kawaida.

**Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 imeongezeka kwa **asilimia 25.54** ukilinganisha na Mwaka wa Fedha unaoisha ambapo bajeti ya Matumizi ya kawaida ilikuwa **Sh.932,816,396,000/=;** Kamati imebaini ongezeko kubwa la bajeti, hivyo ni maoni ya Kamati kuwa Serikali ipange bajeti kulingana na mahitaji halisi. Aidha, ongezeko hilo linaakisi mahitaji ya kifedha kulingana na sababu mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kuongezeka kwa watumishi, kupanda kwa bei ya bidhaa na huduma.

**Mheshimiwa Spika**, Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazoombwa zinatumika vizuri na ili kuhakikisha hili linatekelezwa ipasavyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inawasilisha mbele ya kamati taarifa mbalimbali za utekelezaji wa bajeti kwa mujibu wa Sheria. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama unavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 4**

**Jedwali Na. 4: Mchanganuo wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida 2024/2025 na Uwiano wa Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida 2025/2026**

| FUNGU | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2024/2025 | MAKADIRIO YA FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 | ASILIMIA YA ONGEZEKO/UPUNGUFU (-) |
|---|---|---|---|
| **Fungu 20** – Ofisi ya Rais (Ikulu) | 33,544,557,000/= | 34,804,735,000/= | 3.76 |
| **Fungu 30** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri | 805,676,639,000/= | 1,039,839,675,000/= | 29.06 |
| **Fungu 32** – Ofisi Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora | 58,314,993,000/= | 55,086,788,000/= | -5.54 |
| **Fungu 33** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma | 11,642,650,000/= | 13,958,139,000/= | 19.89 |
| **Fungu 67** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma | 10,831,831,000/= | 13,195,060,000/= | 21.82 |
| **Fungu 94** – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma | 8,740,713,000/= | 9,177,599,000/= | 4.99 |
| **Fungu 04** – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa | 4,065,013,000/= | 4,973,241,000/= | 22.34 |
| **JUMLA KUU** | **932,816,396,000/=** | **1,171,035,237,000/=** | **25.54** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, 2025.*

### 2.6.2 Uchambuzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Ofisi ya Rais – Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 183,315,087,000/=** kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Sh. 114,776,309,000/=** ni fedha za ndani, na **Sh. 68,538,778,000/=/=** ni fedha za nje.
2.0
**Mheshimiwa Spika**, bajeti ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 imeongezeka kwa **Sh. 5,001,110,000/=** sawa na **asilimia 2.81** ukilinganisha na bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama unavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 5**

**Jedwali Na. 5: Mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo 2025/2026**

| FUNGU | BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 | |
|---|---|---|
| | FEDHA ZA NDANI | FEDHA ZA NJE |
| **Fungu 30** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri | 88,934,306,000/= | 68,538,778,000/= |
| **Fungu 32** – Ofisi Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora | 19,755,541,000 /= | - |
| **Fungu 33** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma | 3,000,000,000/= | - |
| **Fungu 67** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma | 1,408,828,000/= | - |
| **Fungu 94** – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma | 500,176,000/= | - |
| **Fungu 04** – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa | 1,177,458,000/= | - |
| **JUMLA KUU** | **183,315,087,000/=** | |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, 2025.*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza jitihada za Serikali kuendelea kupanga bajeti ili kutekeleza miradi mingi zaidi kwa kutumia fedha za ndani.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maoni

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, naomba kukamilisha uchambuzi kwa kubainisha Maoni ya Kamati yanayojenga mtazamo ambao ni msingi wa Ushauri wa Kamati. Maoni hayo ni kama ifuatavyo: -

(a) Serikali ihakikishe upatikanaji wa kiasi chote cha fedha ya bajeti kama iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii, ili kutekeleza mipango iliyokusudiwa kwa mwaka wa fedha unaoisha;

(b) Serikali itengeneze Mfumo wa malipo ambao utakuwa ni mwongozo kwa ofisi za umma na Serikali kwa lengo la kuwasaidia vijana wanaojitolea katika nafasi mbalimbali;

(c) Baada ya Mpiga Chapa wa Serikali kuboreshewa mazingira ya utendaji kazi kwa kiwango kinachoendana na wakati, ni maoni ya Kamati kuwa, machapisho yote na nyaraka za Serikali, zichapishwe na Wakala huyu wa Serikali, ili kulipunguzia Taifa gharama;

(d) Suala la kuajiri watumishi wa kada mbalimbali katika utumishi wa Umma lisimamiwe na taasisi moja;

(e) Ili kupunguza wimbi la ukosefu wa ajira kwa vijana, Serikali ibadilishe kipaumbele cha kutoa mkopo kutoka kada ya Elimu na kuzingatia kada nyingine muhimu

ambazo Taifa linaupungufu wa wataalamu kwa maendeleo mapana ya Taifa; na

(f) Kwa kuwa vijana wengi wamekosa ajira, Serikali iangalie namna nzuri ya kuwafanyia mafunzo ma kuwatafutia nafasi katika soko la ajira nje ya nchi, ili kuwakwamua vijana kutoka katika wimbi la kukosa ajira.

### 3.2 Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** kwa Maoni niliyobainisha kutokana na uchambuzi, naomba kutoa Ushauri wa Kamati kama ifuatavyo: -

(a) Serikali ihakikishe kuwa fedha inayoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii na Taasisi zake inapatikana ipasavyo ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu yaliyopangwa;

(b) Serikali iendelee kuimarisha misingi ya Utawala Bora pamoja na Kuboresha mifumo ya utendaji kazi katika Utumishi wa Umma sambamba na kuboresha mishahara na maslahi ya Watumishi;

(c) Serikali iendelee kusimamia na kutoa mafunzo maalumu ya mara kwa mara kwa Watumishi wa Umma ili kuwezesha utendaji kazi unaozingatia weledi na ustadi mkubwa;

(d) Ili kuondoa tatizo la kila taasisi kuajiri watumishi wake, Serikali ihakikishe kuwa Mifumo ya Ajira inasomana, na mamlaka ya kuajiri yanabaki kwa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;

(e) Serikali iboreshe mfumo wa Kufanya Usaili kwa njia ya Mtandao (Online Aptitude Test – OATS) ili maswali yaendane na nafasi za kazi zinazohitajika.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### Maelezo ya Kuhitimisha

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye taarifa rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa.

1. Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb. – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb. – **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb - Mjumbe.
4. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb - Mjumbe.
5. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb - Mjumbe.
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb - Mjumbe.
7. Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb - Mjumbe.
8. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb - Mjumbe.
9. Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb - Mjumbe.
10. Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb - Mjumbe.
11. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb - Mjumbe.
12. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb - Mjumbe.
13. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb - Mjumbe.
14. Mhe. Yahya Omary Massare, Mb - Mjumbe.
15. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb - Mjumbe.
16. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb - Mjumbe.
17. Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mb - Mjumbe.
18. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb - Mjumbe.
19. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb - Mjumbe.
20. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb - Mjumbe.
21. Mhe. Aziza Seylum Ally, Mb - Mjumbe.
22. Mhe. Joseph Anania Tadayo, Mb - Mjumbe.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. George Boniface Simbachawene (Mb) Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ushirikiano mkubwa ambao ameendelea kuipa Kamati pamoja na Naibu Waziri wake Mhe. Deus Clement Sangu.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioupatia Kamati wakiongozwa na Makatibu Wakuu wa Ofisi hiyo Ndg. Juma Selemani Mkomi Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Ndg Majula Mahendeka Katibu Mkuu Ikulu.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Baraka Ildephonce Leonard kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha, kiupekee nawashukuru Sekretarieti ya Kamati kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**
23 Aprili, 2025

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria, Mheshimiwa Florent Kyombo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaanza moja kwa moja na uchangiaji. Tutaanza na Mheshimiwa Janejelly James Ntate, Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage na Mheshimiwa Rashid Shangazi wajiandae.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipendelea kuwa wa kwanza kuchangia. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema ambaye ametulinda mpaka sasa tunaenda mwishoni mwa ngwe ya Bunge la Kumi na Mbili. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri Simbachawene, Naibu wake Mheshimiwa Sangu, Watendaji wenu Wakuu wakiongozwa na Ndugu Juma Mkomi, wamefanya kazi, hakika wameniheshimisha na wameheshimisha wafanyakazi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Kitabu cha Luka 17:11 – 16, lakini kwa wingi wa udogo wa muda sitaisoma yote, lakini inatupatia mafunzo ya Wakoma 10 walioenda wakatibiwa na Bwana Yesu. Kati ya Wakoma 10, aliyerudi kusema ahsante ni mmoja. Sasa mimi kwa niaba ya wafanyakazi wa Tanzania, ninarudi kusema ahsante kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninarudi kumshukuru? Kwa kipindi cha miaka minne amepandisha vyeo watumishi 429,458, lakini ametoa kibali cha ajira, waajiriwe watumishi 149,000 na ambao wameshaajiriwa ni 102,154 na nyingine ziko kwenye mchakato. Tatu, amelipa malimbikizo ya mishahara ambayo yalikuwa ni mwiba mzito kwa watumishi 130,463 kwa thamani ya bilioni 226.5. Nne, tulikuwa na kitendawili cha kikokotoo akabadilisha, kikokotoo kikawa 40% na 33%, tuna imani Serikali itaendelea kurekebisha. Niseme ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninaongelea mambo mawili kwa sababu mengine yote wamemaliza. Ninaomba nishauri mambo mawili, nitashauri kwenye Sekretarieti ya Ajira na hamisho za Watumishi. Kwa kawaida, kikanuni na kisheria mwajiri namba moja ni Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

lakini akakasimu madaraka hayo kwa Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu Mkuu Kiongozi akakasimu kwa Katibu Mkuu Utumishi wa Umma chini ya Ofisi ya Waziri, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Kwa hiyo, kinachofanyika Menejimenti ya Utumishi wa Umma ni Mheshimiwa Rais anafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo mwaka 2003 Serikali kwa nia njema iliamua kugatua madaraka kuzipa Wizara, Idara za Serikali na Taasisi kuajiri, kupandisha vyeo na kutunza nidhamu ya watumishi. Tulienda vizuri kidogo, lakini tulipofika 2007 moto ukawa moto, wanatangaza ajira, watu hawajafanya *interview* ajira zimejaa. Wanatangaza ajira walioshinda siyo wanaoingia ndani ya kazi. Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne akaunda Tume, Tume ilikuja na mapendekezo kupitia Sheria ya Utumishi, Sura ya 298, kifungu cha (29)(1) ikaunda Sekretarieti ya Ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekretarieti ya Ajira ikaanza tarehe Mosi Machi, 2010 na Katibu wake wa kwanza ndiyo Naibu Katibu Mkuu Utumishi. Jukumu walilopewa na Mheshimiwa Rais wakati anaizindua alisema, jukumu kubwa ni kuajiri Watumishi wa Serikali, Wizara zote, Idara zote na Taasisi isipokuwa wakagatuliwa madaraka Tume ya Utumishi wa Mahakama kidogo na Tume ya Utumishi ya Bunge, lakini na wenyewe, ili waajiri lazima ikama waipate kutoka Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa sababu, wale ndiyo wanatoa *check number*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampenda sana Mheshimiwa Waziri na amenisaidia sana, wakati anakuja hapa kuna mambo ambayo nitaomba anipe majibu. Sekretarieti ya Ajira imevunjwa au inadogoshwa makusudi au ni kitu gani kinachoendelea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanza taratibu, tunaona baadhi ya Wizara zinatangaza kazi na wanaajiri, ikifika katikati mambo yanaharibika, utumishi wa umma wanaanza kulalamikiwa. Tumeona mpaka sasa watu wanatangaza tenda za kufanya ajira, kila kitu kina utaratibu wake, Sekretarieti ya Ajira ina wataalam wa kila aina wa kufanya hizi ajira na ajira tusizichezee, ndiyo maisha ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Wizara wakiwasilisha bajeti walizofanya, walizozitekeleza ni Watumishi wa Serikali, ni watumishi walioajiriwa kwa kufuata vigezo vizuri tu, lakini sasa tunaanza kweli, ninatoa mfano wa *TRA*, nina meseji zipo humu nyingi, *TRA* juzi wametoa tenda kwa *NBAA* ndiyo wafanye ajira. Sekretarieti ya Ajira imeenda wapi? Ninamwuliza Mheshimiwa Waziri. Sasa akija hapa, anipe majibu kama nyie ndiyo waliowakasimu tuelewe? Basi warudishe Sheria hapa tuvunje Sekretarieti ya Ajira, itakuwa haina maana *NBAA* kazi yake ni kuangalia wataaluma wa uhasibu, leo anaingiaje kwenye kuajiri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa moto ulio mtaani huko siyo wa kawaida, lakini wote wanalaumu Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Tuliona mfano wa kuajiri walimu hapa, vikatibuka, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ndiyo wanalaumiwa. Sasa waniambie Sekretarieti ya Ajira imeenda wapi? Inafanya nini na ni kwa sababu gani haiaminiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaanza kuamini taasisi zenye kazi nyingine, tunaanza kujikasimu madaraka ambayo tuliyafuta 2010, hii haitawezekana Mheshimiwa Waziri. Hatutaweza kukubali kuchezea ajira za watoto wa Kitanzania ambao inafanya sasa watoto wa masikini hawapati ajira kwa sababu, kwa kwenda hivi unakuta kazi zimetangazwa, *NBAA* imetangaza, lakini watu wameshaingia kazini. Hili hatutalikubali na hili nalisema kwa uchungu tu kwa sababu, naenda kumaliza miaka yangu mitano, waende wakaliangalie, waende wakalifanyie mchakato na leo wanipe majibu wakati wanahitimisha; hii haitawezekana, hatuwezi kukubaliana nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulisema hapa na mimi ndiyo nilishauri kwamba, waende waanzishe *database* ya kuweka wanaokuwa wameajiriwa wakabaki, tunavyotangaza tena turudi mule tuangalie, itasaidia kuondoa wale ambao wamemaliza vyuo mapema. Tume ya Utumishi wa Bunge inafanya, tunaajiri, tunaweka kwenye *database*, tukitangaza tena tunaajiri, lakini tunarudi kwenye *database* tunaangalia *marks* za wale waliopita, yawezekana hawa waliofanya *marks* zao ndogo kwa hiyo, tunawarudisha kwenye *database* tunachukua yule mwenye

*marks* nyingi, ambaye alikuwa kwenye *database* tunamwajiri, huyu anakaa kwenye kusubiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna siku nilikuwa namwambia Mheshimiwa Spika, labda sasa sisi tuanze kuwa mfano wa kufundisha Sektretarieti ya Ajira, lakini ukiangalia Sektretarieti ya Ajira ipo sawasawa, tatizo linakuja watu wameanza kujipa mamlaka ambayo siyo yao. Naomba Mheshimiwa Waziri asimamaekwenye nafasi yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nije kwenye uhamisho. Menejimenti ya Utumishi wa Umma nyie ndiyo wenye mamlaka ya kuhamisha mtumishi, ndiyo wenye mamlaka ya kupandisha vyeo, ndiyo wenye mamlaka ya kusimamia nidhamu. Leo imefikia, nina barua humu na nitatoa mfano halisi, wao wanakaa wanaona mtumishi fulani anaweza akafaa kwenye sehemu fulani, mtumishi anaweza akaenda mwenye taasisi akamkataa au mwenye Wizara akamkataa au mwenye Wizara au taasisi akamkatalia huyo mtumishi kuondoka. Haya mamlaka wanayatoa wapi? Hawaogopi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, anayekuwa amehamisha ni Mheshimiwa Rais kwa kupitia Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Mamlaka hayo yanatoka wapi ya kumkataa mtumishi uliyeletewa? Kwamba, mimi huyu simtaki. Mfano mmoja ulikuwa kwenye mkoa mmoja, siwezi kutaja, mtumishi alihamishwa kwenda mkoa mwingine, yule pale akamkatalia huondoki na Mheshimiwa Mbunge wa sehemu hiyo yupo humu, akatumiwa meseji. Alivyotumiwa akaniambia, hili Mheshimiwa Janejelly lako, nikamwambia twende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Naibu Katibu Mkuu Utumishi, tulivyofika tukamweleza akasema, hiki kitu hakiwezekani. Nikamwambia ndiyo kimeshawezekana, *14 days* zimeisha yule mtumishi hajaenda, lakini mtumishi kule anaambiwa tumeandika utumishi kuomba usiondoke. Naibu Katibu Mkuu akampigia mkuu wa kule akamuuliza, hiyo barua mliyoleta ipo wapi? Nipe mliyoomba kuzuia uhamisho; barua hana, anampiga nyimbo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alimwambia hivi, narudia kauli yake, kabla hazijapita siku tatu huyo mtumishi awe amefika kituo chake cha kazi. Kingine ni mtumishi alivyofika alituma ujumbe kwamba, kafika. Sasa kwa nini tunafika mahali watumishi tunawanyanyapaa? Kwa nini tunafika mahali kwamba, taasisi fulani zina watu fulani ndiyo wanaweza wakafanya kazi pale wengine hawawezi kufanya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenye mamlaka ya kuwapanga watumishi hao ni Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kwa mamlaka waliyopewa na Mheshimiwa Rais kumfanyia kazi hiyo. Ni nini kinachoendelea pale, waende wakapaangalie wanipe majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo vijana wame-*stuck*, sasa hivi watumishi wame-*stuck*, wamepelekwa sehemu fulani wamekataliwa. Mtu anawaambia, mimi siwezi kukupokea au anaenda ameshaiva kupandishwa *promotion*, anafika pale anasema, sisi hatuwezi kukupandisha. Sasa Serikali si moja hii? Kambi si moja hii? Wote si tunajenga nyumba moja? Sasa inafika nini tunaanza kugombania fito?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba, kuna mahali watu fulani ndiyo wanaweza wakafanya kazi pale, mahali watu fulani hawawezi kufanya kazi pale. Wamefanya mengi mazuri kwa watumishi, wamefanya yaliyo mema, lakini wasipoyaangalia haya mawili, yatachafua kazi yote ambayo wamefanya. Niwaombe, narudia kuomba, waende wakaangalie vizuri kazi zenu kwa nini zinaingiliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga hoja mkono. Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Janejelly James Ntate. Nilimtaja Mheshimiwa Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage, Mheshimiwa Rashid Shangazi na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina wajiandae.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kunipa nafasi ya kuchangia katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na kidogo kwenye Sekretarieti ya Ajira, ambayo kidogo mwenzangu amechangia. Ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu kuniweka hai leo na kunipa nafasi ya kuchangia katika Bunge lako Tukufu, lakini ninaanza kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kwa weledi kuliongoza Taifa letu akisaidiwa na Makamu wake, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, lakini bila kumsahau Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Dotto Biteko, ambaye pia, ni Waziri wa Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Waziri wetu, Mheshimiwa George Simbachawene, Naibu wake, Makatibu Wakuu, watendaji wote wa Wizara hii, wamefanya kazi nzuri sana pamoja na Kamati yetu. Wamekuwa wasikivu, wakisikiliza yote tuliyowapelekea na kuyatendea kazi kwa jinsi Mungu alivyowajalia na kufuata kanuni na miongozo waliyosimama nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Rais Ally Hassan Mwinyi, pamoja na Mheshimiwa Dkt. Nchimbi kupata kibali cha kuwa wagombea wa nafasi ya Urais na Umakamu, kupitia tiketi ya Chama Cha Mapinduzi. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupongeza wewe, Waheshimiwa Wenyeviti wote, Mheshimiwa Spika wetu na Mheshimiwa Naibu Spika. Mmekuwa mahiri sana kuongoza Bunge letu kwa miaka mitano, Watumishi mahiri wa Bunge hili na Watumishi mahiri wa Ofisi hii. Mmefanya kazi nzuri, tumekaa vizuri, tumekuwa salama katika Bunge hili, nawapongeza sana Watumishi wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza sana vyama vya wafanyakazi. Vyama vya wafanyakazi vinaongozwa na Mwenyekiti wetu ambaye anaitwa ndugu Tumaini Nyamuhokya, Mwenyekiti ambaye ni Rais wa *r* ndogo, pamoja na Katibu wake,

ndugu Heri Nkunda. Hawa viongozi wa vyama vya wafanyakazi wametoa ushirikisho mkubwa kwa Serikali na waajiri, ndiyo maana nchi yetu watumishi wametulia, huoni maandamano na huoni migomo, wanastahili pongezi viongozi hawa wa vyama vya wafanyakazi pamoja na wengine wote kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina pongezi kubwa sana kwa Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa yote ya Tanzania, Makatibu Tawala wa Mikoa ya Tanzania, Wakurugenzi na Makatibu Tawala wa Wilaya. Nina pongezi zao nyingi sana, nitasema kwa nini wanastahili pongezi na makofi ya jana kwa Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa hayakuwa ya bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majukumu yote ambayo nimetumikia kwa miaka mitano kwenye Bunge hili, lakini ninalo jukumu mahususi ambalo nilikuja nalo; ni uwakilishi wa wafanyakazi wa Tanzania kwenye Bunge Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Uwakilishi huu umetokana na Chama Cha Mapinduzi ambacho ni chama chenye demokrasia pana. Tunajua vyama vyote vina viti maalum, lakini Chama Cha Mapinduzi kutokana na umahiri wake na upana wa demokrasia kikaona katika viti vyake maalum angalau kitoe viti vichache, kwa ajili ya kundi maalum la wafanyakazi pamoja na makundi mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni demokrasia pana ndani ya Chama Cha Mapinduzi. Hii ipo kwenye Ibara ya 178, 79 na 130 ya Chama Cha Mapinduzi, kinatambua mchango mkubwa wa wafanyakazi katika ujenzi wa uchumi, katika utoaji wa huduma za kijamii, ndiyo maana kikaona umuhimu wa kuweka kundi hili kutoka kwenye viti vyake maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama Cha Mapinduzi kinahitaji pongezi kubwa sana, vyama vingine vipo, lakini havina makundi haya wala havijaona umuhimu wa kutoa nafasi kama hizi kwenye jamii ya Kitanzania. Kwa nini nimesema hivyo? Katika nafasi hii nimeweza kuwatembelea wafanyakazi katika mikoa 23 ya Tanzania Bara. Nimekwenda kuonana nao uso kwa uso katika

halmashauri 89, katika hizo halmashauri 23 ni za mijini, lakini niliamua kwenda pembezoni, halmashauri 64.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata ushirikiano mkubwa sana wa Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo na Waheshimiwa Wabunge Viti Maalum, wamenipa ushirikiano mkubwa sana. Wanasema yale maendeleo kule kwenye halmashauri na mikoa ni kwa sababu, watumishi wametulia, wanafanya kwa uadilifu na uzalendo mkubwa kwa hivyo, nilipata ushirikiano mkubwa. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kule nilipokwenda nilipata ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule nilipokwenda wafanyakazi wanasema hivi, wameona mambo makubwa sana ambayo Mheshimiwa Rais amefanya. Pamoja na mapungufu madogomadogo, lakini Serikali ya Awamu ya Sita ndani ya miaka minne ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, tumekaa humu ndani na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamesemea sana wafanyakazi na mimi nimewasemea sana wafanyakazi. Sitoyarudia, lakini wameyaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiongea nao uso kwa uso, ukawasikiliza, ukawashauri na wao wanaishauri Serikali na wanaishukuru, japo wana machache nitayasema mwishoni. Wanasema wameona Serikali ikishusha kodi ya mapato hii Awamu ya Sita kutoka 9% mpaka 8%. Serikali hii pia, imepandisha kima cha chini cha mshahara kwa watumishi kutoka shilingi 170,000 mpaka shilingi 270,000. Serikali hii imeboresha umri wa watoto, tuliomba humu ndani wanaofaidika na *NHIF* kutoka miaka 18 mpaka 21 na bado wanaomba hadi 25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni maoni yao ya badaye, lakini pia, Serikali hii ilifuta tozo 6%, ili watumishi wale ambao walikuwa wamekopa mikopo, walikuwa wanakatwa, lakini imesababisha pesa ibaki kwa watumishi zaidi ya shilingi trilioni 1.1 baada ya kufuta hii kodi kwa watumishi ambao walikuwa wamekopa mikopo kwenye *Higher Learning Institution*, *sorry* kwenye Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, ilikuwa inakatwa 6%, watumishi kule wameniambia wanaipongeza Serikali ya

Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Imekuwa na moyo mzuri sana kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ndani ya miaka Mheshimiwa Rais anasimamia sana mifumo mbalimbali. Ametenga pesa nyingi kwenye TEHAMA na hii TEHAMA inaongozwa na kaka yangu ndugu Ndomba. Wamefanya kazi kubwa sana, mifumo imerahisisha utendaji kazi, usimamizi wa kazi, mishahara kwa wakati, mambo yamekwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wamenituma niseme, wanasema ahsante sana. Wameona kazi ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ndani ya miaka minne kwa hiyo, hilo naomba walipokee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine wamesema ajira. Ajira zilisimama miaka mitatu kwa sababu ya kupisha vyeti feki na mambo mengine. Nia ilikuwa ni njema, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ndani ya miaka minne ameingia madarakani, ametoa zaidi ya 250,000 kwenye utumishi wa umma, ametoa ajira zaidi ya 80,000 kwenye TAMISEMI, kwenye taasisi zaidi ya 100,002 ajira wanaziona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Sekretarieti ya Ajira. Mwanzoni kwa shida walikuwa wanaajiriwa tu watoto wametoka shule juzijuzi, lakini sasahivi ukiangalia imesikiliza kwamba, wale ambao wamemaliza shule muda mrefu muda wao wa kuajiriwa unapungua, lakini sasa hivi nimesikiliza juzi katika mahesabu, ajira 60,000 mia tano ni watoto wenye miaka 35 mpaka 45. Niipongeze sana Sekretarieti ya Ajira kwa kusikiliza maombi, maana walikuwa huko mitaani, muda wao wa kuajiriwa unaisha, wanaichukia Serikali. Naomba niipongeze sana Sekretarieti ya Ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo yote hayo mazuri watumishi wanasema, wanashauri Serikali izingatie suala la makazi, hasa halmashauri za pembezoni. Wamejenga ofisi mpya kule, watumishi wanatoka mbali sana na makazi ni heshima kwa mtumishi, ni heshima na stara. Wanaamini Mheshimiwa Rais, Dkt.

Samia Suluhu Hassan kwamba, ni msikivu, kafanya mambo mengi. Suala la makazi wanaomba sana lizingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni wamehuisha miundo ya watumishi 160,000 kama bilioni 200 hivi, lakini wanaomba Serikali pia, suala la miundo bado ni changamoto, ina masononeko na malalamiko mengi. Suala lingine watumishi wanasema wanaomba maslahi ya watumishi wa halmashauri za mitaa yaboreshwe, yasipishane sana na watumishi wa taasisi za umma, inasababisha watumishi wa halmashauri kutaka kuhama wote kuelekea kwenye taasisi za umma kwa sababu, maslahi yanatofautiana. Wamenituma hilo niliseme, pamoja na mazuri yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanamwomba mama, pia kila fungu analolipata ahakikishe kidogo anatenga kwa watumishi. Wanashauri pale ambapo fungu litaongezeka, basi aangalie tena mishahara ya wafanyakazi iendane na hali ya maisha ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia vyama vya wafanyakazi ipo mikataba mbalimbali tuliingia. Wanaomba kupitia Mkutano ule wa Mei Mosi wa Arusha, mwaka jana, mikataba sita mbalimbali ya Kimataifa, kupitia *ILO* iangaliwe vizuri, wa watumishi wa ndani. Hii ilitolewa kwenye Mei Mosi kupitia vyama vya wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi yamefanyika, humu ndani ni mashahidi. Nimesema sana wafanyakazi, sirudii leo, lakini wanatambua kazi nzuri ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Wanatambua kwamba, aliingia bila kujua kama atakuwa Mheshimiwa Rais, aliingia akakuta mtikisiko wa kiuchumi dunia nzima, alikuta *corona*, alikuta mambo mengi kwenye nchi hii, lakini kama kuna wakati pesa nyingi zimetolewa kwenye maendeleo, kwenye Halmashauri ni sasa, lakini hakuwaacha watumishi. Wameona, wamesema tuna pesa nyingi mpaka zinakosa usimamizi, tunaomba mama aongeze ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi wanasema kwa pamoja, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, mitano tena kwa

maslahi bora ya wafanyakazi. Nipo tayari kuendelea na hii kazi kufikia ambapo sijafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage, ahsante sana.

Nilimtaja Mheshimiwa Rashid Shangazi, atafuatiwa na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina na Mheshimiwa Mrisho Gambo ajiandae.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, kaka yangu Mheshimiwa George Boniface Simbachawene na Mheshimiwa Naibu Waziri Deus Clement Sangu. Hali kadhalika Katibu Mkuu pamoja na watumishi wote wa Wizara hii, bila kusahau taasisi zote zilizopo chini ya Wizara hii ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya ya kusaidia kazi kwa kiasi kikubwa za Mheshimiwa Rais, ambaye tumeona akifanya mambo makubwa ndani ya nchi hali kadhalika akifanya mambo makubwa hata nje ya nchi. Dunia inatambua kwa hiyo, tunawapongeza sana kwa utendaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza, nianzie hapo alipoishia Mheshimiwa Alice Kairungi Kaijage, amekuwa ni mwakilishi sahihi wa watumishi; na ningeomba vyama vya wafanyakazi pamoja na utumishi waangalie vizuri zile kanuni zao ambazo zinamtaka kwamba agombee kwa kipindi kimoja tu, lakini kwa namna ambavyo amewakilisha ametaja taasisi ambazo amezitembelea na halmashauri hii inaonesha wazi kwamba ana *passion* ya kuwatumikia watumishi na kazi hii anaimudu basi wazitazame vizuri kanuni zao. Hawa ndiyo aina ya

wawakilishi ambao wanapaswa kuwawakilisha watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuzungumzia Wakala wa Serikali Mtandao. Wakala hii imekuwa ikifanya kazi nzuri sana. Kila mara Mheshimiwa Rais alikuwa akihanikiza kutaka mifumo isomane; ili mifumo isomane ni lazima Wakala wa Serikali Mtandao waweze kufanya kazi na wamefanya kazi vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tumeona nchi yetu makusanyo ya mapato yamekuwa makubwa. Pia, tunaona namna ambavyo *compliance* mbalimbali zinafanyika kwa sababu watu hawalazimiki kutembea na fedha na kwamba watu hawalazimiki kwenda kupanga foleni kulipa maduhuli mbalimbali ya Serikali; kwa hiyo, tunawapongeza sana. Sasa, tungeomba Serikali iongeze wigo wa kutanua ule mkongo wa Taifa ili uweze kufika halmashauri zile za pembezoni ili mifumo hii iweze kufanya kazi vizuri na maduhuli yaweze kukusanywa kwa urahisi zaidi kupitia wakala wa Serikali Mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi tunaona wanazo programu kama ya *e-office, e-utendaji* ambayo hata ukiwa ofisini unaweza kuona utendaji mbalimbali unavyofanyika katika ngazi mbalimbali na hii inaongeza ufanisi hasa katika eneo hili la utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ningependa kuzungumzia kuhusu Sekretarieti ya Ajira kama ambavyo Mheshimiwa Kamishina mwenzangu, Mama Janejelly amezungumza. Kwa mujibu wa Sheria Namba 298 Menejimenti ya Utumishi wa Umma kupitia Sekretarieti ya Ajira ndiyo yenye jukumu la kusimamia ajira zote hapa nchini; lakini sasa tumeanza kuona wanaanza kuchepuka au kuchepusha hizi taasisi na kuzipeleka katika taasisi nyingine ambazo kimsingi siyo ambazo zimejikita katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona Mamlaka ya Mapato Tanzania imetoa usimamizi wa mchakato mzima wa ajira kwa *NBAA* ambao kimsingi ni Bodi ya Uhasibu. Ajira ambazo zimeenda

kufanyiwa kazi pale ni ajira tofautitofauti katika maeneo mbalimbali ya Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungeomba tubaki kwenye sheria yetu kama inavyotuelekeza, jukumu hili libaki kwenye Sekretarieti ya Ajira. Tumeona wamefanya kazi kubwa na wamefuata ushauri wa Bunge, kwamba ajira hizi badala ya kuzi-*centralise* tuanze kuzipeleka kwenye mikoa; na tumeona angalau kwa kuanzia walimu pamoja na watumishi katika sekta ya afya wamefanyiwa usaili katika mikoa. Hali hii imepunguza ule mrundikano wa waomba ajira katika maeneo ya majiji, sasa wamewekwa katika maeneo ya mikoa. Tupime ufanisi kule, tukiona kuna ufanisi wa kutosha tuendelee kuimarisha; lakini jukumu hili libaki chini ya usimamizi wa uratibu wa Sekretarieti ya Ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kuchangia ni eneo la *TASAF*. *TASAF* imekuwa ikiendelea kufanya vizuri sana na tunawapongeza kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya na niombe Serikali tunaelekea mwisho wa programu hii ya *TASAF*, niombe kwa wivu mkubwa kabisa kwamba tungetamani kuendelea na mpango huu wa kuzifariji hizi kaya maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma hapa katika ripoti ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 27 kwenye kishikwambi, imeeleza kwamba zaidi ya shilingi bilioni 162 ziliwasilishwa kwa kaya za walengwa 906,000 zenye wanakaya kama 3,769,582 ili waweze kujikimu na mahitaji ya msingi. Sambamba na hilo kumeanza kupita mchakato wa kuwatoa baadhi kwa kusema kwamba wame-*graduate*. Sasa sina shida kama wamefanya tathmini ya kina, lakini bado utaratibu huu unatakiwa ukaangaliwe upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Jimboni Mlalo katika Halmashauri ya Lushoto ninaye mwananchi mmoja anaitwa Stanley Augustino Mrema; hana uhusiano na yule Mrema mwingine ni majina tu; huyu ni mlemavu ambaye anahitaji usaidizi wa 100%. Mama yake aliyekuwa anamlea amefariki, sasa anakaa na raia mwema tu ambaye amejitolea kumsaidia, lakini naye juzi ananiambia ameambiwa kwamba ame-*graduate*. Sasa

nikamwambia hebu nioneshe hiyo *certificate* yako ya ku-*graduate* wala hakunionesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu nimemtaja makusudi ili *Hansard* zisome kwamba kuna watu wa aina hii ambao bado mpango huu unapaswa kuendelea kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo tunawapongeza *TASAF,* wamefanya kazi nzuri sana. Zaidi ya vikundi 66,000 vyenye wanachama zaidi ya 800,000 na la kupendeza zaidi ni kwamba kati yao 80% ni wanawake, wameanzisha vikundi ambavyo vina mtaji wa zaidi ya shilingi bilioni 13 na wametoa mikopo zaidi ya shilingi bilioni 7.9, hili ni jambo jema. Katika zana ile ile ya kusema mifumo isomane tungependa kuona halmashauri zetu kupitia 10% tujaribu kuishauri Serikali kwa kuongeza uratibu kwa *TASAF* na Mfuko ule wa 10% uweze kuyaona makundi haya ili kuyaboresha na kuyajengea uwezo zaidi ili kuendelea kuboresha familia zao, lakini kuwafanya wawe na tija zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, sisi katika Halmashauri ya Lushoto ni wazalishaji wakubwa wa mbogamboga na matunda. Tumeona wenzetu hapa Kibaigwa wana soko kubwa la mahindi na sisi tungetamani tuwe na soko kubwa la mbogamboga. Sasa tumetenga eneo katika Kata ya Lukozi ambapo ndiyo maeneo tunakusanya zaidi mbogamboga. Tungeomba sasa ule mpango wa *TASAF* utufikirie na sisi kutujengea Soko kubwa la Kimataifa la Mbogamboga na *facilities* zake zote zikiwemo *cold rooms* na kadhalika ili mboga hizi tuweze kuzifunga vizuri na kuzisafirisha ndani na nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, ni kuhusu Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Ninawapongeza sana, Mtendaji Mkuu, Mkurugenzi Mkuu, Chalamila wanafanya kazi nzuri sana, hasa ile Programu ya TAKUKURU RAFIKI, wameendelea kutoa ushirikiano mzuri sana, ninadhani Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi. Kwenye Wizara zetu tumekuwa tukitoa elimu kupitia wao, lakini tulikuwa tunawaomba twende nao kwenye mabaraza, kwenye Serikali za

Vijiji kutoa elimu kwa wananchi na walikuwa wanaendelea kutoa elimu katika eneo hili…

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangazi, kuna taarifa. Mheshimiwa Kunambi, taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Mbunge anayechangia sasa, ndugu yangu Mheshimiwa Shangazi. Pamoja na kwamba TAKUKURU wanafanya kazi nzuri sana nchini, lakini wana changamoto ya *facilities* kama vyombo vya usafiri kufika eneo la tukio na kuchukua hatua kwa wakati. Hii ni changamoto kubwa sana. Kwa hiyo, ombi langu ni kwamba wapewe *facilities*. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangazi, unaipokea hiyo taarifa ya Mheshimiwa Kunambi?

**MHE. RASHIDI A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea kwa mikono miwili kabisa, ni taarifa sahihi. Ni kweli wana changamoto ya vyombo vya usafiri na wamepata kiasi lakini tungetamani Serikali ione umuhimu wa kuwapatia vyombo vya usafiri katika wilaya zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko baadhi ya wilaya bado wanapanga kwenye majengo ya watu binafsi. Sasa hii kidogo inaondoa ile dhana nzima ya utawala bora. Huwezi ukapanga kwenye nyumba ya mtu ambaye unamtuhumu halafu kesho unamchunguza; unaweza ukapewa *notice* ndani ya masaa 24. Kwa hiyo tunaomba, kwa kazi nzuri ambayo TAKUKURU wanaendelea kuifanya katika nchi yetu basi eneo hili nalo tuliwekee mkazo wa kibajeti ili waendelee kufanya kazi yao kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Rashid Shangazi. Nilimtaja Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, atafuata Mheshimiwa Dkt. Florent Kyombo na Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge ajiandae.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi uliyonipa ili nijumuike na wenzangu kuipongeza sana hii Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambayo mtumishi namba moja ni Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan akisaidiwa kwa karibu na Waziri George Boniphace Simbachawene. Tunawapongeza kwa namna ambavyo wanaliendesha jopo hili la watumishi wa umma kwa ajili ya kuhakikisha kwamba maendeleo yanapatikana na huduma kwa wananchi zinapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wawakilishi wa wananchi pia tunashukuru sana kwa hatua zinazoendelea za Serikali za kuendelea kutoa nafasi za ajira. Vijana wetu sehemu mbalimbali wanapata ajira kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niungane na Wakristo wote pamoja na watu wote duniani kuomboleza kifo cha Papa Francis.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amezungumza hapa na mimi ninataka kurudia juu ya msiba wa Marehemu Boniphace Gissima Nyamo-Hanga, Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO. Kwa moyo wa dhati kabisa ninasema kwamba alikuwa miongoni mwa watumishi bora sana hapa nchini na tutamkumbuka kwa alama alizoziweka. Amekamilisha Bwawa la Mwalimu Nyerere kwa 100%, amepunguza kwa kiwango kikubwa katakata ya umeme iliyokuwa haina maelezo, ameendelea na alikuwa kwenye hatua nzuri pia hata ya kuvunja mikataba mibovu ya *TANESCO* iliyokuwa inalisumbua Taifa letu. Vilevile kiongozi huyu alikuwa anaendelea kufanya tathmini hata ya kuona namna ya kupunguza gharama za umeme. Tutamkumbuka sana mzalendo huyu, ni moja ya watumishi ambao ni kielelezo kikubwa kwenye Taifa na Taifa letu limepoteza mtu makini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais aliunda Tume ya Maboresho ya Kodi na akaipa miezi sita, miezi hiyo sita imekwisha, hiyo tume tunaitaka sasa iwasilishe hiyo ripoti kwa sababu tuna hamu kubwa ya kujua mapendekezo waliyoyaleta. Mimi kama nilivyosema nitapeleka kwao, nilipeleka maoni na mapendekezo ya kurasa 235 ambayo yalikuwa na mambo mengi humo ndani. Pia ninawapongeza kwa sababu walinijibu kwa wakati; na ninataka ku-*share* na Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipowapelekea zile kurasa 235 za mapendekezo na maoni sekretarieti ya hiyo tume ilinijibu kama ifuatavyo: "Mheshimiwa Mpina, tunakiri kupokea maoni yako kuhusu maboresho ya mfumo wa kodi nchini. Maoni na mapendekezo uliyoyatoa ni mazuri, yameandikwa kwa ufasaha na tutazingatia katika uchambuzi ili kupata mapendekezo ya pamoja ambayo kwa hakika yataleta maboresho ya mfumo wa kodi nchini. Tunakushukuru sana. Nami ninawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninalotaka kulizungumza hapa ni kuhusu mihuri ya Wenyeviti wetu wa Vitongoji. Wenyeviti wetu wa Vitongoji waliondolewa mihuri, sababu ya kuondolewa mihuri haina msingi wowote. Tunaomba Wenyeviti wetu wa Vitongoji warejeshewe mihuri yao. Zilikuwepo sababu zilizokuwa zinatolewa, eti wanauza ardhi, mara wanafanya kile, mara wanafanya kile. Hatujawahi kufanya hivyo, hata Wizara ya Ardhi wapo watumishi ambao wanagawa viwanja zaidi ya viwili, hatujawahi kuinyang'anya mamlaka Wizara ya Ardhi kwa sababu kuna baadhi ya watumishi wa umma wamegawa ardhi mara mbili. Kwa hiyo, Wenyeviti wetu wa Vitongoji warejeshewe mihuri yao. Mheshimiwa Waziri wa Utumishi asimamie hilo kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeongea na mimi niongezee sauti kwa wenzangu waliyozungumzia mishahara ya wenyeviti wa vitongoji, wenyeviti wa vijiji, wenyeviti wa mitaa na madiwani. Tumezungumza muda mrefu sitaki kuongea lakini nilishawishi Bunge hili, hii ndiyo bajeti ya mwisho. Tukifika kule mwisho bajeti ya Serikali tuikwamishe mpaka pale mishahara ya viongozi hawa

itakapopatikana. Hatuwezi kuendelea kukubali tena maelezo mengine zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiandaa hii bajeti yetu ya utumishi na kama tunavyojua, kwamba Wizara ya Utumishi na Utawala Bora kwa kweli ndiyo *engine* ya utekelezaji wa majukumu yote ya Serikali. Ukitaka kufanikiwa unafanikiwa kwenye Wizara hii, ukiamua ku-*fail,* una-*fail* kwenye Wizara hii kwa sababu ndiyo inayoendesha shughuli zote za Serikali. Kwa hiyo, tunataka kuona kwamba kupitia bajeti hii watumishi wetu wakiwa wanaboreshewa mishahara yao, tunataka kuona kupitia bajeti hii madai yote ya watumishi wa umma, malimbikizo ya mishahara, madeni ya posho za uhamisho, madeni ya posho za likizo na maslahi mengine muhimu, hatutaki tena watumishi wetu kuendelea kudai madai hayo ambayo ni halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tuliyapitisha kwenye bajeti husika, hatujui ni kwa nini walienda kukopwa wakati bajeti ilipita hapa. Kwa hiyo, tunataka mwaka huu kupitia bajeti hii, maslahi ya watumishi kabla hatujaondoka Bungeni hapa tarehe 27 Juni, tuwe tumehakikisha watumishi hao wamelipwa mishahara hiyo. Mheshimiwa Waziri wa Utumishi analo jukumu la kuhakikisha kwamba mambo haya yametekelezwa. Suala la kupanda kwa mishahara lisiwe jambo la hisani tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa sana pia nimesoma kiambatisho namba saba kinachohusu taasisi zilizofanyiwa tathmini za usalama wa mifumo ya TEHAMA ambapo ni mifumo 112 tu ndiyo ambayo ilifanyiwa tathmini; lakini nadhani tuna mifumo takribani 800 kama sikosei. Sasa hizi tathmini za kiusalama zinapofanyika kwa udogo namna hii tunapata matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunategemea mifumo ya TEHAMA kukusanya kodi, tunategemea mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya kusimamia matumizi ya Serikali. Sasa hivi mifumo mingi ina matatizo makubwa na ina changamoto nyingi. Mifumo imeanzishwa na kuanza kutumika ikiwa wakati mwingine kanzidata na *server* bado zinamilikiwa na *vendor*; lakini mifumo

mingine inaruhusu fedha mpaka kuingia kwenye mifuko ya watu, kwenda kwenye akaunti za watu. Halafu bado una changamoto hii kubwa ya mifumo yako kufanyiwa ukaguzi. Mkaguzi, *CAG* amelia juu ya ku-*paralyse* kwa mifumo yetu ya ukusanyaji wa mapato juu ya ku-*paralyse* kwa mifumo yetu ya usimamizi wa matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hili jambo litaendelea na mifumo ya TEHAMA ndiyo hii ambayo tunaitegemea, kama mfumo unaweza ukakaa haukaguliwi usalama, mfumo unaendeshwa hujakaguliwa usalama, maana yake mtu yeyote anaweza aka-*temper* nao, mtu yeyote anaweza akaingia kwenye mfumo huo akabadilisha takwimu, mtu yeyote anaweza akaingia kwenye huo mfumo akafuta kumbukumbu usalama wa Taifa letu uko wapi? Usalama wa mapato yetu uko wapi? Jambo hili linasimamiwaje? Hawa *e-GA* wana tatizo gani la kushindwa kuli-*manage* jambo hili? na Waziri wa Utumishi anatuambia nini kuhusu uwezo wa *e-GA* katika kusimamia jambo hili? Ni kwa nini mamlaka zinavunja sheria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi taasisi ambazo zinasimamia miongozo na sheria ya Serikali Mitandao ni 40% tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto hii ya muda, ninashindwa hata sijui nitaongeaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba utawala bora uko wapi Mheshimiwa Waziri Simbachawene? Taarifa ya *CAG, PPRA, FAU,* TAKUKURU zinaendelea kuripoti wizi wa fedha za umma kwa kiwango kikubwa, lakini kuingia mikataba ya usiri ambayo haina baraka za Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ambayo haijabarikiwa na Bunge hili na mikataba hiyo ikaendelea, halafu tuko na Waziri wa Utawala Bora, tuko na Serikali inayosimamia Utawala Bora, haya mambo yanawezekanaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini 40% ya watumishi wa umma hawafanyi kazi na ni taarifa ya Waziri Mwenyewe. Watumishi wengine wamewekwa benchi na mwenzangu amezungumza,

kwa fitina tu na chuki ndani ya mamlaka, lakini wameachwa tu na anayefanya hivyo ameachwa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukabidhi rasilimali za umma kwa wageni. Kwa mfano machimbo ya wachimbaji wadogo, taarifa za *CAG* kutokufanyiwa kazi, mifumo, mikopo na matumizi ya fedha za umma hata nje ya bajeti. Mambo haya yanaruhusiwaje, Waziri wa Utumishi uko hapa, Waziri wa Utawala Bora uko hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu kuna manju mmoja aliwahi kuimba, "*tumoghagi jozwa, olonosabha jilaleja bhademi*", anaitwa Mwanacholicholi. Ni kwa nini tunashindwa kuchukua hatua mahali ambapo sisi tunaweza kuchukua hatua? Kwa mfano, taarifa ya nchi yetu kulipa shilingi trilioni 1.438 katika Mahakama. Tovuti ya *ICSID* inaonesha kuwa baadhi ya makampuni yamelipwa baada ya kupewa tuzo katika Mahakama ya Kimataifa ya Usuluhishi wa Migogoro na Uwekezaji na Biashara, ambapo mpaka sasa hivi nchini kwetu tumeshalipa shilingi trilioni 1.438, tena kwa siku za hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi taarifa zinaoneshwa kwenye Tovuti ya *UCSID* shilingi trilioni 1.438 lakini Bunge hili halijawahi kuelezwa na Waziri wa Utumishi na Utawala Bora, Bunge hili halijawahi kuelezwa na Waziri wa Katiba na Sheria, Bunge hili halijawahi kuambiwa jambo lolote isipokuwa kule kwenye Tovuti ya *UCSID* ndio wanaonesha tu, shilingi trilioni 1.438 ambapo fedha hizi sisi hatujawahi kuzipitisha na hatujawahi kuombwa kibali na hatujawahi kuambiwa kwa nini Serikali ilienda kushindwa katika madai hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine mpaka sasa hivi Serikalini ni kuhusu kashfa ya wahamiaji haramu kuajiriwa Serikalini. Wote tunakumbuka kwamba Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama *(CDF)* Jenerali Jacob John Mkunda alitupa taarifa akisema, "Baadhi ya waomba hifadhi hao na wakimbizi au familia zao wameajiriwa Serikalini kwa nafasi mbalimbali na wengine wamepewa teuzi Serikalini katika nafasi zenye maamuzi". Nafasi za Watanzania zimechukuliwa na wageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tuna mfumo gani wa utumishi ambao unaweza ukaruhusu mpaka mtu mgeni akaajiriwa? Tuna mfumo gani wa utumishi hapa nchini ambao unaweza ukaruhusu mtu ambaye siyo raia wa nchi hii akapata uteuzi ndani ya Serikali? Tuna mfumo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, yanawezekanaje haya? Taarifa hii kwa sababu ilishatolewa, Waziri wa Utumishi na Utawala Bora, una shida gani? Una kigugumizi gani kuitolea taarifa kikamilifu ndani ya Bunge hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni akina nani ambao wameajiriwa ndani ya nchi ambao sio raia wa Tanzania? Ni akina nani ambao wameteuliwa ndani ya nchi yetu ambao sio raia wa Tanzania? Ni akina nani hao na vyeo vyao na hatua zilizochukuliwa na Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shida gani? Kiongozi Mkuu wetu wa Majeshi ametoa nyeti kama hii, halafu inanyamaziwa, haitolewi taarifa, mwaka 2024 na hata mwaka huu, 2025, tatizo ni nini Serikalini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mpina. Tunaendelea na Mheshimiwa Daktari Florent Kyombo, Mheshimiwa Mrisho Gambo, ajiandae.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi ya kuchangia katika Bajeti hii ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi ya pekee, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kweli kwa mapenzi mema ya nchi yake na hasa katika eneo kubwa kuongeza bajeti ya Wizara hii, ambapo sisi wote ni mashuhuda ambao tunaona bajeti ya ofisi hii imeongezeka kwa takribani 25.5%. Ni ongezeko kubwa na lengo

kubwa ni kuendelea kufikia wananchi wake kupitia taasisi ambazo ziko chini ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi ya pekee, nampongeza Mheshimiwa George Boniface Simbachawene na Ndugu yangu *Comrade* Deus Clement Sangu kwa usimamizi mzuri ndani ya Wizara hii. Tunaona, kwa sababu ni mahitaji maalumu ya ajira za watumishi wetu pia na taasisi zote zilizoko chini ya Wizara hii, wamekuwa na weledi kuhakikisha kwamba wanasimamia kwa weledi katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni-*declare* kwamba, mimi ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ambayo inasimamia Wizara hii na pia kama Mjumbe wa Kamati, niendelee kushukuru. Serikali imekuwa ikichukua yale maoni ya Kamati na kuyafanyia kazi ndiyo maana tunaona ongezeko la bajeti katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme, Kamati imeenda kukagua baadhi ya miradi ambayo inasimamiwa kwa mfano na Ofisi yetu ya TAKUKURU *(PCCB)* na mingine inasimamiwa na *TASAF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na miradi ya *PCCB* kule Rombo, kwa kweli tumeona tunaunda mradi ambao thamani ya fedha unaiona, lakini mradi wenyewe ulivyotekelezwa katika eneo hilo, kwa kweli unaakisi Taasisi yetu ya Kupambana na Rushwa kwamba, tungetamani na taasisi nyingine ziende zijifunze jinsi miradi inavyotekelezwa hasa kupitia Taasisi yetu ya TAKUKURU ambayo ni kioo cha haki, lakini na kulinda rasilimali za fedha na utumishi mwema katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, makofi mengi na pongezi nyingi tuendelee kupongeza Taasisi yetu ya TAKUKURU kwa kazi nzuri chini ya Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Mkurugenzi Mkuu, Ndugu yetu Chalamila. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona miradi ya *TASAF,* tumetembea maeneo mbalimbali, tumeenda Zanzibar, tumeona; tumeenda Muheza tumeona, tumeenda Bagamoyo. Miradi hiyo

kwa kweli inaakisi mahitaji ya mwananchi wa kipato cha chini ambaye kwa kweli inaleta mchango katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia katika uchambuzi hata katika eneo la *TASAF,* kwa kweli pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia, anazo njia nyingi za kumfikia mwananchi. Pamoja na kuleta utaratibu mwingine, lakini kupitia *TASAF* hii, tunaona *TASAF* ambayo imejiingiza katika ujenzi wa miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeenda pale Bagamoyo tukaona madarasa yamejengwa katika maeneo ambayo vijana wetu, watoto wetu hawawezi kufika katika shule iliyosajiliwa ilipo. Kwa hiyo, wameamua kujenga darasa kuwasaidia watoto wa darasa la awali na madarasa mengine kwa ambao hawawezi kufika kwenye shule iliyosajiliwa, na hiyo imeleta mahudhurio makubwa katika shule pia imeongeza ufaulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaona ni mchango mkubwa wa kuhakikisha kwamba, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia anahakikisha amemfikia kila Mtanzania katika eneo lake kuhakikisha kwamba, hakuna anayebaki nyuma na hiyo fursa inakuwa ni fursa sawa kwa wote. Pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona katika maeneo mengine *TASAF* imeendelea kujenga miundombinu ya afya ambapo tumeweza kujenga kliniki za akina mama na watoto na hiyo inasaidia kupata huduma za afya na hiyo inapunguza vifo vya watoto na akina mama. Kwa kweli ni mageuzi makubwa sana ambayo Mheshimiwa Rais anafanya kazi kupitia Taasisi yetu ya *TASAF* na hiyo kwa kweli inawafikia wananchi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona ujenzi wa miundombinu mbalimbali. Tumeona barabara zinazofunguliwa na *TASAF,* lakini tumeona katika maeneo ya vijijini, maeneo ambayo yalikuwa hayafikiki sasa yameunganishwa. Tumeona tumeenda kule Samanga na Sembeti kule Marangu daraja ambalo lilikuwa ni changamoto kwa muda mrefu, lakini *TASAF* imeweza kutumia zile

fedha na michango ya wananchi ikaunganisha mawasiliano katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaona ajira zimepatikana katika maeneo hayo, pia, kuongeza thamani ya mazao yanayozalishwa katika maeneo hayo kuweza kufika katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina kila sababu ya kuiombea hii *TASAF* kupitia Serikali yetu Tukufu ya Dkt. Samia kuendelea kutafuta vyanzo vingine vya fedha kuendelea kuiwezesha iendelee kufanya hizi kazi ambazo zimekuwa zinainua wananchi wa kipato cha chini kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, tunaona katika maeneo ya kilimo, kuna maeneo ambayo mifereji ya umwagiliaji imeweza kuchimbwa na kuweza kuongeza thamani katika mashamba ya umwagiliaji na hivyo uzalishaji wa mazao ukaongezeka pia wananchi wakapata chakula na pia ikawainua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika maeneo haya naomba kupitia Wizara yetu ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa Rais pamoja na viongozi wa Serikali tuendelee kutafuta fedha kwa ajili ya kuwezesha Taasisi yetu ya *TASAF* iendelee kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona vikundi…

**TAARIFA**

**MHE. SALUM MOHAMMED SHAAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. SALUM MOHAMMED SHAAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba, katika pongezi zote anazozitoa juu ya *TASAF,* hata mimi jimboni kwangu *TASAF* imenipelekea zaidi ya shilingi milioni 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu kwamba, *TASAF* inafanya kazi nzuri, inafanya kazi kubwa, na zile fedha kule jimboni kwangu zinafanyiwa kazi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kyombo unaipokea taarifa hiyo ya Mheshimiwa Salum Shaafi kutoka Pemba?

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Mheshimiwa Shaafi naipokea kwa mikono miwili. Yeye ni Mjumbe wa Kamati, na pia tumekwenda wote pamoja kutembelea miradi ya *TASAF,* naye anaona kwa macho. Nashukuru kwa hizo pongezi kwa kazi nzuri ya Mheshimiwa Dkt. Samia ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naendelea na mchango kwamba katika eneo la *TASAF*. Pia tunaona vikundi mbalimbali vya walengwa wanaotokana na *TASAF* vimeendelea kufanya kazi kubwa na sasa hivi tuna vikundi zaidi ya 66,000 ambavyo vina wanufaika zaidi ya 800,000, na bado vinaendelea kukusanya fedha katika akaunti zake zaidi shilingi bilioni 13, na bado kwenye mzunguko vinakopeshana zaidi ya shilingi bilioni tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwenye eneo hili, tunajua Mradi wa *TASAF* mtu akisha-*graduate* anatoka katika uchangiaji huo. Kwa hiyo, tuombe sasa vikundi hivi viingizwe katika mfumo wa halmashauri ili sasa ile 10% na yenyewe hao walengwa ambao walikuwa wanajulikana kwamba walitoka katika kaya ambazo zinalengwa, basi waweze kupata pia mikopo ya 10% ili pale *TASAF* ambapo inakuwa wame-*graduate,* basi wananchi wetu hawa waendelee kupata mikopo kupitia vikundi vyao, ile ya 10% kutoka halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limefanyika kwa weledi mkubwa ni ubunifu kupitia Mheshimiwa Rais Dkt. Samia wa *TASAF* kuwa na ushirikiano na Bodi ya Mikopo. Katika eneo hilo tunaona wale vijana wote wanaotambulika kuwa wanatoka kwenye kaya zenye mahitaji, *TASAF* imekuwa

ikisimamia na Bodi ya Mikopo imekuwa ikiwapatia mikopo kwa 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linaashiria kwamba Mheshimiwa Rais ameamua kutumia njia nyingine ya ziada kusaidia wananchi wake hawa kuhakikisha kwamba wanapata mikopo wanaosoma na hivyo kupunguza vijana ambao siku zote wangekuwa ni vibarua, wakawa vijana ambao wanaweza kuajiri na kuajiriwa pale wanapohitimu masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naendelea kupongeza juhudi hizi za *TASAF*. Naomba sasa Serikali iendelee kuwa na jicho la pekee katika eneo hili kuhakikisha kwamba, taasisi yetu hii ambayo iko chini ya Mheshimiwa Rais inaendelea kupata uwezeshaji wa kufanya kazi nzuri kama tulivyoona katika sekta mbalimbali; sekta ya elimu, afya, kilimo na ya miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine utakuwa unaenda kwenye soko la ajira na hasa nitajikita katika eneo la walimu. Ilikuwa ni nia ya dhati kwa Serikali yetu, wakati wa mahitaji ya walimu wengi nchini kwetu, Serikali iliamua kutoa mikopo kwa 100% kwa hii taaluma ya ualimu. Tulipata *enrolment* nyingi sana kuingia Chuo Kikuu kwa walimu na kweli Tanzania sasa hivi ina hazina ya vijana wetu ambao wamehitimu katika hii taaluma ya ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ni lazima tukubaliane, Serikali imeendelea kutoa ajira za kutosha kwa walimu lakini bado mahitaji katika shule zetu na yenyewe bado yapo na Serikali bado inapambana kuendelea kutoa ajira zingine ili kuweza kuhakikisha kwamba shule zinakuwa na walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikwambie, hata kama Serikali ingeendelea kutafuta ajira za walimu wote, kwanza hawawezi kutosha, kwani shule zetu ni chache kuliko idadi ya walimu walioko katika soko; lakini bado Serikali inaendelea kutoa mikopo ya 100% kwa walimu kuendelea kusoma. Huko mbele tutaenda kugota na walimu watakosa ajira kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni jukumu la Serikali kufanya *Training need assessment,* mahitaji ya taaluma ambayo inatakiwa kwa muda huu katika nchi yetu. Kama tunaona soko la walimu, wametafutwa walimu ni kweli wamepatikana lakini ajira tulizonazo haziwezi kutosha kwa wingi wa walimu tulionao, basi waweze kubadilisha mfumo na wakibadilisha mfumo wanatafuta ile taaluma ambayo nchi inahitaji kwa wingi, lakini na hawa walioko ambao wameshahitimu tuombe Serikali sasa iongeze juhudi kuwatafutia ajira za nje ya nchi katika taaluma tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wanaenda kufundisha Kiswahili, wanaenda kufundisha Kifaransa, wanaenda kufundisha lugha nyingine ili sasa na hao walioko hapa katika ajira ambao wako nchini, basi wote waweze kupatiwa ufumbuzi na wote waweze kujiajiri. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naona ni kengele ya pili, ninaomba nikushukuru kwa nafasi na ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Florent Kyombo. Nilimtaja Mheshimiwa Mrisho Gambo.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kushukuru tena kupata nafasi ya kuweza kuchangia kwenye Bunge lako Tukufu, na nitajielekeza kwenye hoja tatu tu. Kuna mambo ya Utumishi, pia kuna mambo ya Utawala Bora ambapo najua TAKUKURU wamo humu ndani na masuala mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka yangu yote inayokaribia mitano katika Bunge hili nimekuwa najenga hoja kuhusiana na ujenzi wa Stendi ya Jiji la Arusha. Sasa watu watashangaa naongelea stendi kwenye Utumishi, lakini hapa kwa sababu kuna utawala bora, wapo TAKUKURU ambao nadhani wana kazi ya kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alifanya kazi kubwa, katutafutia mradi ambao unaitwa Mradi wa *TACTIC* ambao unakwenda kuweka historia kwa kujenga stendi ya kisasa kwenye Jiji la Arusha. Mchakato wa kumpata mzabuni unavyokwenda unatia mashaka na ndiyo maana hapa nataka niwaombe TAKUKURU waongeze sikio na jicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilitangazwa *tender* kwa ajili ya kumpata mkandarasi tarehe 19 Januari, 2024, mkandarasi akapatikana kwa shilingi 23,591,762,064/=. Baada ya kupatikana huyu mkandarasi, Mkurugenzi wa Jiji akatoa barua *(Letter of Acceptance)* kwa mkandarasi tarehe 27 Mei, 2024 na mkandarasi huyo alikuwa anaitwa *MS China Jiangxi Cooperation for International Economic and Technical Corporation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo Mkurugenzi akapokea maelekezo kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI ya kutaka Mkandarasi aliyeshinda kwa shilingi bilioni 23 asipatiwe kazi badala yake apatiwe kazi Mkandarasi aliye-*bid* kwa shilingi 31,036,152,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelekezo hayo ambayo tofauti yake sasa ya aliyeshinda kama *lowest bidder* na huyu wa pili anatakiwa kupewa ni shilingi bilioni 7.4 ambayo ingeokolewa ingesaidia barabara, ingesaidia vivuko na vitu vingine, na tungekuwa tumeongeza heshima kwa jitihada za Mheshimiwa Rais kwenye kutafuta fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, michakato ikaendelea ikaonekana kuna ugumu, Mkurugenzi wa Jiji la Arusha ambaye alipokea maelekezo uliyoyasema kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI, 12 Septemba, 2024, ilipofika tarehe 3 Februari, 2025 akai-*cancel tender* hiyo. Baada ya kuona kwamba aliyeshinda *bid* ni ndogo huku na maelekezo mambo yakakutana katikati hapo mchakato ukafutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato ulipofutwa ikatangazwa tena *tender* na moja ya kigezo, walisema mkandarasi awasilishe

ushahidi wa kuwa amefanya miradi isiyopungua ya dola milioni 46 na aliwasilisha miradi siyo chini ya dola 147,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, *tender* ikatangazwa tena wakati tayari Mkandarasi alishapewa na *notice* ya kuwa *awarded* kwamba ameshinda hiyo *contract*. *Tender* ilipotangazwa…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mrisho Gambo samahani…

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Hayo unayozungumza nafikiri yameshapelekwa kwenye Kamati ya Maadili, yataenda kujadiliwa kule. Kama una hoja nyingine ya ziada naomba uzungumze. *(Makofi)*

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Hapana. Hili jambo ni jipya kabisa, halihusiani na zile hoja nne za asubuhi. Ni jipya kabisa, naomba nipate haki ya kuchangia, kwa sababu…

**MWENYEKITI:** Si ni jambo la hilo soko ambalo unazungumzia?

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Hapana, Siyo soko. nazungumzia stendi, ni jambo jipya kabisa.

**MWENYEKITI:** Hiyo stendi pia si imezungumziwa asubuhi?

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Hapana. Haijaingia kwenye hizo hoja. Hili ni jambo jipya kabisa. Naomba nipate nafasi ya kuchangia kwa sababu TAKUKURU wapo hapa na Wizara hii inahusika na TAKUKURU…

**MWENYEKITI:** Basi naomba ujitahidi usiguse jambo lolote ambalo limeshazungumzwa asubuhi na kupelekwa maamuzi yake kwenye Kamati ya Maadili.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadaye ikatangazwa tena *tender,* akapatikana Mkandarasi mwingine mmoja akashinda kwa shilingi bilioni 30, mwingine shilingi bilioni 31. Anataka apewe aliyeshinda kwa shilingi bilioni 31 siyo wa shilingi bilioni 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa kuna jambo la kufanya kwa wenzetu wa TAKUKURU kupitia Ofisi ya Rais, Utumishi, ili tukaokoe hizi fedha ambazo Mheshimiwa Dkt. Samia anazitafuta kwa jasho na damu dunia nzima ili kuwasaidia wananchi wa Jimbo la Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizingatia maelezo yangu mimi simtuhumu mtu hapa, naeleza *scenario* na ninatoa nafasi kwa taasisi zinazohusika zikafuatilie ili ukweli ukijulikana hatua zichukuliwe, ikiwa vinginevyo tutakubaliana pia na matokeo. Kwa hiyo, na hao waliopo sasa hivi, mmoja ameshahamia kule *PPRA* ambao kwa maoni yangu mimi, wote hawa mmoja 30 mmoja 31 bado wanazidisha gharama zile zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ikichunguzwa na ikadhibitika, tutafute namna yoyote ikiwezekana, akipatikana aliye-*bid* chini tutaweza kuokoa gharama kubwa zaidi na wananchi watapata stendi yao kama Rais alivyokuwa anaifanyia kazi pamoja na masuala mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona hilo jambo niliseme kwa sababu ni jambo naona lina maslahi mapana katika Jimbo letu la Arusha Mjini na stendi ambayo kama isingekuwa haya mambo niliyoyasema hapa, pengine siku nyingi tungeshapata mkandarasi na kazi pengine ingeweza kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kwenye upande huu wa Utawala Bora ambayo pia na TAKUKURU wapo, nataka nitumie fursa hii kwa kweli kutoka kwenye dhati ya moyo wangu kuwapongeza sana TAKUKURU na hasa kupitia Mkurugenzi wake Chalamila na wasaidizi wake walioko Mkoa Arusha na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tuna changamoto kubwa sana kwenye upande wa bodaboda. Kuna hela zilichukuliwa kwenye akaunti, waliochukua walikuwa wanajulikana, nimelalamika Bungeni kwa muda mrefu, lakini wahusika hawakupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nazungumza nikiwa na furaha kwa sababu tayari TAKUKURU wameshamkamata mmoja wa wahusika walioiba fedha za bodaboda, ambaye alikuwa ni Mwenyekiti wa umoja huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado wanaendelea na jitihada za kuwatafuta wahusika wengine. Tunaomba wahusika wote watafutwe na wanapokamatwa wapelekwe Mahakamani. Lengo letu sisi, zile fedha zipatikane, zirudi ili zikawasaidie bodaboda kama malengo yetu ya awali yalivyokuwa wakati tunatafuta zile fedha za kuweza kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawapongeza sana TAKUKURU najua mmefanya haya kutokana na uongozi imara wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ili waweze kuhangaika na rushwa na ufisadi kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ni kuhusiana na *TASAF*. Wenzetu wa *TASAF,* na hili Mheshimiwa Simbachawene analijua vizuri. Tulikwenda pale na Mheshimiwa Mhagama kabla hajawa Waziri wa Utumishi, akaenda, na Askofu Sosi yuko pale, akaahidi kwamba kile kivuko kitajengwa na *TASAF* na akatoa mpaka *deadline,* lakini mpaka leo kivuko hakijajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilienda kumtembelea Askofu akanipa hizo *concern,* nikamfikishia Mheshimiwa Waziri Simbachawene na akaongea na Baba Askofu, akaelekeza Kivuko cha *TASAF* cha Betheli ambacho kiko Shule ya Msingi Kijenge na chenyewe kijengwe. Mpaka leo bado hakijajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kuomba watu wetu wa *TASAF* wakipe uzito kivuko kile kwa sababu, pale kuna shule ya msingi watoto wanasoma, pale kuna watu

wanaabudu kwenye Kanisa, kikitengenezwa kitasaidia sana kuondoa changamoto kwa wananchi wetu wa Kata ya Kimandolu pia na eneo la Kijenge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna Mradi wa *TASAF* kule Engutoto *Block 'J'* ulipitishwa kwenye vikao vyote vya halmashauri, fedha pia zilipatikana lakini mpaka leo kile kivuko hakijajengwa na wananchi walishaambiwa na walishaandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Simbachawene na kivuko hiki cha *Block 'J'* kule Engutoto Njiro na chenyewe pia kiende kikajengwe kwa sababu kilifuata taratibu zote na kikapitishwa na fedha zikatoka, lakini mwisho wa siku kivuko bado hakijajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nini kilitokea? Kuna mamlaka ya kufuatilia ndiyo maana wakati mwingine tunapewa malalamiko kwamba Mbunge hahudhurii vikao. Nilihudhuria kikao cha Baraza la Bajeti la juzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya bajeti ikasomwa pale, taarifa inamalizwa kusomwa, hata hatujaijadili, tukaambiwa kuna kiongozi anakuja kama mgeni. Kiongozi akaja pale, watu wakaanza kulia, bajeti ikafungwa na ndiyo bajeti yenyewe ambayo imeletwa TAMISEMI kwenye vikao haikujadiliwa. Sasa hapo utawala bora uko wapi?

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo…

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Taarifa iko wapi?

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko hapa.

**MWENYEKITI:** Ndiyo Mheshimiwa Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingetaka ni-*interrupt* hoja za mwenzangu, lakini nataka niipongeze sana *TASAF* kwamba wamejenga kivuko pale kwetu Samanga kwenda Sembeti, na kivuko hicho kimetembelewa na Kamati. Kamati ilihusika na imekiona ni cha hali ya juu sana. Kwa hiyo, na huko kwake itafanyika tu, asiwe na wasiwasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mrisho Gambo unaipokea Taarifa hiyo ya Mheshimiwa Dkt. Kimei.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea, maana najua imenisaidia pia kuendelea kujijenga jimboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sekunde kidogo kwa sababu dakika zangu amechukua Mheshimiwa Kimei.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia nusu dakika, muda umeisha, kengele imelia.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitumie fursa hii kutoka kwenye sakafu ya moyo wangu, kwa kweli kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametatua changamoto nyingi sana za watumishi, wana miaka mingi walikuwa hawajapanda madaraja, lakini kwa Mheshimiwa Dkt. Samia walipanda madaraja. Mishahara ilikuwa haijapanda kwa Mheshimiwa Dkt. Samia mishahara imepanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, malimbikizo yalikuwa hayajalipwa, lakini kwa Mheshimiwa Dkt. Samia malimbikizo yamelipwa. Bado watumishi wamenituma nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia, lakini naomba niendelee kumkumbuka na ikiwezekana apandishe mishahara yao na siyo tu watumishi wa umma, lakini pia watumishi wa sekta binafsi ambao kiuhalisia mishahara yao imekuwa midogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta binafsi zinajiamulia wakati mwingine kwa sababu malengo yaliyowekwa ni madogo wanatembelea mule mule. Kwa hiyo, tunaomba mtusaidie pia kuwasimamia angalau kima chao cha chini cha sekta binafsi kifanane angalau na kima cha chini cha Serikali ambacho ni kikubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mrisho Gambo. Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa kipindi cha asubuhi umeishia hapa.

Kwa hiyo, tutaendelea na wachangiaji wengine jioni, nitawataja wale ambao wataanza ambao ni Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta na Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuwataja hao, niwatakie mchana mwema. Nasitisha Shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.02 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Joseph K. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Hoja za Serikali, tunaendelea na uchangiaji, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Mchana huu tunaanza na Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge atafuatiwa na Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya na Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko ajiandae.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utawala Utumishi wa Umma na Utawala Bora, inayoongozwa na bosi wangu wa kipindi hicho, kaka yangu Mheshimiwa Boniface Simbachawene. Niseme tu kwamba kwa ambavyo ametutendea haki Mheshimiwa Simbachawane kwenye maeneo mbalimbali ambayo mamlaka ilimpa dhamana ya kusimamia, amefanya vyema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ofisi hii ya Mheshimiwa Rais yeye akiwa Waziri wa Nchi, niseme tu kwamba pasipo na kupepesa macho wala kumung'unya mdomo, Mheshimiwa Simbachawene anastahili pongezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara kadhaa nimeshuhudia baada ya mijadala ya Bungeni mara nyingi yeye huwa anarudi ofisini kwenda kusikiliza hoja mbalimbali za Watanzania na kuzitatua; na mwenyewe nimemkuta ofisi akifanya shughuli hiyo nami nikiwa mteja wake amenihudumia ipasavyo. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msaidizi wake rafiki yangu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, ndugu yangu Mheshimiwa Deus, niseme tu kwamba wana Kwela hawakufanya

makosa kukuchagua, na nina imani kwa *spirit* ya kazi uliyonayo katika nchi yetu, na pia katika Jimbo lako, wana Kwela wanakwenda kukurudisha tena utumikie nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami katika mchango wangu, kwa upekee wake kabisa, nitazungumzia Watumishi wa Umma Kada ya Ualimu. Kwa muktadha wa mchango wangu, nitazungumzia walimu wa shule za msingi, walimu wa sekondari na walimu wa Vyuo vya Ualimu ambao kimsingi taratibu zao za kazi zinafanana, lakini pia yale ambayo yanawasibu katika mazuri na yale ya misukosuko kidogo katika kazi yanafanana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kupeleka salamu za walimu kwenda kwa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan zikipitia kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ndugu yangu, kaka yangu Mheshimiwa Simbachawene. Walimu wa Tanzania wanasema, wanamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba sasa wanafanya kazi katika mazingira bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameboreshewa mazingira ya ufundishaji, na mazingira ya kutunza watoto wetu. Leo hii tunapozungumza, kila kona ya nchi kuna madarasa ya kutosha, mazuri, vyoo vya kutosha kwa ajili ya watoto wetu na viko katika hali nadhifu, nyumba za walimu; ni mchakato ambao Mheshimiwa Rais ameendelea nao katika kipindi chake chote cha uongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika hilo walimu wa Tanzania wanasema wanampongeza sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kana kwamba haitoshi, wanasema kwamba kilio chao cha siku nyingi cha upandishwaji wa madaraja na hata yale ambayo yamelimbikizana, kipindi cha Uongozi wa Rais Dkt. Samia tumekuja kushuhudia kwamba walimu

wetu wakipandishwa madaraja kila pale inapostahili kufanyiwa hivyo. Wanashukuru sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili wana ombi moja tu, kwamba fedha za likizo sasa kwa kweli wanashukuru wanazipata, lakini wanaomba tu, badala ya kupitia kwa waajiri wao, zitoke Hazina, walipwe moja kwa moja ili kuondoa usumbufu na adha, na pia kutofautiana kati ya mwajiri mmoja na mwajiri mwingine, hilo ndiyo ombi la walimu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, niseme tu kwamba kumekuwa na mashauri ya kinidhamu ya walimu kwa muda mrefu. Kwa uchache sana niseme kwamba kuna walimu wetu 14 ambao mashauri yao yalishathibitishwa kwamba hawana hatia na Tume ya Utumishi wa Walimu tangu mwaka 2023. Ilikuwa ni tarehe 4 Machi, 2023, Katibu wa Tume anamwandikia Katibu Mkuu Utumishi ku-*clear* kwamba walimu wetu hawa hawana hatia, na kwa maana hiyo wanaombewa kibali cha kurudi kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ni walimu kutoka Halmashauri zetu mbalimbali nchini, wanaomba Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma chini ya ndugu yangu, kaka yangu Mheshimiwa Simbachawene, tupe msukumo katika jambo hili ili walimu wetu hawa ambao wamesafishwa na Mamlaka yao ya nidhamu, warudi kazini waweze kutumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo langu la tatu la uchangiajia, nilikuwa nina rai kwamba tutoe motisha kwa watumishi mbalimbali kwa mujibu wa majukumu na uzito wa kazi zao. Hapa nijitolee tu kuwa, kama chachu ya kuanza kusaidia ofisi yetu ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora nifanye kwa uchache tu kitu kinachoitwa *job analysis,* kwa maana ya mchanganuo wa kazi za walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la msingi la mwalimu ni kufundisha, lakini katika ufundishaji wake kuna vitu mbalimbali ambavyo kabla ya ufundishaji anaviandaa vikiwemo; *scheme of work, lesson plan, lesson notes, log book, class journal,*

*attendance list* na vingine; na hapa nina mlolongo wa nyaraka ambazo walimu wanazitumia, hizi hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchache wake tu hizi zote ni nyaraka ambazo walimu wetu wanazitumia wanapofundisha Watoto. Hizi ni kwa uchache tu, lakini zipo nyingi. Hizi hapa zote; zipo *Scheme of Work* zote zipo hapa, mpaka *Teaching Aid* anapokuwa darasani, mwalimu analazimika kuandaa kitu ambacho itakuwa ni msaada kwa watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni *Teaching Aid* ya Mwalimu wa *Mathematics,* akifundisha *product of two linear equations*. Kwa maana, hapa anatafuta eneo, *area of this rectangle*. Hii ni kazi ya walimu wetu. Pamoja na kazi ya ufundishaji na zana zote hizi ambazo walimu wetu wanaziandaa. Walimu wetu hawa wamekuwa wakitumia *reference book* mbalimbali, vitabu vya kiada na vitabu vya ziada

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wamekuwa wakitoa majaribio mbalimbali ya *quiz* za darasani, mitihani ya kila wiki, mitihani ya kila mwezi, mitihani ya kila muhula, mitihani ya kila mwaka na wanakuwa na jukumu kubwa la kusahihisha *scripts. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimkuta mwalimu amejifungia kwa wale ambao wenza wao ni walimu watakuwa ni mashuhuda kwamba, kama baba ni mwalimu, mama yuko kitandani amepumzika anamwacha baba anasahihisha *scripts* za watoto. Kama baba ni kada nyingine mama ni mwalimu, baba amepumzika kitandani usiku, mama anasahihisha *scripts* za watoto mpaka saa saba za usiku, ni lundo. Hiyo ni *workload* kubwa ya walimu wetu katika hii nchi yetu hii. *(Makofi)*

**MHE. DKT. BASHIRU A. KAKURWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa. Niko hapa Bashiru, niko hapa taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa haya taarifa, karibu.

**TAARIFA**

**MHE. DKT. BASHIRU A. KAKURWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango mzuri, siyo mara nyingi kutoa taarifa, lakini mchango wake kwa uzito wake nathibitisha anayoyasema. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ni Mwalimu, na mke wangu ni Mwalimu. Unapofika wakati wa kusahihisha, wakati wote tuko darasani, ni kama vile tumeahirisha ndoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu haruhusiwi kutoa taarifa, kwa niaba yake naye ni mwalimu anaweza akathibitisha. Hata Mheshimiwa Spika naye anaweza akathibitisha. Kwa hiyo, mchango huu una uzito wa aina yake na ndiyo maana kwa walimu motisha wetu mkubwa sana huwa ni wito. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Bashiru Kakurwa, ahsante. Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyevu na heshima kubwa ninapokea taarifa. Niweke taarifa sahihi tu hapa kwamba aliyetoa toa taarifa ni mwalimu wangu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, aliyenifundisha *Political Science* mwaka 2001 mpaka 2004. Kwa maana hiyo, siwezi kuwa na pingamizi wala kigugumizi kwa taarifa yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nakurejeshea dakika zote ambazo ametumia Dkt. Bashiru. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Pamoja na yote haya, walimu bado wanakazi ya kuingiza taarifa zao katika mifumo. Sasa hivi tunakwenda *e-Government* lakini walimu wetu wamekuwa na mzigo mkubwa wa kuingiza taarifa, kwani mifumo ni mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mfumo unaoitwa *Info* Taaluma, kuna mfumo unaitwa *PEPMIS,* kuna mfumo unaoitwa

*BEMIS,* kuna mfumo unaoitwa *MadeniMIS,* kuna mfumo unaoitwa *SIS,* mifumo ni mingi na kwa maana hiyo walimu wanatumia bongo zao kwa muda mwingi sana kufanya kazi za ziada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiondoa majukumu ya kitaaluma ya walimu wetu, wamekuwa na majukumu mengine yasiyokuwa ya taaluma zao ikiwemo usimamizi wa miradi. Sote ni mashahidi kwamba miradi yote ambayo Serikali yetu pendwa inatekeleza katika shule zetu kwa maana ya ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu, vyoo na kadhalika, wasimamizi wakubwa ni walimu hao hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu hawa leo wamekuwa ndio ma-*procurement officer,* wanaingia katika mifumo kutafuta wazabuni wa kujenga majengo yetu, walimu hawa leo ndio wamekuwa ma-*project manager* wa kusimamia miradi katika shule zetu, walimu hawa leo ndio wamekuwa ma-*engineer* wa kusimamia majengo yetu katika shule zetu. Haya ni majukumu nje ya taaluma zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nani siyo shuhuda kwamba walimu wetu wamekuwa wakihusika katika majumu pia ya kitaifa? Leo hii tumeshawasha Mwenge na umeanza kuzunguka katika Mikoa yetu, lakini nani siyo shuhuda kwamba walimu wetu wamekuwa ndiyo chachu ya Mwenge? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiona vijana wa halaiki wanasherehesha kwenye Mwenge pale, ni kazi ya walimu wetu. Ukiona *club* za wapinga rushwa kwa ajili ya kukidhi vigezo vya Mwenge, ni kazi za walimu wetu; ukiona shughuli za Kitaifa kama vile Sensa, Uchaguzi, programu mbalimbali za lishe, chanjo mbalimbali, majukumu hayo wanatekeleza walimu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na majukumu haya ya kimsingi ya taaluma zao na ya ziada, nakuja na mapendekezo kwamba, kutokana na uchambuzi nilioufanya kwa muhtasari wake, walimu kuna kitu cha ziada wanatakiwa wafanyiwe katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirejee kitabu kitakatifu cha Biblia, kitabu cha Isaya, Sura ya sita mstari ule wa nane nanukuu: "kisha nikasikia sauti ya Bwana akisema, nimtume nani, naye ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu?" *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza Bunge lako Tukufu, nani atakwenda kufanya kazi kwa ajili ya kuwapa motisha, kuwapa moyo, kuwatia nguvu walimu wetu? Kila mtu ana jibu lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitamani Bunge letu hili la Kumi na Mbili, ambalo Mheshimiwa Spika wetu ni Mwalimu, ingekuwa ni chachu ya hiki ambacho ninakipendekeza. Napendekeza kupitia Ofisi ya Rais, Utawala Bora na Menejimenti ya Utumishi wa Umma, tuanzishe Sera Maalumu kwa ajili ya Motisha kwa Walimu *(Teacher Motivation Policy Framework)* na itakapobidi, kwa sababu andiko linasema nimtume nani? Mimi nitakuwa namba moja kwenda kusaidia Ofisi ya Rais kuandaa *framework* hii ya Sera. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kassinge, ahsante sana, ahsante sana…

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, nakushukuru kwa kunivumilia na kwa kuniongezea muda ule wa kufidia. Baada ya taarifa hii, naomba kusema kwamba naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, mwalimu ahsante sana. Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya atafuatiwa Mheshimiwa Mwalimu Husna Juma Sekiboko na Mheshimiwa Mwalimu Margaret Simwanza Sitta ajiandae.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi nami niweze kutoa mchango wangu katika hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Utumishi kwa kazi nzuri wanazozifanya. Kipekee Mheshimiwa Waziri toka aingie Ofisi hiyo ametatua changamoto nyingi za kiutumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimpongeze Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anazozifanya hususan kwa kukubali kuridhia kuboresha na kutengeneza mifumo ikiwemo mifumo ya ukusanyaji mapato na mifumo mbalimbali. Tumeona kabisa mapato yameongezeka Serikali za Mitaa pamoja na Serikali Kuu, lakini Mheshimiwa Rais akaenda mbele zaidi akataka mifumo hii iweze kuunganishwa ili iweze kuleta tija zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee leo niongelee Mfumo wa Watumishi uliopo Ofisi ya Utumishi ambao umeleta maboresho makubwa katika Wizara hiyo. Wengi tulishuhudia katika miaka ya nyuma kulikuwa kuna wimbi kubwa sana la watumishi hewa, kulikuwa na wimbi kubwa sana la mishahara hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia maboresho ya mifumo, changamoto hii imeweza kutatuliwa kwa kufanya mawasiliano ya taasisi na Wizara kwa muda muafaka ili kuwaondoa watumishi waliofariki kwenye mfumo, waliostaafu, walioacha kazi pamoja na changamoto mbalimbali ili iweze kuokoa fedha za Serikali ambazo zingeweza kulipwa kama mishahara isiyostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza pia kwa kufanya kazi ya kupunguza malimbikizo ya mshahara kupitia mfumo huu. Ni dhahiri kwamba mtumishi anaingizwa kwanza kwenye mfumo ndiyo anapata barua ya ajira, hali kadhalika hata aliyepanda daraja anaingizwa kwanza mfumo ndiyo anapata barua ya kubadilishiwa daraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona tumepunguza kwa kiasi kikubwa mlundikano wa malimbikizo ya mishahara, lakini natambua madeni ya mishahara bado yapo. Nami nikiwa Mjumbe wa Kamati ya Bajeti nashuhudia namna Serikali

inavyolipa madeni kwa watumishi yakiwemo ya likizo, mishahara pamoja na ya matibabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kupongeza, kama tutakumbuka, tulikuwa na uhakiki wa watumishi mwaka 2016 na zilijitokeza changamoto nyingi kuathiri madaraja ya watumishi, nami nilikuwa na hoja yangu ya watumishi ambao walipata barua kwa pamoja, wengine wakapandishwa madaraja, wengine wakasimamishwa kupisha uhakiki. Leo nimesimama mbele nikiishukuru na kuipongeza Serikali. Sasa, wale watumishi wa kipindi kile madaraja yao yanaenda sambamba, wote wamerekebishiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke pia, zoezi hili la mwaka 2016, liliathiri mserereko wa madaraja kwa watumishi walioajiriwa mwaka 2013, 2014 na 2015 na kusababisha watumishi hawa kutumikia daraja moja kwa muda mrefu sana. Mathalani ajira ya mwaka 2013 walikuja kupandishwa mwezi Mei, 2019. Kwa hiyo, kukawa na miaka mitano zaidi badala ya ile mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watumishi wa mwaka 2014/2015 wenyewe wakarekebishiwa mwaka 2021. Kwa hiyo, wakachelewa kwa miaka sita na miaka mitano. Naomba sasa Serikali kwa kuwa yale mliyafanya, na tuendelee sasa kuwarekebishia, ili waende sambamba na madaraja ambayo yanawastahili ili tuondoe ile kero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, naipongeza Serikali, upande wa Serikali za Mitaa ilipochukua jukumu la kuwachukua Watendaji wa Kata pamoja na Vijiji kuwaingiza *payroll* ya Serikali Kuu. Tuliondoa mzigo mkubwa na walikuwa wakinyanyasika na wakati mwingine walikuwa hawakopesheki kwenye benki kwa sababu mishahara yao ilikuwa haitabiriki watalipwa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu walikuwa hawaujui hata mwisho wa mwezi kwa sababu ilikuwa ni Mkurugenzi atakapojisikia kuwalipa au halmashauri itakapokuwa na mapato ndiyo itawalipa mshahara. Pia, iliathiri michango katika hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaweza tukashuhudia watumishi wengi, Watendaji wa Kata na *VEO* wanaostaafu wameshindwa kupata mafao yao sahihi kulingana na madeni ambayo hayajalipwa na Wakurugenzi wao. Wengine wamediriki kuandika barua *PSSSF* kuwaomba, nilipe tu mafao yangu bila michango ambayo haijalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi, hatuwatendei haki. Naomba kwa mfano, Halmashauri ya Meatu mafao ambayo hayajachangiwa na Mkurugenzi kwa *WEO* na *VEO* ni shilingi milioni 43.7 ukiongeza na riba ni shilingi milioni 45.6. Jumla wanadaiwa shilingi milioni 89.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wengi waliostaafu wanalia, mafao yao yameshindwa kulipwa. Naiomba Serikali, kama tulichukua madeni mengine ya watumishi, naomba basi hata huu mzigo tuuchukue mtaji kwa Wakurugenzi, tuingize Serikali Kuu, ili waweze kuchangiwa ile michango yao wapate mafao yao wanayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia mshahara wa *VEO* unasikitisha, ni mdogo halafu anakosa mafao yake. Huyu ana watoto wapo Chuo Kikuu, ana mahitaji yanatakiwa katika familia. Kama vipi, Serikali iweke mkakati madhubuti utakaowataka Wakurugenzi haya malimbikizo ya michango wakayalipe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, hawa Watendaji walioondolewa kwenye utumishi kwa sababu walikuwa ni Darasa la Saba, wakarudishwa, wengine mpaka leo hawajalipwa mishahara yao na Mkurugenzi. Naomba na wenyewe waweze kusaidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu ajira mbadala ambavyo imeathiri upungufu wa walimu katika Halmashauri ya Meatu. Naiomba Serikali inieleze, kwa nini tuliiacha ajira mbadala kurudishia wale watumishi ambao walistaafu, waliofariki na kuacha kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani, katika Wilaya ya Meatu, kwa miaka mitano waliohama; niongelee elimu msingi peke yake ni walimu 165 na walioajiriwa ni walimu 122. Kwa hiyo, kulikuwa kuna tofauti ya walimu 45. Ukiangalia pale haijafidia tu wale waliohama, bado tuna pengo kubwa la watumishi upande wa elimu msingi ambapo mahitaji ni walimu 1,700, na upungufu ni 650. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba basi Serikali, pamoja na inavyoendelea kuajiri, irudishe ile ajira mbadala, kwa sababu tuna pengo kubwa, kwani tunapokua na maendeleo, changamoto huwa zinakuja kutokana na maendeleo. Tuna Shule za Msingi mpya nyingi pamoja na Sekondari ambazo pia zimechangia upungufu wa walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali pia ilifanyie kazi hili. Pia, wale watumishi wanaojitolea ambao hawajaajiriwa, tuliambiwa kwamba tutaletewa mkakati ili wasomeke pia itakapotoka ajira wawe wanatambulika. Tofauti na mwanzo walipokuwa wakiomba, Wakurugenzi wanapeleka watu ambao hata hawajajitolea kwenye yale maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa miradi mizuri tuliyopewa na *TASAF*. Tumepewa mabweni Bukundi, Imalaseko tumejengewa Daraja la Mawe zuri, tuna zahanati nzuri Itongo nyumba za watumishi Iramba Ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya. Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, atafuatiwa na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara ajiandae.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi. Awali ya yote, nitumie fursa hii kumpongeza na kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajadili Ofisi ya Rais, Utumishi. Wizara hii kwa mujibu wa sheria, Waziri mwenye dhamana ni Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Yeye tunampongeza kwa sababu tumeona mabadiliko makubwa katika Utumishi wa Umma nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale ambao wanatoka kwenye utumishi kama mimi, tutakumbuka miaka michache tu iliyopita, kila aina ya kada ya Utumishi tulikuwa na wimbi kubwa sana la madai ya watumishi, malimbikizo, madai ya safari za kiutumishi, madai ya uhamisho na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa kipindi kifupi ndani ya utendaji na utekelezaji wa kazi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tumeshuhudia kupungua kwa kiasi kikubwa kwa malalamiko ya Watumishi wa Umma. Kwa kweli kwa dhati kabisa tunamshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Simbachawene. Mheshimiwa Waziri kwanza wewe ni darasa, sisi Wabunge hasa wale wachanga wenzangu tumekuwa tukijifunza mambo mengi kupitia kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ambalo nataka niliseme leo kwa dhahiri, Mheshimiwa Simbachawene wewe ni mkweli sana. Siyo tu ndani ya Bunge, lakini hata kwenye Vyombo vya Habari tumekushuhudia ukizungumza ukweli na kuwashibisha Watanzania juu ya mambo ya ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Simbachawene tunakushukuru na tunakupongeza sana. Kaka yangu Mheshimiwa Deus wewe ulikuwa Mwenyekiti mwenzangu nafahamu. Wewe ni mtu mwema, kiongozi hodari na uwezo wako hauna mashaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza na kuwashukuru sana Watumishi wote wa Umma nchini kote. Kama kuna Mbunge

aliyekuja humu ndani, amemtegemea Mtumishi wa Umma. Kama kuna mwananchi yupo nyumbani anapata maji, anapata umeme, anasafiri kwenye barabara na anapata matibabu anahudumiwa na Mtumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza sana Watumishi wa Umma kokote mlipo Tanzania, kazi yenu ni kazi njema, Mwenyezi Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ingelikuwa uamuzi wangu, baada ya mchango wa Mheshimiwa Janejelly na baada ya mchango wa Mheshimiwa Ally Kassinge, nisingesimama kuzungumza. Mheshimiwa Janejelly amezungumza vizuri, kwa ufasaha kuhusu changamoto za Utumishi wa Umma kwa sasa. Mheshimiwa Janejelly amezungumza namna ambavyo Sekretarieti ya Ajira imeamua kukunja mikono na kuacha kazi zake kwa taasisi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianzie hapa. Ajira za Tanzania ni mali ya Watanzania wote, nami inamwelewa sana Mheshimiwa Simbachawene. Aliwahi kuzungumza akasema, hizi ajira ambazo tunatangaza ni chache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania ambao wanazihitaji ni wengi kupita maelezo, lakini tunatumia vigezo mbalimbali angalau kuwapata wachache wanaohitajika, lakini haina maana kwamba, hao Watanzania ambao hawapati ajira hawana sifa. Namnukuu Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni nini? Watanzania wengi wenye sifa wanatamani kuajiriwa siyo tu kwenye Serikali, hata kwenye mashirika binafsi, lakini ajira zilizopo ni chache. Sasa, ni namna gani Serikali inatoka kwenye lawama? Hakuna namna ambavyo Serikali itatoka kwenye lawama ya ukosefu wa ajira nchini kwa sababu huyu ndio mzazi, mama na baba wa Watanzania ambaye tunategemea alishe Watanzania wote kwa matarajio yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kutoa ajira Serikalini na kuipa taasisi fulani ifanye mchakato wa ajira na usaili, halafu ikwambie hawa ndio wa kuajiriwa, waajiri, hili halipo sawa. Halipo sawa kwa sababu wewe ndio unajua unamhitaji mtumsihi wa namna gani kwenda kufanya shughuli gani? Wewe ndio unajua njaa ya Watanzania kwenye soko la ajira, na mahitaji ya Serikali katika ajira ambazo zimetangazwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uki-*hire* na ku-*outsource* ukampa mtu binafsi akaenda kutafuta watumishi akakuletea wewe, hilo ni bomu ambalo mwisho wa siku Watanzania tutapata tabu nalo. Ni lazima kama Serikali tukubali, kama mtoto unayemlea, uliyemzaa mwenyewe hashibi chakula unachompatia, hawezi kwenda kushibishwa kwa jirani. Huwezi kumwambia mjomba wake mlishe huyu labda ataridhika, haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kukwepa. Nafahamu tunakwepa pengine upendeleo kwenye ajira na vitu vya namna hiyo, lakini mwisho wa siku mwarobaini wake siyo ku-*outsource* usaili na udahili wa wanafunzi. Hii siyo sahihi, na haileti picha nzuri kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tuliyoiamini ina vyombo vya ulinzi na usalama na vyombo vya kiutumishi. Tunategemea vyombo hivyo vi-*screen* viondoe upendeleo na vifanye *vetting* na viwasaidie Watanzania kupata watumishi wanaotakiwa, siyo abadani kutafuta kampuni na kuikabidhi jukumu la ajira. Hiyo haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo haikubaliki, tunatamani kuona Serikali yetu inafanya jambo hili hasa ukizingatia kwamba jambo la ajira ni jambo la kiusalama. Lazima Serikali yetu ifanye kazi hii kwa mikono yake na siyo kumpatia mtu mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mfumo wa Ajira, sasa watoto wanaitwa kutoka Mara, Tanga, Zanzibar wanakusanywa kwenye Majiji mawili au matatu. Gharama ya huyo mtoto kusafiri na kwenda kuishi haiangaliwi na bado atashindwa kwenda kuingia kwenye usaili, ataambiwa hana sifa. Hii haipo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwapunguzie gharama hawa watu wanatafuta ajira na wanatoka kwenye kaya masikini. Kwa nini hii mifumo ya ajira wasiende kufanyiwa usaili kwenye maeneo yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru na kuwapongeza sana TAMISEMI, wameanza kufanya hivyo kwenye Ajira za Ualimu na Afya. Leo nimeona Tangazo la Polisi, nawashukuru na kuwapongeza Mambo ya Ndani wameenda kufanya hivyo, wanafanya *screening* kule kwenye mikoa wanapotoka wananchi. Suala la kuwaita sehemu moja, hii haipo sawa, tunachochea mambo ambayo hayakubaliki kimsingi na kimaadili ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizungumzia watumishi haki zao, kwanza, mtumishi anatumia akili ubongo, hatumii nguvu. Anatumia akili, kama ni mwalimu kufundisha, kama ni daktari kufanya matibabu, lakini anatumia zaidi akili. Lazima awe *free* na ametulia aishi katika mazingira tulivu. Lazima ahudumiwe vizuri na aishi katika mazingira ambayo yanamruhusu kuwekeza muda na maisha yake kwenye utumishi zaidi kuliko kwenye mambo mengine. Je, hili tunalifanya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtumishi wa Umma kuomba uhamisho tu siku hizi imekuwa ni *Jihad;* mimi nataka kuhama hapa nikahudumie wazazi wangu, wapo sehemu fulani. Namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Simbachawene na mwaka 2023 alisimama, na mwaka 2024 alitoa tamko na waraka kwamba anayeamua kuifuata familia yake aruhusiwe kuifuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni njia ya kuendelea kujenga maadili ya nchi yetu, lakini Mheshimiwa Simbachawene bado wanazuia wale wanaowafuata wake na waume zao, hawapewi uhamisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo lazima tuamue kama kweli tuna dhamira ya kuwasaidia watumishi ili waweze kuwa *productive* kwenye maisha na maeneo yao ya kazi. Ni lazima tukubaliane kwamba Waraka uliotolewa na Serikali wa kumruhusu

mtumishi kumfuata mwenza kwa ajili ya kwenda kukaa kwenye eneo ambalo anaweza kuhudumia familia yake vizuri, liweze kukubaliwa na lichukuliwe ni kipaumbele katika hamisho za watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize na suala la *TASAF*. Niliwahi kutembelea Korogwe na niliwahi kusema humu ndani. Nilipita Korogwe nikakuta familia moja masikini sana, babu ana miaka zaidi ya 80, mke wake ana miaka zaidi ya 70. Mke wake ni mgonjwa, dhaifu na bahati mbaya hawakuwahi kupata mtoto na hawana ndugu, wanaishi pale Korogwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *with time* nikaja hapa nikaomba, jamani zipo kaya ambazo mnasema zime-*graduate*. Kaka yangu Mheshimiwa Shangazi amesema asubuhi, wana-*graduate,* lakini hawapewi vyeti. Zina-*graduate* lakini bado ni masikini wa kupindukia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikaomba, jamani hebu fanyeni uchunguzi, zile kaya ambazo bado ni masikini ziendelee kusaidiwa kupitia Mpango wa *TASAF,* ili waweze kunusuru maisha yao. Nataka nikwambie, baada ya miezi sita yule mama alifariki kwa njaa, matatizo na shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana wananchi wa Korogwe, walikuwa wanachanga, kila mwanamke alikuwa anatoa chakula kupelekea ile kaya, lakini watu wa *TASAF* walikiri walisema, ame-*graduate,* hastahili tena kuhudumiwa na *TASAF*. Hii siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuangalie hao wanaoambiwa wame-*graduate* wana-*graduate* kwa mtindo gani, na katika mazingira yapi, kwa nia ipi? Nadhani kama tunaelekea mwisho wa huu Mfuko wa *TASAF,* lakini tunapoenda kuanza mfuko mwingine lazima tuangalie haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, hii habari ya ku-*graduate* tuangalie tuone, kama ina tija kwa wananchi ama haina tija kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ile habari ya kuwafanyisha kazi eti ni Mradi wa *TASAF,* sioni kama ina tija kwa sababu wengi wanaokwenda kutumika kwenye hizo kazi ni wazee na watu wazima ambao hawana uwezo wa kufanya hizo kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi hii, na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko. Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga ajiandae.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi nami nichangie hoja iliyoko Mezani. Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pili, ninawashukuru wananchi wa Urambo na familia yangu kwa ushirikiano wao wanaonipatia. Pia, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo amenisaidia miradi mingi ya maji, umeme, barabara, na afya mingi mno kiasi ambacho wananchi wa Urambo nao wanasema ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara husika na Waziri husika Mheshimiwa Simbachawene, Naibu wake, Makatibu Wakuu na Watendaji wote kwa kazi kubwa wanayoifanya. Hongereni sana kwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nitoe kwanza kifupi yale nitakayozungumzia angalau wayapate, ili hata kama muda utaisha, basi wawe wameyapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, nitazungumzia suala la umuhimu wa *TSC (Teachers Service Commission)* ambayo iliundwa kwa madhumuni ya kuhudumia walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nitazungumzia umuhimu wa Serikali kurekebisha mishahara ya walimu na wafanyakazi kwa ujumla wanaopandishwa madaraja kabla hawajastaafu, ili kuwawezesha kupata haki zao, kuliko ilivyo sasa ambao wengi kwa mfano wa kwangu wapo 52 ambao hawakurekebishiwa mishahara yao na sasa hivi wanapata shida kupata haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, nitazungumzia kuhusu Watendaji wa Kata na Vijiji. Nianze kwa Kata ambao wanaomba posho yao iongezwe kidogo kutokana na kazi kubwa wanazozifanya, na pia zitoke moja kwa moja Serikali Kuu. Pia, wanaomba Watendaji wa Vijiji na wao wafikiriwe kupata posho, ili iwawezeshe kufanya kazi zao; na mwishoni nitazungumzia umuhimu wa *TASAF* kama walivyozungumza wenzangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana wote waliotangulia kuongea. Wote wameongea vizuri sana kuhusu umuhimu wa kuangalia haki za wafanyakazi. Hongereni wote mlioongea kuhusu umuhimu wa kuangalia haki za wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nitaanza na walimu. Kwa muda mrefu suala la *TSC – Teachers Service Commission* limezungumziwa, nikiwepo mimi mwenyewe humu Bungeni. Kama walivyoongea wenzangu, Mheshimiwa Mwalimu Ally kule, Mheshimiwa Husna na wengine wote ambao wamezungumzia, walimu ni wengi mno. Nilikuwa ninaangalia idadi yao, wanapata kama 294,402 kwa hesabu niliyoipata. Kuwahudumia hawa watu ilionesha tangu mwanzo kwamba ni kazi kubwa sana kuhakikisha kwamba msawazisho unakwenda vizuri, yaani wote wanakwenda vizuri kwa idadi inayotakiwa katika maeneo mbalimbali, na kuwapatia haki zao kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini ndiyo maana Serikali ikaona kuna umuhimu wa kuwa na chombo kimoja ambacho kitawaangalia hawa kwa ukaribu. Ndiyo maana wa kutunga sheria hii ambayo ninayo hapa, ambayo imewapa *TSC* majukumu kutokana na ukubwa wao wa kazi waliyopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaambiwa kwanza ninyi mta-*appoint*, mta-*promote* na mta-*discipline teachers*. Pia, wanaambiwa kwamba mtaangalia *distribution of teachers*. Halafu pia wanaambiwa ninyi mta-*supervise teachers in service training programmes*, lakini pia wanaambiwa wata-*conduct research* na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi ukiangalia eneo hili la (c) la sheria yake kwenye *functions*, wanasema *appoint*, *promote*. Mimi ninaamini Serikali iliiona hii, kwamba kuhudumia hao watu wengi siyo rahisi, kuwe na chombo maalum. Sasa, nataka niiulize Serikali je, malengo yaliyowekwa yameonekana hayafai au kuna haja ya kubadilisha? Kwa sababu kinachoendelea sasa hivi sicho kilichokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali waiangalie hii sheria upya. Je, inajibu matakwa yaliyotakiwa wakati huo? Kama haijibu, basi iangaliwe upya, lakini kuwe na sheria ambayo inaeleza wazi kabisa. Halafu kinachoendelea siyo, ukiangalia hizo *TSC* hasa kwenye ngazi za Wilaya, wanatakiwa watendaji kazi wanne, lakini sehemu nyingi yupo mmoja na wakiongezewa Mkurugenzi anawaazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha wanazopata ni ndogo mno, hawawezi kufanya. Hawana usafiri, hawaingizwi kwenye *system* ya *e*-Wafanyakazi *(e-Employees)*, ule Mfumo wa *e-Wafanyakazi* hawamo. Sasa, ndiyo maana hata utaona kwamba, kama walivyoongea wenzangu waliotangulia, zilipokuja hizi ajira za walimu *TSC* hawakuhusika kabisa, lakini wao kwa sheria hii ndiyo wameambiwa ku-*appoint*, ku-*promote* na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ombi langu la kwanza, sheria iangaliwe upya. Kwa heshima na taadhima, naomba sheria iangaliwe upya ili kama kweli ilikusudiwa, basi ifanyiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumza mwenzangu hapa, kwamba mwalimu anataka kuhama, anaambiwa wewe weka tangazo. Tangazo mtu aombe yuko Rukwa, huko amtafute

Mwalimu mwingine wa Urambo anayetaka kuhama. Ni vitu ambavyo haviwezekani. Ndiyo maana walikuja na sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba, narudia tena, sheria hii iangaliwe ili kweli malengo yaliyokuwepo kama bado yapo, yafanyiwe kazi, sheria hii ifanye kazi kama ilivyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa sehemu nyingi kama nilivyosema, kazi walizonazo kutokana na sheria wamepunguziwa kabisa, kwa hiyo, naomba *TSC* ingaliwe upya kwa heshima na taadhima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nazungumzia suala la wafanyakazi wanaokaribia kustaafu. Naiomba Serikali iwaone wale ambao wanastahili kupandishwa madaraja, wapandishiwe madaraja yao, warekebishiwe mishahara. Mimi nina orodha ya walimu, wamechanganyika na watu wa afya pia. Ninao 52, ukitaka niwaweza kutoa hapa nikawapa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, 52 ambao mpaka sasa hivi wanahangaika, wanadaiwa na *PSSSF*. Walipe fedha wao ndiyo waweze kupata pensheni. Kwa hiyo, wanakwenda kukopa, ninayo orodha hapa. Wanakwenda kukopa ili wapeleke *PSSSF* ili waweze kupata pensheni yao. Ni haki hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali itaweka utaratibu wa watu kurekebishiwa mishahara kabla hawajastaafu, kwa kweli wapewe haki zao kama wanavyostahili. Kama nilivyosema, hapa sasa siyo walimu tu, hata na wafanyakazi wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka kulizungumzia ni Watendaji wa Kata. Wanaomba, kutokana na kazi zao walizopewa, wanaomba waongezewe posho kidogo ili waweze kufanya kazi yao; posho ya madaraka ili waweze kufanya kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, wanaiomba Serikali kwamba fedha hizi zitoke Serikali Kuu moja kwa moja ili kuondoa usumbufu wanaoupata. Pia, Watendaji wa Vijiji nao pia wanaomba

waangaliwe kupata posho kidogo ya madaraka ili iweze kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka kuzungumzia ni suala la *TASAF*. Kama alivyoongoea mwenzangu, *TASAF* ilipoundwa, tunaishukuru sana Serikali yetu ya Tanzania, *TASAF* ilivyoundwa ilikuwa ni kuwasaidia wale wasiokuwa na uwezo. Sasa, itakuwaje mtu anaambiwa, eti tayari ameshakomaa au ame-*qualify*, wakati unamwona kabisa ni mzee ambaye hawezi kufanya chochote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ombi langu kwa Serikali, Serikali iongeze fedha *TASAF* kwa ajili ya watu wanaopata misaada ya *TASAF* ili wanapoingiza wengine, kusiwe na haja ya kuwatoa wale wengine ambao wanasema wamekomaa au nini. Ukiwaona wanaoambiwa wamekomaa, hawajakomaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba tu fedha ziongezwe kwa heshima na taadhima kabisa ili wale wazee waliokuwa wanapata waendelee kupata, halafu wapya waweze kuingizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, narudia kusema *TSC* iangaliwe upya, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mama Sitta. Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara atafuatiwa na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, na Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi ajiandae.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nianze moja kwa moja kwa kumpongeza Waziri Simbachawene pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri mnayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, simsifii Mheshimiwa Simbachawene kwa sababu tu nimemwona, ila niseme ni Waziri anayefikika, Waziri msikivu, halafu anatekeleza. Licha ya kwamba ni *Senior*, hata sisi *Form One* tunamkaribia, yaani tunaweza kueleza shida.

Kwa hiyo, aendelee hivyo. Leo nimepata nafasi ya kuona hata viongozi wengine anaowaongoza kwenye Wizara hapo nje, yaani ukiwaangalia tu wana furaha, inaonekana ni jinsi gani anafanya kazi vizuri na hao viongozi wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza moja kwa moja na yale ambayo wenzangu wameyazungumza kuhusu ajira zile za *TRA*. Kama alivyosema Mheshimiwa Janejelly, Mheshimiwa Husna, hizi ajira zimeleta maneno huko nje, zimeleta maneno kwa sababu kila mtu alishangaa. Hawa *NBAA* wanakuwa na nguvu gani ya kuwanyang'anya ninyi kazi yenu mnayotakiwa kuifanya? Ilikuwaje wao ndio wakafanya hiyo *interview* na siyo Sekretarieti ya Ajira? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna malalamiko mengi, wale waliotoka mbali wanafika pale kwenye chumba wanawaambia, jina lako halipo. Hebu fikiria mtoto ametoka Ukerewe. Kwa hiyo, hili jambo limekuwa baya kiasi kwamba nimeona nishauri ikafanywe *review* ya kilichotokea na ikiwezekana kuwaondoa kabisa hao. Taasisi nyingine zisifanye hizi *interview*, badala yake Sekretarieti ya Ajira ndiyo ifanye hiyo kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu nimeshangaa Mheshimiwa Simbachawene, jambo limekwenda, wamekaa kimya, yaani wamewanyanyasa au imekuwaje? Nimeshangaa sana. *(Makofi)*

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Omari.

**TAARIFA**

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumpa taarifa mchangiaji. Kwanza wafahamu nini maana ya *NBAA*. *NBAA* ni *National Board of Accountancy and Auditors.* Ni Bodi ambayo inasimamia Wahasibu na Wakaguzi, pamoja na mambo ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiutaratibu wenzetu wa *TRA*, kimsingi nadhani hawakufanya kosa kuwakabidhi *NBAA* kwa sababu inaweza ikafanyika katika taasisi nyingine zozote zile. Kwa hiyo, tusije tukaikosea Bodi ya *NBAA* kwa kuiona kwamba ni taasisi ambayo haiwezi kusimamia kazi hii, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninadhani Mheshimiwa Mbunge alimaanisha *competency* ya suala la kuajiri. *Competent entity* katika *context* hii ni Sekretarieti ya Ajira. *(Makofi)*

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ntara, unapokea taarifa?

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei. Halafu hata amenipotezea muda wangu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwani ile Sekretarieti, nchi inachagua Sekretarieti ya Ajira, ina maana wale mle ndani wote ni mambumbumbu? Mle ndani wanazo taaluma zote, ndiyo maana wanaweza wakafanya usaili. Watu wamechaguliwa Sekretarieti ya Ajira, wewe unafikiri wale ni vilaza? Wale wanaweza kuajiri au kufanya *interview* katika sekta zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekretarieti ya Ajira ni *combination* ya watu wenye utaalamu. Hilo tusilikwepe, Mheshimiwa Waziri Simbachawene, nendeni mkafanye *review*, chukueni madaraka yenu, simamieni utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kulizungumzia leo ni hili la kuhusu shughuli za vyuo vikuu. Mheshimiwa Waziri, unajua nilisema vyuo vikuu vinatakiwa vijitegemee. Kazi ni kubwa, viwe huru katika taaluma. Wizara ya Elimu inaweza kuingilia tu kwenye mambo ya sera, labda na kuviwezesha, lakini kwenye taaluma tuviache vyuo vikuu viwe huru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nasema hivyo? Tuliongea wakati ule, tumeongea mwaka jana, 2024 kwamba hakuna Wahadhiri, wamepungua sana, Maprofesa ndio usiseme. Vyuo vikuu vikiachwa huru vinaweza vikaajiri. Leo hii wanafanya *interview,* wale *Tutorial Assistants*, wakishafanikiwa, majina yanapelekwa Utumishi, eti ndiyo wapate ajira. Jamani, tunaua kabisa *value* ya chuo kikuu. Wale wanatakiwa wafanye *interview* wenyewe, waajiri kama tulivyoajiriwa sisi wengine tulivyobaki pale kwenye vyuo vikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wao wanaweza wakajua huyu Mhadhiri ana miaka 61, ana miaka 65, anaweza kuendelea kufundisha, wao ndiyo waamue. Usiwapangie eti Mhadhiri vyuo vikuu miaka 65 aondoke. Hivi mimi hapa mnafikiri siwezi kufundisha? Nina miaka 65. Leo Prof. Ishumi bado anafanya kazi, Prof. Rwekaza Mukandala bado anafanya kazi chuo kikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe wakati nasoma *Ph.D*, aliyenisimamia ni Profesa aliyekuwa na miaka 80. Hawa watu hapa kichwani huwa zinafanya kazi. Bado zinafanya kazi, kwa hiyo, tukifanya hivyo vyuo vikuu havitakuwa na shida ya Wahadhiri wala Maprofesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii wanashindwa kuchukua Maprofesa kutoka nje ya nchi. Nawaambia, ukienda kwenye vyuo vyetu vikuu, yaani vimekuwa ni *local Universities*. Sijui niziite *local school, I don't know,* kwa sababu, unakuta pale chuoni Mhadhiri Prof. Komba, Prof. Haule, na hawa Wapare wanaitwaje?

**MBUNGE FULANI:** Mbaga.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Prof. Mbaga, Prof. Mosha. Tunataka mchanganyiko. Wapewe uwezo wa kuleta Maprofesa kutoka nje ya nchi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaambia ukweli, tusilichukulie mzaha hili jambo. Yaani nakwambia, vyuo vikuu hadhi yake inashuka, *I am telling you*. Tuwaache, tuwaache wafanye

*interview* pale, waajiri *Assistant Lecturers,* waajiri *Professors* kutoka nje ya nchi. Ndiyo maana ya *University*, lakini ukichukua walimu wote wametoka Tanzania, hiyo *university,* hilo neno halipo tena. Tuwaache! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mnawawekea umri wa kustaafu, waacheni. Nimesema waacheni, wao wanajua huyu Prof. Shumi anapiga kazi. Leo Prof. Ndalichako ataweza kwenda kuendelea kufanya kazi chuo kikuu! Sasa, huyo amefikisha miaka 65, eti mnampa mikataba. Nasema *freedom* ndani ya *university* iendelee. Hilo nitalisema, hii ni mara yangu ya nne ninalizungumza hilo. Tuwaache! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua wale ni watu wa kujitegemea kabisa, wanayo mabaraza yao, yaani ile ni Serikali inayojitegemea ya chuo kikuu. Wanayo mabaraza yao. Pale, kuna Baraza, kuna *Senate*, kuna vikao, leo ninyi mnaenda kuwatawala tawala, unawaambia hapa hapana, unasema huyu ana miaka 70; jamani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Prof. Ndakidemi pale, amesema kwa mfano akitoka hapa anaenda kufundisha. Bado anafundisha chuo kikuu. Hili leo nimelisema kwa sauti, na Waziri Mkuu yuko hapo. Nililizungumza mbele yake na leo Wizara ya Utumishi, hebu naomba wafanyeni hawa kuwe na *autonomy* ndani ya *university*. Tukifanya hivyo, nakwambia *universities* zetu zitaonekana kabisa zina *value*. *Otherwise, we are killing this area of university*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa ubora wake, kuna hili suala la maadili. Suala la maadili nalisema kwa sababu gani? Ndiyo tulitunga sheria. Tunaangalia maadili kwa watumishi wa umma. Hapa nikifanya jambo ovyo ovyo tu, nenda unaitwa ofisi ya maadili, lakini kuna hizo *private sector*, hivi hamuwezi kubadiliasha hizi sheria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *private areas* ambapo watu maadili ni ya ovyo. Leo tumesikia jambo moja la mtu sijui anaitwa Mwijaku, sijui Mwanjaku huko, amekwenda amechezea

wanafunzi katika vyuo vikuu. Sasa hayo maadili yanakwenda wapi? Polisi watamchukua, na ninyi wa maadili je? Yaani nimeona hivi vitu tuviangalie. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Maadili Mzee Mwangesi apige kote, hebu angalieni kama mnaweza kubadilishabadilisha kanuni hapo. Kama wote ni Watanzania, wanaharibu mambo, maadili ya ovyo, lakini mtumishi wa umma anapelekwa kwenye maadili; huyu wa *private sector* anayefanya vitu vya ovyo katika hii jamii, lini atapelekwa kwenye maadili? Hili mlichukue na mkalifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba sana, kama kuna kiongozi wa *TASAF* hapo, nafikiri yupo. Wanafunzi wa vyuo vikuu wanaokuwa na shida sana ya fedha ili waweze kulipa ada, Mheshimiwa Waziri mlolongo unakuwa ni mrefu kiasi kwamba mpaka waje wapate sijui hiyo idhini ya hela, tayari wenzao kule wameshasoma. Naomba unikutanishe na huyo bosi wa *TASAF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ndio mwakilishi wa vyuo vikuu jamani, na ninataka nirudi hapa. Naomba mnikutanishe na kiongozi wa *TASAF* tuone namna gani tutasaidia wanafunzi wa vyuo vikuu. Kama wanahitaji msaada wa fedha za *TASAF,* wapate mara moja. Akisema Mwakilishi wa Vyuo Vikuu kwamba huyu ana shida, kwa nini msimwamini? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani mimi naweza kumchukua tu mtoto nikasema huyu ni maskini, wakati kweli sio maskini! Naomba kwa hilo tena mlifanyie kazi. *(Makofi)*

*(Hapa, kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Muda umeisha?

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, muda wako umeisha. *(Makofi)*

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara. Sasa namuita Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mheshimiwa Santiel Kirumba ajiandae.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adhimu kwa ajili ya kuchangia katika Wizara hii muhimu na katika bajeti yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo amekuwa akiifanya katika kuiongoza nchi hii. Tunampongeza kwenye maeneo matatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ni kuiongoza nchi kwa amani na utulivu na mshikamano mkubwa. Amefanya vizuri sana kwenye hili eneo. Eneo la pili, kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kila mahali, kila kona, kila Mkoa, kila Wilaya, mpaka kwenye vijiji ametekeleza miradi mingi sana. Tunampongeza sana kwa kazi nzuri ambayo ameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu, amekuwa kinara wa kutafuta vyanzo vya fedha ambazo zimesaidia sana katika kutekeleza hii miradi mingi hii ambayo imefanyika. Kwa hiyo, tunampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapompongeza Mheshimiwa Rais, maana yake tunawapongeza na wasaidizi wake wote. Hao ndio wamefanya kazi na mafanikio haya. Bila wao kufanya kazi vizuri, mafanikio haya yasingekuwepo. Kwa hiyo, tunazipongeza taasisi zote zilizoko chini ya Ofisi ya Rais kwa kazi nzuri ambayo zimekuwa zikifanywa. Hongereni sana kwa kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri Simbachawene, mnyenyekevu, mwadilifu, mtu mwenye hekima, anafanya kazi nzuri sana na anajituma vizuri sana. Kama hiyo haitoshi, yuko Naibu wake, Mheshimiwa Sangu, anafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani kwa hivi wanavyofanya kazi pamoja, basi wananchi wa kwenye maeneo yao watawarudisha tena awamu nyingine, waendelee kuongoza na waendelee kukalia hivi viti kuwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa za Utumishi wa Umma na Utawala Bora zimeshaelezwa, lakini mimi nataka niseme kazi kubwa ambayo wamefanya ni kuhakikisha kuwa, utumishi wa umma unafanya kazi, unatekeleza majukumu yao kwa weledi, kwa maarifa na kwa uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo kazi wameitekeleza vizuri sana kwa kweli. Wameitekeleza na kuhakikisha kwamba, wakati wa kutekeleza haya majukumu sheria, kanuni, taratibu na miongozo inazingatiwa ipasavyo. Kwa kweli, kwa hili tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo wamelifanya vizuri ni kusimamia utendaji kazi wa Watumishi wa Umma pamoja na masilahi yao. Tulikuwa na changamoto ya masilahi ya Watumishi wa Umma kwa kipindi kadhaa hapo, lakini sasa hivi kwa kiwango kikubwa wameshughulikia sana masilahi ya Watumishi wa Umma japo haijafikia kiwango tunachotamani kufika, lakini wamejitahidi sana kwa uwezo wa nchi yetu tulipofika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Watumishi wa Umma kwa kweli wamezingatia sana kupandisha mishahara, wamezingatia sana madaraja na maeneo mengine na bado tunahitaji zaidi kujiongeza, kufanya zaidi, ili Watumishi wa Umma wawe na afya njema, waweze kufanya kazi kwa weledi, vizuri zaidi. *(Makofi)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni kusimamia utoaji wa vibali vya ajira, na pia kusimamia ajira mbalimbali. Kwa hapa

naomba nijikite kidogo kwenye eneo hili. Kazi ya kutoa vibali ni nzuri sana, ili tujue *size* ya utumishi wa umma, hicho ni kitu kizuri sana, lakini kuhakikisha kwamba, tunapata watu wanaostahili kuajiriwa katika nafasi mbalimbali, hiyo ni kazi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kazi hii baada ya kupata uzoefu ndiyo maana tulianzisha Sekretarieti ya Ajira Serikalini. Hii sekretarieti imefanya kazi nzuri, lakini hapa mwishoni kumeanza kuwa na kutetereka na tunaona kabisa sasa baadhi ya maeneo hawatumii Sekretarieti ya Ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tunapotaka kwenda sasa tunataka turudi tulipokataa na tulipotoka. Kwa hiyo, ni vizuri Sekretarieti ya Ajira tukaiwezesha kwa rasilimali, kwa vitendea kazi na kwa uwezo, ili iendelee kutoa ajira kwa watu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni muhimu, sasa hivi changamoto iliyo kubwa ni baadhi ya vijana wanaitwa kwenye *interview,* wanatoka Mbozi, wanatoka Vwawa, wanatoka Songea, wanatoka Kagera, kuja kufanya *interview* hapa Dodoma. Hii hapana, hatukubaliani nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotakiwa ni kwamba, hii Sekretarieti ya Ajira iweke utaratibu hawa vijana waitwe kwenye *interview,* wafanye kwenye mikoa yao kule walipo. Wekeni utaratibu, na hilo linawezekana. Sasa hivi kwa dunia ilipofika kwa Sayansi na teknolojia hatuhitaji vijana wasafiri umbali mrefu kutoka huko waje huku kwa ajili ya kuja kufanya *interview* halafu asifanikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wafanye kwenye mikoa ile. Kila mahali uwekwe utaratibu mzuri, iwezesheni Sekretarieti wafanye kazi nzuri. Nina imani kabisa matatizo yatapungua na tutaondoa hizi changamoto ambazo tunazipata sasa hivi. Kwa hiyo, Sekretarieti ya Ajira ni muhimu sana tukaifanyia mabadiliko, tukaiongezea uwezo ili iweze kutekeleza hayo majukumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka miaka ya nyuma Wizara ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora tulitekeleza mabadiliko makubwa kwenye Utumishi wa Umma *(Public Service Reform Program)* na tulikuwa na mabadiliko mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na *Local Government Reform Program*, *Public Service Reform Program*, *Legal Reform Program* na maeneo mengine kulikuwa na mabadiliko mengi ambayo tuliyafanya, lakini mimi nataka nijikite kwenye eneo moja kwamba, baada ya zile *reforms* kutekelezwa, tumetekeleza tumefika. Je, tumewahi kufanya tathmini? Tukaangalia *success stories* za ile *reforms* na wapi tumekwama, ili tuweze kuboresha, tuweze kufanya vizuri zaidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili kwa kweli naona kama bado hatujalifanyia kazi. Tunahitaji kulifanyia utafiti, mafanikio ya *Public Service Reform Program*, tunahitaji kufanya utafiti tuangalie *Local Government Reforms Program* kama imekidhi yale mahitaji tuliyokuwanayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mambo tuliyokuwa tunayatarajia kwenye *reforms program* ilikuwa ni kuwa na mikataba ya kazi, siyo mikataba ya ajira, mikataba ya kazi *(OPRAS)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwepo na *OPRAS,* ambapo tuliamini mfanyakazi anapofanya kazi awe na malengo ya kazi na mwisho wa mwaka tumpime kwa malengo yake. Akiwa amefanya vizuri maana yake apandishwe cheo hata mara mbili hata mara tatu kwa sababu, anakuwa amefikia malengo, lakini hilo limekufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunazungumzia watu kupandishwa hata bila ya kujali kwamba amechangia vipi katika uzalishaji, amefanya vipi katika utendaji wake wa kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili nadhani kuna haja ya kuliangalia vizuri ili tuhakikishe watumishi wa umma wanapanda

kwa vigezo vya utendaji kazi. Kwa hiyo, *OPRAS* ambayo mnayo sasa hivi, hii ya mfumo, sijui kama mnaisimamia na kuhakikisha kwamba, mmei-*link* na *performance* pamoja na *pay,* ili kusudi waweze kupata masilahi vizuri. Sijui, lakini naamini kwamba, ile *OPRAS* ni kitu muhimu sana na itatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sanjari na hilo, kwenye *OPRAS* tuna mashirika ya umma mengi, tuna taasisi za umma nyingi. Tuna idara zinazojitegemea, na tuna wakala. Lengo la mabadiliko ya wakala ilikuwa ni kwamba, zile zilikuwa ni idara za Serikali, baadaye zikue zianze kujitegemea ziwe mamlaka zinazojitegemea, lakini hadi tumeanzisha mpaka leo sijui kama mmeshafanya tathmini kuangalia ni wakala zipi zimefanya vizuri sasa zihame kutoka kuwa wakala ziende kuwa mamlaka zinazojitegemea, ili zipunguze kutegemea mapato au mishahara kutoka Serikalini. Hizi wakala zinatakiwa zijitegemee, zizalishe, hiyo ndiyo itatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kumekuwa na wimbi kubwa la taasisi nyingi za umma kukimbilia kuingiza mishahara. Wanaenda kwenye Utumishi wa Umma, wote wanataka mishahara. Tutafika mahali tutashindwa kulipa mishahara kwa Watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashirika yenye uwezo wa kuzalisha kibiashara tuyaache yazalishe kibiashara, yalipe wafanyakazi wao na faida wachangie kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Hapo ndiyo tutapata mapato, lakini siyo watu wameshindwa ku-*perform* mnawarudisha kwenye Serikali Kuu wanaanza kupata mishahara, hapana. Wazalishe kwanza, wakishazalisha ziada walete kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, itatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mkiliangalia hilo suala la wakala, suala la mashirika ya umma, yale yanayoweza kujiendesha kibiashara yajiendeshe kibiashara. Tutapunguza hizi hasara na mwisho, msaini mikataba ya utendaji kati ya taasisi na taasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi ikishindwa kufikia yale malengo, hatua za kinidhamu zichukuliwe. Huo ndiyo utawala bora, na huo ndiyo uwajibikaji. Uwajibikaji ni muhimu. Hatuwezi kuendelea kwamba, eti watu wamefanya kazi, mambo hayajaenda, tuache, hapana. Lazima tuchukue hatua, hapo ndiyo tutaweza kufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo nataka kulipendekeza ni mafunzo kwa Watumishi wa Umma. Nchi yoyote duniani inategemea Utumishi wa Umma. Mtumishi wa Umma unatakiwa uwe na weledi, uwe na maarifa, uwe na uwezo wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtumishi wa Umma anachofundishwa chuoni ni tofauti na kinachokuwepo kule kazini, ndiyo maana lazima anapoingia kwenye *Public Service* anatakiwa afundishwe Maadili ya Utumishi wa Umma, afundishwe namna ya kufanya kazi za Utumishi wa Umma, afundishwe namna na mienendo, namna ya kupanda, kila kitu kinachotakiwa kufanyika ndani ya Utumishi wa Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zilizofanikiwa, ukiangalia nchi kama Singapore, Mtumishi wa Umma anaenda kwenye mafunzo masaa 102 kwa mwaka, nchi kama India anaenda mafunzo karibu masaa 200 kwa mwaka, nchi kama China wana utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingi zilizoendelea Watumishi wa Umma lazima waende ku-*recharge brain*, waende kusoma, waongeze ujuzi na maarifa ndipo kunakuwa na mabadiliko makubwa ya utendaji kazi katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hapa watu wengi wamebakizwa hawafanyi hiyo kazi. Chuo cha Utumishi wa Umma, Chuo cha Uongozi, kilitakiwa kipewe hiyo kazi; kilipewa hiyo kazi, lakini kimsingi bado hiyo kazi hawajaifanya inavyotakiwa. Tukifanya hivyo, Watumishi wa Umma watakuwa na weledi, watawajibika, watakuwa na maadili, wataweza kuchangia na

kufanya kazi inayostahili na hapo ndipo tutaweza kufikia malengo tunayotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja, bajeti hizi zipite, Mheshimiwa Rais akafanye kazi vizuri, taasisi zake ziendelee kuchapa kazi, Mawaziri mkachape kazi. Mungu awabariki, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hasunga. Sasa namwita Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, atafuatiwa na Mheshimiwa Santiel Kirumbi. Mheshimiwa Edward Olelekaita ajiandae.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia bajeti ya Wizara hii ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Hata mimi nampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake. Kusema ukweli, kipindi hiki ameweza kuweka mifumo mizuri ambayo watumishi wa umma wanaweza kufanya utendaji mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawapongeza sana, lakini vilevile nampongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa sana aliyoifanya katika kipindi hiki na hasa kupeleka fedha nyingi kwa wananchi kwenye majimbo yote, hususan kwenye kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata katika Wizara hii tunaona maono ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuweza kusaidia maono ya vijana, ambapo kuna changamoto kubwa sana ya ajira. Kwa hiyo, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameliona hili kwa vijana wake na ndiyo maana ameweza kujenga fursa nyingi za ajira kupitia Wizara hii. Nampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kipindi chake ameweza kutoa ajira rasmi zaidi ya 149,000, hongera sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, na vilevile amejenga fursa nyingi za ajira nje ya mfumo rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, alivyoweza kupeleka fedha nyingi za miradi ya ujenzi kule kwenye kata na kule kwenye majimbo, hii imejenga fursa kwa sababu, kuna vijana, kule kuna *local artisans* wameweza kufanya kazi ya ujenzi. Kwa hiyo, hii imekuwa ni fursa ya ajira. Pia kule kuna akina mama ntilie, nakuna wazabuni ambao wameweza kupeleka vifaa. Hii bado ni ajira, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maono yake pia, kuendelea kuwekeza katika viwanda, hii ni sehemu ambayo inaweza ika-*accommodate* hii nguvukazi kubwa sana, ambapo tunajua kwa Watanzania ukiangalia *demography* ya idadi ya watu, Tanzania zaidi ya nusu ni vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna kila sababu ya kuangalia hii changamoto kubwa ya ajira kwa vijana, lakini uwekezaji pia alioweza kuufanya kwenye kilimo, kilimo kimekuwa kinavutia kwa vijana. Kwa bahati nzuri sana, sasa vijana angalau wamepata ajira, wanazalisha mbogamboga na wananenepesha mifugo kupitia *BBT*. Hongera sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, vijana wa Tanzania wanakuangalia na vijana wa Tanzania wana changamoto kubwa sana ya ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu vilevile ni juu ya Sekretarieti ya Ajira, nawapongeza sana. Kuna mambo mengi sana tumeshauri kwa Sekretarieti ya Ajira na kwa bahati nzuri wamesikia japokuwa kuna changamoto ndogo ndogo bado zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kusogea kufanya usaili kwenye mikoa, mimi nawapongeza sana, mnawasaidia wale vijana ambao uwezo wao wa kuja kuwa-*centralize,* kuja kwenye usaili ni mdogo. Sasa tunapowafuata mikoani kule, kwa kweli, tunawasaidia sana, lakini changamoto ni kwamba, wanadahiliwa vijana wengi sana kuliko ambavyo ikama inahitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, wanaotakiwa labda ni vijana 50, labda idara fulani inahitaji vijana 50, halafu unawaita kwenye usaili watu zaidi ya 2,000 au 4,000, halafu ilivyo sasa hivi

unawaita kwenye mitihani *(interview),* wanaanza *written day one,* baadaye unafanya *selection* unawapeleka kwenye *oral*. Ile *written* wanafanya *the same day;* wanafanya leo mchana, baadaye unamwambia *selected,* ili aingie *oral* kesho yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi hawa 2,000 au 4,000, kweli kuna uhalali upi kwamba umeweza kupitia makaratasi yote haya, ili uone kwamba umemtendea haki? Umemsaili, amesogea sasa kwenda kwenye *oral?* Ni kwa nini pengine hata isifanyike *screening? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii tumeshashauri tu kwamba, kwenye *screening* tuangalie waliohitimu muda wa nyuma zaidi. Kwa mfano, kuna wahitimu wamemaliza vyuo tangu 2017, 2018, 2019, unamwita siku moja kwenye usaili pamoja na yule aliyemaliza mwaka wa 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yule ambaye ameshakaa miaka 10 uraiani, anayejua bodaboda yake, anayejua alikuwa kwenye kilimo chake, anayejua alikuwa kwenye mifugo yake, namna gani anaweza aka-*compete* pengine na huyo ambaye amemaliza mwaka jana, 2024!

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu *bad enough,* una m-*select* yule aliyemaliza mwaka 2024 na yule ambaye ana miaka kumi huku nyuma unamwacha. Ni vizuri sana tukafanya *screening* kuliko kuendelea kuwasumbua na wengine wamejitolea na taarifa zao zipo. Nafikiri tuendelee kutenda haki, lakini kwa kweli, imeleta mwanga na matumaini kwa vijana wa wakulima vijijini kwa jinsi usaili huu ulivyoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo ni gumu sana, baada ya kupelekwa kwenye *oral,* ni nani anatakiwa kupeleka majibu kwamba, sasa huyu ameajiriwa au hajaajiriwa kwa sababu, jambo gumu zaidi ambalo vijana wanaendelea kutusumbua, hizi barua za ajira zinaendelea kutolewa kama kijiko. Unakaa wiki moja, wameajiriwa sijui vijana wangapi, unaendelea wiki ya pili wameajiriwa wengine, mwezi huu wameajiriwa hawa, mwezi ujao wameajiriwa hawa. Wale wengine wanaendelea

kuwa na matumaini wakisubiri barua, pengine ajira hakuna na wanaendelea kutusumbua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, Mheshimiwa Waziri upo hapa, hiyo *intake* ambayo mmeshaifanyia usaili, wapate barua kwa kipindi kimoja na majina yatolewe kwenye mtandao wote, ili wale vijana kule sasa wapate amani, wajue kwamba, yupo kwenye ajira, au hayupo kwenye ajira. Vinginevyo, tunaendelea kuwaweka kwenye *tension* isiyo na sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliseme hili la *TRA* ambalo nami limenisikitisha vibaya sana. Kuna vishoka huko mitaani, kitu kinachosikitisha, wanajifanya wanawajua watu wa hii bodi ambayo imeteuliwa, ambayo kazi imekuwa *outsourced,* wanawaibia vijana huko. Ujue kwamba ajira ni changamoto, wanapita kwa vijana wanachukua shilingi laki tano, au milioni, milioni tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo ni baya sana. Angalau Sekretarieti ya Ajira sasa hivi tumeona kabisa matumaini makubwa kwamba wanatenda haki na wanaenda vizuri. Mimi nafikiri huu mfumo, Mheshimiwa Waziri atakuwa ameshauelewa, maana Serikali hii ni sikivu. Hii ajira ya *TRA* ni changamoto, vijana wanaibiwa, vijana wamekuwa *stressed*. Kwa vyovyote vile, tumeomba na tunaomba Waziri alishikilie hili, lirudi katika Sekretarieti ya Ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine ni kuhusu stahiki za watumishi. Watumishi hawa wachache wanatakiwa kuwahudumia Watanzania walio wengi na wawahudumie wakiwa na utulivu, wawahudumie wakiwa na morali ya kazi. Ukim-*frustrate* Mtumishi wa Umma ujue huduma inayotolewa kwa wananchi pia haitakuwa bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, suala la kupandisha cheo ni stahiki na ni haki. Muundo wa Utumishi unataka kila baada ya miaka mitatu Mtumishi wa Umma apande cheo daraja moja, lakini mtumishi hujamwonya, hujamfukuza kazi, hajaomba

likizo bila mshahara, anakaa zaidi ya miaka sita, mingapi, humpandishi cheo! Hivi hili ni kosa la nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa mfano mdogo tu ambao Mheshimiwa nitamwomba Mheshimiwa Waziri tuufuatilie. Kuna walimu wameajiriwa mwaka 2008/2009, 2014/2015, hao mpaka sasa hivi hawajapata *promotion* yoyote, yaani hawajapanda daraja hata moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri afuatilie, na kama lina ukweli, wapande sasa kwa mserereko. Wakipanda kwa mserereko, ningepaswa kujua, natamani sana kujua, Mheshimiwa Waziri, wala nisifikirie kushika shilingi. Bajeti yako ya sasa imezingatia kuweka bajeti kwa kila *arrears* ya hawa ambao wameachwa na sasa wapande kwa mserereko? Kwa hiyo, natamani sana kulijua, pamoja na watumishi wa idara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni madeni ya watumishi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rahhi, muda wako umeisha tafadhali. Hitimisha tafadhali.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yustina Rahhi. Tunakushukuru.

Nilikosea kutamka jina la Mheshimiwa Santiel Kirumba, naomba nirejee. Sasa namkaribisha Mheshimiwa Santiel Kirumba. Ajiandae Mheshimiwa Edward Olelekaita na mtoa hoja ajiandae.

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza ningependa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuteuliwa na Chama cha Mapinduzi kwa nafasi ya kwenda kugombea Urais. Pia, napenda kumpongeza

Katibu wangu wa chama, Dkt. Nchimbi, kwa kuaminika, kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais mtarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema ndani ya miaka minne, Mheshimiwa Rais, ameweza kufanya kazi kubwa katika ofisi hii ya Utumishi. Amefanya kazi kubwa kutokana na kwamba, amezingatia vigezo vyote vya maadili, kanuni na sheria na hivyo, imeweza kuwafanya watumishi wengi kupanda vyeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuja kuangalia kwa namna moja au nyingine kwa kipindi chote cha Mheshimiwa Rais alichokaa madarakani kwa miaka minne watumishi takribani 400,000, wameweza kupandishwa madaraja. Kwa kipindi kirefu walichokuwa wamekaa, walikuwa hawajapandishwa madaraja, lakini kwa Mheshimiwa Rais, hili limewezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais pia, katika kipindi chake ameweza kuongeza likizo ya uzazi kwa mwanamke, ambaye alijifungua watoto njiti. Kwa namna moja au nyingine, utaona Mheshimiwa Rais amemgusa kila mtu. Pia, napenda kuwapongeza Mawaziri ambao wameteuliwa katika ofisi hii, ni wasikivu na wanafikika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili Mheshimiwa Simbachawene tuliweza kupambana naye sana, tuliweza kumfikia kwa ukaribu na tukaweza kupitisha sheria hii ya uzazi mpaka wiki 40, na sasa hivi hata baba anapata siku saba kwa kumsaidia mke wake ambaye amejifungua mtoto njiti. Kwa hiyo, hiyo ni hatua kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, napenda kusema, Mheshimiwa Rais ameongeza umri wa wategemezi kutoka miaka 18 hadi 21, na hii imeongeza katika *NHIF* wategemezi hao ni 65,000 wameongezeka, na Serikali inatumia takribani shilingi bilioni tatu katika kuwahudumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utaona hata kama tuna changamoto nyingine za kiutumishi, lakini kwa namna moja au nyingine Serikali imekuwa ikipambana katika kutatua changamoto ndogo ndogo. Kwa hiyo, kwa miaka minne ya

Mheshimiwa Rais, amefanya kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba kila mtumishi na kila mwananchi kwa namna yoyote anamfikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliongelea tena suala lingine la walimu. Mheshimiwa Rais mwaka 2024 alielekeza kwamba watumishi wa kada ya ualimu wapandishwe mshahara. Ni kweli Mheshimiwa Rais amejitahidi kuwapandisha madaraja, lakini ninyi mnaelewa, tumewekeza kwa namna moja au nyingine kwa kiasi kikubwa sana katika sekta ya elimu. Tumejitahidi kujenga madarasa, na tumejitahidi kuwashushia vitendea kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, walimu hawa wanahitaji angalau Mheshimiwa Waziri aweze kuwafikiria kwa namna nyingine. Kwa mwaka huu, kuna neno wanasema, "umejipangaje?" Lile suala la walimu kupandishiwa mshahara limefikia hatua gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wao wenyewe wanaelewa tukienda kufanya mikutano ya kata, mikutano mitatu unakuwa umeshachoka. Fikiri mwalimu huyu anafanya kazi ya kufundisha watoto, na sehemu nyingine, kama mimi ninavyotoka sehemu za kijijini, unakuta shule moja, ni kweli Serikali imeajiri, lakini hata kwetu pia tuna changamoto ya ajira ya kada ya ualimu. Unakuta kule kuna shule nyingine ina upungufu wa walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu afundishe Darasa la Tatu, afundishe la kwanza, afundishe la nne; na mwalimu huyu huyu inamlazimu kuhakikisha kuwa watoto wote wanafaulu. Watoto wale wasipofaulu, Serikali inatupia lawama shule ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda kuwaambia, kwamba hili suala la kumwongezea tena motisha mwalimu ili aweze kufundisha kwa starehe inapaswa aangaliwe kwa jicho lingine la kumpandishia mshahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la ajira, kila mtu amekuwa akililalamikia, lakini pia mwaka 2024 kuna Mheshimiwa Mbunge aliweza kuchangia. Hili suala la ajira hebu tulishushe katika kila Halmashauri. Kila Halmashauri iwe na *database* ili iweze

kusaidia kutatua changamoto ya ajira. Tunaweza tukawa tunalalamikia kwamba kuna changamoto ya ajira kwamba bado ajira hazitoshelezi, lakini kila Mkoa una mradi wa kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukupa mfano, katika Mkoa wetu wa Shinyanga tuna miradi ya mkakati wa *SGR,* tuna mradi wa kimkakati wa bomba la mafuta, tuna mradi wa umeme mkubwa wa *solar.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hapa Bunge nilipouliza swali kwenye Mradi wa *SGR* na bomba la mafuta bado takwimu zilionesha kwamba ni ndogo, lakini ukija huku ukisoma kwenye taarifa zao wanakwambia kuwa tumeajiri watu labda 400,000, tumeajiri labda watu 2,000 au 5,000. Sasa, ukija *in real sense,* ukienda kwenye ile miradi, wale watu wasomi wa eneo lile, hawanufaiki na miradi ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kuna wakati unakwenda kukagua miradi, ukiwauliza je, wananchi wameshirikishwaje kwenye huu mradi ili waweze kuulinda na kuutumikia? Unakuta wananchi wa eneo lile hawana taarifa ya huo mradi husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, unakuta wale watu ambao tunawapa miradi hii ya kimkakati, ajira zile wanazozitangaza wanazitangaza kwenye mtandao. Kwa hiyo, mtu lazima ajiriwe kwa kupitia mtandao. Ile inakuwa changamoto kwa wale watu ambao wanatoka katika zile halmashauri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba, kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI alielekeza kwamba sasa hivi halmashauri zitakuwa zikiajiri. Ni wakati sahihi Utumishi pia kushirikiana na halmashauri hizi ili kuhakikisha kwamba ni kweli zile ajira zinazosemwa na ile miradi ya kimkakati, kweli zimewafikia wananchi ili tuache kuisubiri Serikali Kuu kuajiri, tupambane na hii miradi na kutatua changamoto ya ajira huku chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Santiel, nakushukuru. Mheshimiwa Edward Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Niseme kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria. Nashukuru kwa nafasi ya kuwa mchangaji wa mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyosema wengine, tumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa aliyofanya kwa miaka hii katika sekta zote nchini. Ametujengea Waheshimiwa Wabunge heshima kubwa sana kwenye Majimbo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hakuna Jimbo unaweza ukazungumza habari ya miradi ya maendeleo kwa miaka minne ya Mheshimiwa Dkt. Samia, ametubeba sana. Kwa hiyo, kwa kweli kwa kuwa mtumishi namba moja wa nchi hii ameonesha *standards* nzuri, tunachotakiwa sisi wengine ni kuiga ili Watanzania wapate huduma hii ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia anataka Watanzania wapate. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Simbachawene amepata sifa nyingi sana hapa. Mimi kama Mjumbe wa Kamati nina-*confirm.* Kama kuna Mheshimiwa Waziri ambaye tunashirikiana naye vizuri sana kwa *level* ya Kamati na kutoa ushirikiano wa mfano ni Mheshimiwa Simbachawene. *He is very humble,* hana dharau. Ukimwomba saa yoyote kukutana, mnakutana, na anakusikiliza vizuri sana. Kwa hiyo, kwa kweli mzee siyo bure umedumu kwenye Bunge hili. Nakuombea maisha marefu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Naibu Waziri wake ni chuma. Ame-*catch up* haraka sana. Tangu ateuliwe kwa kweli Kamati imefurahia kazi zake, na tumezunguka naye kwenye miradi mingi

ya maendeleo. Anafanya kazi nzuri sana na yupo kwenye mikono salama ya ulezi na atafika mbali *brother. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Katibu Mkuu na viongozi wote wa Wizara hii kwa ushirikiano waliotoa kila wakati kwa Kamati, na ushauri ambao tumetoa kama Kamati wamekuwa wanachukua kila wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utumishi duniani; watumishi ndio *engine* ya kuendesha Serikali. Kwa hiyo, watumishi ni watu muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa. Pale nchi yetu inapoongeza fursa na uchumi wetu unavyoongezeka, tukiendelea kujali maslahi yao na kuboresha mishahara yao na maslahi, tutatengeneza *public services* nzuri sana ambayo itatoa huduma nzuri sana kwa Watanzania na utawala bora utakuwa bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nao kwa sababu hali ya nchi yetu wanaifahamu, na wanajua, ikiongezeka tuwajali, kuanzia Wenyeviti wa Vijiji, Watendaji, watu wamezungumza, na watumishi wote, na Walimu wamezungumza hapa ma-*guru* kabisa, na kazi za walimu kwa kweli ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *in fact,* siku hizi hata walimu ukiacha kazi zile alizosema Mheshimiwa hapa, wanafanya kazi za ulezi. Siku hizi kazi yetu sisi ni kupeleka tu watoto shule. Tulikuwa tunalipa ada na Mheshimiwa Dkt. Samia ameondoa ada; sasa hata kazi ya wazazi siku hizi ni kuzaa tu halafu na kupeleka watoto wakafundishwe elimu; kusoma, na kuandika lakini pia na malezi siku hizi wanapata kwa walimu wetu. Kwa hiyo, walimu ni watu muhimu sana kwa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Taifa limeendelea bila kuwa na walimu. Wote waliokaa hapa wamepitia mikono ya walimu na wametajwa watu wengi hapa; Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Spika Mwalimu wangu, na akina Mheshimiwa Dkt. Balozi Kakurwa, wapo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa likitaka kujenga misingi imara, ni lazima tuwajali wale watumishi ambao ndio wanaotuwekea misingi kwenye Taifa. Kwa hiyo, kwa kweli kama walivyosema Kamati, Watumishi wa Umma ni *engine* kwa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, tunachotegemea na sisi ni kwamba watoe huduma nzuri kwa Watanzania. Watanzania wanataka huduma nzuri sana. Uwe daktari au mwalimu uwe na lugha nzuri tu. Mkianzia kwa viongozi wenu wao ni *humble,* Makatibu Wakuu, Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa Mheshimiwa Dkt. Samia. Sasa kama hawa wakubwa ni *humble* kiasi hicho, wewe ambaye ni mtumishi uliyepata ajira, utaachaje kuwa *humble* na ukatoa huduma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivyo, na kwa sababu unajua ajira imekuwa jambo kubwa sana, na ni kwa sababu moja tu, nchi yetu tangu tumepata uhuru ongezeko la vijana wanaosoma limekuwa ni kubwa sana, kila mahali, hata kuliko *capacity* ya Serikali kuajiri. Kwa hiyo, kwenye suala hili la ajira, na kama walililivyoshauri Kamati, tufanye huu mjadala wa Kitaifa kila wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili siyo suala la utumishi pekee, nadhani tuwe na makongamano ya Kitaifa, tuwe tunazungumza habari ya ajira na namna bora ya kuweka sawasawa ili liwe jukumu letu wote. Tupate mawazo kutoka kwa Watanzania kuhusu namna ya kufanya ili suala la ajira lipate mawazo mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana, kama walivyosema Kamati na Waheshimiwa Wabunge hapa, kwamba tukiwa na taasisi bora ambayo ndiyo inaratibu suala la ajira likaongeza uwazi, likaongeza *professionalism* na mambo mengi, itaondoa manung'uniko. Isipokuwa na uwazi mzuri sana, itaanza kujenga matabaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namna ya pekee ya kuondoa hilo ni kuwa na taasisi moja, kama walivyopendekeza

Kamati na Waheshimiwa Wabunge hapa, ambayo ndiyo inajengewa misingi ya kutengeneza suala la ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ajira, ni utaifa. Tunataka tuone Taifa, tukiona ajira; tunataka kuona *inclusivity,* na tunataka kuona watu wanaojitolea. Kujitolea ni suala la kizalendo. Tunataka ajira hizi zi-*reflect* umoja wa Taifa letu. Tusipokuwa na chombo maalumu ambacho kina-*vet* hii *process* tutatengeneza matabaka ambayo hayana maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama walivyosema Kamati, taasisi yetu inayohusika na mambo ya ajira ikipewa jukumu hili nao wakaongeza *creativity* kwenye ajira zetu, nadhani Watanzania watafurahi na kila mtu ataridhika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila Mheshimiwa Mbunge hapa leo umemsikia, kila mtu angetaka leo katika ajira zinazotoka aone angalau vijana wawili au watatu wanatoka kwenye Jimbo lake, Kwa misingi hiyo hiyo ya kuendeleza utaifa na *inclusivity*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu TAKUKURU, wamekuwa *creative* sana. Ule mradi wao wa kusema TAKUKURU Rafiki, ukiendelezwa zaidi; unajua tunachotaka ni kwamba badala ya kuanza kukamatana na kusubiri mtu afanye kosa akamatwe, tujenge vijiji, na tuwe na wenyeviti wenye weledi wa kufanya kazi zao vizuri sana. Kwamba leo tuwe na *role modal* ya kijiji ambayo unaweza mkatupeleka tukasema huyu mwenyekiti amefanya kazi zake vizuri sana na wenyeviti wote wanatakiwa wafuate hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii TAKUKURU Rafiki sasa, ulikuwa ni ubunifu mzuri sana, na ninampongeza Mkurugenzi wa TAKUKURU na Taasisi yote ya TAKUKURU kwa kuja na mpango huu wa TAKUKURU Rafiki. Tunataka taasisi zetu ziwe bora zaidi, tunataka utawala bora uwe bora zaidi. Kwa hiyo, wakati mwingine tu-*invest* kwenye kuwafundisha zaidi na kujenga uwezo wao kama walivyosema wengine hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamesema watu kuhusu vyuo vikuu. Vyuo vikuu vinahitaji *independence* kabisa, nami ninakubaliana. Alishasema Mheshimiwa Prof. Kitila hapa; mimi si mnywaji wa *wine;* alisema hivi, *wine* inavyozidi kukaa zaidi ndivyo inavyozidi kuwa bora zaidi. Nami nakubaliana naye. Profesa anavyozidi kuwa *aged* ndivyo anavyokuwa bora zaidi. Kwa hiyo, kuna wakati mwingine badala ya kusema tu tuwaachie tutengeneze mpango ambao kuna maprofesa, tutakubaliana huyu aendelee hata akiwa na miaka *100, why not. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingine duniani kuna Profesa anakuja na *wheel chair* kwenye *lecture theatre* huku akiwa na *over 100 years, but it doesn't matter.* Hata hivyo, haiwezekani kwamba ni kwa *every professor, no.* Lazima tutakuja na mpango maalum wa kuwa-*recognize* wale *gurus* kwenye maeneo fulani fulani. Awe ni mwalimu bingwa, awe ni Profesa ama awe ni Jaji Mahakamani. Kwenye sekta zetu hizi tukiweza kulinda hiyo, tutakuwa tumeweka msingi wa Taifa na Taifa letu likawa bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapotengeneza ajira za nje huko, lazima kuwe na *freedom* ya *universities* ili tuweze kuleta maprofesa kutoka nje, ili tuweze kuandaa vijana waweze kuajirika huko duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Edward Olelekaita. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuungana na viongozi wenzangu wote kumshukuru sana, Mwenyezi Mungu kwa kutujalia baraka zake katika nyanja mbalimbali za ustawi wa Taifa letu kwa kuwa ametuepusha na majanga mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Mbulu Mjini nachukuwa nafasi hii kuungana nao kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi anavyoliongoza Taifa letu na kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 - 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli yapo mambo mengi sana yametekelezwa katika jimbo langu la Mbulu Mjini na nchi yetu kwa ujumla. Hakika haijapata kutokea hali iliyotuwezesha chama chetu kuwa na haiba kubwa sana kwa Watanzania na majirani zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa George Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa jinsi wanavyotumikia nafasi zao nyakati zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati yetu na Wajumbe wote Kamati ya Kudumu ya Bunge kwa taarifa yao nzuri iliyowasilishwa mbele ya Bunge letu. Hongereni sana kwa kazi kubwa mnayoifanya, Mwenyezi Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Wizara hii kwa kupokea maombi yangu ya fedha za kujengwa Ofisi ya TAKUKURU Wilaya ya Mbulu, na kazi ya ujenzi imeanza, hongera sana kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali nzima ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa mchango wangu kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri na Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Serikali iangalie utaratibu mzuri wa kutoa fedha za *TASAF* kwa ajili ya miradi ya jamii, kwani bado kumekuwa na viporo vya miradi ambayo bado havijaanza kutoa huduma kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Serikali iangalie upya utaratibu wa usaili kwa vijana wahitimu wa vyuo hususan sekta ya afya na elimu, kwa kuwa zoezi la usaili limepokelewa kwa hisia tofauti na kusababisha manung'uniko makubwa sana kwa kundi hilo. Hivyo basi, ushauri wangu ni kwamba uchujaji wa vijana wa ajira ufanywe na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kwa kutumia vigezo vyao vya ufaulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Wizara itazame upya mfumo wa kuratibu, kubaini kuwalipa watumishi wa mamlaka ya Serikali za Mitaa na Serikali Kuu ambao wana madai ya muda mrefu Serikalini kwa kuwa sisi kama wawakilishi wao, tumepokea maombi mengi ya madai yao pindi tunapopata vikao vya pamoja. Hata hivyo, kuna utata wa madeni hayo, nani amezalisha na nani anapaswa kumlipa mtumishi huyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kwa namna ya pekee, naomba Serikali ijitahidi sana kutoa fedha za bajeti ya Wizara hii muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa let,u kwa kuwa tunahitaji kufanikisha mipango yote ya Wizara ikiwemo fedha za bajeti ya uendeshaji na miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Naomba kuwasilisha.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nampongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge; na Naibu wake Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge pamoja na watendaji wa Serikali katika Wizara hii wakiwemo Juma Selemani Mkomi, Katibu Mkuu; na Xavier Mrope Daudi, Naibu Katibu Mkuu kwa kazi nzuri wanayofanya kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita kwenye changamoto ya ajira kwa vijana wanaohitimu vyuo mbalimbali na mapendekezo ya kutatua changamoto hii. Jambo hili limepewa kipaumbele katika taarifa ya Kamati ya Kudumu ya

Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria. Nami nimeona niweke msisitizo kwenye hili jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchini Tanzania, idadi ya wahitimu wa vyuo vikuu imeongezeka kwa kasi katika miaka ya hivi karibuni. Hali hii imetokana na jitihada za Serikali na sekta binafsi kuboresha upatikanaji wa elimu ya juu. Pamoja na mafanikio haya, changamoto kubwa imeibuka. Wahitimu wengi wanakosa ajira baada ya kuhitimu mafunzo ya vyuoni katika fani mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira kwa vijana ni suala nyeti na muhimu kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya Tanzania. Kwa mujibu wa Sensa ya Mwaka 2022, zaidi ya nusu ya idadi ya watu nchini Tanzania ni vijana wenye umri wa chini ya miaka 35. Takwimu hizi zinaonesha kuwa nguvu kazi kubwa ya Taifa ni vijana ambao wanategemewa kwa ajili ya maendeleo ya sasa na ya baadaye. Sehemu kubwa ya vijana hawa wana changamoto ya ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya ukosefu wa ajira kwa vijana imekuwa ikiongezeka kwa kasi, hali inayotishia ustawi wa Taifa na maendeleo endelevu. Ukosefu huu wa ajira kwa wahitimu wa vyuo vikuu ni tatizo kubwa. Wasomi wengi hukosa ajira zinazolingana na taaluma zao. Ikiwa hali hii haitapatiwa ufumbuzi, inaweza kuathiri maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya Tanzania kwa miaka ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hii, bila fursa za ajira, ni kwamba nchi yetu inapoteza rasilimali muhimu za watu wenye elimu na ujuzi. Hali hii inasababisha Taifa letu kushindwa kufaidika na uwekezaji mkubwa uliofanywa katika elimu ya juu, hivyo basi wasomi wanakosa fursa ya kuchangia kikamilifu katika uchumi wao binafsi na wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana wetu wasomi wetu unaweza kusababisha migogoro ya kijamii na kisiasa. Kwa mfano, wahitimu wasio na ajira wanaweza kujiingiza katika vitendo vya uhalifu au maandamano, na hali hii inaweza kuhatarisha amani na utulivu

wa nchi ambapo athari hizi zinaweza kuwa na madhara makubwa kwa umoja wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni tumeshuhudia kuwepo wa jumuiya isiyo na usajili iliyojiita Umoja wa Walimu Wasio na Ajira *(NETO)*. Vuguvugu la watu hawa lilisababisha viongozi wao kukamatwa na Jeshi la Polisi kwani walijitokeza na kuilalamikia Serikali juu ya haki yao ya kupata ajira ambayo wameisubiri kwa muda mrefu tangu walipomaliza masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yakijitokeza makundi mengine yenye nguvu ya kudai haki za ajira katika fani nyingine, hii itasababisha migogoro na Serikali, jambo ambalo linaweza kudhoofisha imani ya wananchi kwa Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili la ukosefu wa ajira kwa vijana wetu ni kubwa na inatakiwa Serikali ikae na wadau mbalimbali na kuja na mkakati wa kukabiliana na suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali ni kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ianzishe programu ya kitaifa ya kuwezesha uwepo wa ajira za muda na kujitolea. Serikali na mashirika yasiyo ya Kiserikali yanapaswa kuunda na kuanzisha programu maalumu zitakazowezesha vijana kujitolea na kufanya kazi za muda. Hii itawasaidia wahitimu kupata uzoefu unaohitajika kwa miaka ijayo. Ajira za muda na programu za kujitolea zinaweza kuwasaidia wahitimu kupata uzoefu na kuongeza uwezekano wa kuajiriwa baadaye, baada ya kupata uzoefu.

(ii) Serikali inapaswa kuboresha sheria na sera zinazohusu ajira na biashara. Ni vyema kuweka sera zinazoendana na mazingira ya sasa ya soko la ajira, pamoja na kuhakikisha kwamba sheria zinazoendana na ajira, zinatetea maslahi ya vijana. Pia ni muhimu kuweka sera rafiki za kusaidia ukuaji wa sekta zinazoweza kuzalisha ajira nyingi kama vile ufugaji, uvuvi, kilimo, utalii, na viwanda vidogo vidogo.

(iii) Serikali inapaswa kuboresha mfumo wa elimu ili kuhakikisha kwamba unawaandaa vijana vyema kwa soko la ajira. Hii inajumuisha kuimarisha mafunzo ya ufundi stadi na elimu ya vitendo, pamoja na kuhakikisha kwamba mitaala inazingatia ujuzi unaohitajika katika soko la ajira la sasa na la baadaye ndani na nje ya nchi.

(iv) Serikali kupitia mabalozi wa Kitanzania waliopo nchi tofauti duniani, wawatafutie ajira vijana wetu katika nchi zenye uhitaji ili Watanzania wapate ajira katika nchi hizo. Hili linawezekana kwa sababu hata nchi yetu huajiri watumishi kutoka mataifa mengine kwenye maeneo yenye pengo la wataalamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ikilipa jambo hili kipaumbale, basi Watanzania walio wengi watapata ajira na kupunguza mzigo kwa Taifa. Kwa mfano, juhudi zikifanyika, Watanzania wengi wanaweza kupata ajira za kwenda kufundisha Kiswahili kwenye mataifa yenye uhitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali, kwani kwenye kutekeleza hili, wameanza kuhuisha kanzidata ya Watanzania wenye sifa na nia ya kuajiriwa katika mashirika ya kikanda na Kimataifa katika nyanja mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, tatizo la ajira kwa vijana nchini Tanzania linahitaji suluhisho la haraka na la kimkakati. Tunahitaji kuwa na Taifa ambalo vijana wake wana ajira zenye tija na fursa za maendeleo, na hivyo kusaidia kujenga uchumi endelevu na jamii yenye ustawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo na ushauri wangu, naunga mkono hoja.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee naomba kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kutimiza vyema miaka minne kwa kuongoza nchi yetu akiwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuimarisha miundombinu hususan barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, huduma za kiuchumi na kijamii kama vile ujenzi wa madarasa, hospitali, zahanati na vituo vya afya, huduma za maji, utawala bora, pamoja na kuhamasisha uwekezaji na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri iliyotukuka ya kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa uzoefu na weledi wake, kama ilivyo kwa Watanzania walio wengi, nina imani kubwa kwa Mheshimiwa Nchimbi na kumtakia afya njema na kila la heri kwenye mchakato ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kutekeleza majukumu ya kumsaidia Waziri Mkuu, ikiwa na pamoja na jukumu la kuendelea kuisimamia ipasavyo sekta ya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Spika na Naibu Spika na pia uongozi wote wa Bunge kwa uongozi mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Taifa letu katika ya ushindani wa Kimataifa *(National competitiveness)*.

Mheshimiwa Mwenyeiti, bajeti hii ambayo ni ya mwisho, inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa

Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026. Katika kipindi chake akiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, tathmini zinathibitisha mafanikio makubwa ya utekelezaji na usimamizi wa Mpango wa Kwanza na wa Pili na kusababisha Taifa letu la Tanzania linafanya vizuri mno kuinua uchumi katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mapitio ya kipindi cha bajeti 2024/2025, Serikali kupitia Wizara ya Utumishi na Utawala Bora imesimamia kwa uadilifu na ufanisi mkubwa masuala yote ya utumishi na hasa kurudisha uwabikaji kazini na kuleta ufanisi mkubwa hasa kwenye utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mbeya Vijijini limenufaika kupitia miradi ya *TASAF* ambapo imebadilisha maisha ya wananchi katika vijiji husika. Pia kwa kusimamia vizuri rushwa na upendeleo umepungua kwa kiasi kikubwa na kuleta ufanisi mkubwa sehemu za kazi na hata miradi kukamilika kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo makubwa, napendekeza kuendeleza mafunzo ili kuboresha weledi wa watumishi ikiwemo upanuzi wa Chuo cha Watumishi Mbeya na eneo muafaka kwa ujenzi wa chuo kipya na cha kisasa ni Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ambapo kuna maeneo mazuri ikiwemo yaliyokuwa mashamba ya *Tanganyika Packers* Mbalizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mahitaji makubwa ya elimu ya mafunzo ya uongozi kwa viongozi wa ngazi mbalimbali. Napendekeza Serikali irudishe utaratibu wa mafunzo maalumu ya viongozi kwa kushirikiana na vyuo vikuu ikiwemo Mzumbe, *UDSM, IFM* na hata nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo yanayohitajika ni kama vile *Executive Development Pragrammes* kwa viongozi kulingana na ngazi zao. Mafunzo nje ya nchi ni muhimu kwa kuleta ujuzi kutoka nje hasa nchi zilizoendelea na hata zile zinazoendelea na zinazofanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na upungufu mkubwa wa watumishi katika sekta mbalimbali, napendekeza Serikali iendelee kutoa ajira zaidi hasa kwenye maeneo ya kuchochea uchumi na pia sekta ya afya, elimu na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na idadi kubwa ya wahitimu kukosa ajira na wametapakaa kila kona ya Tanzania hasa vijijini, napendekeza Serikali kuhakikisha ajira zinatolewa kwa usawa wa maeneo yote ya Tanzania kulingana na sifa. Serikali iangalie kuboresha sera za kikodi ili zichochee kuongeza ajira pamoja na kukuza uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na majukumu na unyeti wa mashirika ya kadhaa ya umma ikiwemo ushindani wa kupata watalaamu wazuri, mashirika haya yaruhusiwe moja kwa moja kutoa ajira ili yaendane na mahitaji yao na Tume ya Ajira wawe na jukumu la ushauri na udhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi kama *CAG* kisheria anatakiwa awe huru ikiwemo uhuru wa kuajiri; na hata taasisi kama mabenki, *TANESCO*, Bandari, *TRA* ni muhimu wakapewa uhuru wa kuajiri kulingana sifa ili kupata watalaamu wazuri kiushindani na pia kulingana na bajeti za mashirika husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maboresho ya mfumo wa *TASAF*, napendekeza pia kuboresha zaidi mfumo huo ikiwemo msukumo wa miradi, ilenge maeneo yatakayochochea uzalishaji wa mali ili zisaidie jamii kwa upana mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maeneo ya uzalishaji, msukumo ujumuishe kuimarisha masoko ya bidhaa zitakazozalishwa katika maeneo ya mradi. Miradi ilenge kuboresha elimu na hata kusomesha watoto wanaotoka kwenye kaya maskini ya maeneo husika. Serikali iboreshe taratibu za kupata maeneo ya miradi ya *TASAF* ili kupunguza malalamiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa namkaribisha Mheshimiwa Sangu, Naibu Waziri, Utumishi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Awali ya yoyote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema ambaye amenijalia leo kusimama ndani ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza ikiwa ni bajeti yangu ya kwanza nikiwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, nichukue nafasi hii kwa moyo wangu wa dhati kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwanza kwa kuniamini na kuniteua katika nafasi hii, na pili, kuendelea kuniamini, nami nimeendelea kuwepo katika Ofisi yake hii nikimsaidia pia Waziri wangu Mheshimiwa Simbachawene. Hakika namshukuru sana Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nawashukuru na kuwapongeza viongozi waandamizi wasaidizi wa Mheshimiwa Rais, akiwemo Makamu wa wetu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango; Waziri Mkuu wetu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa; Naibu Waziri Mkuu wetu Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko na viongozi wote waandamizi wanaomsaidia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, nashukuru sana na kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene kwa kazi nzuri anayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejiona ni mtu mwenye bahati kufanya kazi na Mheshimiwa Simbachawene. Katika mambo matatu ambayo ninajivunia, kwamba nimeingia kwenye darasa jipya, kwanza, ni uchapakazi. Ni kiongozi mchapakazi; pili, ni kiongozi mwenye hekima na busara ya hali ya juu. Ukiwa na

Mheshimiwa Simbachawene utachota hekima na busara, hasa sisi vijana ambao tunachipukia katika uwanja wa siasa, kwetu amekuwa mwalimu mzuri katika suala la hekima na busara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa alilonalo Mheshimiwa Simbachawene ni upendo, siyo mchoyo wa maarifa. Uzoefu wake na utajiri wa maarifa alioupata katika nyanja mbalimbali alizotumikia Serikali, anakushirikisha mpaka wewe mwenyewe unaona kwamba hili ni darasa tosha. Kwa kweli namshukuru sana Mheshimiwa Simbachawene. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuwapongeza viongozi waandamizi katika Ofisi ya Rais, nikianza na Katibu Mkuu Kiongozi, Mheshimiwa Balozi Dkt. Moses Kusiluka, bila kusahau Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Ikulu ndugu yangu Mahendeka ambao wote hawa wakishirikiana; na pia na Katibu Mkuu Utumishi ndugu yangu Juma Selemani Mkomi, wote wamekuwa wakitoa ushirikiano mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kumsahau Naibu Katibu Mkuu wetu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ndugu Xavier Mrope Daudi, wote hawa wakishirikiana pia na viongozi wote walio chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, wamekuwa ni nguzo imara ya kutoa ushauri wote wakiwa na nia ya kuunganisha nguvu ya kumshauri Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huo wote ni kazi ya kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kutimiza majukumu yake. nawapongeza wote na Wakuu wa Taasisi zote zilizo chini ya Ofisi ya Rais Ikulu, Utumishi na Utawala Bora kwa kazi kubwa wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia Spika wetu wa Bunge, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, anafanya kazi kubwa ambayo pia inafanya tunaendelea kujifunza mambo mengi, hasa katika Bunge hili la Kumi na Mbili. Tumeona kazi kubwa anayoifanya; na hata katika Bunge la Dunia huko *IPU,* anafanya kazi ya kutuheshimisha Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wasaidizi wake, akiwemo wewe ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Utawala, Katiba na Sheria pamoja na Makamu Mwenyekiti wetu ambaye anafanya kazi kubwa, ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Kyombo na Wajumbe wote wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tumefurahi sana kufanya kazi na ninyi. Kama Wizara ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, tunafurahi sana kwa kuwa ushauri wetu, maelekezo yenu yametujenga zaidi katika kutekeleza majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja ya Wizara hii. Tangu ilivyoanza hoja ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ikaja hoja ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI na baadaye ikaja hoja yetu sisi Utumishi, Waheshimiwa Wabunge wote michango yao imetujenga sana. Wametupa michango ambayo yote nia yake ni kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuwaahidi, kama mlivyotupa sifa ya kuwa wasikivu, usikivu huo huo tulionao tutauendeleza ili yale mliyotushauri tuhakikishe yanatokea na sisi sote tuone kwamba yale mlitichangia katika Wizara yetu yanajenga na yanaleta tija kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na jambo moja ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi, suala la *TASAF.* Nitaanza kwa kutoa historia ndogo kidogo. Dunia ilikutana mwaka Septemba, 2015 katika mkutano mmoja maarufu unasema, *UN Sustainable Development Goal Summit* ambao lengo lake Septemba, 15 ilikuja kutafakari dunia namna gani itakavyopambana na changamoto zinazoikabili dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa ambalo lilikuwa linaisukuma dunia, lilikuwa ni uharibifu wa mazingira, umasikini uliokithiri na mambo yanayoendana na haya. Ndipo pale wakaja na malengo ya maendeleo endelevu, tunayoyaita *SDGs* 17 ambazo ni *Sustainable Development Goals* 17. Sasa hizi zilikuwa

*casted* kila nchi na bara likaenda kutekeleza kwa namna ambavyo lingeweza kupambana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu nichukue fursa hii kuendelea kumshukuru Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, pamoja na kutafuta mbinu nyingi ya kufikia hiyo ajenda tunasema 2030 kwenye *TASAF* amechukuea *initiative* kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TASAF* katika programu ya tatu alikuwa na mpango wa kunusuru kaya masikini. Waheshimiwa Wabunge wameiongelea kwa namna nyingi. Mimi naomba nieleze namna ambavyo Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki cha awamu ya pili ya *TASAF* Mheshimiwa Rais aliweza kutoa fedha shilingi trilioni 1.1. Lengo la fedha hizi ni kwenda kunusuru kaya masikini zilizokuwa zinaishi kwenye wimbi kubwa la umasikini, ambapo fedha hizi zimefanikiwa kufikia kaya 1,378,916. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kaya hizo, kuna wanakaya milioni tano, fedha hizi zilienda kufanya nini? Hapa nataka nieleze kwa sababu kuna mambo mengi yameelezwa. Hizi fedha zilikuwa siyo za kugawiwa tu, zimetengenezewa programu maalumu. Programu ya kwanza iliyofanyika kupitia Programu ya *TASAF*, kwanza ilikuwa ni kwenda kutoa ruzuku kwenye kaya maskini na ile ruzuku ilikuwa inatolewa kwa kutolewa masharti maalumu. Kama familia ina watoto wanaosoma shule, utakavyokuwa unahimiza watoto kwenda kusoma na ndivyo kipato cha kaya kitaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unahudhuria vizuri *clinic* na hospitali, hicho kipato cha kaya kitaongezeka. Kwa hiyo, hii ilisukuma mwamko wa kwenye jamii, jamii ikaamka ikawapeleka watoto wengi shule, jamii ikaamka ikaanza kuhudhuria kwenye matibabu, jamii ikaamka ikaingia pia katika programu ya kuwekeza na kuweka akiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka ninavyoongea hivi, kupitia programu ya *TASAF* tayari kuna wanufaika 880,000 ambao wamenufaika na programu hii, wanajiwekeza katika vikundi vya akiba na kukopa, ambapo fedha walizowekeza huko ni takribani shilingi bilioni 13 na katika fedha hizo shilingi bilioni 13 tayari mpaka sasa wanakopeshana shilingi bilioni 7.9. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni *achievement* kubwa. Maana yake ni nini? Kwanza, wamepata *discipline* ya ujasiriamali; pili, ni *financial literacy* kwa maana ya menejmenti ya fedha. Kwa hiyo, hatukuishia tu hapo, katika kaya hizi, amesema Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara kuhusu habari ya Bodi ya Mikopo. Naomba niseme, *success story* na hii, sifa kubwa imwendee Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipoanza mahusiano kati ya *TASAF* na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, watoto waliokuwa wanatoka kwenye kaya maskini walikuwa 656, leo hii ninavyoongea katika Bunge hili, tayari watoto wanaonufaika kutoka kaya maskini kupitia Programu ya mahusiano *(MOU)* iliyoingiliwa kati ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu na *TASAF* ni vijana 12,500 ambao wananufaika na wanapata mkopo kwa 100%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikutoe hofu Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, jambo hili tumeliwekea utaratibu mzuri, waratibu wetu wa wilaya wanawatambua hawa watoto, wanawapeleka *TASAF* Makao Makuu, wakifika *TASAF* wanawapeleka Bodi ya Mikopo Elimu ya Juu, wakifika pale hakuna urasimu, hakuna *bureaucracy* yoyote, kijana anapata mkopo 100% na Serikali inaisimamia hili ili litokee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, haijaishia hapo, tumeenda mbali zaidi. Kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, hawa vijana wanaotoka kaya maskini watakapokuwa wamemaliza Darasa la Saba na wakashidwa kuendelea, wanapata fursa ya kwenda *VETA* chini ya ufadhili wa mifuko ya kuwezesha wananchi kiuchumi iliyo chini ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi zote ni *initiatives* ambazo lengo la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha katika zile *SDG*, ikiwa *SDG one, goal one* ilikuwa ni *no poverty,* kuondoa na kutokomeza umaskini, anatekeleza kwa vitendo na kwa kweli Mheshimiwa Rais amefanya jambo hili na kwa kweli anastahili pongezi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikimalizia hapo, *TASAF* kuna jambo limezungumzwa sana, wazee kujitolea, na wazee kufanyishwa kazi. Naomba hii dhana iwe wazi, *TASAF* haina programu ya kulazimisha wazee kufanyishwa kazi. Ile kwanza ni hiari na tume-*limit age* kati ya miaka 18 mpaka hapo 65; na hiyo ni hiari ya mtu kwenda kufanya hiyo kazi, halazimishwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, na kwa kuwa jambo hili ni shirikishi, sisi tutaongeza usimamizi kuhakikisha kwamba wale wazee wengine wanaopenda tu kwamba mimi nikafanye kazi, lakini baadaye inaonekana kwamba *TASAF* wanalazimishwa kwenda kufanya kazi, kwa hiyo, niwaondoe shaka Waheshimiwa Wabunge, hili jambo tutaliweka vizuri na kuhakikisha kwamba linaondoa sintomfamu ambayo ipo *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye suala la watumishi, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais, amefanya *incentive* kubwa sana. Nikianza na suala la malimbikizo ya mishahara, jambo hili Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo mahususi na tumeanza kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niliaarifu Bunge lako Tukufu kwamba mpaka tulivyokuwa tunafunga mwezi Machi, tayari tulikuwa tumetambua watumishi takribani 130,464 ambao walikuwa wanadai malimbikizo, na hii fedha ya kuwalipa ilikuwa ni bajeti ya shilingi bilioni 207. Naomba niendelee kuwahakikishia kuwa Serikali ipo kwenye mpango wa kuhakikisha hawa watumishi tunamaliza kuwalipa malimbikizo yao ya mishahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie Bunge lako Tukufu kutoa rai kwa waajiri. Baadhi ya waajiri wamekuwa na kasumba ya kutokuleta mapema madai hayo ya malimbikizo, wanakaa nayo huko, hatimaye wanafanya madai hayo yanakuwa ya muda mrefu, wanasababisha malalamiko kwa watumishi wakati Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa maelekezo na ameruhusu bajeti hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wetu ulikuwa, kati ya mwaka huu wa fedha na ujao tuwe tumemaliza wa zamani ili waje wapya, hao ambao tutakuwa tunawa-*sort* na idadi yao itakuwa ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, kwenye suala hili tutalisimamia na niendelee kuwasisitiza waajiri, na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ifikapo tarehe 31 Mei wale waliokuwa *pending* ambao hawajaleta Ofisi ya Rais - Utumishi madai hayo ya malimbikizo ya mishahara wayalete ili tuyafanyie kazi, tuyahakiki na baadaye tuyapeleke Hazina kusubiria malipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la madaraja *(promotion)*. Waheshimiwa Wabunge wengi wameongelea na wamegusia hasa kundi kubwa la walimu waliopata ajira mwaka 2008, 2009, 2012 na 2013, pia wengine walioachwa huku, naomba kwanza nishukuru kwa pongezi zenu kwa Mheshimiwa Rais ku-*acknowledge* kwamba kazi kubwa imefanyika katika kupandisha watumishi madaraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwape neno lingine la matumaini. Katika mwaka huu wa fedha tunaokwenda kuumaliza tayari, tumetenga bajeti ya shilingi bilioni 226 kwa ajili ya kwenda kupandisha madaraja watumishi 219,042; na hili tunaenda kulisimamia na mpaka kufika Machi tayari tulikuwa tumebakiwa na watumishi 48,042. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili niwasisitize pia waajiri, kama kuna mtumishi mwenye sifa ambaye alikuwa anastahili

kupata hiyo *promotion* wahakikishe tarifa zinakuja Ofisi ya Rais, Utumishi ili sisi tuchakate. Lengo la Mheshimiwa Rais anataka tunapoanza huko mbele tuwe na wale wapya wanaodai *promotion* na siyo wa zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, yale makundi 2009, 2008, 2012, na 2013 niwaondoe shaka. Tunaenda kusimamia kuhakikisha madaraja yao wanayapata kwa msererereko ili walingane *seniority* na wale wenzao waliowatangulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, hoja ni nyingi, lakini tuahidi, hoja zote zile mlizotoa tutawajibu kwa maandishi kila Mbunge na tutamfikishia hoja zote. Kwa kuwa muda ni mdogo, tungeweza kumjibu kila mmoja, na kutoa ufafanuzi wa kila mmoja, lakini zote tumezipokea, mtaona tutawajibu; na kwa sababu bado tupo ndani ya Bunge hili, tutaendelea kutaarifiana namna ambavyo tunatekeleza majukumu haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Naibu Waziri, Sektretarieti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, inakushukuru sana kwa kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge na kuchukua *commitment* za kuendelea kufanya kazi hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba mniruhusu nimkaribishe mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri, Boniface Simbachawene. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia hoja yetu. Tumebahatika kupata wachangiaji wengi, ukichukua wa leo 16; waliochangia Ofisi ya Waziri Mkuu, watatu; na Ofisi ya Rais,

TAMISEMI, mmoja; tumepata wachangiaji takribani 20. Tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa niseme tu, hoja zilizosemwa ni nyingi sana, na zote ni hoja muhimu kwa sababu zinahusu sekta ambayo ni muhimu kwa Taifa, na kwa nchi yoyote duniani. Mtumishi wa Umma kama alivyosema Mheshimiwa Olelekaita, ndiyo injini na msingi wa maendeleo wa Taifa lolote lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hoja zote hapa ni za msingi na pengine kwa sababu ya muda, tunaweza tusipate nafasi ya kuzijibu ipasavyo, nitajaribu kwa kugusa baadhi ya zile nitakazobahatika kuzijibu, na kwa wale ambao kwa namna moja au nyingine sitakuwa nimewataja au kugusa kabisa hoja zao, basi tutazijibu kwa maandishi ili ziweze kuwafikia mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na hoja zilizotolewa na Kamati, kwa sababu Kamati ndiyo msingi wa hoja yetu, nao ndio walioleta hoja hii hapa Bungeni. Kamati imekuwa na maeneo ya muhimu sita. Imehimiza fedha inayoidhinishwa na Bunge iweze kupatikana kwa wakati, lakini imehimiza zaidi kuimarisha zaidi misingi ya utawala bora na kuimarisha mifumo ya utendaji kazi Serikalini; na hili limesemwa na Waheshimiwa Wabunge wengine, lakini pia kuboresha mishahara na maslahi ya watumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemsikia Mheshimiwa Kassinge hapa anasema juu ya walimu na wengine mmesema juu ya wengine. Leo nimepata na ushabiki mwingine wa Ndugu yangu, Katibu Mkuu Mstaafu wa CCM, Mheshimiwa Dkt. Kurwa kumbe naye ni mwalimu mzuri ingawa ni *agemate* wangu, lakini inaonekana nami alinifundisha pia mahali fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ya Kamati imekuwa ni kuboresha mafunzo kwa watumishi wa umma ambayo itaongeza weledi na ustadi, lakini kuondoa tatizo la kila taasisi kujadili na kuimarisha mifumo ya ajira, na pia kuboresha mifumo

ya ufanyaji usaili. Hizi zimekuwa ndizo hoja za Kamati na ndioyo zilizojenga msingi wa michango mingine iliyofuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwashukuru sana Kamati ya Bunge ya Katiba, Utawala na Sheria kwa kazi kubwa ambayo mmefanya katika kipindi chote ambacho tumekuwa na ninyi, nami nimefanya kazi nanyi takribani miaka miwili na kidogo, na ndiyo maana Mheshimiwa Naibu Waziri amesema hapo, kwa kweli tumekuwa na malezi mazuri sana ya Kamati ambayo yeye ndio anayeiongoza; Mheshimiwa Dkt. Mhagama, Naibu Makamu wako Mheshimiwa Kyombo pamoja na Wajumbe wote wa Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wa Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria ni watu wazuri ambao wametenda haki na wamekuwa wazalendo kwa nchi yetu. Nawapongeza na kuwaombea kila la heri kwenye majimbo na kwa maeneo waliyotoka ya uwakilishi yaliyoletwa humu Bungeni, watambue kwamba wamekuwa na mchango uliotukuka katika kuwawakilisha huku Bungeni kupitia Kamati waliyopangwa na Mheshimiwa Spika. Kwa hiyo, naamini tutakutana hapa baada ya uchaguzi mwezi Oktoba *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zilizosemwa ni nyingi, nianze na maeneo mahususi hasa hii inayohusu watumishi na utumishi wa umma kama rasilimali muhimu katika Taifa. Utumishi na watumishi wa umma una historia ndefu. Tulikuwa na utumishi wa kikoloni na baadaye tukapata uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipopata uhuru tukawa na utumishi unaofuta ukoloni na kuwa na uhuru wa kujiamulia mambo yetu wenyewe na kwa hiyo, tulikuwa hatuna wasomi na baadaye tukaja kwenye *reforms* ambazo zimefanyika katika utumishi wa umma na zilizopelekea mafanikio makubwa ya awamu zote za uongozi wa nchi yetu; na hata ilipokuja Awamu hii ya Sita ilikuja kuweka miguu yake kwenye utumishi wa umma, huu ambao umetupa mafanikio makubwa haya tunayoyaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ilivyo na matukio makubwa na mafanikio makubwa yaliyofanyika katika nchi yetu, kwa kweli ukiubeza utumishi wa umma na watumishi wa umma wa nchi hii utakuwa hautendi haki. Pamoja na changamoto zilizopo wamefanya kazi kubwa, wamefanya kazi nzuri, chochote utakachojivunia na kukiona, wamefanya watumishi hawa hawa wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jukumu letu kama ambavyo Kamati imesema kuendelea kujenga uwezo wa watumishi wa umma, na kuleta *reforms* mbalimbali. Niwaambie tu, tayari tumeanza kutayarisha *reforms* ya utumishi wa umma utakaokwenda sambamba na wakati huu wa sasa na ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia uchumi huu ambao tumeufikia wakati wa chini na baadaye kwenda wakati wa juu, ni lazima tubadilishe utumishi wetu wa umma. Utumishi wa umma ambao utakutana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia, utumishi wa umma utakaokutana na *artificial intelligence,* lazima na wenyewe ubadilike uende kwa kasi ile ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania hawa waliohudumiwa kwa vipindi vyote toka tupate uhuru, siyo hao watakaohudumiwa baada ya miaka mitano ijayo. Watahitaji kasi, uwazi, umakini lakini wanahitaji haki katika kutendewa wajibu na watumishi wa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme kwamba tunatambua hilo kama Serikali na tutahakikisha kwamba *reform* hiyo inayokuja, inayoandaliwa, basi ikiwezekana iwashirikishe wadau muhimu ikiwemo Bunge, kuhakikisha kwamba tunajenga utumishi wa umma utakaoishi miaka mingine 50 ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni ajira. Katika ajira hizi, katika kipindi cha miaka fulani nyuma ajira zilisimama; na ziliposimama zika-*create gap* ambayo imeleta shida sasa na kukuta baadhi ya kada zikiwa zina wahitimu wengi sana sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika suala la ajira kuna fursa lakini kuna changamoto lakini pia kuna maoni yametolewa mengi sana Waheshimiwa Wabunge. Nataka niseme, maoni yote yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli tumeyachukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna pongezi zilizotokana na maendeleo ya utumishi wa umma, na kama kuna maarifa ambayo yametolewa hapa, sisi tunayachukuwa na kwa kweli pongezi zote ziende kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa sababu ni katika kipindi chake amepandisha madaraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, malimbikizo ya madeni ya mishahara na madeni yasiyo ya mishahara yamelipwa kwa kiasi kikubwa sana. Ufahamu tu kwamba katika kipindi cha Mama Samia, pia tumekuwa na vipaumbele mbalimbali katika nchi, na pia watumishi wa umma hawakuachwa nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi yamesemwa na wawakilishi wa utumishi, wametoa maoni yao hapa wakina Mheshimiwa Janejelly, wameeleza namna ambavyo Mheshimiwa Rais amefanya mambo makubwa kwa watumishi ukilinganisha na siku zilizopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni mbalimbali pia yametolewa kuhusiana na ajira. Kweli idadi ya ajira zimeongezeka na zimekuwa nyingi. Katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa vibali vya ajira 149,000. Ni idadi kubwa sana, lakini hata hivyo tuna upungufu wa ajira kwa baadhi ya waajiriwa wa baadhi ya kada. Hata hivyo, ajira mbadala kwa wale wanaotoka kwa namna moja au nyingine, ikiwemo na wanaostaafu huwa wanafidiwa, ametoa vibali takribani 39,934.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu Waheshimiwa Wabunge, pamoja na changamoto zilizosemwa, lakini idadi hii ya watumishi ni kubwa sana kwa vibali tulivyovipata kwa miaka hii mitatu, lakini niwaambie tu habari njema, na waajiriwa ambao wamefanya

usaili na wapo kwenye *database,* nataka niwajulishe tu, Mheshimiwa Rais siku ya jana ametoa kibali cha kuajiri watumishi wengine wapya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, samahani kidogo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ametoa kibali cha kuajiri watumishi wapya kwa mwaka huu huu, 33,212. Ajira hizi tukizigawanya tutapata za walimu takribani 10,000 lakini bado ajira mbadala na kwenye walimu tutapata pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikizungumzia kada ya walimu tu, nimejaribu kushauriana na wenzangu kwenye ofisi, tumesema kwa kweli kwenye hizi ajira sasa hatuna haja ya kufanyisha usaili upya kwa upande wa kada ya walimu. Tutakwenda kwenye *database* kwenda kuendelea kupakua wale waliosalia ili tuendelee kuhakikisha kwamba tunawamaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo rahisi kuwamaliza kwa sababu waliofaulu mpaka sasa hivi ambao wapo wanangojea kupatikana kwa nafasi bado ni wengi na kama tulivyosema kwamba usaili ni utaratibu tu wa kujaribu kugombania hizo ajira chache zinazopatikana, lakini kimsingi karibu wote wameandaliwa vizuri na wapo tayari kwa ajili ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana walipokuja wale vijana wa *NETO* nikasema wacha tuzungumze kwa sababu kusema ukweli wana haki ya kusikilizwa, na vijana wale walisema mambo makubwa sana, na kwa kweli mimi niliwaelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme, kama tumejenga miundombinu ya shule zetu, sekondari na msingi kwa kiasi tulichofanya, kama tumeongeza madarasa kwa kiasi tulichofanya, kama tumeongeza udahili kwa kiasi ambacho tumeongeza udahili kwa kiasi ambacho kimesemwa, kwa nini

tusiongeze idadi ya walimu ili wa-*fit* idadi ya mahitaji inayotakiwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana hawaishii pale, nami nataka niwasemee kwa sababu huko wanasemwa sana na wenzao. Wanasema, tumesema uchumi wetu umekua, sasa tupo uchumi wa kati, lakini tukisoma ripoti ya *CAG* tunasikia mara kuna hela imepotea na nini na nini. Tunafikiri, hii yote ingeangaliwa sisi tungepata ajira ya kuziba hili *gap* na kwenda kufundisha wenzetu ambao ni watoto wanaohitaji elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukisikia hoja kama hiyo mzazi unasema huyu mtoto ni mkorofi? Sio mkorofi. Mtoto anaomba kazi unasemaje mkorofi? Sio mkorofi. Kwa hiyo, nafikiri kazi ya Serikali ni kuendelea kutafuta fursa ya kuhakikisha kwamba inaajiri idadi ya kutosha kwa mahitaji ya Serikali, lakini siyo rahisi kwa Serikali kuajiri wahitimu wake wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Serikali duniani imewahi kuajiri wahitimu wake wote. Fani zipo mbalimbali, hii elimu tunayoisema sasa kwa sababu ya mahitaji yaliyopo na ukiangalia na upungufu tulionao, lakini kwa kada nyingine ninadhani kabisa kwamba sekta binafsi iendelee kuimaraishwa ili isaidie kuajiri wahitimu wengi zaidi. Kwa kada nyingine tunadhani kabisa kwamba sekta binafsi iendelee kuimarishwa ili isaidie kuajiri wahitimu wengi zaidi na katika kufanya hivyo, tutaisaidia nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wowote wa uchumi ni lazima uende sambamba na *absorption capacity* ya *human capital* ya nchi kwenda kufanya kazi, lakini isihesabiwe kwamba kuwa na wahitimu wengi ni balaa au mkosi. Kuwa na wahitimu wengi waliomaliza vyuo vya kati na vyuo vikuu ni mafanikio ya kujenga *human capital* ya maana katika nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wala tusijutie bali tuendelee kutafuta *solution* ya namna ya kuwapatia ajira vijana hao au wao kujiajiri na wengine kuajiri wenzao wengine. Kwa hiyo,

hili nadhani ni *cross cutting* na ni lazima wote tulione hivyo na tushughulike nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi kama Serikali tumekuja na *solution* ambayo ilitoka hapa Bungeni na Kamati yako imeshiriki katika kutusaidia kuboresha, kwamba, katika utumishi wa umma hakuna msamiati unaoitwa ajira za kujitolea, lakini sisi tumedhani kwa kushirikiana na wadau katika Serikali, Wizara ya Elimu, Wizara ya Afya, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na wengine, tukasema tufikiri tufanye nini maana kuna kundi kubwa limekaa na wengine wanaenda kulima matikiti wakati hawakusomea matikiti na huku tuna upungufu wa mwalimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine wanaenda kufanya shughuli ambazo hawapaswi kufanya. Mfano, *Clinical Officer* anaendesha bodaboda wakati angeenda kutibu, na tuna upungufu pale wa daktari wa kutibu. Tukasema tuweke utaratibu mzuri wa kujitolea. Kwa hiyo, tumekuja na huu msamiati wa ajira za kujitolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni matokeo ya maoni ya Bunge hili, nasi tumefanyia kazi na katika ajira hizi tumeeleza namna ambavyo hao wanavyopatikana kujitolea watapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tumezungumzia habari ya uwazi na ushindani katika kujitolea huko, kwa sababu kwa sasa hivi, kujitolea kulikuwepo na kulikuwa kunafanyika, lakini ilikuwa ni kujuana na pengine kuonekana kwamba huyu mtu anayekuja kujitolea, amepotea hivi, pengine hana maana, lakini tumetaka kurasimisha na kuweka mfumo ambao utasaidia hao wanaojitolea waweze kupata hata stahiki zao za kujikimu wakati wanajitolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tumezungumzia hata namna wanavyopaswa kuhitimisha huko kujitolea kwao. Kwa hiyo, kimsingi, kujitolea kumewekewa mwongozo ambao utasaidia kuhakikisha kwamba wanaojitolea wanatendewa haki na wanapimwa. Pia hata utekelezaji wa majukumu hayo waliyopewa na usimamizi wao unakuwa uko dhahiri na wa wazi ili

waweze kutumia ujuzi wao na kuonesha uzalendo katika kujenga nchi yao, badala ya kuonekana huko mitaani wananung'unika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa mwongozo huu utaanza kutumika mwezi Julai, mwaka 2025 na tayari umekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa hapa eneo lingine linalohusu wahadhiri wa vyuo vikuu na kwamba vyuo vyetu havina wahadhiri wa kutosha kwa sasa. Pia, suala la kustaafu mapema kama ambavyo amesema Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara na hata akina Mheshimiwa Prof. Ndakidemi, wamekuja kwenye siasa, siyo ajabu wangekuwa wanafundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili tumefanya marekebisho makubwa. Kwanza, usaili wa wahadhiri unafanywa na vyuo vikuu vyenyewe; pili, utawala wao wa kiutumishi utafanyika na vyuo vikuu vyenyewe; tatu, umri wa kustaafu tuliuongeza na sheria hii siyo ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka mimi nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati iliyobadilisha hii sheria katika Bunge lile lililopita, tukauongeza umri wa kustaafu na kufanya miaka 65 lakini tukasema anaweza akaajiriwa tena kwa ajira ya mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya hivyo kwa sababu gani? Siyo wote wanaostaafu wakawa wana afya nzuri kama walivyokuwa kazini. Umri unapokwenda, inahitaji kidogo kufanya *vetting* ili kusema huyu mtu unataka aendelee na utumishi au asiendelee. Halafu utumishi wa umma unakuja kuwasajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika utumishi wa umma na nchi yetu hii yenye misingi ya kijamaa, ni lazima tuwe na utumishi wa umma mmoja. Tusiwe na utumishi wa umma ambao ni *scatter*. Ndiyo maana hata katika ajira zozote zile zitakazofanyika kokote kule, basi watumishi hawa wataitwa watumishi wa umma na daftari lao la watumishi litakuwa ni hili moja ambalo liko Wizara ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukishaingiza kwenye lile daftari, hatuna maana ya kuingilia uhuru wao wa kuwapata wahadhiri, lakini pia kuwasimamia. Hayo mambo yanafanyika kwenye vyuo vikuu vyenyewe. Pia, hata hao waliotoka vyuo vikuu wameendelea kufundisha vyuo vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Taifa hatukupata hasara ya moja kwa moja kwa sababu wameenda kufanya kazi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hiyo, nadhani siyo jambo baya, lakini tutaendelea kuhakikisha kwamba vyuo vikuu vinazalisha wahadhiri wengi zaidi kadri iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejitahidi kugusa baadhi ya maeneo yale ambayo yameguswa na Waheshimiwa Wabunge wengi, lakini nizungumzie hili la maslahi ya watumishi na hasa kwa mguso mkubwa wa maslahi na motisha kwa walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba walimu wana majukumu makubwa. Ni kweli kama ilivyosemwa hapa kwamba walimu wanafanya kazi mpaka muda ambao ni wa ziada na ni kweli kwamba walimu katika nchi yetu tumewadogosha. Nadhani Serikali tumesikia, Serikali imesikia, tutatafakari na ndiyo maana sera ya elimu na walimu katika nchi yetu sasa imeboreshwa ili kuhakikisha kwamba tunapata walimu bora na wazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma kidogo walimu walikuwa wanachukuliwa wale walimu wale wa *division one* na *two* hukuti mtu akiwa mwalimu. Ifike mahali sasa wa *division one* na *two* ndiyo wanaotakiwa kusomea ualimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukizungumzia masuala ya maslahi, hakutakuwa na hiyo dharau au *mindset* iliyokuwepo. Nilikuwa naongea na Mheshimiwa Profesa Mkenda, naye maoni yake ni hayo na ninadhani wakati wa bajeti yake atalizungumza hili vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kwamba suala la walimu kuwa na maslahi yasiyotosheleza na wengine kufanya kazi kwenye mazingira magumu bila kuangalia posho za ziada au

motisha, limekuwa likisemwa kwa muda mrefu, na kama Serikali tumelisikia na tunalichukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, yaliyosemwa ni mengi, lakini nimejaribu kugusa yale ya jumla, lakini yako yale mahsusi ambayo yamezungumzwa. Liko moja lilisemwa na Mheshimiwa Japhet Hasunga, amesema mambo mengi, lakini niliguse hili moja la upandishwaji wa vyeo. Kimsingi, mpaka sasa upandishwaji wa vyeo siyo *automatic*, unatokana na *performance* ya mtumishi husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma tulikuwa na *OPRAS* na sasa tuna *PEPMIS* ambayo inapima utendaji kazi wa mtumishi husika kwa siku, kwa wiki, kwa mwezi na kwa mwaka. Upimaji huu unatusaidia sana kwa sababu hausemi uongo. Majukumu yameainishwa na anaripoti kwa siku. Kwa hiyo, kama ni mtoro au kama alikuwa anarandaranda itaonesha kwamba huyu hakufanya majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo huu unatupa matokeo *in real time*, umekuwa msaada mkubwa na umeboresha sana utendaji, lakini binadamu hawaaminiki, wanaweza wakacheza nao. Kimsingi mtu hapandi *automatic*, ni lazima awe amefanya kazi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika, wamezungumzia utendaji wa kitaasisi kutimiza malengo. Mfumo wake unaitwa *PIPMIS* ambao unapima utendaji wa taasisi ili iweze ku-*graduate* kutoka hatua moja kwenda hatua nyingine na wenyewe umekuwa na msaada mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lilizungumzwa jambo hapa linalohusiana na Sekretarieti ya Ajira na majukumu yake kwa mujibu wa sheria, na vibali vinavyotolewa na Katibu Mkuu Utumishi kwa taasisi na baadhi ya mashirika kufanya usaili yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, sheria inaruhusu hilo kufanyika. Katibu Mkuu Utumishi anaweza akaruhusu taasisi

ikafanya usaili wa watu kwa sababu mahsusi. Pili, liko sharti kwamba, pamoja na kibali hicho, bado Sekretarieti ya Ajira itapaswa kuweka macho yake pale kuangalia kama taratibu zote zimezingatiwa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hata kama ajira zitafanyika na taasisi yoyote ile, bado jicho la sekretarieti litakuwepo. Hapa limezungumziwa jambo kuhusu Usaili wa *TRA* ambao unaendelea sasa na ambao kimsingi bado haujafika mwisho na umekuwa na maelezo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme, maoni yenu Waheshimiwa Wabunge, mawazo yenu na kwa sababu pia Kamati imelisema hili, na kwa idadi kubwa mmelisema, tumeyasikia na tutakwenda kushauriana ndani ya Serikali ili tuweze kuona kama kuna mambo hayako sawa, basi tuweze kuyaweka sawa ili manung'uniko haya yaweze kupungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo lilisemwa na Waheshimiwa Wabunge, ni lile la uhamisho wa watumishi. Kama nilivyosema, uhamisho wa watumishi ni jambo gumu kulitekeleza na tunaendelea kulitekeleza kidogo kidogo, lakini tunaogopa kuleta mtikisiko wa utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba tuliwaahidi hapa katika Bunge lililopita kwamba tutafanya msawazo na katika huo msawazo tutajitahidi sana ku-*balance*. Siyo tu wale watakaohama kufuata wenza wao au kwa mazingira mengine ya ugonjwa kwa sababu, jamani watumishi wa umma ni binadamu. Yaani huwezi ukamwambia binadamu, utakaa hapa na nimekwambia utakaa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, tija yake hutaiona na kazi hiyo hatafanya, hasa kama unamzungumzia mwalimu anayepaswa kwenda kufundisha halafu ana mke wake, yupo sijui wapi, au mume wake yuko mbali, kimsingi ataingia pale darasani,

anachofundisha haelewi na anaowafundisha hawaelewi kwa sababu ana kadhia zinazomkabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi tunathamini mchango wa watumishi wa umma. Tunaamini hatuna watumishi wa umma wanaotosha, na tunajua mamlaka nyingine hasa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinachukia sana kuhamisha watumishi, lakini ni ubunifu tu wa Maafisa Utumishi na Waajiri kuhakikisha kwamba, tunapowapelekea waajiri waajiriwa wapya, basi wana wa-*place* katika maeneo yale ambayo watumishi wale wametoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kama litakuwa ni jambo gumu nasi tunapochukua hatua hii, tutajitahidi sana kuhakikisha kwamba tunaifanya kwa kuangalia na kushauriana na waajiri ili tusije tukaleta mtikisiko wa utendaji kazi katika maeneo husika. Japo jambo hili kwa kweli watumishi wamelifurahia, ila ni vizuri busara na hekima zikatumika na waajiri kuhakikisha kwamba wanatoa ruhusu kwa watumishi ambao wana changamoto za kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamezungumzwa maeneo mengine ambayo yameguswa na watumishi wengi na hasa hili la Mheshimiwa Joelson Mpina, amezungumzia mambo mengi, lakini niseme tu, yale masuala yote aliyoyaainisha na bahati nzuri umetupatia mchango wake kwa maandishi, tutayachukua na kwenda kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako yanayohusiana na mifumo, na tathmini ya mifumo yana maelezo yake. Pengine kwenye hotuba anaweza akawa hakuipata vizuri, lakini yana maelezo yake. Taasisi nyingi zimefanyiwa tathmini na zimeunganishwa na zinafanya kazi vizuri. Ile takwimu aliyoisoma kwenye hotuba yetu pengine haikueleweka vizuri, lakini kuna maelezo yake. Tutampatia na mifumo mingine yote, imefanyiwa tathmini na inatusaidia sana katika kuboresha utendaji kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mihuri ya wenyeviti, tutajaribu kushauriana na wenzetu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa sababu nakumbuka nilipokuwa Waziri wa Tawala

za Mikoa na Serikali za Mitaa, ndipo hili lilitokea. Kidogo kulikuwa kuna *misuse* ya hii mihuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama imefika hatua kwamba ina kazi nyingine za msingi, basi tutajaribu kuangalia, lakini muhuri wa Mtendaji wa Kijiji au wa Mtaa nadhani bado upo, ila kuna muhuri wa Mwenyekiti. Kwa hiyo, tutajaribu kuliangalia na lenyewe kwa uzito wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya yote, Mheshimiwa Mpina tutayachukua na kuyafanyia kazi ikiwemo lile la Taarifa ya Tume ya Mheshimiwa Rais ya Masuala ya Kodi. Haya yote ni mambo yanayoendelea kufanyiwa kazi na yote tunayachukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, walizungumizia *issue* ya ku-*graduate* kwa wale ambao walikuwa wanasaidiwa na *TASAF*. Mheshimiwa Naibu Waziri amelizungumzia, lakini kwa sababu limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi, niseme tu, katika kupata msaada wa fedha pia kuna matumizi yasiyo sahihi ya fedha kwa wanufaika lakini wengi wao kwa kweli wamenufaika na imebadilisha maisha yao sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama kuna makosa, kule kwenye halmashauri zetu, wako Maafisa wa *TASAF* na tunaishi nao kule, tuwe tunajaribu kushirikiana nao katika kupeleka mawazo yetu na pia kuonesha kama kuna upungufu, basi mnaweza mka-*sort out* kule kule. Sisi pia kwa upande wa *TASAF* Makao Makuu, wanajitahidi sana kutumia taarifa wanazozipata kutoka halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zilizosemwa ni nyingi, lakini niseme tu, kama kuna sifa na pongezi ambazo mmezitoa, zimwendee Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Rais Mwinyi, Rais wa Zanzibar wamekuwa ni manahodha makini sana katika kuendesha nchi yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda katika miradi mingi mikubwa inayofanyika ambayo mingine imesimamiwa na Ikulu na mmeona kwenye taarifa yetu, yote hiyo ni kielelezo kwamba pengine kama siyo utashi na kama siyo nyota ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, utekelezaji wake ungekuwa mgumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaye Rais makini, mwenye maono na mwenye bahati na uongozi wake. Nchi imetulia na haiendeshwi kwa vurugu, lakini bado mambo makubwa yanatokea. Tumekamilisha miradi mikubwa, sina sababu ya kuitaja, ambayo inaipaisha nchi yetu na kuipa heshima sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ukienda kule Zanzibar, Zanzibar ya Mwinyi kweli inang'aa. Zanzibar ya Mwinyi kweli inawaka. Miundombinu ya barabara, bunifu mbalimbali za kuboresha Uchumi wa Zanzibar, uchumi wa utalii na Uchumi wa Buluu, vimeibadilisha Zanzibar kwa kiasi kukubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ninayehudumu katika Ofisi ya Rais, nataka niseme kwamba, nimepata bahati kuhudumu katika Ofisi ya Rais katika kipindi ambacho kumekuwa na mafanikio makubwa kwa Serikali zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda niwashukuru viongozi hawa na nichukue msemo aliousema Mheshimwia Prof. Kabudi kwamba, haumpongezi kiongozi wako ila unamshukuru, na ukimpongeza ina maana kuna siku hautampongeza, lakini Mheshimiwa Kabudi anasema, lazima umpongeze kiongozi wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi tunawashukuru kwa kazi hii kubwa waliyoifanya kwa Tanzania na ndiyo maana nataka nikubaliane na Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi kwa kuwapitisha wawe wagombea wetu kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina shaka wale Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, waliyaona haya yaliyofanyika na kwa uhakika walionao juu ya kazi nzuri wanayoifanya wakaona hakuna sababu ya kuchelewa, tuwapitishe ili tukafanye shughuli nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninaamini miaka mitano ijayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar zitakuwa na mafanikio makubwa na maendeleo makubwa sana sana. Ndiyo maana hata huko duniani kwingine Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa akipewa nishani mbalimbali *(awards)*. Tunakumbuka aliyopewa juzi ya *Global Goalkeepers Award,* ambayo inatambua uongozi na mchango wake katika kuimarisha afya ya uzazi na kupunguza vifo vya uzazi. Hii ni tuzo kubwa na ya heshima kubwa sana duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nikaja kuangalia kumbe tuzo siyo hiyo tu, ziko tuzo karibu 11 katika kipindi cha miaka mitatu. Kuna tuzo ya Babacar Ndiaye, inayotambua jitihada alizozifanya katika ujenzi wa miundombinu bora nchini; tuzo ya Taasisi ya Afrima ya Nchini Marekani, ambayo inatambua uongozi wake wa kimageuzi lakini ziko tuzo nyingine; tuzo ya *P-Rain Africa Award*; tuzo ya dhahabu ambayo inatekelezwa kutokana na malengo la maendeleo endelevu na tuzo nyingine ya Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuzo ni nyingi, lakini iko tuzo nyingine iliyotolewa na *Red Cross*; iko tuzo ya hapa nyumbani ya Wizara ya Elimu; iko Tuzo ya *Care Impact* na ipo Tuzo ya Taasisi ya *International Iconic* ya kutambua mchango wake katika sekta ya utalii na kuchochea ongezeko la idadi ya watalii hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuzo ya 11 ni tuzo ya Baraza la Wanawake wa CHADEMA (BAWACHA) iliyotambua mchango wa Rais katika kuleta maridhiano, kuboresha demokrasia hapa nchini na kuimarisha upendo na mshikamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuzo hizi ni kielelezo kwamba Rais wetu anafanya yale ambayo Watanzania wanayatarajia. Tumshukuru kwa kazi nzuri anayoifanya na tumwombee kwa Mungu amjalie uhai ili katika kipindi kingine cha miaka mitano tuendelee kupata matunda yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Kamati ya Matumizi

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tuketi.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 004 – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*....................................Sh. 2,148,598,000

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.................Sh. 288,351,000
Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*…….............................Sh. 281,145,000
Kifungu 1004 – *Information and Communication Technology Unit*…………………………Sh. 253,340,000
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*……..……………......Sh. 139,602,000
Kifungu 1007 – *Government Communication Unit*…..........................Sh. 84,680,000
Kifungu 1008 – *Procurement Management Unit*…......Sh. 142,485,000
Kifungu 4001 – *Archive Management Division*…….....Sh. 590,067,000
Kifungu 4003 – *Records Management Division*…........Sh. 710,444,000
Kifungu 4004 – *Founders of The Nation, Presidential Libraries and Museum Division*……..Sh. 334,529,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 020 – Ofisi ya Rais, Ikulu**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*..................................Sh. 34,804,735,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 030 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*.............................Sh. 1,024,633,125,400
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.............Sh. 1,438,959,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Coordination Division*....……………..Sh. 1,235,530,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*................................Sh. 826,832,000
Kifungu 1005 – *Information and Communication Technology Unit*...........................................Sh. 665,846,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*........Sh. 949,090,000
Kifungu 2001 – *Cabinet Secretariat*..........................Sh. 5,308,119,000
Kifungu 2002 – *Government Communication*.............................Sh. 0
Kifungu 2003 – *Good Governance and Reforms*

*Coordination Division*.........................Sh. 2,246,052,000
Kifungu 2004 – *Public Service Administration and Complaints Division*.................................... Sh.1,641,879,600
Kifungu 2005 – *Monitoring and Evaluation Unit*..........Sh. 894,242,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 032 – Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*...................................Sh. 28,664,743,492
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.................Sh. 787,336,000
Kifungu 1003 – *Government Communication Unit*….Sh. 847,524,080
Kifungu 1004 – *Procurement Management Unit*........Sh. 428,349,832
Kifungu 1005 – *Internal Audit Unit*.................................Sh. 318,676,000
Kifungu 1006 – *Planning Division*................................Sh. 1,129,821,500
Kifungu 1007 – *Legal Service Unit*................................Sh. 507,616,500

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Watu wa Serikali ninawaangalia midomo, bajeti yenu hii. Naona kila mtu yuko na pilika hapo, ninasikia sauti za Wabunge kule.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*..........Sh. 807,103,008
Kifungu 2001 – *Policy Development Division*...........Sh. 2,653,663,683
Kifungu 2002 – *Management Services Division*........Sh. 1,288,658,500
Kifungu 2003 – *Establishment Division*……................Sh. 1,543,469,000
Kifungu 2004 – *Ethic Promotion Division*......................Sh. 692,346,000
Kifungu 2005 – *Human Capital Division*.....................Sh. 1,661,506,000
Kifungu 2006 – *Performance Contracting*..................Sh. 611,131,000
Kifungu 3001 – *Human Resource*

*Development Division*.....................Sh. 11,071,700,497
Kifungu 3004 – *Division of Salary and Remuneration*…………………………...Sh. 936,000,348
Kifungu 4002 – *Management Information System Division*..…………………….Sh. 1,137,142,560

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 033 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*.....................................Sh. 2,693,639,454
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.................Sh. 709,289,560
Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*......................................Sh. 999,141,000
Kifungu 1004 – *Government Communication Unit*….Sh. 363,440,200
Kifungu 1005 – *Procurement and Management Unit*…………..…………Sh. 357,245,000
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*………………..……....Sh. 457,668,500
Kifungu 1007 – *Information and Communication Technology Unit*……….........................Sh. 679,177,656
Kifungu 1008 – *Legal Services Unit*…………………….....Sh. 401,318,860
Kifungu 2001 – *Public Leaders Ethics Enforcement Division*............................Sh. 847,711,000
Kifungu 2002 – *Public Leaders Ethics Promotion Division*…...........................Sh. 715,479,000
Kifungu 2004 – *Zonal Office – Northern Zone*…………Sh. 554,117,650
Kifungu 2005 – *Zonal Office – Southern Zone*………...Sh. 501,128,850
Kifungu 2006 – *Zonal Office – Central Zone*...............Sh. 827,171,000
Kifungu 2007 – *Zonal Office – Eastern Zone*..…………Sh. 678,642,700
Kifungu 2008 – *Zonal Office – Southern Highlands*…..Sh. 692,951,900
Kifungu 2009 – *Zonal Office – Lake Zone*………………Sh.704,524,550
Kifungu 2010 – *Zonal Office – Western Zone*..….........Sh. 735,138,500
Kifungu 2011 – *Zonal Office – Dar-es-Salaam*……....Sh. 1,040,353,620

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 067 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*....................................Sh. 4,044,455,450
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…………..Sh. 547,742,800
Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*............................Sh. 619,218,900
Kifungu 1004 – *Government Communication Unit*…Sh. 348,064,000
Kifungu 1005 – *Legal Services Unit*……….…….……Sh. 292,521,340
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*..…..Sh. 349,022,485
Kifungu 1007 – *Management Information Systems Unit*.......................................Sh. 1,149,093,025
Kifungu 1008 – *Internal Audit Unit*………………………Sh. 302,991,000
Kifungu 2001 – *Recruitment Management Unit*……Sh. 2,843,056,000
Kifungu 2002 – *Quality Control*…………….…………Sh.2,698,895,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 094 – Tume ya Utumishi wa Umma**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*...................................Sh. 3,586,181,774
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…………..Sh. 384,314,000
Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*…..........................Sh. 679,916,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*………………………Sh. 244,128,000
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*..……Sh.186,060,000
Kifungu 1006 – *Legal Services Unit*………………….….Sh. 395,024,000
Kifungu 1007 – *Government Communication Unit*….Sh. 290,097,000
Kifungu 1008 – *Information and Communication Technology Unit*………………….……Sh. 244,443,000
Kifungu 1009 – *Guidelines Formulation, Dissemination and Research*……………………….......Sh. 381,821,500
Kifungu 2006 – *Appeals and Complains Department*.......................................Sh.1,435,612,275

Kifungu 2007 – *Human Resource Standards and Compliance Department*.........Sh. 1,350,001,451

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 004 – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa**

Kifungu 4001 – *Archive Management Division*……...Sh. 944,139,000
Kifungu 4003 – *Records Management Division*……..Sh. 233,319,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 030 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri**

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Coordination Division*…………......Sh. 157,473,084,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 032 – Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*....................................Sh. 6,400,000,000
Kifungu 1006 – *Planning Division*………….………..Sh. 6,486,541,000
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*……………...........................................Sh. 0
Kifungu 2001 – *Policy Development Division*………Sh. 4,269,000,000
Kifungu 2005 – *Human Capital Management Division*……………………...............Sh. 0
Kifungu 3001 – *Human Resource*

*Development Division*……………….Sh. 2,600,000,000
Kifungu 4002 – *Management Information System Division*……….........…………………….Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 033 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*.....................................Sh. 980,000,000
Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*.....……………...Sh. 2,020,000,000
Kifungu 1007 – *Information and Communication Technology Unit*.......................Sh. 0
Kifungu 1008 – *Legal Services Unit*…………….…......................Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 067 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma**

Kifungu 1007 – *Management Information Systems Unit*......................................Sh. 1,408,828,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 094 – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma**

Kifungu 1008 – *Information and Communication Technology Unit*......................................................Sh. 500,176,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi. Mtoa Hoja Taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 123(3) (a) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi zake, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. Sasa nitawahoji Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mmehojiwa hapa na wote mmesema, 'ndiyo'. Kwa hiyo nitumie nafasi hii kutangaza rasmi kwamba Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 sasa yamepitishwa rasmi na Bunge.

Kwa hiyo, baada ya kusema hayo, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Makatibu Wakuu wote na Naibu Makatibu Wakuu wote na Watumishi wote wa ofisi hii kwa kupitishiwa makadirio yenu ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha ujao na tunawatakia kila la heri katika utekelezaji. *(Makofi)*

Nitumie fursa hii kuwashukuru kwa ushirikiano ambao mnautoa kwa Kamati yetu. Kamati yetu pia nawashukuru. Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote ahsanteni sana kwa kazi nzuri ya kuisimamia ofisi hii muhimu sana. *(Makofi)*

Pia, Waheshimiwa Wabunge wote ambao mmepata nafasi ya kushiriki mjadala huu na mmemsikia Mheshimiwa Waziri akihitimisha, lakini pia Mheshimiwa Naibu Waziri akihitimisha kwamba hoja zenu zote wamezisikia hata kama hawakupata nafasi ya kuzijibu na ushauri pia mlioutoa wameupokea na wataendelea kuufanyia kazi. Kwa hiyo, na ninyi tunawashukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nimeletewa ujumbe hapa na Mheshimiwa Gambo, kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 70 anataka kuzungumza maneno ambayo tutamsikiliza, kisha tutatoa uamuzi, Mheshimiwa Gambo.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, utakumbuka leo asubuhi wakati wa mjadala wa timu maalum ambayo uliielekeza kutokea TAMISEMI, ilitokea sintofahamu na ndani ya Bunge hili kiasi ambacho ilileta picha ambayo imekuwa siyo nzuri sana. Nimeenda kukaa na kutafakari, kwa hiyo, naomba nitumie fursa hii kutokana na sintofahamu hiyo, basi niliombe radhi Bunge lako Tukufu pamoja na wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, makofi hayo yanaashiria kwamba Wabunge wameridhika, kwa hiyo, naomba nisiongeze zaidi ili nisije nikaharibu taswira na dhamira yangu njema niliyokuwanayo kwenye jambo hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri naona umesimama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, kama utakumbuka, mchana wakati wa Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini alitoa hoja ambazo ulielekeza ile siku ya kwanza kwamba Serikali ije ijibu. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI jana alitoa maelezo ya kina juu ya tuhuma mbalimbali zikiwemo za ubadhirifu na ukiukwaji wa maadili na nyingine zote alizozisema, na mwishoni ulipotoa maelekezo Mheshimiwa Waziri amekuja kujibu ndiyo hiyo anasema ilikuwa purukushani.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu maneno haya aliyoyasema Mheshimiwa kayarudia tena leo kwenye hotuba ya Ofisi ya Rais, sasa ikisemwa tu purukushani na Hansadi inabaki na maneno yale yale, mimi niliomba Mheshimiwa Spika afafanue kama anakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri aliyoyasema. Maana baada ya Mheshimiwa Waziri kusema taarifa ya Serikali ndipo yeye akajibu. Neno hili purukushani haliondoi tafsiri ya maneno yote yale na tuhuma zote alizozisema ndani ya Hansadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo, naomba ufafanuzi au vinginevyo kwa sababu Serikali hii ya Awamu ya Sita na Bunge hili kazi yake ni kutetea haki, waende kule ambapo ulikuwa umetoa maelekezo, vinginevyo atoe ufafanuzi kwa sababu kuna maelezo yake na maelezo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, halafu mbaya zaidi, labda nimfundishe tu mdogo wangu, Spika yule akikaa pale Mezani, akitoa *ruling*

huruhusiwi kikanuni kurudia maneno yale yale, lakini umerudia mara ya pili tena wakati wa mchango. Siyo kwamba namtisha, lakini mimi ningependa tuweke *record* sawa, kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa Serikali ameshatoa maelezo.

Mheshimiwa Spika, ningependa aseme, purukushani haina maana ya kuondoa yale maneno aliyoyasema. Naomba umpe nafasi nyingine ili atoe ufafanuzi, ni kitu gani hicho anachokiombea radhi? Maana purukushani hakusema katika maelezo. Kwenye Hansadi hakuna neno 'purukushani,' kuna maelezo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ameomba fursa ya kusimama hapa Mheshimiwa Gambo na akaomba radhi kwa kilichotokea asubuhi, lakini hiyo radhi ni kwa Bunge, siyo radhi kwa Spika, kwa sababu nilipopeleka hoja hiyo kwenye Kamati yetu ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, siyo kwa sababu alikikosea Kiti, ni kwa sababu ya hoja yake aliyokuwa ameisema na alitaka afafanue zaidi, nikasema aende akafafanue huko ili tujue uhalisia ukoje?

Sasa amesimama Mheshimiwa Waziri akieleza sasa ule mlolongo wa mambo yaliyotokea na kwamba radhi ambayo Mheshimiwa Gambo ameomba ni ile inayohusu jambo ambalo lilitokea kabla mimi ya kupeleka kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, na asema hapa kwamba Mheshimiwa Gambo ametafakari, akagundua kwamba aombe radhi.

Sasa kwa maelezo aliyotoa Mheshimiwa Waziri hapa, ni kwamba Mheshimiwa Gambo alipata nafasi ya kutoa mchango wake wakati tunajadili Makadirio ya Mapato na Matumizi kwenye Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Katika mchango ule kwa sababu kulikuwa na tuhuma mbalimbali ambazo alikuwa amezisema Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMIm nikawa nimemwambia aende akafuatilie hilo jambo kisha nitampa nafasi ili aweze kutoa ufafanuzi hapa Bungeni ama kutoa taarifa.

Leo Mheshimiwa Waziri amepewa nafasi ya kutoa taarifa ambayo baada ya kutoa taarifa ile Mheshimiwa Gambo akawa

kuna maneno anaona kwamba hayakusemwa sawasawa, alitumia maneno haya. Sasa kusemwa sawasawa kuna mawili; kwa sababu ndiyo yale yale ya kutumia lugha iliyopo kwenye Kanuni, ni aidha Mheshimiwa Waziri amesema uongo ama anasema sivyo sawasawa, na mambo kama hayo.

Sasa wakati ule wa kuweka mambo sawa, ili Taarifa zetu Rasmi za Bunge zikae vizuri, Mheshimiwa Gambo akasema Mheshimiwa Waziri wakati mimi sasa namwuliza, amesema uongo kwa sababu ndiyo kanuni zetu zinavyosema, akasema hivyo. Kwa hiyo, radhi aliyokuwa anaomba ilikuwa inahusu hiyo hoja ya yeye kupelekwa sasa kwenye Kamati, siyo yeye peke yake, ni yeye pamoja na Mheshimiwa Waziri ili kule sasa ndiyo wakaeleze halafu kisha Bunge lije lielezwe hapa, nani alikuwa anasema uhalisia wa jambo, kwa sababu hapa nisingeweza kuendeleza mjadala pamoja na Mheshimiwa Gambo.

Sasa, kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri hapa, ni kwamba pamoja na kile kilichotokea mapema asubuhi nikiwa nimekaa hapa kwenye Kiti na baada ya kuelekeza jambo hili liende kwenye Kamati, ni kwamba limejitokeza sasa jambo jipya kwamba Mheshimiwa Gambo amechangia kwenye Wizara nyingine iliyo pia chini ya Ofisi ya Rais, akizungumzia tena jambo lile ambalo tayari lilishatolewa ufafanuzi na Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Kwa hiyo, hoja ya Mheshimiwa Waziri kama nimeelewa vizuri, ni kwamba, hii radhi inayoombwa ni ya hayo yote pamoja na hili lililochangiwa sasa kwenye Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora au inaombwa ile ya TAMISEMI pale, sasa nafikiri ndicho ulichokusudia Mheshimiwa Lukuvi.

Waheshimiwa Wabunge, kama hivyo ndivyo, pamoja na kwamba muda wetu umekwenda sana, mtuvumilie kidogo ili hili tuliweke sawa.

Mheshimiwa Gambo mchango wako kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, mimi sijausikia, ulikuwa unahusu hoja ambazo ulishazisema kwenye TAMISEMI na asubuhi zimetolewa ufafanuzi na Mheshimiwa Waziri

wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI au ni hoja tofauti kabisa? Baada ya kutoa hayo maelezo yako nitaweza kutoa sasa uamuzi.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, hoja niliyoitoa ilikuwa inahusiana na jambo tofauti kabisa, linahusiana na sakata la ujenzi wa stendi ya Jiji la Arusha ambayo hata kwenye majibu yale ya Mheshimiwa Waziri haikuwa sehemu ya hoja, ilikuwa ni hoja mahsusi ambayo haihusiani na zile hoja nne ambazo leo Mheshimiwa Waziri alizitolea ufafanuzi. Kama nimepitiwa, nipo tayari kukumbushwa ili niweke rekodi vizuri.

**SPIKA:** Mchango ulikuwa unahusu ujenzi wa stendi, haya kwenye taarifa fupi aliyoitoa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI asubuhi katika yale mambo aliyojielekeza kwake kuna hoja moja ya ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri, ujenzi wa soko la machinga; tatu, utengaji wa bajeti ya shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya kubomoa maduka eneo la stendi ndogo kutokuwa na tija na Halmashauri, na mambo kama hayo.

Haya ndiyo mambo yaliyofafanuliwa. Sasa hapa ngoja niangalie jina la hiyo stendi, maana haya ya stendi ndogo, natafuta jina la stendi humu. Mheshimiwa Waziri, unayo sijui yale maelezo yako? Hii stendi ndogo inayozungumzwa ni ipi? Pengine Mheshimiwa Gambo hii stendi ndogo inayoelezwa kwenye maelezo ya Mheshimiwa Waziri ya asubuhi ni ipi? Ni tofauti na stendi uliyochangia kwenye Utumishi na Utawala Bora?

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, ndiyo, ni tofauti, kwa sababu ile ni stendi mpya ya mabasi ambayo bado haijajengwa. Hii ni stendi ndogo ambayo ilitengewa *1.6 billion* mpaka pakawa pana ile sintofahamu. Kwa hiyo, ni stendi mbili tofauti.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, hizo ni stendi mbili tofauti, naweza kusema nadhani wa TAMISEMI au nani anatoka Arusha? Mimi sijui hizi stendi kama zipo tofauti.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sikuwepo ndani

ya Bunge, siwezi kufahamu hoja zake alizozungumza, nimesikia tu kwenye mitandao.

**SPIKA:** Sawa. Mheshimiwa Mbunge anasema hizi stendi ni tofauti kwa maana ya kwamba hiyo nyingine inaitwa, stendi gani Mheshimiwa Gambo; na hii stendi ndogo inaitwa jina gani?

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, hiyo inaitwa hivyo hivyo, Stendi Ndogo ya Jiji la Arusha; ile nyingine ni Stendi Mpya ya *Bondeni City* ambayo hata bado haijaanza kujengwa, ipo kwenye mchakato. Kwa hiyo, ni vitu viwili tofauti. Ndiyo maana hata Mheshimiwa Mwenyekiti wakati anaendesha kikao aliuliza hili jambo ni jipya au lilizungumzwa asubuhi? Nikamwambia ni jambo jipya kwa sababu halikuwa sehemu ya mjadala wa Wizara ya TAMISEMI.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, nilitaka tu niweke rekodi sawa, kwamba mchango alioutoa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ndiyo uliokusababisha wewe Mheshimiwa Spika ukamwambia atoe maelezo, haya yalikuwa hayajasikika. Mimi nilikuwa namwambia tu kama mdogo wangu, lakini nia yangu nilikuwa nataka kujua, hii purukushani anayoisema ya asubuhi maana yake anakubaliana na maelezo ya Serikali. Kwa kuomba radhi kwake, anakubaliana na maelezo ya Serikali?

Mheshimiwa Spika, mimi sijaelewa purukushani ni ipi iliyotokea mpaka anaomba radhi, kwa sababu *issues* alizozisema haziwezi kufutika kwa neno hilo moja. Mimi ningetegemea aseme kwamba kilichosababisha ni kwamba mimi nilitoa maelezo, Serikali imetoa maelezo nimeyaelewa, *unless* kuna jambo moja ambalo anahisi lilileta purukushani ndiyo analiombea radhi.

Mheshimiwa Spika, maana yake amesema tu purukushani, sasa mimi sijaelewa zile tuhuma zinafutikaje kwa purukushani? Serikali imetoa maelezo jinsi tuhuma zilivyoshughulikiwa na ukweli

halisi uliopo, ukatoa nafasi kule wanaweza kupata taarifa zaidi ya hizo naye anaweza kupata nafasi ya kutoa taarifa zaidi.

Mheshimiwa Spika, nilitaka tu ufafanuzi, hiyo omba yake radhi ni purukushani ipi? Ni kipande gani cha taarifa ya Serikali anachokiombea radhi? Au kwa maneno gani yeye anayoyaombea radhi aliyotamka humu ndani?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimepata fursa ya kupitia Hansadi ya yale majadiliano ya asubuhi, ukipitia Hansadi ama Taarifa zetu Rasmi za Bunge katika ile kuuliza na kujibiwa, kuuliza na kujibiwa, Mheshimiwa Gambo mwisho akatumia sasa maneno ya kwenye Kanuni kwamba Mheshimiwa Waziri amesema uwongo kwamba yeye alikuwa Mkuu wa Mkoa, kwamba mradi ulianza yeye akiwa Mkuu wa Mkoa mwaka 2019.

Sasa wakati anataka kuleta hoja nyingine, maana kwenye taarifa anasema anazo mbili, mimi sikutaka tena kumruhusu kuleta ya pili kwa sababu niliona sasa ni kama tunajadiliana humu ndani na ninyi. Nafahamu humu ndani kazi zinafanyika kwa Kamati ndiyo maana huwa sizungumzi moja kwa moja na Mheshimiwa Mbunge mmoja mmoja, nikasema waende kule kwenye Kamati ili huu uwongo wa Mheshimiwa Waziri uliosemwa hapa yeye akathibitishe kule.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 70 ndiyo inayozungumza kuhusu kutokusema uwongo Bungeni na inatoa fursa hii ambayo ndiyo amepewa hapo Mheshimiwa Gambo.

Kwa hiyo, kama ningekuwa namwongoza Mheshimiwa Gambo namna ya kuomba hiyo radhi, ningekuwa nasema anaweza sasa yeye kufuta maneno yale yaliyokuja baada ya taarifa ya Mheshimiwa Waziri kuashiria kwamba yale yote amekubali. Yaani taarifa yake, kama vile alivyokuwa amekaa kabla hajaomba mwongozo ndiyo amekubali. Kwa nini? Kwa sababu amesema mchango wake wa leo unazungumzia stendi tofauti, kwa hiyo, tunashughulika na ile ya asubuhi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Gambo anachotaka kusikia Mheshimiwa Waziri ili sasa tuongozane vizuri kikanuni, ni kwamba baada ya Serikali kutoa ufafanuzi kuhusu hoja ambazo uliziweka kwenye mchango wako ulipokuwa unachangia, siku ambayo sikumbuki tarehe, lakini siku uliyokuwa unachangia kwenye bajeti ya TAMISEMI, ule ufafanuzi uliotolewa na Mheshimiwa Waziri umeukubali na kwa hivyo yale yote mengine yanaondoka. Nadhani ndiyo hoja yako Mheshimiwa Waziri?

Kanuni ya 70 ukisoma fasili ya (7) na ya (8) ikiwa Mheshimiwa Gambo umeelewa sasa haya maelezo nikuongoze kwenye hizo Kanuni mbili halafu tunakuwa tumemaliza. Umeelewa maelezo niliyotoa?

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, nipo tayari kwa mwongozo wako.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa hii Kanuni inataka maneno yafutwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge ni kwamba anapaswa kufuta kauli yake, kwa hiyo yeye ameomba radhi na amefuta kauli. Sasa sema hayo maneno mawili ili Mheshimiwa Waziri asikie yakitokea kwako, maana yupo jirani yako hapo. Kwa hiyo, wewe futa haya maneno baada ya ule ufafanuzi nilioutoa mimi baada ya taarifa ya Mheshimiwa Waziri halafu omba radhi, tutoke hapo.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, nime-*withdraw* na ninaomba radhi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sema ninafuta badala ya neno nina-*withdraw,* napenda Kiswahili. *(Kicheko)*

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, nimefuta maneno hayo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, baada ya Mheshimiwa Gambo kuomba radhi na kufuta maneno hayo, sasa

kwa sababu hayo maneno ya kusema kwamba maneno ya Mheshimiwa Waziri hayakuwa yamekaa sawasawa, ama kwa kutumia sasa Kanuni zetu alikuwa amesema uwongo, kwa kuwa yameondoka kwenye Taarifa Rasmi za Bunge, anakuwa haendi tena kwenye Kamati yetu ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kwa sababu hakuna kinachompeleka tena huko.

Kwa hiyo, Bunge kwa makofi hayo naamini mmeafikiana na msamaha huo, ndiyo maana sijawahoji kwa sababu ingekuja Taarifa ya Kamati hapa, ningewahoji. Kwa hiyo, hata kuiondoa hii hoja kwenye Kamati ingebidi mhojiwe, lakini nimeona watu wote mnapiga makofi. Au kuna mtu hajaridhika na huo msamaha? *(Makofi)*

Sawa, sasa ili Kanuni zetu zikae sawa watu wasije wakaja kunikamata siku nyingine, basi wacha niwahoji nikiwa nimesimama.

Waheshimiwa Wabunge, wanaoafiki hoja hii kuondolewa kwenye Kamati yetu ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya Mhe. Mrisho M. Gambo na Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Iliondolewa kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, basi hoja imeondolewa rasmi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo sasa nitafuatilia huu mchango uliotolewa mchana ulikuwa unahusu jambo gani? Kwa sababu kwa mujibu wa Mheshimiwa Waziri alivyosema ni kama na wenyewe unahusu tena ubadhirifu wa aina fulani. Kwa hiyo, nitafuatilia halafu tutaweza kulifanyia kazi hilo pia kwa sura hiyo ili wananchi wajulishwe usalama wa fedha zao kama upo na kama zimeliwa, basi hatua ziweze kuchukuliwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 Asubuhi.

*(Saa 2.01 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 24 Aprili, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*